JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HALI YA UCHUMI WA TAIFA KATIKA MWAKA 2021

Kimetolewa na:
Wizara ya Fedha na Mipango
Dodoma - Tanzania
Juni 2022

HALI YA UCHUMI WA

TAIFA KATIKA MWAKA 2021

YALIYOMO

Orodha ya Majedwali viii
KIREFU/TAFSIRI YA MANENO xii
MATUKIO MUHIMU YA KIUCHUMI KWA MWAKA 2021 xviii
SURA YA 1 1
HALI YA UCHUMI WA TAIFA 1
Ukuaji wa Uchumi 1
Mizania Mpya za Bidhaa na Huduma 6
Mwenendo wa Bei 7
Ukuzaji Rasilimali 9
SURA YA 2 35
FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA 35
Ujazi wa Fedha 35
Mikopo kwa Sekta Binafsi 36
Amana katika Benki za Biashara 37
Mwenendo wa Viwango vya Riba 37
MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA 38
Huduma za Benki 38
Huduma za Mawakala wa Benki 38
Mwenendo wa Viashiria vya Sekta ya Benki 39
Maboresho katika Sekta ya Benki 39
Huduma Jumuishi za Fedha 40
Huduma Ndogo za Fedha 41
Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana 41
Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma 43
Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii 43
Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi 44
Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya 44
Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa 46
Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania 48
Benki ya Biashara Tanzania 48
Soko la Bidhaa Tanzania 49
SURA YA 3 54
FEDHA ZA SERIKALI 54
Utangulizi 54
Mwenendo wa Mapato 55
Mapato ya Ndani 55
Mikopo ya Ndani 56
Mikopo ya Nje yenye Masharti ya Kibiashara 56
Mwenendo wa Matumizi 56
Deni la Serikali 57
Deni la Nje 58
Deni la Nje kwa Wakopeshaji 58
Deni la Ndani 59
Deni la Ndani kwa Wakopeshaji 59

Tathmini ya Uhimilivu wa Deni 60
SURA YA 4 65
SEKTA YA NJE 65
Bidhaa Zilizouzwa Nje 65
Bidhaa Asilia 65
Bidhaa Zisizo Asilia 66
Mapato ya Huduma 68
Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi 69
Malipo ya Huduma 69
Mwenendo wa Biashara Baina ya Tanzania na Nchi Mbalimbali 70
Mizania ya Malipo na Nchi za Nje 75
SURA YA 5 88
HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA 88
Hali ya uchumi wa dunia 88
Mwenendo wa Biashara Duniani 90
Ushirikiano wa Uchumi Kimataifa 91
Ushirikiano wa Kiuchumi Barani Afrika 92
Ushirikiano wa Kiuchumi katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika 93
Ushirikiano wa Kiuchumi Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki 93
SURA YA 6 95
RASILIMALI WATU 95
Idadi ya Watu 95
Mgawanyiko wa Watu Kimkoa 95
Sensa ya watu na Makazi 96
Nguvu Kazi na Ajira 97
SURA YA 7 102
UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI 102
Usajili wa Miradi ya Uwekezaji 102
Mgawanyiko wa Usajili wa Miradi Kisekta 102
Mgawanyiko wa Miradi Kimkoa 103
Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje 104
Mazingira ya Biashara na Uwekezaji 105
Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 106
Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati 108
Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi 108
SURA YA 8 110
MASUALA MTAMBUKA 110
Mapambano Dhidi ya UKIMWI 110
Mazingira 110
Ulinzi na Usalama wa Raia 111
Utambuzi na Usajili wa Watu 113
Udhibiti wa Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu 114
Msajili wa Jumuiya 114
Usajili, Ufilisi na Udhamini 114
Utawala Bora 115
SURA YA 9 116

HALI YA UMASKINI NA MAENDELEO YA WATU **116**
Utangulizi 116
Hali ya Umaskini 116
Maendeleo ya Watu 119
SURA YA 10 ..... **123**
TATHMINI YA ATHARI ZA KIUCHUMI NA KIJAMII ZA UVIKO - 19 ..... **123**
Utangulizi 123
Mwenendo wa viashiria mbalimbali 124
Hatua zilizochukuliwa kukabiliana na athari za uviko - 19 128
Mpango wa kukabiliana na athari za kijamii na kiuchumi zitokanazo na uviko - 19 130
Fursa zitokanazo na uviko - 19 135
Hitimisho 135
SURA YA 11 ..... **137**
KILIMO NA USHIRIKA **137**
UZALISHAJI WA MAZAO YA KILIMO **137**
Mazao ya Chakula 137
Mazao ya Biashara 138
Mazao ya Bustani 139
Mazao ya Mbegu za mafuta 139
Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo 140
Mwenendo wa Bei na Masoko ya Mazao 141
Huduma za Ugani 141
Utafiti 142
Mafunzo ya Kilimo 142
Umwagiliaji 142
MIFUGO **142**
Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake 142
Biashara ya Mifugo na Mazao yake 143
Uzalishaji wa Chanjo za Mifugo 145
Uzalishaji wa Malisho na Utengenezaji wa Vyakula vya Mifugo 146
Mafunzo ya Mifugo 146
Utafiti wa Mifugo 146
Huduma za Ugani katika Mifugo 147
UVUVI **148**
Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi 148
Ukuzaji Viumbe Maji 148
Uvunaji wa Samaki 149
Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi 149
Mwenendo wa Uuzaji na Uingizaji wa Mazao ya Uvuvi Nje ya Nchi 150
Uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi 150
Mafunzo ya Uvuvi 151
Maendeleo ya Ushirika 151
SURA YA 12 ..... **165**
MALIASILI NA UTALII **165**
Misitu na Nyuki 165
Wanyamapori 166

Utalii 167
Malikale 169
SURA YA 13 176
MADINI 176
Leseni za Utafutaji na Uchimbaji wa Madini 176
Vibali vya Uuzaji wa Madini 176
Dhahabu 176
Almasi 177
Vito vya Thamani 177
Tanzanite 177
Makaa ya Mawe 177
Madini Mengine 178
Madini Ujenzi 178
Masoko ya Madini 178
SURA YA 14 182
VIWANDA NA BIASHARA 182
Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani 182
Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo 182
Usajili wa Biashara na Viwanda 185
Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa 185
Udhibiti Ubora wa Viwango na Vipimo 186
Usawa wa Ushindani na Udhibiti wa Bidhaa Bandia 188
Shirika la Maendeleo la Taifa 189
Uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Uwekezaji 189
SURA YA 15 196
UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI 196
UJENZI 196
Mtandao wa Barabara Nchini 196
Barabara, Madaraja, Vivuko na Magari 198
Mfuko wa Barabara 199
Nyumba na Majengo ya Serikali 199
Usajili wa Makandarasi 199
Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi 201
Baraza la Taifa la Ujenzi 201
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi 202
MAENDELEO YA ARDHI 202
Utayarishaji wa Hatimiliki, Ukaguzi na Uhakiki Milki 202
Usajili wa Hatimiliki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria 203
Uthamini wa Mali 204
Upimaji wa Mashamba na Viwanja 204
Mipango ya matumizi ya Ardhi 205
Urasimishaji wa Makazi Holela 207
Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 208
Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara 208
SURA YA 16 209
UCHUKUZI, MAWASILIANO, SANAA NA MICHEZO 209

UCHUKUZI **209**
Usafiri wa Barabara 209
Usafiri kwa Njia ya Reli 209
Usafiri wa Anga 211
Usafiri kwa njia ya Maji 213
Uchukuzi Kwenye Maziwa 218
Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania 218
MAWASILIANO **219**
Huduma za Posta 219
Huduma za Simu 220
Huduma za Intaneti 221
Huduma za Utangazaji 221
Utoaji wa Leseni za Mawasiliano 221
Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano 222
Sekta ya Habari 222
UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO **223**
Utamaduni 223
Maendeleo ya Sanaa 224
Maendeleo ya Michezo 227
SURA YA 17 ..... **236**
NISHATI **236**
Ufuaji wa Umeme 236
Utafutaji wa Mafuta na Gesi 237
Uagizaji Mafuta 238
Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Kwenda Nchi Jirani 239
Mwenendo wa Bei za Mafuta 239
Nishati Jadidifu 240
Nishati mbadala ya Gesi inayotokana na Petroli 240
SURA YA 18 ..... **243**
MAJI **243**
Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji 243
Ubora wa Maji 243
Huduma ya Maji Mijini 244
Uchimbaji wa Visima 245
Uondoaji wa Majitaka 245
SURA YA 19 ..... **248**
ELIMU MAFUNZO YA UFUNDI NA TEKNOLOJIA **248**
Elimu ya Awali 248
Elimu ya Msingi 248
Elimu ya Sekondari 249
Elimu katika Vyuo vya Ualimu 250
Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu 250
Elimu ya Ufundi na Mafunzo 251
Elimu ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 251
Teknolojia na Ubunifu 251
Elimu ya Juu 252

SURA YA 20 ..... **258**
AFYA NA MAENDELEO YA JAMII **258**
AFYA **258**
Vituo vya Kutolea Huduma za Afya 258
Huduma za chanjo kwa Watoto Chini ya Mwaka Mmoja 258
Dawa na Vifaa Tiba 259
Afya ya Uzazi na Mtoto 259
Huduma za Matibabu ya Kibingwa 260
Udhibiti wa Malaria 260
Udhibiti wa Kifua Kikuu 261
UVIKO - 19 261
Lishe 262
Mafunzo katika Kada za Afya 262
MAENDELEO YA JAMII **262**
Ustawi wa Jamii 262
Mafunzo ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii 263
Huduma ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto 263
Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Watoto 264
Maendeleo ya Wanawake na Jinsia 265
Huduma za Ustawi kwa Wazee 266
Mashirika yasiyo ya kiserikali 266

Orodha ya Majedwali

Ukurasa

Jedwali A Takwimu Muhimu Katika Uchumi - Tanzania Bara …….....xix

Jedwali B Mwenendo wa Viashiria vya Kiuchumi, 2013-2019…….....xx

Jedwali 1 Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika) 11

Jedwali 1A Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (Bei za miaka inayohusika) 12

Jedwali 2 Mchango wa shughuli za kiuchumi katika pato la taifa kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika) ….....13

Jedwali 2A Mchango wa shughuli za kiuchumi katika pato la taifa kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (Bei za miaka inayohusika) ….....14

Jedwali 2B Pato la Taifa na Matumizi yake, kwa bei za soko (Bei za miaka inayohusika) ….....15

Jedwali 3 Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi, (Kwa Bei za mwaka 2015) 16

Jedwali 3A Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko – Sehemu inayouzika na isiyouzika (Kwa Bei za mwaka 2015) …….....17

Jedwali 4 Ukuaji wa Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi (Bei za mwaka 2015) 18

Jedwali 4A Ukuaji wa Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (Bei za mwaka 2015) ….....20

Jedwali 4B Pato la Taifa na matumizi yake, kwa bei za soko (Bei za mwaka 2015) 21

Jedwali 5 Ukuzaji Rasilimali kwa aina ya shughuli (bei za miaka inayohusika) 22

Jedwali 6 Ukuzaji Rasilimali kwa aina ya shughuli (Bei za mwaka 2015) …….....23

Jedwali 7A Mchango katika Ukuzaji Rasilimali kwa aina ya Shughuli (Kwa Bei za Miaka inayohusika) 24

Jedwali 7B Ukuzaji wa Rasilimali katika Sehemu za Uchumi wa Kitaifa na Binafsi (Kwa bei za Miaka inayohusika) …….....25

Jedwali 8 Fahirisi za bei za rejereja ya bidhaa zitumiwazo na watu wa kipato cha chini Dar es Salaam (2020 = 100) ….....26

Jedwali 9 Fahirisi za Bei za rejereja ya bidhaa zitumiwazo na watu wa kipato cha chini D'Salaam (Jan - Des 2020 = 100) ….....27

Jedwali 10 Fahirisi za bei za bidhaa na huduma zitumiwazo na watu wa kima cha kati Dar es Salaam (2020 = 100) 28

Jedwali 11 Fahirisi ya Bei za bidhaa na huduma zitumiwazo na watu wa kima cha kati D'Salaam (Jan - Des 2020 =100) ….....29

Jedwali 12 Fahirisi ya Bidhaa na Huduma zitumiwazo na wenye kipato cha juu Dar es Salaam (Jan - Des. 2020=100)…….....30

Jedwali 13 Fahirisi ya gharama ya maisha ya wenye kipato cha juu Dar es Salaam (2020 =100) …….....31

Jedwali 14 Fahirisi ya bei ya bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini - Tanzania Bara (2020=100) ….....32

Jedwali 15 Fahirisi ya Bei ya Bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini - Tanzania Bara (2020 =100) …….....33

Jedwali 16 Fahirisi mbali mbali za bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini – Tanzania Bara (2020 =100) ….....34

Jedwali 17 Mwenendo wa karadha na ujazi wa fedha - Tanzania Bara.....50

Jedwali 18 Viwango vya ukuaji wa karadha na ujazi wa fedha - Tanzania Bara….....51

Jedwali 19 Mwenendo wa Viwango vya ubadilishaji fedha kati ya Shilingi na dola ya Marekani.....52

Jedwali 20 Mwenendo wa amana katika benki za biashara ….....52

Jedwali 21 Viwango vya wastani vya riba (asilimia) 53

Jedwali 22 Mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali 61

Jedwali 23 Mgawanyo wa Matumizi ya Serikali kwa huduma za Serikali (Sh. Mil) …....63

Jedwali 24 Thamani ya Bidhaa za biashara baina ya Tanzania na nchi za nje (Sh. Mil 78

Jedwali 25 Kiasi na thamani ya bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (Sh. Mil) 79

Jedwali 26 Kiasi na thamani ya bidhaa za asilia na zisizo asilia zilizouzwa nchi za nje ...80

Jedwali 27 Wastani wa bei za bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (Sh./tani) …….....83

Jedwali 28 Wastani wa bei za bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (US$/tani) 84

Jedwali 29 Mizania ya malipo na nchi za nje (US$ milioni) …….....86

Jedwali 30 Idadi ya watu nchini Tanzania kimkoa mwaka 2012-2021….....100

Jedwali 31 Kituo cha Uwekezaji Tanzania: Miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa.....109

Jedwali 32 Uzalishaji wa miwa na sukari nchini….....153

Jedwali 33 Pamba iliyonunuliwa na mauzo nchini….....154

Jedwali 34 Eneo lililopandwa michai na majani mabichi yaliyopatikana ….....155

Jedwali 35 Kahawa iliyonunuliwa na mauzo nchini ….....156

Jedwali 36 Eneo lililopandwa mkonge na katani iliyopatikana ….....157

Jedwali 37 Maua ya pareto yaliyonunuliwa na mauzo ya bidhaa za pareto nchini ..…...158

Jedwali 38 Muhtasari wa kiasi cha mazao muhimu ya biashara yaliyonunuliwa.....159

Jedwali 39 Uzalishaji katika sekta ya uvuvi mwaka 2010 2021….....160

Jedwali 40 Mwenendo wa ukuzaji viumbe maji mwaka 2017-2021…….....161

Jedwali 41 Mwenendo wa uuzaji wa samaki nje ya nchi mwaka 2011-2021 …….....162

Jedwali 42 Mauzo ya Sangara nje ya nchi ….....163

Jedwali 43 Uingizaji wa Mazao ya Uvuvi kutoka nje ya nchi ….....164

Jedwali 44 Idadi ya wageni waliotembelea Hifadhi za Taifa na Mapato ……171

Jedwali 45 Mauzo ya bidhaa za misitu katika masoko ya nje…….....172

Jedwali 46 Idadi na Mapato yatokanayo na Uwindaji wa Kitalii ….....173

Jedwali 47 Mwenendo wa biashara ya utalii ….....174

Jedwali 48 Watalii waliotembelea Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.....175

Jedwali 49 Uchimbaji wa madini: Kiasi kilichopatikana ….....180

Jedwali 50 Thamani ya madini yaliyotolewa vibali kwa ajili ya kuuzwa nje ya nch 181

Jedwali 51 Matumizi ya saruji nchini ….....190

Jedwali 52 Uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwandani 191

Jedwali 53 Viwanda - Idadi ya Watu walioajiriwa….....192

Jedwali 54 Viwanda - Gharama za kazi 193
Jedwali 55 Viwanda - Muhtasari wa matokeo 194
Jedwali 56 Viwanda - muhtasari wa matokeo kimkoa 195
Jedwali 57 Shirika la Reli Tanzania (TRL) 228
Jedwali 58 Reli ya Uhuru Tanzania.....229
Jedwali 59 A Usafirishaji kwa meli: Dar es Salaam 230
Jedwali 59 B Usafirishaji kwa meli: Tanga 231
Jedwali 59 C Usafirishaji kwa meli: Mtwara 232
Jedwali 60 Huduma za posta 233
Jedwali 61 Idadi ya wanaotumia simu za mezani na viganjani.....234
Jedwali 62 Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) 235
Jedwali 63 Uwezo wa mitambo ya umeme na umeme uliotengenezwa …….....241
Jedwali 64 Mauzo ya umeme kwa watumiaji mbalimbali 242
Jedwali 65 Mauzo ya umeme kwa mikoa 242
Jedwali 66 Uzalishaji wa maji na mapato yatokanayo na maji mijini.....246
Jedwali 67 Mahitaji na kiwango cha upatikanaji wa maji katika miji 247
Jedwali 68 Shule za sekondari za Serikali - Idadi ya wanafunzi kwa kidato 254
Jedwali 69 A Idadi ya wanafunzi na walimu katika shule za msingi na sekondari..... 255
Jedwali 69 B Idadi ya taasisi za elimu.....256
Jedwali 70 Shule za sekondari za binafsi - Idadi ya wanafunzi kwa kidato 257
Jedwali 71 Idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya.....267
Jedwali 72 Idadi ya wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya 268
Jedwali 73 Idadi ya vitanda katika hospitali zote nchini.....269
Jedwali 74 Udahili wa Wanafunzi katika Taasisi za Ustawi na Maendeleo ya Jamii…..270

KIREFU/TAFSIRI YA MANENO

AfCFTA	African Continental Free Trade Area (Eneo Huru la Biashara Afrika)
AfDB	Africa Development Bank (Benki ya Maendeleo ya Afrika)
AGTIF	Agricultural Input Trust Fund (Mfuko wa Pembejeo za Kilimo)
ART	Antiretroviral Therapy
ASA	Agricultural Seed Agency (Wakala wa Mbegu za Kilimo)
ATCL	Air Tanzania Company Limited (Kampuni ya Ndege Tanzania)
BAKITA	Baraza la Kiswahili la Taifa
BASATA	Baraza la Sanaa la Taifa
BMT	Baraza la Michezo la Taifa
BRELA	Business Registrations and Licensing Agency (Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni)
CAMARTEC	Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology (Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini)
CBE	College of Business Education
CCRT	Catastrophe Containment Relief Trust (Msaada wa Kukabiliana na Maafa)
COASCO	Co-operative Audit and Supervision Corporation (Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika)
COSOTA	Chama cha Hakimiliki Tanzania
CPB	Cereal and other Produce Board (Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Tanzania)
CT	Computed Tomography
DART	Dar Rapid Transit Agency (Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka)
DSE	Dar es Salaam Stock Exchange (Soko la Hisa la Dar es Salaam)
EAC	The East African Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki)
ECOSOC	Economic and Social Concil (Baraza la Uchumi na Jamii la Umoja wa Mataifa)
EMD	Emergence Medical Department (Kitengo cha Wagonjwa wa Dharura)
EMS	Express Mail Service (Huduma ya Kutuma Fedha, Nyaraka na Vifurushi kwa njia ya Haraka)

EPZ	Export Processing Zone (Maeneo Maalumu ya Uwekezaji)
EPZA	Export Processing Zones Authority (Mamlaka ya Mauzo Nje)
FCC	Fair Competition Commission (Tume ya Ushindani)
FETA	Fisheries Education and Training Agency (Wakala wa Mafunzo ya Uvuvi)
FYDP III	National Five - Year Development Plan Phase Three (Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano)
GWh	Saa za Gigawati
HPI	Heifer Project International (Shirika la Mitamba Duniani)
ICU	Intensive Care Unit (Vyumba vya Wagonjwa Mahututi)
iCHF	Improved Community Health Fund (Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa)
IMF	International Monetary Fund (Shirika la Fedha la Kimataifa)
KPI	Key Performance Indicator
LITA	Livestock Training Agency (Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo)
LPG	Liquified Petroleum Gas (Gesi inayotokana na Petroli)
M1	Narrow Money Supply (Ujazi wa fedha kwa Tafsiri Finyu)
M2	Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana)
M3	Extended Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana Zaidi)
MAKISATU	Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu
MOI	Muhimbili Orthopaedic Institute (Taasisi ya Mifupa Muhimbili)
MPRU	Marine Parks and Reserves Unit (Kitengo cha Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu)
NCAA	Ngorongoro Conservation Area Authority (Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro)
NDC	National Development Corporation (Shirika la Maendeleo ya Taifa)
NEEC	National Economic Empowerment Council (Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi)
NEMC	National Environment Management Council (Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira)
NFRA	National Food Reserve Agency (Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula)

NHC	National Housing Corporation (Shirika la Nyumba la Taifa)
NHIF	National Health Insurance Fund (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya)
NIDA	National Identification Authority (Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa)
NSSF	National Social Security Fund (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii)
OPV	Oral Polio Vaccine
OSHA	Occupational Safety and Health Authority (Occupational Safety and Health Authority)
PPE	Personal Protective Equipment (Mavazi ya Kujikinga)
PPP	Public Private Partnership (Ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi)
PSSSF	Public Service Social Security Fund (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma)
PWP	Public Works Programme
REPOA	Research on Poverty Alleviation (Taasisi ya Utafiti wa Jinsi ya Kupunguza Umaskini)
RUWASA	Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini
SACCOS	Savings and Credit Co-operative Society (Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo)
SADC	The Southern African Development Community (Jumuiya ya maendeleo Kusini mwa Afrika)
SAT	Sustainable Agriculture Tanzania (Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania)
SEZ	Special Economic Zone (Maeneo Maalumu ya Uwekezaji)
SGR	Standard Gauge Railway (Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa)
SIDO	Small Industries Development Organization (Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo)
TADB	Tanzania Agricultural Development Bank (Benki ya Maendeleo ya Kilimo)
TAFICO	Tanzania Fisheries Corporation (Shirika la Uvuvi Tanzania)
TAKUKURU	Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa
TAM	Tathimini ya Athari katika Mazingira
TANAPA	Tanzania National Parks (Hifadhi za Taifa Tanzania)

TANESCO	(Tanzania Electricity Supply Company) (Shirika la Ugamvi wa Umeme Tanzania)
TANROADS	Tanzania National Roads Agency (Wakala wa Barabara Tanzania)
TANTRADE	Tanzania Trade Development Authority (Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania)
TARI	Tanzania Agricultural Research Institute (Taaasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania)
TARURA	Tanzania Rural and Urban Roads Agency (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini)
TASAC	Tanzania Shipping Agencies Corporation (Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania)
TASAF	Tanzania Social Action Fund (Mfuko wa Maendeleo ya Jamii)
TAWA	Tanzania Wildlife Management Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori)
TAZARA	Tanzania Zambia Railway Authority (Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia)
TBA	Tanzania Buildings Agency (Wakala wa Majengo Tanzania)
TBS	Tanzania Bureau of Standards (Shirika la Viwango Tanzania)
TCAA	Tanzania Civil Aviation Authority (Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania)
TCB	Tanzania Commercial Bank (Benki ya Biashara Tanzania)
TCDC	Tanzania Cooperative Development Commission (Tume ya Maendeleo ya Ushirika)
TCRP	Tanzania COVID – 19 Socio Economic Response Plan (Mpango wa Kukabiliana na athari za kijamii na kiuchumi zitokanazo na UVIKO-19)
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TEMDO	Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organisation (Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania)
TEMESA	Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency (Wakala wa Ufundi na Umeme)
TEUs	Twenty Equivalent Units (Urefu wa Futi Ishirini)

TFS	Tanzania Forest Service Agency (Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania)
TI	Transparency International
TIE	Tanzania Institute of Education (Taasisi ya Elimu Tanzania)
TIC	Tanzania Investment Centre (Kituo cha Uwekezaji)
TICTS	Tanzania International Container Terminal Services (Kampuni ya Kupakua na Kupakia Makasha Tanzani)
TIRP	Tanzania Intermodal and Rail Development Project (Mradi wa Kuboresha Reli ya Kati)
TIRA	Tanzania Insurance Regulatory Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania)
TIRDO	Tanzania Industrial Research and Development Organization (Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania)
TMA	Tanzania Meteorological Agency (Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania)
TMDA	Tanzania Medicines and Medical Devices Authority (Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba)
TMX	Tanzania Merchantile Exchange (Soko la Bidhaa Tanzania)
TMRC	Tanzania Mortgage Refinance Company (Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania)
TPA	Tanzania Ports Authority (Mamlaka ya Bandari Tanzania)
TRA	Tanzania Revenue Authority (Mamlaka ya Mapato Tanzania)
TRC	Tanzania Railway Corporation (Shirika la Reli Tanzania)
TVLA	Tanzania Veterinary Laboratory Agency (Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania)
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
UNDP	United Nations Development Programme (Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa)
UNFPA	United Nations Population Fund (Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu)

UNHCR	United Nations High Commissioner for Refugees (Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi)
UNESCO	United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni)
UPU	Universal Postal Union (Ummoja wa Posta Duniani)
USAID	United States Agency for International Development
UVIKO - 19	Ugonjwa wa Virusi vya Korona
VETA	Vocational Education and Training Authority (Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi)
VVU	Virusi vya Ukimwi
WCF	Workers Compensation Fund (Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi)
WEO	World Economic Outlook
WHO	World Health Organisation (Shirika la Afya Duniani)
WMA	Weight and Measurement Agency (Wakala wa Vipimo)
WTO	World Trade Organisation (Shirika la Biashara Duniani)
ZFDA	Zanzibar Food and Drug Agency (Wakala wa Chakula na Dawa Zanzibar)

MATUKIO MUHIMU YA KIUCHUMI KWA MWAKA 2021

TAREHE	MWEZI	TUKIO
17	Machi	Aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alifariki dunia katika Hospitali ya Mzena Mkoani Dar-es-Salaam kutokana na maradhi ya moyo.
19	Machi	Aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
10	Juni	Kusomwa kwa bajeti ya mwaka 2021/22 ambayo ni ya kwanza kwa Serikali ya Awamu ya Sita.
29	Juni	Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa alizindua Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26)
28	Julai	Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alizindua rasmi utolewaji wa chanjo dhidi ya ugonjwa wa UVIKO - 19.
14	Septemba	Serikali ilizindua Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.
10	Oktoba	Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alizindua rasmi Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO - 19.

TAKWIMU MUHIMU KATIKA UCHUMI - TANZANIA BARA

Jedwali Na. A

Maelezo	2016	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko (%)
Idadi ya Watu Tanzania Bara (Milioni)	48.7	51	52.6	54.3	55.9	57.7	3.2
Pato la Taifa kwa Bei za miaka inayohusika (Sh. Milioni)	108,362,324	118,744,498	129,043,901	139,641,854	151,166,383	161,525,759	6.9
Pato la Taifa kwa Bei za mwaka 2015 (Sh. Milioni)	100,828,393	107,657,405	115,141,329	123,196,736	129,130,182	135,517,813	4.9
Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika (Sh.)	2,225,099	2,327,395	2,452,406	2,573,324	2,653,790	2,798,224	5.4
Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za 2015 (Sh.)	2,070,398	2,110,088	2,188,195	2,269,888	2,306,682	2,347,670	1.8
Kasi ya Upandaji Bei (asilimia)	5.2	5.3	3.5	3.4	3.3	3.7	12.1
Urari wa Biashara ya Bidhaa (US$ milioni)	-3589.8	-3040.95	-3853.51	-3415.5	1,517.20	1,852.10	22.1
Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho wa Mali (US$ milioni)	-2,740.50	-1,827.10	-2248.3	-1490.9	-1,459.90	-2,465.80	68.9
Saruji Iliyotumika (Tani '000)	6,028,794	4,359,163	4,577,117	6,104,108	5,887,775	6,742,932	14.5
Umeme Uliouzwa (GWH)r	5,496.10	5,565.80	5,876.60	6,161.00	6,199.40	6,766.90	9.2
Utalii (Mapato US$ milioni)	2,131.60	2,199.80	2,432.90	2,604.50	714.5	1,402.50	96.3
Reli: Uchukuzi Mizigo (Tani '000)	198	341	379.3	355.1	339.7	370.3	9.0
Elimu: Wanafunzi katika Shule za Msingi ('000) *	8639.2	9317.8	10,112	10,605	10,925	11,196.80	2.5
Elimu: Wanafunzi katika Shule za Sekondari ('000) *	1807	1908.9	2,149	2,338	2,473	2,671.90	8.0
Hospitali: Idadi ya Vitanda	59,757	60,952	62,203	80,164	84,162	86,131	2.3
Mauzo Nje ya Mazao Muhimu ya Biashara (Mil. US$)							
Bidhaa Asilia							
Kahawa	153.69	126.27	148	152.2	145	155	6.9
Pamba	46.76	36.76	68.38	91.8	87.5	81.3	-7.1
Katani	17.23	28.73	32.54	19.3	17.6	20.2	14.8
Chai	44.79	49.13	45.82	45.7	32.4	32.9	1.5
Tumbaku	339.2	195.81	269.95	146.5	148.7	127.5	-14.3
Korosho	320.24	529.7	109.56	353.1	359.6	159	-55.8
Karafuu	10.47	55.42	0.36	9.1	17.1	51.8	202.9
Bidhaa zisizo Asilia							
Madini	1930.02	1694.48	1615.4	2,326.70	3369.1	3103.17	-7.9
Bidhaa za Viwanda	684.86	676.27	894.29	851.8	908.6	1213.2	33.5
Samaki na Mazao ya Samaki	143.7	193.01	181.85	168	139.6	164.3	17.7
Mazao ya Mboga na Maua	274.1	148.65	147.7	202.4	274.1	373	36.1
Bidhaa zilizouzwa tena (Re-export)	194.07	143.16	186.71	242.8	87.7	90.2	2.9
Bidhaa nyinginezo	271.64	223.29	340.4	394.3	474.2	819.1	72.7
Ujazi wa Fedha							
Ujazi wa Fedha - M3 (Sh. bilioni)	22,877.80	24,714.30	25,823.50	28,313.10	29,920.60	34,558.00	15.5
Karadha (Sh. bilioni)	23,775.80	24,977.20	26,249.30	28,103.30	26,139.60	30,030.50	14.9
Fedha za serikali	**2016/17**	**2017/18**	**2018/19p**	**2019/20**	**2020/21**	**2021/22**	**Badiliko (%)**
Mapato ya Ndani ya Serikali (Sh. milioni)	16,639,831.50	17,944,887.00	18,529,558.00	21,069,956.80	20,562,328	25,691,700	24.9
Matumizi ya Kawaida ya Serikali (Sh. milioni)	11,625,865.80	12,852,304.00	13,806,788.90	14,201,148	14,883,723	16,801,260	12.9
Matumizi ya Maendeleo ya Serikali (Sh. milioni)	7,272,824.30	7,615,768.30	8,493,838.50	9,301,503	11,661,402	14,977,615	28.4

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI MKUU NA BAJETI (2016 - 2021)

JEDWALI B

Mwaka wa Kalenda	2016	2017	2018	2019	2020	2021
PATO LA TAIFA						
Ukuaji halisi wa Pato la Taifa (mp)	6.9%	6.8%	7.0%	7.0%	4.8%	4.9%
Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika (mp)	14.9%	9.6%	8.7%	8.2%	8.3%	5.1%
Uwiano wa Uwekezaji na Pato la Taifa (Investment/GDP)	32.8%	30.6%	30.8%	32.1%	32.2%	33.2%
Uwiano wa Akiba kwenye Benki na Pato la Taifa (Savings/GDP)	17.2%	15.8%	16.3%	17.3%	17.2%	18.0%
MWENENDO WA BEI NA VIWANGO VYA RIBA						
Kasi ya Upandaji wa Bei (mwisho wa kipindi)	6.5%	4.0%	3.3%	3.8%	3.2%	4.2%
Kasi ya Upandaji wa Bei (wastani wa mwaka)	5.2%	5.3%	3.5%	3.4%	3.3%	3.7%
GDP deflator Inflation (bp)	7.1%	2.5%	2.0%	0.9%	0.7%	0.7%
GDP deflator Inflation (MP)	7.5%	2.6%	1.6%	1.1%	1.1%	1.3%
Riba za Mikopo (mwaka mmoja)	14.2%	13.7%	18.3%	16.7%	15.7%	16.4%
Riba za Amana za muda maalum (miezi 12)	10.8%	11.5%	11.7%	8.8%	8.3%	8.3%
Tofauti ya riba za amana na za mikopo (mwaka)	3.4%	2.2%	6.6%	7.9%	7.5%	8.1%
Kiwango cha ubadilishanaji fedha kwa Dola (wastani wa mwaka)	2,188.0	2,240.8	2,275.4	2,299.8	2,305.6	2,309.2
UJAZI WA FEDHA						
Kiwango cha ukuaji wa M3	3.4%	8.0%	4.5%	9.6%	5.7%	15.50%
Kiwango cha ukuaji wa M2	5.3%	10.4%	3.8%	11.8%	8.2%	17.60%
Mikopo Chechefu	10.3%	11.5%	10.7%	9.8%	9.8%	8.5%
Kiwango cha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi	7.2%	1.7%	4.9%	11.1%	3.1%	10.0%
UWIANO WA MIZANIA YA MALIPO YA NJE NA PATO LA TAIFA						
Bidhaa zilizouzwa nje	9.8%	8.5%	7.5%	8.8%	9.7%	9.8%
Bidhaa na huduma zilizouzwa nje	17.0%	15.7%	14.6%	15.8%	13.0%	14.3%
Bidhaa zilizonunuliwa kutoka nje	17.0%	14.2%	14.9%	14.4%	12.0%	14.5%
Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje	21.4%	18.0%	18.2%	17.3%	13.9%	17.0%
Urari wa malipo ya kawaida	-5.5%	-3.4%	-3.9%	-2.4%	-1.7%	-3.0%
Akiba ya fedha za kigeni (miezi)	**4.5**	**6.1**	**4.6**	**5.9**	**5.3**	**6.2**
UWIANO WA BAJETI YA SERIKALI NA PATO LA TAIFA						
Mwaka wa fedha	**2015/16**	**2016/17**	**2017/18**	**2018/19**	**2019/20**	**2020/21**
Mapato ya ndani	13.9%	14.7%	14.6%	13.9%	14.6%	13.3%
Mapato ya kodi	12.2%	12.4%	12.3%	11.6%	12.1%	11.2%
Matumizi (Bila rollover)	17.5%	16.6%	16.7%	16.7%	16.7%	17.2%
Matumizi ya kawaida	13.2%	10.2%	10.1%	10.4%	9.8%	9.6%
Matumizi ya maendeleo	4.3%	6.4%	6.5%	6.4%	6.9%	7.6%
Misaada	0.5%	1.0%	0.8%	0.3%	0.6%	0.5%
Nakisi (kabla ya misaada)	-3.9%	-2.4%	-2.6%	-3.5%	-2.5%	-4.3%
Nakisi (baada ya misaada)	-3.4%	-1.4%	-1.9%	-3.2%	-1.9%	-3.9%
Mikopo ya nje	1.1%	1.5%	1.4%	0.9%	1.6%	1.7%
Mikopo ya ndani (kutoka benki)	1.5%	-1.0%	-0.3%	1.8%	-0.3%	1.2%

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

SEHEMU YA KWANZA

MAENDELEO YA UCHUMI JUMLA

SURA YA 1

HALI YA UCHUMI WA TAIFA

Ukuaji wa Uchumi

1. Mwaka 2021, thamani halisi ya Pato la Taifa ilifikia shilingi milioni 135,517,812.70 ikilinganishwa na shilingi milioni 129,130,182.02 mwaka 2020, sawa na ukuaji wa asilimia 4.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 mwaka 2020. Kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji kulitokana na: uwekezaji wa kimkakati hususani katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, ujenzi wa barabara, reli na viwanja vya ndege; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini hususani dhahabu na makaa ya mawe; na kuongezeka kwa mikopo katika sekta binafsi ambayo imechochea shughuli za kiuchumi. Sekta zilizokua kwa viwango vikubwa katika kipindi husika ni pamoja na: sanaa na burudani (asilimia 19.4); umeme (asilimia 10.0); madini (asilimia 9.6); na habari za mawasiliano (asilimia 9.1). Sekta za malazi na huduma ya chakula pamoja na sanaa na burudani ambazo mwaka 2020 ziliathiriwa kwa kiasi kikubwa na UVIKO - 19 zilianza kukua kwa viwango chanya mwaka 2021 kufuatia kuimarika kwa huduma za utalii ambazo zina mchango mkubwa katika sekta hizo. **Kielelezo Na. 1.1** kinaonyesha mwenendo wa ukuaji kwa baadhi ya sekta.

Kielelezo Na. 1.1: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi (asilimia)



2. Mwaka 2021, Pato ghafi la Taifa lilikuwa shilingi milioni 161,525,759.61 kwa bei za mwaka husika ikilinganishwa na shilingi milioni 151,166,443.71 mwaka 2020. Aidha, idadi ya watu Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa watu 57,724,380 mwaka 2021 ikilinganishwa na watu 55,966,030 mwaka 2020. Kutokana na mwenendo huo, wastani wa Pato kwa Mtu (GDP per capita) kwa mwaka liliongezeka kwa asilimia 3.6 na kufikia shilingi 2,798,224.23 mwaka 2021 kutoka shilingi 2,701,039.25 mwaka 2020. Kiasi hicho ni sawa na dola za

Marekani 1,211.77 mwaka 2021 kwa mtu kwa mwaka ikilinganishwa na dola za Marekani 1,171.51 mwaka 2020.

3. Ukuaji wa shughuli za kiuchumi za kilimo ambazo zinajumuisha kilimo cha mazao, mifugo, misitu na uvuvi zilipungua na kufikia asilimia 3.9 mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.9 mwaka 2020. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na kutokuwa na mvua za kutosha na za wakati katika baadhi ya maeneo ya uzalishaji. Shughuli ndogo za mifugo ndizo zilikuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji wa asilimia 5.0 ikifuatiwa na shughuli ndogo za uzalishaji mazao (asilimia 3.6), shughuli ndogo za misitu (asilimia 3.5) na shuguli ndogo ya uvuvi (asilimia 2.5) ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.0, asilimia 5.0, asilimia 3.2 na asilimia 6.8 mwaka 2020, mtawalia. Aidha, mchango wa shughuli za kilimo katika Pato la Taifa ulipungua na kufikia asilimia 26.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 26.4 mwaka 2020. Shughuli ndogo za mazao, mifugo, misitu na uvuvi zilichangia katika Pato la Taifa kwa asilimia 14.6, asilimia 7.0, asilimia 2.8 na asilimia 1.8 mwaka 2021, mtawalia.

4. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kilimo sehemu ya kuuza kilikuwa asilimia 3.9 na sehemu isiyouzika asilimia 3.5 mwaka 2021. Aidha, sehemu ya kuuza kwa shughuli ndogo za kiuchumi za kilimo cha mazao zilikua kwa asilimia 3.6, mifugo (asilimia 5.1), misitu (asilimia 3.5) na uvuvi (asilimia 2.5) mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 3.2, asilimia 4.2, asilimia 3.3 na asilimia 4.8 kwa sehemu isiyouzika, mtawalia.

5. Shughuli za kiuchumi za uchimbaji madini na mawe ni miongoni mwa shughuli zilizokuwa na ukuaji mkubwa mwaka 2021 ambapo kiwango cha ukuaji kilikuwa asilimia 9.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.2 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini ya dhahabu, chumvi, makaa ya mawe, jasi na gesi asilia. Vilevile, mchango wa shughuli za uchimbaji madini na mawe kwenye Pato la Taifa uliongezeka na kufikia asilimia 7.2 mwaka 2021 kutoka asilimia 6.6 mwaka 2020.

6. Mwaka 2021, kiwango cha ukuaji wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani kilikuwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwaka 2020. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za viwandani katika soko pamoja na muitikio wa wananchi kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini. Hata hivyo, mchango wa shughuli hizi katika Pato la Taifa ulipungua na kufikia asilimia 7.8 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 8.3 mwaka 2020.

7. Shughuli za ufuaji, usafirishaji na usambazaji umeme zilikua kwa asilimia 10.0 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 5.5 mwaka 2020. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa ufuaji wa umeme kutoka katika vyanzo vyote na kuongezeka kwa kasi ya usambazaji wa umeme vijijini. Hata hivyo, mchango wa shughuli za uzalishaji na usambazaji umeme

katika pato la taifa bado ni mdogo ambapo zilichangia asilimia 0.2 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 0.3 mwaka 2020.

8. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za usambazaji maji na udhibiti majitaka kiliongezeka na kufikia asilimia 6.5 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 5.8 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kuboreshwa kwa miundombinu ya uzalishaji maji. Mchango wa shughuli hizi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.5 mwaka 2021 kama ilivyokuwa mwaka 2020. Aidha, shughuli za usambazaji maji na udhibiti wa majitaka sehemu inayouzika zilikua kwa asilimia 6.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 5.9 kwa sehemu isiyouzika.

9. Mwaka 2021, shughuli za kiuchumi za ujenzi zilikua kwa asilimia 4.3 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 9.1 mwaka 2020. Ukuaji huo ulichangiwa na kuwepo kwa shughuli za ujenzi wa madarasa ya shule, vituo vya afya, nyumba za makazi na biashara na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege. Aidha, shughuli za ujenzi sehemu inayouzika na isiyouzika zilikua kwa asilimia 4.3 na asilimia 4.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.1 na asilimia 8.8 mwaka 2020, mtawalia. Vilevile, mchango wa shughuli za kiuchumi za ujenzi katika Pato la Taifa ulipungua na kufikia asilimia 13.8 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 14.1 mwaka 2020.

10. Shughuli za biashara na matengenezo zilikua kwa asilimia 3.5 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 2.1 mwaka 2020. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa bidhaa zilizouzwa zikiwemo bidhaa za kilimo na bidhaa zilizozalishwa viwandani; kuimarika kwa upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi; kuboreshwa kwa mazingira ya ufanyaji biashara nchini na kuongezeka kwa biashara za kikanda baada ya kulegezwa/kuondolewa kwa vikwazo vilivyowekwa kukabiliana na athari za maambukizi ya UVIKO - 19. Aidha, shughuli hii ni ya tatu kwa ukubwa katika kuchangia Pato la Taifa na ilichangia asilimia 8.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 8.6 mwaka 2020.

11. Mwaka 2021, shughuli za kiuchumi za huduma za malazi na chakula zilikua kwa asilimia 6.7 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 13.7 mwaka 2020. Hii inaashiria kuimarika kwa uchumi hususan katika sekta ya utalii ambayo iliathirika kwa kiasi kikubwa mwaka 2020 kufuatia hatua zilizochukuliwa na mataifa mbalimbali duniani ikiwemo kuzuia safari za anga ili kuepuka maambukizi ya UVIKO - 19. Baada ya kuondolewa kwa vikwazo hivyo, takriban watalii 922,692 waliingia nchini mwaka 2021 ikilinganishwa na watalii 620,867 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 48.6. Aidha, mchango wa shughuli za kiuchumi za huduma za malazi na chakula katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.1 mwaka 2021 ikilinganihshwa na asilimia 1.0 mwaka 2020.

12. Mwaka 2021, shughuli za usafirishaji na uhifadhi mizigo zilikua kwa kiwango cha asilimia 3.5 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2020. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na baadhi ya shehena ya mizigo kuhudimiwa na nchi jirani baada ya kuondolewa kwa vikwazo vya usafiri na usafirishaji kufuatia kupungua kwa maambukizi ya UVIKO - 19. Aidha, ukuaji chanya ulitokana na kuongezeka kwa shehena ya mizigo iliyohudumiwa katika bandari nchini; kuongezeka kwa abiria na shehena ya mizigo iliyosafirishwa kwa njia ya barabara, reli na anga; na kuongezeka kwa ufanisi katika huduma za upakiaji na upakuaji wa mizigo bandarini. Vilevile, shughuli za usafirishaji na uhifadhi mizigo zilichangia asilimia 7.1 katika Pato la Taifa mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 7.4 mwaka 2020.

13. Shughuli za huduma na mawasiliano zinajumuisha huduma za utayarishaji, uchapishaji na usambazaji wa taarifa mbalimbali kupitia vyombo vya habari kama vile radio, magazeti, luninga, tovuti pamoja na huduma za mawasiliano kwa njia ya simu. Shughuli hizi zilikua kwa asilimia 9.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2020. Kasi ya ukuaji ilichangiwa na kuongezeka kwa muda wa maongezi, huduma za ujumbe mfupi uliotumwa na kuongezeka kwa idadi ya wateja waliopata huduma za fedha kupitia mitandao ya simu pamoja na huduma za utangazaji na huduma za inteneti kwa ujumla. Aidha, mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.5 mwaka 2021 kama ilivyokuwa mwaka 2020.

14. Shughuli za kiuchumi katika huduma za fedha na bima zilikua kwa asilimia 4.9 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2020. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji kulitokana na kuongezeka kwa kiwango cha amana, mikopo kwa sekta binafsi, kupungua kwa mikopo chechefu na kupanuka kwa huduma za shughuli za bima. Mchango wa shughuli za huduma za fedha na bima katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 3.4 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2020.

15. Mwaka 2021, shughuli za kiuchumi za huduma za upangishaji nyumba zilikua kwa asilimia 4.5 kama ilivyokuwa mwaka 2020. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za malazi hususan katika maeneo ya mjini. Kwa upande mwingine, kiwango cha ukuaji wa shughuli za upangishaji wa nyumba sehemu ya kuuza kilikuwa asilimia 4.5 na sehemu isiyouzika asilimia 4.1 mwaka 2021. Aidha, mchango wa shughuli za kiuchumi za huduma za upangishaji nyumba katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.8 mwaka 2021 kama ilivyokuwa mwaka 2020.

16. Shughuli za kitaaluma, sayansi na ufundi zilikua kwa asilimia 6.8 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 7.3 mwaka 2020. Ukuaji wa shughuli hizo ulichangiwa na kuongezeka kwa huduma za kisheria na uhasibu. Mchango wa shughuli hizi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.7 mwaka 2021 kama ilivyokuwa mwaka 2020.

17. Shughuli za utawala wa umma na ulinzi zinajumuisha shughuli zinazofanywa na Serikali kwa maana ya sekta ya umma, shughuli za mahakama, uhamiaji, mambo ya nje, ulinzi na usalama, na usimamizi wa programu za Serikali. Mwaka 2021, shughuli za utawala wa umma na ulinzi zilikua kwa asilimia 5.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.8 mwaka 2020. Ukuaji huo ulitokana kuongezeka kwa ulipaji wa malimbikizo ya madai ya wafanyakazi; utekelezaji wa kazi za ulinzi na usalama; na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla. Mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 3.6 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 3.7 mwaka 2020.

18. Shughuli za huduma za utawala na usaidizi zilikua kwa asilimia 6.9 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 7.8 mwaka 2020. Shughuli hizo zinajumuisha ukodishaji wa vifaa, mashine na mitambo, utafutaji wa ajira, huduma za utalii, ulinzi wa mali na watu, utoaji huduma ofisini, uwakala wa kampuni za usafiri na haki ya kutumia matokeo ya kitaaluma. Mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 2.6 mwaka 2020.

19. Mwaka 2021, kiwango cha ukuaji wa shughuli za utoaji huduma za elimu kiliongezeka na kufikia asilimia 5.1 ikilinganishwa na asilimia 3.3 mwaka 2020. Ukuaji wa shughuli hizo ulitokana na kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari za umma na binafsi. Aidha, shughuli za huduma za elimu zilichangia asilimia 2.3 katika Pato la Taifa kama ilivyokuwa mwaka 2020. Kwa upande mwingine, kiwango cha ukuaji wa shughuli za afya na huduma za ustawi wa jamii kilikuwa asilimia 5.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 6.5 mwaka 2020. Ukuaji huo ulitokana na kuendelea kuboreshwa kwa utoaji wa huduma za afya kwa jamii katika ngazi zote za kutolea huduma. Mchango wa shughuli za afya na utoaji huduma kwa jamii katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.4 mwaka 2021 kama ilivyokuwa mwaka 2020.

20. Mwaka 2021, shughuli za kiuchumi za sanaa na burudani zilikuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji ikilinganishwa na shughuli nyingine zote za kiuchumi baada ya ukuaji wake kuporomoka mwaka 2020 kutokana na athari za UVIKO - 19. Shughuli za kiuchumi za sanaa na burudani zilikua kwa asilimia 19.4 mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 4.4 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi na matumizi ya watalii ambao ni watumiaji wakubwa wa bidhaa na huduma zinazotolewa katika sekta hii zikiwemo vinyago. Hata hivyo, mchango wa shughuli za sanaa na burudani katika Pato la Taifa umeendelea kuwa asilimia 0.3 kama ilivyokuwa mwaka 2020. Aidha, kiwango cha ukuaji wa shughuli za kaya binafsi katika kuajiri kilikuwa asilimia 3.1 mwaka 2021 kama ilivyokuwa mwaka 2020. Mchango wa shughuli za kaya binafsi katika Pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 0.2 kama ulivyokuwa mwaka 2020.

21. Kasi ya ukuaji wa shughuli ya huduma nyingine za jamii iliendelea kuongezeka hadi asilimia 8.5 mwaka 2021 kutoka ukuaji wa asilimia 5.0 mwaka 2020. Ukuaji wa shughuli

hiyo ulichangiwa na kuongezeka kwa watalii, idadi ya watu katika maeneo ya mjini na mahitaji ya huduma za jamii. Mchango wa shughuli hiyo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.8 mwaka 2021 kama ilivyokuwa mwaka 2020.

Kielelezo Na. 1.2: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa



Mizania Mpya za Bidhaa na Huduma

22. Mwaka 2021, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilifanya marejeo ya fahirisi za bei za taifa kutoka mwaka 2015 hadi 2020 kwa kutumia matokeo ya utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi ya mwaka 2017/18. Faharisi mpya ya bei za bidhaa na hudumu imejumuisha mikoa 26 ikilinganishwa na mikoa 25 iliyokuwa awali. Hii imetokana na kujumuishwa kwa mkoa mpya wa Songwe ambao awali ulikuwa sehemu ya mkoa wa mbeya. Aidha, fahirisi mpya zinajumuisha jumla ya makundi 13 ikilinganishwa na makundi 12 yaliyokuwa awali. Idadi ya bidhaa zinazotumika kwenye fahirisi ya bei za huduma na bidhaa imeongezeka na kufikia bidhaa 383 kutoka kutoka bidhaa 278. Kati ya hizo, bidhaa 132 ni vyakula na vinywaji baridi na bidhaa 251 zisizo za vyakula. Kutokana na mabadiliko hayo, takwimu za mfumuko wa bei zilianza kukokotolewa kwa kutumia mwaka wa kizio wa 2020 = 100 kuanzia Januari 2021. **Jedwali Na. 1.1** linaonesha mgawanyo wa makundi mbalimbali ya bidhaa na huduma na mizania zake.

Jedwali Na. 1.1: Mizania Mpya za Bei za Bidhaa na Huduma (Asilimia)

A	Makundi Makuu *(Main Groups)*	Mizania (*Weights*)		
		2010	**2015**	**2020***
1	Vyakula na vinywaji baridi	47.8	38.5	28.2
2	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	3.3	3.7	1.9
3	Mavazi ya nguo na viatu	6.7	8.3	10.8
4	Nishati, maji na makazi	9.2	11.6	15.1
5	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	6.7	6.3	7.9
6	Gharama za afya	0.9	2.9	2.5
7	Usafirishaji	9.5	12.5	14.1
8	Mawasiliano	2.1	5.6	5.4
9	Utamaduni na burudani	1.3	1.6	1.6
10	Elimu	1.7	1.5	2
11	Hoteli na migahawa	6.4	4.2	6.6
12	Biman na huduma za fedha	-	-	2.1
13	Bidhaa na huduma nyingine	4.5	3.1	2.1
	Jumla - fahirisi bidhaa zote		**100**	**100**
B	**Makundi Mengine Maalum**			
1	Fahirisi za msingi (*Core Index)*	43.3	54.3	73.9
2	Fahirisi Isiyojumuisha fahirisi za msingi *(Non-Core Index)*		-	26.1
3	Fahirisi za nishati, mafuta na bili za maji	5.7	8.7	5.7
4	Fahirisi za huduma		-	37.2
5	Fahirisi za bidhaa		-	62.8
6	Fahirisi za bidhaa na huduma za elimu		-	4.1
7	Bidhaa zote isipokuwa bidhaa za vyakula na vinywaji visivyo na kilevi	49.0	62.9	71.8

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
*Mizania Mpya (2020 = 100)

Mwenendo wa Bei

23. Mfumuko wa bei uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 3.3 mwaka 2020. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kulichangiwa na sababu zilizo nje ya uwezo wa udhibiti wa Serikali zikiwemo: kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia kutokana na athari za UVIKO - 19; kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la ndani kutokana na kuongezeka kwa bei na gharama za usafirishaji wa bidhaa na huduma kutoka nje, hususan bidhaa za petroli, mafuta ya kula, mbolea, chuma na malighafi za viwandani; na kupungua kwa upatikanaji wa mazao ya chakula katika baadhi ya masoko ya ndani kutokana na mabadiliko ya tabianchi hususan katika maeneo yanayotegemea mvua za vuli. Hata hivyo, mfumuko wa bei ulibakia ndani ya lengo la nchi la asilimia 3 hadi 5, vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika vya asilimia 8.0 na kati ya asilimia 3 hadi 7 mtawalia.

24. Mwaka 2021, idadi kubwa ya makundi makuu ya bidhaa na huduma yalionesha kuongezeka kwa mwenendo wa bei ikilinganishwa na mwaka 2020. Kundi la migahawa na

huduma za malazi lilikuwa na ongezeko kubwa zaidi, ambapo mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 4.9 ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2020. Hii ilifuatiwa na kundi la burudani, michezo na utamaduni na kundi la mavazi na viatu, ambapo mfumuko wa bei uliongezeka na kufikia asilimia 2.7 na asilimia 4.6 kutoka asilimia 0.1 na asilimia 2.2 mwaka 2020, mtawalia. Mfumuko wa bei wa vyakula na vinywaji baridi uliongezeka kufikia asilimia 4.3 mwaka 2021 kutoka asilimia 4.1 mwaka 2020. Hata hivyo, mfumuko wa bei kwa kundi la nishati, maji na makazi ulipungua kutoka asilimia 7.6 mwaka 2020 na kufikia asilimia 4.1 mwaka 2021. **Jedwali Na. 1.2** linaonesha mwenendo wa bei kwa makundi makuu ya bidhaa na huduma.

Jedwali Na. 1.2: Fahirisi za Kitaifa za Bei ya Mtumiaji (NCPI) na Viwango vya Mfumuko wa Bei Mwaka 2016 - 2021 (Msingi 2020 - 100)

Mwaka		Vyakula na Vinywaji Baridi	Vinywaji Vikali na Tumbaku	Mavazi na Viatu	Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo	Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi	Afya	Usafiri	Habari na Mawasiliano	Burudani, Michezo na Utamaduni	Huduma za Elimu	Migahawa na Huduma za Malazi	Huduma za Bima na Fedha	Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko	Fahirisi Bidhaa Zote
2016	**Fahirisi za Bei**	83	93	89	72	90	94	93	101	97	94	92	95	92	86
2017		91	96	92	77	92	96	93	101	99	95	93	96	95	90
2018		93	98	95	86	95	97	96	100	98	97	95	97	97	94
2019		96	100	98	93	98	99	99	100	100	99	98	100	99	97
2020		100	100	100	100	100	100	100	100	100	100	100	100	100	100
2021		104	102	105	104	103	103	103	102	103	101	105	100	103	104
2017	**Mfumuko wa Bei**	9.1	3.3	3.5	7.6	2.9	2.6	0.5	-0.7	2.4	0.9	1.2	1.4	3.3	5.3
2018		3.0	1.6	2.9	12.0	2.5	1.3	2.5	-1.2	-0.9	2.4	1.3	1.3	1.7	3.5
2019		2.9	2.4	3.0	7.9	3.9	1.8	3.1	0.1	1.5	1.8	4.2	2.8	2.4	3.4
2020		4.1	-0.1	2.2	7.6	1.8	0.8	1.4	0.4	0.1	1.3	1.5	0.0	1.0	3.3
2021		4.3	2.2	4.6	4.1	3.2	2.7	3.3	1.8	2.7	1.1	4.9	0.3	2.8	3.7

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

25. Mfumuko wa bei usiojumuisha chakula na nishati uliongezeka kwa nukta za asilimia 1.8 na kufikia asilimia 4.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 2.3 mwaka 2020. Aidha, mfumuko wa bei wa chakula na nishati ulikuwa asilimia 2.5 mwaka 2021. Mfumuko wa bei wa bidhaa ulikuwa wa juu zaidi kwa wastani wa asilimia 4.0 ikilinganishwa na wa huduma ulioongezeka kwa wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2021.

26. Fahirisi ya bei kwa bidhaa na huduma zitumiwazo na makundi ya watu wa tabaka la kipato cha chini na cha juu iliongezeka mwaka 2021 na kufikia asilimia 2.4 na asilimia 3.0 kutoka asilimia 2.1 na asilimia 2.4 mwaka 2020, mtawalia. Hii ilitokana na kuongezeka kwa fahirisi ya bei za bidhaa na huduma zinazotumiwa kwa wingi na makundi hayo. Hata hivyo, fahirisi ya bei kwa watu wa tabaka la kati ulipungua na kufikia 2.4 mwaka 2021 kutoka asilimia 3.5 mwaka 2020 kutokana na kupungua kwa fahirisi ya bei za bidhaa na huduma

zinazotumiwa kwa wingi na kundi hili ikiwemo chakula na burudani. **Jedwali Na. 1.3** linaonyesha mwenendo mfumuko wa bei za bidhaa na huduma kulingana na tabaka la walaji.

Jedwali Na. 1.3: Mfumuko wa Bei za Bidhaa na Huduma Zitumiwazo na Walaji Kulingana na Tabaka la Kipato

Mwaka	Vyakula na Vinywaji Baridi	Vinywaji Vikali na Tumbaku	Mavazi na Viatu	Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo	Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi	Afya	Usafiri	Habari na Mawasiliano	Burudani, Michezo na Utamaduni	Huduma za Elimu	Migahawa na Huduma za Malazi	Huduma za Bima na Fedha	Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko	Fahirisi Bidhaa Zote
WAKAZI WENYE KIPATO CHA CHINI														
2017	3.3	1.8	1.1	-0.2	3.1	1.6	2.6	0.3	5.9	10.3	0.5	2.6	0.5	1.8
2018	4.3	0.1	3.1	7.7	1.9	0.1	0.4	0.0	0.9	2.7	0.1	2.2	1.5	3.0
2019	4.3	0.8	4.0	5.3	1.9	3.1	0.2	1.0	3.4	0.0	2.2	4.0	2.2	3.3
2020	1.3	0.0	1.2	10.1	0.6	0.9	-0.1	0.2	-0.4	0.0	0.6	0.0	0.3	2.2
2021	0.6	7.3	3.1	2.9	3.9	1.9	-7.4	1.4	3.8	10.3	5.5	0.0	0.7	2.4
WAKAZI WENYE KIPATO CHA KATI														
2017	4.2	1.9	1.4	3.5	3.3	2.4	2.9	0.4	1.5	-0.1	0.6	2.6	0.8	2.8
2018	7.6	-0.1	2.1	1.8	1.3	0.3	1.9	0.0	-1.0	8.6	0.1	2.2	1.5	3.5
2019	5.4	0.4	3.5	6.8	2.2	4.5	0.1	1.5	1.8	0.0	2.7	4.0	2.4	4.0
2020	4.5	0.1	1.3	8.6	0.5	0.7	-0.7	0.5	-0.6	0.0	0.7	0.0	0.2	3.3
2021	1.2	4.2	0.7	-1.1	4.1	4.0	2.7	1.3	0.5	5.4	10.1	0.4	0.7	2.4
WAKAZI WENYE KIPATO CHA JUU														
2017	9.0	2.1	1.8	1.3	5.4	2.5	4.9	0.1	0.3	-0.1	0.8	2.6	3.3	4.2
2018	6.8	0.2	2.5	5.6	1.1	0.1	6.4	0.7	-0.4	7.8	1.0	2.1	0.6	4.6
2019	4.3	0.0	2.4	8.1	2.0	4.1	2.8	1.3	-0.6	1.5	3.7	4.1	0.1	3.5
2020	7.6	0.2	1.4	7.0	0.5	0.6	-1.8	0.5	-0.7	0.0	0.6	0.0	-0.1	2.4
2021	3.9	11.2	3.4	0.1	8.2	3.3	1.8	1.3	-1.3	3.0	7.0	0.2	1.5	3.0

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Ukuzaji Rasilimali

27. Mwaka 2021, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka husika ulifikia shilingi bilioni 65,122.35 kutoka shilingi bilioni 59,652.18 mwaka 2020. Aidha, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka 2015 uliongezeka kwa asilimia 7.2 na kufikia shilingi bilioni 55,848.05 kutoka shilingi bilioni 52,074.09 mwaka 2020. Uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za miaka husika ulifikia asilimia 40.3 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 39.5 mwaka 2020.

28. Ukuzaji rasilimali za kudumu zinajumuisha majengo; vifaa vya usafiri; mitambo na vifaa vingine; rasilimali za mazao na mifugo; na haki za umiliki, utafiti na maendeleo na huduma za kitaalamu. Mwaka 2021, ukuzaji rasilimali za kudumu kwa bei za mwaka husika

ulikuwa shilingi bilioni 69,050.95 ikilinganishwa na shilingi bilioni 64,048.51 mwaka 2020. Aidha, ukuzaji rasilimiali za kudumu kwa bei za mwaka 2015 uliongezeka kwa asilimia 5.1 na kufikia shilingi bilioni 60,434.11 kutoka shilingi bilioni 57,519.76 mwaka 2020. Vilevile, thamani ya rasilimali za mazao ya mifugo ilikua kwa asilimia 6.9 kwa bei za mwaka 2015 ikifuatiwa na ujenzi majengo (asilimia 5.8), mitambo na vifaa vingine (asilimia 3.5), haki ya umiliki, na utafiti na maendeleo na huduma za kitaalamu (asilimia 1.8), na mitambo na vifaa (asilimia 1.4). Hata hivyo, thamani ya vifaa vya usafiri ilipungua kwa asilimia 2.2.

29. Mwaka 2021, thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za mwaka 2015 ilipungua kwa shilingi bilioni 4,586.06 ikilinganishwa na upungufu wa thamani wa shilingi bilioni 5,445.68 mwaka 2020. Vilevile, thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za mwaka husika ilipungua kwa shilingi bilioni 3,928.60 mwaka 2021 ikilinganishwa na upungufu wa thamani wa shilingi bilioni 4,396.33 mwaka 2020

30. Mwaka 2021, ukuzaji rasilimali katika sekta ya umma inayojumuisha Serikali Kuu, mashirika na taasisi za Serikali kwa bei za miaka husika ulikuwa shilingi bilioni 20,888.12 ikilinganishwa na shilingi bilioni 19,790.99 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Aidha, ukuzaji rasilimali katika sekta binafsi kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 8.8 na kufikia shilingi bilioni 48,162.83 mwaka 2021 kutoka shilingi bilioni 44,257.52 mwaka 2020. Sekta ya umma ilichangia asilimia 30.3 ya rasilimali zote za kudumu mwaka 2021 na sekta binafsi ilichangia asilimia 69.7.

PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO
(Bei za Miaka Inayohusika)

Jedwali Na. 1 **Shilingi Milioni**

	SHUGHULI YA KIUCHUMI	2016	2017	2018	2019	2020	2021
A	**Kilimo, Misitu na Uvuvi**	**29,739,111**	**34,154,594**	**35,962,728**	**37,192,537**	**39,965,584**	**42,233,161**
	Kilimo cha Mazao	16,474,729	19,703,004	21,003,720	20,686,963	22,867,540	23,513,172
	Mifugo	8,205,007	8,857,939	9,240,100	10,345,069	10,609,888	11,256,597
	Misitu	3,094,767	3,310,076	3,459,581	3,738,360	3,947,993	4,578,311
	Uvuvi	1,929,747	2,245,558	2,218,731	2,379,172	2,494,162	2,836,934
	Huduma za katika shughuli za Kilimo	34,861	38,017	40,596	42,973	46,001	48,146
	Viwanda na Ujenzi	**26,937,139**	**29,735,584**	**34,851,874**	**39,944,212**	**44,950,342**	**47,844,421**
B	Uchimbaji Madini na Mawe	5,299,362	5,206,217	6,573,059	7,213,403	9,947,971	11,587,501
C	Viwanda	8,467,126	9,102,282	10,418,776	11,860,403	12,531,009	12,635,164
D	Umeme	472,868	413,351	348,527	369,917	398,084	380,057
E	Maji safi na Maji taka	433,132	519,909	566,562	628,187	745,222	876,939
F	Ujenzi	12,264,650	14,493,826	16,944,950	19,872,302	21,328,055	22,364,760
	Huduma	**42,747,407**	**45,066,596**	**48,059,561**	**51,417,505**	**55,219,451**	**59,019,313**
G	Biashara na Matengenezo	9,861,678	10,843,499	11,793,201	12,264,511	12,935,145	14,056,161
H	Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	7,549,484	7,897,993	8,381,276	9,622,792	11,172,778	11,527,736
I	Malazi na Huduma ya chakula	1,523,035	1,602,543	1,653,792	1,764,898	1,506,711	1,715,764
J	Habari na Mawasiliano	1,739,556	1,829,360	1,948,180	2,052,242	2,196,758	2,375,162
K	Fedha na Bima	5,268,866	4,789,632	4,947,301	4,927,613	5,259,757	5,414,784
L	Upangishaji Majengo	3,162,290	3,334,171	3,553,630	3,834,061	4,253,172	4,524,204
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	617,914	726,707	817,442	903,234	986,133	1,088,002
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	2,661,978	3,027,384	3,306,554	3,640,720	3,992,260	4,408,969
O	Utawala na Ulinzi	4,846,491	4,986,287	5,131,630	5,354,893	5,530,738	5,876,655
P	Elimu	2,673,289	2,864,290	3,081,718	3,322,028	3,440,525	3,649,794
Q	Afya na Huduma za Jamii	1,540,484	1,681,353	1,816,738	1,920,963	2,060,600	2,213,814
R	Sanaa na Burudani	285,626	322,353	374,924	427,887	416,049	513,448
S	Huduma nyingine za Kijamii	831,216	959,152	1,037,612	1,140,417	1,217,190	1,358,754
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	185,501	201,872	215,564	241,246	251,635	296,065
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	**99,423,658**	**108,956,774**	**118,874,163**	**128,554,255**	**140,135,377**	**149,096,895**
	Ongeza kodi katika bidhaa	8,938,667	9,787,724	10,169,738	11,087,600	11,031,006	12,428,863
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	**108,362,324**	**118,744,498**	**129,043,901**	**139,641,854**	**151,166,383**	**161,525,759**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO- SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA
(BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)

Jedwali Na. 1A **Shilingi Milioni**

	SHUGHULI YA KIUCHUMI	2016	2017	2018	2019	2020	2021
	A: SEHEMU INAYOUZIKA						
	Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)	**97,295,383**	**106,025,246**	**114,220,803**	**124,491,292**	**134,775,067**	**144,341,827**
A	**Kilimo, Misitu na Uvuvi**	**19,628,661**	**22,561,096**	**22,410,625**	**23,371,988**	**24,989,749**	**26,542,072**
	Kilimo cha Mazao	9,729,649	11,822,710	11,350,635	11,179,456	12,357,863	12,706,770
	Mifugo	6,322,457	6,877,739	6,661,287	7,457,872	7,648,783	8,115,002
	Misitu	1,706,926	1,680,599	2,229,486	2,409,141	2,544,237	2,950,438
	Uvuvi	1,834,769	2,142,032	2,128,621	2,282,546	2,392,865	2,721,717
	Huduma za katika shughuli za Kilimo	34,861	38,017	40,596	42,973	46,001	48,146
	Viwanda na Ujenzi	**26,111,436**	**28,749,158**	**33,722,200**	**38,766,672**	**43,704,002**	**46,531,497**
B	Uchimbaji Madini na Mawe	5,299,362	5,206,217	6,573,059	7,213,403	9,947,971	11,587,501
C	Viwanda	8,467,126	9,102,282	10,418,776	11,860,403	12,531,009	12,635,164
D	Umeme	472,868	413,351	348,527	369,917	398,084	380,057
E	Maji safi na Maji taka	301,821	372,032	395,810	438,862	525,028	617,826
F	Ujenzi	11,570,259	13,655,276	15,986,029	18,884,087	20,301,908	21,310,949
	Huduma	***42,616,618***	***44,927,268***	***47,918,240***	***51,265,032***	***55,050,310***	***58,839,395***
G	Biashara na Matengenezo	9,861,678	10,843,499	11,793,201	12,264,511	12,935,145	14,056,161
H	Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	7,549,484	7,897,993	8,381,276	9,622,792	11,172,778	11,527,736
I	Malazi na Huduma ya chakula	1,523,035	1,602,543	1,653,792	1,764,898	1,506,711	1,715,764
J	Habari na Mawasiliano	1,739,556	1,829,360	1,948,180	2,052,242	2,196,758	2,375,162
K	Fedha na Bima	5,268,866	4,789,632	4,947,301	4,927,613	5,259,757	5,414,784
L	Upangishaji Majengo	3,031,501	3,194,842	3,412,309	3,681,588	4,084,032	4,344,286
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	617,914	726,707	817,442	903,234	986,133	1,088,002
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	2,661,978	3,027,384	3,306,554	3,640,720	3,992,260	4,408,969
O	Utawala na Ulinzi	4,846,491	4,986,287	5,131,630	5,354,893	5,530,738	5,876,655
P	Elimu	2,673,289	2,864,290	3,081,718	3,322,028	3,440,525	3,649,794
Q	Afya na Huduma za Jamii	1,540,484	1,681,353	1,816,738	1,920,963	2,060,600	2,213,814
R	Sanaa na Burudani	285,626	322,353	374,924	427,887	416,049	513,448
S	Huduma nyingine za Kijamii	831,216	959,152	1,037,612	1,140,417	1,217,190	1,358,754
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	185,501	201,872	215,564	241,246	251,635	296,065
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	**88,356,716**	**96,237,522**	**104,051,065**	**113,403,692**	**123,744,061**	**131,912,964**
	Ongeza kodi katika bidhaa	8,938,667	9,787,724	10,169,738	11,087,600	11,031,006	12,428,863
	B: SEHEMU ISIYOUZIKA						
	Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)	**11,066,941**	**12,719,252**	**14,823,098**	**15,150,563**	**16,391,316**	**17,183,931**
A	Kilimo, Misitu na Uvuvi	**10,110,449**	**11,593,497**	**13,552,103**	**13,820,550**	**14,975,836**	**15,691,089**
	Mazao	6,745,080	7,880,294	9,653,085	9,507,507	10,509,677	10,806,402
	Mifugo	1,882,549	1,980,200	2,578,812	2,887,197	2,961,106	3,141,595
	Misitu	1,387,841	1,629,477	1,230,096	1,329,219	1,403,757	1,627,874
	Uvuvi	94,978	103,526	90,110	96,626	101,296	115,218
	Viwanda na Ujenzi	**825,703**	**986,427**	**1,129,674**	**1,177,540**	**1,246,340**	**1,312,924**
E	Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka	131,311	147,877	170,752	189,325	220,194	259,113
F	Ujenzi	694,392	838,550	958,922	988,215	1,026,146	1,053,812
	Huduma	**130,789**	**139,328**	**141,321**	**152,473**	**169,140**	**179,919**
L	Upangishaji Majengo	130,789	139,328	141,321	152,473	169,140	179,919
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	**108,362,324**	**118,744,498**	**129,043,901**	**139,641,854**	**151,166,383**	**161,525,759**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

MCHANGO WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KATIKA PATO LA TAIFA (GDP) KWA BEI ZA SOKO
(Bei za Miaka Inayohusika)

Jedwali Na. 2 **Asilimia**

	SHUGHULI YA KIUCHUMI	2016	2017	2018	2019	2020	2021
A	**Kilimo, Misitu na Uvuvi**	**27.4**	**28.8**	**27.9**	**26.6**	**26.4**	**26.1**
	Kilimo cha Mazao	15.2	16.6	16.3	14.8	15.1	14.6
	Mifugo	7.6	7.5	7.2	7.4	7.0	7.0
	Misitu	2.9	2.8	2.7	2.7	2.6	2.8
	Uvuvi	1.8	1.9	1.7	1.7	1.6	1.8
	Huduma za katika shughuli za Kilimo	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
B	Uchimbaji Madini na Mawe	4.9	4.4	5.1	5.2	6.6	7.2
C	Viwanda	7.8	7.7	8.1	8.5	8.3	7.8
D	Umeme	0.4	0.3	0.3	0.3	0.3	0.2
E	Maji safi na Maji taka	0.4	0.4	0.4	0.4	0.5	0.5
F	Ujenzi	11.3	12.2	13.1	14.2	14.1	13.8
G	Biashara na Matengenezo	9.1	9.1	9.1	8.8	8.6	8.7
H	Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	7.0	6.7	6.5	6.9	7.4	7.1
I	Malazi na Huduma ya chakula	1.4	1.3	1.3	1.3	1.0	1.1
J	Habari na Mawasiliano	1.6	1.5	1.5	1.5	1.5	1.5
K	Fedha na Bima	4.9	4.0	3.8	3.5	3.5	3.4
L	Upangishaji Majengo	2.9	2.8	2.8	2.7	2.8	2.8
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	0.6	0.6	0.6	0.6	0.7	0.7
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	2.5	2.5	2.6	2.6	2.6	2.7
O	Utawala na Ulinzi	4.5	4.2	4.0	3.8	3.7	3.6
P	Elimu	2.5	2.4	2.4	2.4	2.3	2.3
Q	Afya na Huduma za Jamii	1.4	1.4	1.4	1.4	1.4	1.4
R	Sanaa na Burudani	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3	0.3
S	Huduma nyingine za Kijamii	0.8	0.8	0.8	0.8	0.8	0.8
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	0.2	0.2	0.2	0.2	0.2	0.2
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	**91.8**	**91.8**	**92.1**	**92.1**	**92.7**	**92.3**
	Ongeza kodi katika bidhaa	8.2	8.2	7.9	7.9	7.3	7.7
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	**100.0**	**100.0**	**100.0**	**100.0**	**100.0**	**100.0**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

MCHANGO WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KATIKA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO- SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA (BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)

Jedwali Na. 2A **Asilimia**

	SHUGHULI YA KIUCHUMI	2016	2017	2018	2019	2020	2021
	A: SEHEMU INAYOUZIKA						
	Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)						
A	**Kilimo, Misitu na Uvuvi**	**18.1**	**19.0**	**17.4**	**16.7**	**16.5**	**16.4**
	Kilimo cha Mazao	9.0	10.0	8.8	*8.0*	*8.2*	7.9
	Mifugo	5.8	5.8	5.2	*5.3*	*5.1*	5.0
	Misitu	1.6	1.4	1.7	*1.7*	*1.7*	1.8
	Uvuvi	1.7	1.8	1.7	*1.6*	*1.6*	1.7
	Huduma za katika shughuli za Kilimo	0.03	0.03	0.03	***0.03***	***0.03***	0.0
B	Uchimbaji Madini na Mawe	4.9	4.4	5.1	*5.2*	*6.6*	7.2
C	Viwanda	7.8	7.7	8.1	*8.5*	*8.3*	7.8
D	Umeme	0.4	0.3	0.3	*0.3*	*0.3*	0.2
E	Maji safi na Maji taka	0.3	0.3	0.3	*0.3*	*0.3*	0.4
F	Ujenzi	10.7	11.5	12.4	*13.5*	*13.4*	13.2
G	Biashara na Matengenezo	9.1	9.1	9.1	*8.8*	*8.6*	8.7
H	Uchukuzi na Uhifadhi mizigo	7.0	6.7	6.5	*6.9*	*7.4*	7.1
I	Malazi na Huduma ya chakula	1.4	1.3	1.3	*1.3*	*1.0*	1.1
J	Habari na Mawasiliano	1.6	1.5	1.5	*1.5*	*1.5*	1.5
K	Fedha na Bima	4.9	4.0	3.8	*3.5*	*3.5*	3.4
L	Upangishaji Majengo	2.8	2.7	2.6	*2.6*	*2.7*	2.7
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	0.6	0.6	0.6	*0.6*	*0.7*	0.7
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	2.5	2.5	2.6	*2.6*	*2.6*	2.7
O	Utawala na Ulinzi	4.5	4.2	4.0	*3.8*	*3.7*	3.6
P	Elimu	2.5	2.4	2.4	*2.4*	*2.3*	2.3
Q	Afya na Huduma za Jamii	1.4	1.4	1.4	*1.4*	*1.4*	1.4
R	Sanaa na Burudani	0.3	0.3	0.3	*0.3*	*0.3*	0.3
S	Huduma nyingine za Kijamii	0.8	0.8	0.8	*0.8*	*0.8*	0.8
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	0.2	0.2	0.2	*0.2*	*0.2*	0.2
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	**81.5**	**81.0**	**80.6**	***81.2***	***81.9***	**81.7**
	Ongeza kodi katika bidhaa	8.2	8.2	7.9	***7.9***	***7.3***	7.7
	B: SEHEMU ISIYOUZIKA						
	Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)	**10.2**	**10.7**	**11.5**	***10.8***	***10.8***	***10.6***
A	Kilimo, Misitu na Uvuvi	9.3	9.8	10.5	9.9	9.9	9.7
	Mazao	6.2	6.6	7.5	6.8	7.0	6.7
	Mifugo	1.7	1.7	2.0	2.1	2.0	1.9
	Misitu	1.3	1.4	1.0	1.0	0.9	1.0
	Uvuvi	0.1	0.1	0.1	0.1	0.1	0.1
E	Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka	0.1	0.1	0.1	0.1	0.1	0.2
F	Ujenzi	0.6	0.7	0.7	0.7	0.7	0.7
L	Upangishaji Majengo	0.1	0.1	0.1	0.1	0.1	0.1
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	**100.0**	**100.0**	**100.0**	**100.0**	**100.0**	**100.0**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

PATO LA TAIFA NA MATUMIZI YAKE KWA BEI ZA SOKO (Bei za Miaka inayohusika)

Jedwali Na. 2B **Shilingi Milioni**

Aina ya Matumizi	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Pato la Taifa kwa Bei za Soko (GDPmp)	**108,362,324**	**118,744,498**	**129,043,901**	**139,641,854**	**151,166,383**	**161,525,759**
Matumizi ya Mwisho (Final consumption)	**74,761,715**	**81,577,249**	**87,731,958**	**93,002,322**	**100,644,101**	**107,720,387**
Serikali	9,824,677	10,097,404	10,468,798	10,978,620	11,115,184	11,864,451
Binafsi	64,699,505	71,211,545	76,966,654	81,712,049	89,204,342	95,489,298
Taasisi binafsi Zinazotoa huduma za kijamii	237,532	268,299	296,506	311,653	324,574	366,638
Ukuzaji rasilimali	**34,865,346**	**40,427,427**	**49,493,556**	**55,762,365**	**59,652,181**	**65,122,346**
Rasilimali za kudumu	35,492,828	42,141,921	50,387,086	59,440,540	64,048,512	69,050,945
Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani	1,105,406	1,006,179	1,215,104	1,273,337	1,838,290	1,954,173
Ongezeko la limbikizo	-1,732,887	-2,720,674	-2,108,634	-4,951,512	- 6,234,622	- 5,882,772
Mauzo nje	**17,717,213**	**17,993,324**	**19,160,137**	**22,160,020**	**20,028,362**	**23,166,003**
Bidhaa-fob	9,177,377	8,924,522	10,066,069	12,305,060	14,617,648	15,522,621
Huduma	8,539,835	9,068,803	9,094,069	9,854,960	5,410,714	7,643,382
Uagizaji	**20,665,232**	**20,320,749**	**23,103,332**	**24,152,270**	**21,051,375**	**26,957,297**
Bidhaa-fob	15,602,694	15,816,338	18,797,200	20,120,379	18,098,427	22,985,015
Huduma	5,062,538	4,504,411	4,306,132	4,031,891	2,952,948	3,972,282
Makosa na Mapungufu	1,683,283	-932,752	-4,238,418	-7,130,583	-8,106,886	-7,525,680

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI (Bei za mwaka 2015)

Jedwali Na. 3 **Shilingi Milioni**

	SHUGHULI YA KIUCHUMI	2016	2017	2018	2019	2020	2021
A	**Kilimo, Misitu na Uvuvi**	**26,436,338**	**28,008,976**	**29,504,198**	**30,802,027**	**32,323,876**	**33,577,189**
	Kilimo cha Mazao	13,996,348	14,895,622	15,659,175	16,351,312	17,174,743	17,785,972
	Mifugo	7,506,593	7,876,592	8,266,049	8,676,074	9,107,854	9,562,643
	Misitu	3,034,569	3,180,379	3,334,791	3,495,187	3,608,190	3,735,011
	Uvuvi	1,864,627	2,020,292	2,206,242	2,239,892	2,391,613	2,451,430
	Huduma za katika shughuli za Kilimo	34,201	36,091	37,941	39,562	41,475	42,133
	Viwanda na Ujenzi	**25,817,955**	**28,565,774**	**31,344,128**	**34,976,982**	**37,536,062**	**39,584,470**
B	Uchimbaji Madini na Mawe	4,356,709	4,588,624	4,659,195	5,485,112	5,878,342	6,442,881
C	Viwanda	8,213,364	8,889,818	9,623,501	10,184,558	10,646,279	11,155,762
D	Umeme	869,262	877,667	928,174	994,879	1,049,610	1,154,204
E	Maji safi na Maji taka	417,899	444,660	477,510	510,411	540,159	575,213
F	Ujenzi	11,960,720	13,765,005	15,655,747	17,802,021	19,421,672	20,256,410
	Huduma	**40,549,564**	**42,689,011**	**45,369,789**	**48,114,453**	**50,176,728**	**52,662,916**
G	Biashara na Matengenezo	9,260,703	9,821,248	10,396,691	10,965,038	11,196,339	11,590,493
H	Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	7,324,856	7,815,845	8,736,561	9,493,191	10,293,276	10,658,344
I	Malazi na Huduma ya chakula	1,480,052	1,525,619	1,604,391	1,645,950	1,419,654	1,514,711
J	Habari na Mawasiliano	1,718,548	1,824,471	1,989,717	2,133,312	2,313,029	2,524,564
K	Fedha na Bima	4,235,515	4,115,393	4,094,972	4,281,167	4,412,967	4,629,490
L	Upangishaji Majengo	3,077,086	3,211,895	3,354,518	3,505,485	3,663,972	3,827,460
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	606,207	694,291	763,332	821,636	881,833	942,013
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	2,611,498	2,892,463	3,054,288	3,311,753	3,569,800	3,817,047
O	Utawala na Ulinzi	4,793,820	4,907,113	5,064,968	5,238,491	5,438,146	5,714,547
P	Elimu	2,665,336	2,859,171	3,046,789	3,257,406	3,365,355	3,538,281
Q	Afya na Huduma za Jamii	1,497,896	1,611,999	1,746,731	1,833,514	1,953,479	2,065,677
R	Sanaa na Burudani	280,131	307,907	350,027	389,225	372,120	444,488
S	Huduma nyingine za Kijamii	814,529	912,404	971,690	1,037,083	1,089,265	1,181,814
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	183,387	189,193	195,113	201,203	207,492	213,987
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	**92,803,857**	**99,263,761**	**106,218,115**	**113,893,462**	**120,036,665**	**125,824,576**
	Ongeza kodi katika bidhaa	8,024,535	8,393,644	8,923,215	9,303,274	9,093,517	9,693,237
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	**100,828,393**	**107,657,405**	**115,141,329**	**123,196,736**	**129,130,182**	**135,517,813**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA (Bei za mwaka 2015)

Jedwali Na. 3A **Shilingi Milioni**

	SHUGHULI YA KIUCHUMI	2016	2017	2018	2019	2020	2021
	A: SEHEMU INAYOUZIKA						
	Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)	**96,464,568**	**103,029,270**	**110,210,543**	**118,007,109**	**123,675,641**	**129,855,948**
A	**Kilimo, Misitu na Uvuvi**	**22,914,869**	**24,357,439**	**25,671,332**	**26,820,733**	**28,173,836**	**29,282,339**
	Kilimo cha Mazao	11,852,633	12,666,159	13,361,566	13,975,902	14,689,553	15,222,449
	Mifugo	6,458,453	6,797,008	7,080,239	7,435,167	7,820,592	8,221,672
	Misitu	2,720,412	2,853,656	3,002,559	3,147,670	3,248,720	3,363,649
	Uvuvi	1,849,169	2,004,525	2,189,028	2,222,432	2,373,496	2,432,436
	Huduma za katika shughuli za Kilimo	34,201	36,091	37,941	39,562	41,475	42,133
	Viwanda na Ujenzi	**25,070,677**	**27,685,960**	**30,352,531**	**33,879,613**	**36,347,577**	**38,338,286**
B	Uchimbaji Madini na Mawe	4,356,709	4,588,624	4,659,195	5,485,112	5,878,342	6,442,881
C	Viwanda	8,213,364	8,889,818	9,623,501	10,184,558	10,646,279	11,155,762
D	Umeme	869,262	877,667	928,174	994,879	1,049,610	1,154,204
E	Maji safi na Maji taka	326,898	350,019	369,545	396,149	420,891	448,945
F	Ujenzi	11,304,444	12,979,833	14,772,116	16,818,914	18,352,455	19,136,493
	Huduma	**40,454,486**	**42,592,227**	**45,263,466**	**48,003,489**	**50,060,712**	**52,542,086**
G	Biashara na Matengenezo	9,260,703	9,821,248	10,396,691	10,965,038	11,196,339	11,590,493
H	Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	7,324,856	7,815,845	8,736,561	9,493,191	10,293,276	10,658,344
I	Malazi na Huduma ya chakula	1,480,052	1,525,619	1,604,391	1,645,950	1,419,654	1,514,711
J	Habari na Mawasiliano	1,718,548	1,824,471	1,989,717	2,133,312	2,313,029	2,524,564
K	Fedha na Bima	4,235,515	4,115,393	4,094,972	4,281,167	4,412,967	4,629,490
L	Upangishaji Majengo	2,982,008	3,115,112	3,248,194	3,394,521	3,547,957	3,706,630
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	606,207	694,291	763,332	821,636	881,833	942,013
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	2,611,498	2,892,463	3,054,288	3,311,753	3,569,800	3,817,047
O	Utawala na Ulinzi	4,793,820	4,907,113	5,064,968	5,238,491	5,438,146	5,714,547
P	Elimu	2,665,336	2,859,171	3,046,789	3,257,406	3,365,355	3,538,281
Q	Afya na Huduma za Jamii	1,497,896	1,611,999	1,746,731	1,833,514	1,953,479	2,065,677
R	Sanaa na Burudani	280,131	307,907	350,027	389,225	372,120	444,488
S	Huduma nyingine za Kijamii	814,529	912,404	971,690	1,037,083	1,089,265	1,181,814
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	183,387	189,193	195,113	201,203	207,492	213,987
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	**88,440,032**	**94,635,626**	**101,287,328**	**108,703,835**	**114,582,124**	**120,162,711**
	Ongeza kodi katika bidhaa	8,024,535	8,393,644	8,923,215	9,303,274	9,093,517	9,693,237
	B: SEHEMU ISIYOUZIKA						
	Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)	**4,363,825**	**4,628,135**	**4,930,787**	**5,189,627**	**5,454,541**	**5,661,865**
A	Kilimo, Misitu na Uvuvi	3,521,469	3,651,537	3,832,866	3,981,294	4,150,040	4,294,850
	Mazao	2,143,714	2,229,463	2,297,609	2,375,410	2,485,190	2,563,522
	Mifugo	1,048,140	1,079,584	1,185,810	1,240,908	1,287,262	1,340,971
	Misitu	314,157	326,723	332,233	347,517	359,470	371,362
	Uvuvi	15,458	15,767	17,214	17,459	18,117	18,995
	Viwanda na Ujenzi	**747,278**	**879,814**	**991,597**	**1,097,369**	**1,188,485**	**1,246,185**
E	Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka	91,001	94,641	107,966	114,262	119,268	126,268
F	Ujenzi	656,276	785,173	883,632	983,107	1,069,217	1,119,916
	Huduma	**95,078**	**96,783**	**106,323**	**110,964**	**116,016**	**120,830**
L	Upangishaji Majengo	95,078	96,783	106,323	110,964	116,016	120,830
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	**100,828,393**	**107,657,405**	**115,141,329**	**123,196,736**	**129,130,182**	**135,517,813**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI (Bei za mwaka 2015)

Jedwali Na. 4 **Asilimia**

	SHUGHULI YA KIUCHUMI	2016	2017	2018	2019	2020	2021
A	**Kilimo, Misitu na Uvuvi**	**4.8**	**5.9**	**5.4**	4.4	4.9	3.9
	Kilimo cha Mazao	5.4	6.4	5.2	4.4	5.0	3.6
	Mifugo	4.9	4.9	4.9	5.0	5.0	5.0
	Misitu	3.9	4.8	4.9	4.8	3.2	3.5
	Uvuvi	1.2	8.4	9.2	1.5	6.8	2.5
	Huduma za katika shughuli za Kilimo	4.0	5.5	5.2	4.3	4.8	1.6
B	Uchimbaji Madini na Mawe	7.4	5.3	1.5	17.7	7.2	9.6
C	Viwanda	10.8	8.2	8.3	5.8	4.5	4.8
D	Umeme	8.8	1.0	5.8	7.2	5.5	10.0
E	Maji safi na Maji taka	6.9	6.4	7.4	6.9	5.8	6.5
F	Ujenzi	14.5	15.1	13.8	13.7	9.1	4.3
G	Biashara na Matengenezo	5.9	6.1	5.9	5.5	2.1	3.5
H	Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	5.7	6.7	11.8	8.7	8.4	3.5
I	Malazi na Huduma ya chakula	4.1	3.1	5.2	2.6	-13.7	6.7
J	Habari na Mawasiliano	2.2	6.2	9.1	7.2	8.4	9.1
K	Fedha na Bima	1.1	-2.8	-0.5	4.5	3.1	4.9
L	Upangishaji Majengo	4.3	4.4	4.4	4.5	4.5	4.5
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	17.0	14.5	9.9	7.6	7.3	6.8
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	19.6	10.8	5.6	8.4	7.8	6.9
O	Utawala na Ulinzi	5.4	2.4	3.2	3.4	3.8	5.1
P	Elimu	10.4	7.3	6.6	6.9	3.3	5.1
Q	Afya na Huduma za Jamii	5.6	7.6	8.4	5.0	6.5	5.7
R	Sanaa na Burudani	12.7	9.9	13.7	11.2	-4.4	19.4
S	Huduma nyingine za Kijamii	13.5	12.0	6.5	6.7	5.0	8.5
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	3.2	3.2	3.1	3.1	3.1	3.1
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	**7.3**	**7.0**	**6.9**	**7.2**	**5.4**	**4.8**
	Ongeza kodi katika bidhaa	2.0	4.6	6.3	4.3	-2.3	6.6
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	**6.9**	**6.8**	**7.0**	**7.0**	**4.8**	**4.9**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Kielelezo 1.3: UKUAJI HALISI WA PATO LA TAIFA (Kwa bei za mwaka 2015) Asilimia



UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, KWA BEI ZA SOKO -SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA (Bei za mwaka 2015)

Jedwali Na. 4A **Asilimia**

	SHUGHULI YA KIUCHUMI	2016	2017	2018	2019	2020	2021
	A: SEHEMU INAYOUZIKA						
	Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)						
A	**Kilimo, Misitu na Uvuvi**	**4.4**	**6.3**	**5.4**	**4.5**	**5.0**	**3.9**
	Kilimo cha Mazao	4.6	6.9	5.6	4.6	5.1	3.6
	Mifugo	5.3	5.2	4.2	5.0	5.2	5.0
	Misitu	3.5	4.9	5.2	4.8	3.2	3.5
	Uvuvi	1.1	8.4	9.2	1.5	6.8	2.5
	Huduma za katika shughuli za Kilimo	4.0	5.5	5.2	4.3	4.8	1.6
B	Uchimbaji Madini na Mawe	7.4	5.3	1.5	17.7	7.2	9.6
C	Viwanda	10.8	8.2	8.3	5.8	4.5	4.8
D	Umeme	8.8	1.0	5.8	7.2	5.5	10.0
E	Maji safi na Maji taka	8.1	7.1	5.6	7.2	6.2	6.5
F	Ujenzi	15.1	14.8	13.7	13.9	9.1	4.5
G	Biashara na Matengenezo	5.9	6.1	5.9	5.5	2.1	3.5
H	Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	5.7	6.7	11.8	8.7	8.4	3.5
I	Malazi na Huduma ya chakula	4.1	3.1	5.2	2.6	- 13.7	6.7
J	Habari na Mawasiliano	2.2	6.2	9.1	7.2	8.4	9.1
K	Fedha na Bima	1.1	-2.8	-0.5	4.5	3.1	4.9
L	Upangishaji Majengo	4.4	4.5	4.3	4.5	4.5	4.5
M	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	17.0	14.5	9.9	7.6	7.3	6.8
N	Huduma zinazohusiana na Utawala	19.6	10.8	5.6	8.4	7.8	6.9
O	Utawala na Ulinzi	5.4	2.4	3.2	3.4	3.8	5.1
P	Elimu	10.4	7.3	6.6	6.9	3.3	5.1
Q	Afya na Huduma za Jamii	5.6	7.6	8.4	5.0	6.5	5.7
R	Sanaa na Burudani	12.7	9.9	13.7	11.2	- 4.4	19.4
S	Huduma nyingine za Kijamii	13.5	12.0	6.5	6.7	5.0	8.5
T	Shughuli za Kaya katika kuajiri	3.2	3.2	3.1	3.1	3.1	3.1
	Jumla ya Ongezeko la Thamani	**7.3**	**7.0**	**6.9**	**7.3**	**5.4**	**4.9**
	Ongeza kodi katika bidhaa	2.0	4.5	6.3	4.3	-2.3	6.6
	B: SEHEMU ISIYOUZIKA						
	Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)	6.8	6.1	6.4	5.2	5.1	3.4
A	Kilimo, Misitu na Uvuvi	7.3	3.7	5.0	3.9	4.2	4.0
	Mazao	10.0	4.0	3.1	3.4	4.6	3.6
	Mifugo	2.1	3.0	9.8	4.6	3.7	5.0
	Misitu	8.0	4.0	1.7	4.6	3.4	3.5
	Uvuvi	7.5	2.0	9.2	1.4	3.7	2.5
E	Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka	3.0	4.0	14.1	5.8	4.4	6.5
F	Ujenzi	5.2	19.6	12.5	11.3	8.8	4.7
L	Upangishaji Majengo	1.7	1.8	9.9	4.4	4.6	4.5
	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	**6.9**	**6.8**	**7.0**	**7.0**	**4.8**	**4.9**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

PATO LA TAIFA NA MATUMIZI YAKE KWA BEI ZA SOKO (Bei za Mwaka 2015)

Jedwali Na. 4B **Shilingi Milioni**

Aina ya Matumizi	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Pato la Taifa kwa Gharama zake (GDPbp)	**92,803,857**	**99,263,761**	**106,218,115**	**113,893,462**	**120,036,665**	**125,824,575.7**
Kodi za uzalishaji	**8,024,535**	**8,393,644**	**8,923,215**	**9,303,274**	**9,093,517**	**9,693,237.0**
Pato la Taifa kwa Bei za Soko (GDPmp)	**100,828,393**	**107,657,405**	**115,141,329**	**123,196,736**	**129,130,182**	**135,517,813**
MATUMIZI YA PATO LA TAIFA						
Pato la Taifa kwa Bei za Soko (GDPmp)	**100,828,393**	**107,657,405**	**115,141,329**	**123,196,736**	**129,130,182**	**135,517,813**
Matumizi ya Mwisho	**70,594,782**	**73,603,189**	**77,376,434**	**79,848,346**	**83,537,553**	**89,719,802**
Serikali	9,667,251	9,771,806	9,965,992	10,310,060	10,443,010	10,806,031
Binafsi	60,697,766	63,578,381	67,135,273	69,253,213	72,795,644	78,597,469
Taasisi binafsi Zinazotoa huduma za kijamii	229,766	253,003	275,169	285,073	298,899	316,302
Ukuzaji rasilimali	**33,795,169**	**38,338,123**	**44,669,633**	**49,349,298**	**52,074,086**	**55,848,045**
Rasilimali za kudumu	34,878,462	40,376,858	46,705,540	53,777,604	57,519,761	60,434,105
Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani	902,490	858,566	776,123	925,034	1,096,591	1,161,299
Ongezeko la limbikizo	-1,985,783	-2,897,301	-2,812,030	- 5,353,340	- 6,542,266	- 5,747,360
Mauzo nje	**16,137,713**	**15,480,491**	**15,316,635**	**17,905,766**	**15,120,923**	**17,542,456**
Bidhaa-fob	8,060,826	7,805,507	7,608,448	9,797,768	10,233,587	10,956,030
Huduma	8,076,886	7,674,984	7,708,187	8,107,998	4,887,336	6,586,426
Uagizaji	**20,331,252**	**18,879,441**	**22,025,703**	**22,051,517**	**19,922,401**	**24,657,063**
Bidhaa-fob	15,631,116	15,311,240	18,593,941	18,940,515	17,554,127	21,502,293
Huduma	4,700,136	3,568,202	3,431,761	3,111,002	2,368,274	3,154,770
Makosa na Mapungufu	631,981	-884,958	-195,670	-1,855,158	-1,679,979	-2,935,427

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

UKUZAJI RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI (Bei za Miaka inayohusika)

Jedwali Na. 5 **Shilingi Milioni**

Aina	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Majengo	27,721,670	33,872,241	41,694,655	50,181,960	52,999,306	57,576,873
Vifaa vya Usafiri	1,514,772	1,413,888	1,763,519	1,933,144	2,241,661	2,346,122
Mitambo na Vifaa	3,430,297	3,756,643	3,400,915	3,508,102	4,323,003	4,476,996
Mitambo na Vifaa vingine	1,366,982	1,441,018	1,688,577	1,785,118	2,146,400	2,221,094
Rasilimali za Mazao ya Mifugo	425,361	461,511	510,723	566,744	649,195	653,287
Haki ya Umiliki, Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu	1,033,744	1,196,620	1,328,698	1,465,471	1,688,947	1,776,573
Rasilimali za kudumu	35,492,828	42,141,921	50,387,086	59,440,540	64,048,512	69,050,945
Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani	1,105,406	1,006,179	1,215,104	1,273,337	1,838,290	1,954,173
Ongezeko la limbikizo	-1,732,887	-2,720,674	-2,108,634	-4,951,512	-6,234,622	-5,882,772
Jumla ya Ukuzaji Rasilimali	34,865,346	40,427,427	49,493,556	55,762,365	59,652,181	65,122,346

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

UKUZAJI RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI (Bei za Mwaka 2015)

Jedwali Na. 6 **Shilingi Milioni**

Aina	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Majengo	27,512,753	32,836,681	38,590,978	45,205,617	47,526,349	50,304,357
Vifaa vya Usafiri	1,373,682	1,173,050	1,778,192	2,128,145	2,189,915	2,140,871
Mitambo na Vifaa	3,268,709	3,473,892	3,136,401	3,075,952	3,862,605	3,918,313
Mitambo na Vifaa vingine	1,323,953	1,335,724	1,525,517	1,563,289	1,878,735	1,943,925
Rasilimali za Mazao ya Mifugo	385,150	414,428	434,150	472,426	534,673	571,763
Haki ya Umiliki, Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu	1,014,215	1,143,083	1,240,303	1,332,176	1,527,483	1,554,876
Rasilimali za kudumu	34,878,462	40,376,858	46,705,540	53,777,604	57,519,761	60,434,105
Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani	902,490	858,566	776,123	925,034	1,096,591	1,161,299
Ongezeko la limbikizo	-1,985,783	-2,897,301	-2,812,030	-5,353,340	-6,542,266	-5,747,360
Jumla ya Ukuzaji Rasilimali	**33,795,169**	**38,338,123**	**44,669,633**	**49,349,298**	**52,074,086**	**55,848,045**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

MCHANGO KATIKA RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI (Bei za miaka inayohusika)

Jedwali Na. 7A **Asilimia**

Aina	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Majengo	79.5	83.8	84.2	90.0	88.8	88.4
Vifaa vya Usafiri	4.3	3.5	3.6	3.5	3.8	3.6
Mitambo na Vifaa	9.8	9.3	6.9	6.3	7.2	6.9
Mitambo na Vifaa vingine	3.9	3.6	3.4	3.2	3.6	3.4
Rasilimali za Mazao ya Mifugo	1.2	1.1	1.0	1.0	1.1	1.0
Haki ya Umiliki, Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu	3.0	3.0	2.7	2.6	2.8	2.7
Rasilimali za kudumu	101.8	104.2	101.8	106.6	107.4	106.0
Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani	3.2	2.5	2.5	2.3	3.1	3.0
Ongezeko la limbikizo	-5.0	-6.7	-4.3	-8.9	-10.5	-9.0
Jumla ya Ukuzaji Rasilimali	**100.0**	**100.0**	**100.0**	**100.0**	**100.0**	**100.0**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

UKUZAJI WA RASILIMALI KATIKA SEHEMU ZA UCHUMI WA KITAIFA NA BINAFSI
(Bei za Miaka Inayohusika)

Jedwali Na. 7B **Shilingi Milioni**

Sekta	2016	2017	2018	2019	2020	2021
A. Rasilimali za kudumu	35,492,828	42,141,921	50,387,086	59,440,540	64,048,512	69,050,945
1. Serikali:	8,944,186	10,914,757	13,124,780	14,979,006	16,588,565	17,400,826
2. Mashirika:	745,349	1,011,406	1,106,303	1,248,250	1,537,164	1,690,069
3. Taasisi:	851,827	1,095,690	1,056,017	1,426,572	1,665,261	1,797,221
4. Sekta binafsi	24,951,465	29,120,067	35,099,986	41,786,712	44,257,522	48,162,829
C: Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani	1,105,406	1,006,179	1,215,104	1,273,337	1,838,290	1,954,173
D. Ongezeko la Limbikizo	-1,732,887	-2,720,674	-2,108,634	-4,951,512	-6,234,622	-5,882,772
E. Jumla la Ukuzaji Rasilimali	34,865,346	40,427,427	49,493,556	55,762,365	59,652,181	65,122,346

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

FAHIRISI ZA BEI ZA REJAREJA YA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR-ES-SALAAM (2020=100)

Jedwali Na. 8

MWAKA	BIDHAA ZOTE		CHAKULA	
	FAHIRISI	BADILIKO ASILIMIA	FAHIRISI	BADILIKO ASILIMIA
2004	26.88	6.4	24.29	6.8
2005	29.10	8.3	26.07	7.3
2006	32.47	11.5	28.75	10.3
2007	35.49	9.3	31.43	9.3
2008	41.64	17.3	36.21	15.2
2009	48.64	16.8	43.25	19.4
2010	55.07	13.2	51.02	18.0
2011	59.15	7.4	54.63	7.1
2012	70.25	18.8	67.31	23.2
2013	76.82	9.3	74.36	10.5
2014	82.71	7.7	79.76	7.3
2015	87.17	5.4	84.47	5.9
2016	90.94	4.3	87.52	3.6
2017	92.63	1.9	90.53	3.4
2018	94.44	2.0	94.59	4.5
2019	97.99	3.8	98.93	4.6
2020**	100.00	2.1	100.00	1.1
2021	102.37	2.4	100.58	0.6

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Jan-Dec. 2020 = 100
*Mchanganuo wa Bidhaa na Huduma umebadilishwa kutoka COICOP 1999 hadi COICOP 2018

FAHIRISI ZA BEI ZA REJAREJA ZA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CA CHINI DAR ES SALAAM (JAN - DEC 2020 = 100)

Jedwali Na. 9

Mwaka	Vyakula na Vinywaji Baridi	Vinywaji Vikali na Tumbaku	Mavazi na Viatu	Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo	Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi	Afya	Usafiri	Habari na Mawasiliano	Burudani, Michezo na Utamaduni	Huduma za Elimu	Migahawa na Huduma za Malazi	Huduma za Bima na Fedha	Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko	FAHIRISI BIDHAA ZOTE
2016	87.5	96.4	91.0	81.2	92.8	94.6	109.2	98.5	95.2	91.5	96.6	91.8	95.5	90.9
2017	90.5	99.2	92.1	81.9	95.7	96.0	109.1	98.9	96.8	95.0	97.1	94.1	96.1	92.6
2018	94.6	99.2	95.0	86.6	97.5	96.1	95.5	98.8	97.8	100.2	97.2	96.2	97.5	94.4
2019	98.9	100.0	98.8	91.4	99.4	99.1	100.2	99.8	100.1	100.1	99.4	100.0	99.7	98.0
2020	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0
2021	100.6	107.3	103.1	102.9	103.9	101.9	92.6	101.4	103.8	110.3	105.5	100.0	100.7	102.4

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Jan-Dec. 2020 = 100

**Mchanganuo wa Bidhaa na Huduma umebadilishwa kutoka COICOP 1999 hadi COICOP 2018

FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI - DAR-ES-SALAAM (2020 =100)

Jedwali Na. 10

Mwaka	MIEZI					Badiliko Asilimia
	Robo ya Kwanza	Robo ya Pili	Robo ya Tatu	Robo ya Nne	Wastani	
2005	29.79	30.20	31.37	31.83	30.80	7.9
2006	32.74	33.65	33.74	34.34	33.62	9.2
2007	35.66	37.01	37.90	39.32	37.47	11.5
2008	41.44	42.66	43.73	45.01	43.21	15.3
2009	47.58	48.95	51.51	53.23	50.32	16.4
2010	54.58	55.17	55.61	56.03	55.35	10.0
2011	58.04	59.17	60.03	61.56	59.70	7.9
2012	66.98	69.69	70.64	71.21	69.63	16.6
2013	74.81	75.68	75.59	75.55	75.41	8.3
2014	79.30	80.45	80.71	79.89	80.09	6.2
2015	82.48	84.54	85.94	85.45	84.60	5.6
2016	87.19	89.15	88.69	88.67	88.43	4.5
2017	89.26	91.18	91.12	91.43	90.75	2.6
2018	90.35	92.69	92.89	93.83	92.44	1.9
2019	95.62	96.95	96.51	97.36	96.61	4.5
2020*	99.87	99.99	100.26	99.89	100.00	3.5
2021	101.71	102.57	101.87	103.45	102.40	2.4

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Jan - Dec. 2020 = 100

*Mchanganuo wa Bidhaa na Huduma umebadilishwa kutoka COICOP 1999 hadi COICOP 2018

FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI DAR ES SALAAM (Jan - Dec. 2020 =100)

Jedwali Na. 11

	Vyakula na Vinywaji Baridi	Vinywaji Vikali na Tumbaku	Mavazi na Viatu	Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo	Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi	Afya	Usafiri	Habari na Mawasiliano	Burudani, Michezo na Utamaduni	Huduma za Elimu	Migahawa na Huduma za Malazi	Huduma za Bima na Fedha	Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko	FAHIRISI BIDHAA ZOTE
2016 Robo ya kwanza	79.89	97.38	91.86	79.69	92.13	88.27	116.19	96.93	97.00	92.49	92.22	100.00	93.42	87.19
Robo ya pili	81.89	96.70	92.62	81.88	93.27	92.20	116.60	97.56	97.62	92.08	97.01	100.00	94.25	89.15
Robo ya tatu	81.54	97.71	91.84	78.94	92.45	94.48	117.52	98.11	97.69	92.08	97.91	100.00	94.21	88.69
Robo ya nne	80.46	98.93	92.23	81.13	94.47	95.22	116.78	98.23	98.55	92.08	96.91	100.00	95.57	88.67
2017 Robo ya kwanza	82.97	99.44	92.86	77.42	96.21	94.94	118.25	98.24	97.80	92.08	97.16	100.00	95.04	89.26
Robo ya pili	86.50	99.96	93.37	80.04	95.94	94.54	119.22	98.24	98.31	92.08	96.99	100.00	95.49	91.18
Robo ya tatu	84.65	100.20	93.69	84.71	96.03	94.62	116.14	98.23	98.04	92.08	97.32	100.00	95.94	91.12
Robo ya nne	84.56	100.19	93.80	86.42	96.25	94.94	116.83	98.17	98.52	92.08	97.32	100.00	95.30	91.43
2018 Robo ya kwanza	87.41	99.43	93.46	82.62	96.44	94.88	94.15	98.17	97.69	100.03	96.12	100.00	95.48	90.35
Robo ya pili	92.18	99.43	94.58	84.42	97.15	95.01	94.50	98.07	98.37	100.03	96.12	100.00	96.96	92.69
Robo ya tatu	91.69	99.43	96.00	85.55	97.52	95.08	94.95	98.02	98.17	100.03	96.66	100.00	97.39	92.89
Robo ya nne	91.00	99.57	97.63	89.50	98.39	95.20	98.33	98.07	98.72	100.03	97.90	100.00	98.28	93.83
2019 Robo ya kwanza	93.66	99.85	98.02	90.52	99.33	98.34	100.45	99.40	99.92	100.03	99.34	100.00	99.95	95.62
Robo ya pili	96.72	99.85	98.57	90.39	99.55	99.59	101.06	99.87	100.12	100.03	99.47	100.00	100.03	96.95
Robo ya tatu	95.12	99.85	99.20	91.58	99.39	99.60	101.06	99.15	101.01	100.03	99.45	100.00	99.44	96.51
Robo ya nne	97.19	99.85	99.17	92.21	99.71	99.69	100.61	99.30	99.70	100.03	99.04	100.00	99.67	97.36
**2020 Robo ya kwanza	101.46	99.85	99.85	96.53	99.93	99.71	100.93	99.54	99.97	100.00	99.05	100.00	99.25	99.87
Robo ya pili	99.72	99.85	99.96	101.49	99.99	100.04	99.31	100.15	99.99	100.00	99.05	100.00	99.88	99.99
Robo ya tatu	99.38	99.85	99.95	102.39	100.04	100.12	99.53	100.15	100.02	100.00	100.95	100.00	100.30	100.26
Robo ya nne	99.44	100.44	100.24	99.59	100.03	100.12	100.23	100.15	100.02	100.00	100.95	100.00	100.57	99.89
2021 Robo ya kwanza	100.68	104.06	100.68	99.92	102.79	103.70	100.91	101.36	100.06	104.76	107.20	100.00	100.21	101.71
Robo ya pili	102.03	104.31	99.99	97.98	104.06	103.97	102.50	101.24	100.64	105.60	110.88	100.57	100.75	102.57
Robo ya tatu	99.63	103.90	100.16	97.71	104.07	103.97	103.47	101.25	100.57	105.53	110.88	100.57	100.69	101.87
Robo ya nne	102.36	104.56	101.79	99.97	105.36	104.32	103.99	101.54	100.55	105.54	111.53	100.57	100.99	103.45

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Dec. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2004 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi haziwezi kuungwa na fahirisi zilizonzia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (Jan - Dec. 2020 =100)

Jedwali Na. 12

	Vyakula na Vinywaji Baridi	Vinywaji Vikali na Tumbaku	Mavazi na Viatu	Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo	Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi	Afya	Usafiri	Habari na Mawasiliano	Burudani, Michezo na Utamaduni	Huduma za Elimu	Migahawa na Huduma za Malazi	Huduma za Bima na Fedha	Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko	FAHIRISI BIDHAA ZOTE
2017 Robo ya kwanza	78.2	98.9	93.4	80.7	96.5	95.7	90.9	97.5	98.7	91.5	94.4	100.0	98.5	88.0
Robo ya pili	82.1	99.6	94.0	80.9	96.8	95.3	92.3	97.5	99.2	91.5	94.9	100.0	98.6	89.5
Robo ya tatu	85.1	100.0	94.1	82.4	96.5	94.9	93.7	97.5	98.0	91.5	95.2	100.0	99.4	90.8
Robo ya nne	87.3	100.0	94.4	84.1	96.4	95.6	95.5	97.7	98.4	91.5	94.8	100.0	100.4	92.2
2018 Robo ya kwanza	87.9	100.0	94.8	84.5	96.7	95.5	96.4	97.9	98.9	94.3	94.8	100.0	98.3	92.6
Robo ya pili	88.9	100.0	95.8	86.4	97.6	95.5	98.7	98.0	99.5	100.0	95.0	100.0	99.7	94.1
Robo ya tatu	89.8	99.6	97.0	87.1	97.9	95.5	99.8	98.0	99.8	100.0	95.6	100.0	100.6	94.9
Robo ya nne	89.5	99.7	97.6	88.7	98.2	95.4	101.4	98.0	99.3	100.0	97.7	100.0	100.8	95.6
2019 Robo ya kwanza	90.9	99.8	97.9	89.1	99.3	98.4	101.5	99.4	99.8	100.0	99.6	100.0	100.8	96.4
Robo ya pili	93.6	99.8	98.5	94.5	99.6	99.8	102.3	99.9	100.4	100.0	99.7	100.0	100.8	98.1
Robo ya tatu	92.9	99.8	99.0	95.3	99.5	99.7	102.0	99.1	101.0	100.0	98.9	100.0	100.4	97.9
Robo ya nne	94.3	99.8	99.2	95.9	99.7	99.7	101.6	99.3	99.2	100.0	99.3	100.0	99.0	98.2
**2020 Robo ya kwanza	99.6	99.8	99.9	97.9	99.9	99.7	101.8	99.5	100.0	100.0	99.4	100.0	98.7	100.0
Robo ya pili	99.1	99.8	100.0	100.8	100.0	100.1	99.4	100.2	100.0	100.0	99.4	100.0	100.2	99.7
Robo ya tatu	100.0	99.8	100.0	101.4	100.1	100.1	99.4	100.2	100.0	100.0	100.6	100.0	100.5	100.1
Robo ya nne	101.3	100.7	100.2	99.8	100.1	100.1	99.5	100.2	100.0	100.0	100.6	100.0	100.6	100.3
2021 Robo ya kwanza	102.8	104.6	102.6	100.3	107.1	102.9	100.6	101.3	98.6	102.4	105.4	100.0	100.7	102.2
Robo ya pili	104.7	113.5	103.1	99.7	108.1	103.3	101.7	101.0	98.6	103.6	107.4	100.2	101.6	103.1
Robo ya tatu	102.7	113.2	103.1	99.6	108.1	103.3	102.3	101.0	98.6	103.0	107.3	100.2	101.5	102.8
Robo ya nne	105.5	113.7	104.8	101.0	109.3	103.7	102.7	102.0	99.0	103.0	108.1	100.2	102.1	104.0

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Dec. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2004 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi haziwezi kuungwa na fahirisi zilizonzia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WENYE KIPATO CHA JUU DAR-ES-SALAAM (2020=100)

Jedwali Na. 13

Mwaka	MIEZI				Wastani	Badiliko Asilimia
	Robo ya Kwanza	Robo ya Pili	Robo ya Tatu	Robo ya Nne		
2004	26.21	26.88	27.33	27.93	27.09	6.2
2005	28.44	28.66	29.40	31.13	29.41	8.6
2006	32.05	32.58	32.91	33.95	32.87	11.8
2007	35.69	36.76	37.80	38.71	37.24	13.3
2008	41.34	42.41	45.61	46.87	44.06	18.3
2009	48.83	49.40	52.13	53.48	50.96	15.7
2010	53.65	54.89	55.68	56.08	55.08	8.1
2011	58.14	59.87	61.61	64.01	60.91	10.6
2012	66.02	67.25	68.02	69.54	67.71	11.2
2013	72.31	72.40	73.30	74.39	73.10	8.0
2014	76.65	76.71	77.69	78.90	77.49	6.0
2015	80.48	81.87	83.13	84.59	82.52	6.5
2016	85.46	86.73	86.65	86.98	86.45	4.8
2017	87.99	89.47	90.83	92.16	90.11	4.2
2018	92.65	94.11	94.87	95.59	94.31	4.7
2019	96.37	98.13	97.92	98.21	97.66	3.6
2020*	99.96	99.70	100.08	100.26	100.00	2.4
2021	102.17	103.08	102.81	104.03	103.02	3.0

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Jan-Dec. 2020 = 100

*Mchanganuo wa Bidhaa na Huduma umebadilishwa kutoka COICOP 1999 hadi COICOP 2018

FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA KWA ROBO MWAKA 2017 - 2021 - TANZANIA BARA (2020 =100)

Jedwali Na. 14

Mwaka	Robo za Mwaka	Vyakula na Vinywaji Baridi	Vinywaji Vikali na Tumbaku	Mavazi na Viatu	Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo	Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi	Afya	Usafiri	Habari na Mawasiliano	Burudani, Michezo na Utamaduni	Huduma za Elimu	Migahawa na Huduma za Malazi	Huduma za Bima na Fedha	Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko	Fahirisi Bidhaa Zote
2017	Robo ya kwanza	89.1	95.2	91.2	75.0	91.8	95.6	93.4	101.0	98.8	94.4	93.3	96.4	93.6	89.3
	Robo ya pili	92.6	96.1	92.4	75.7	92.3	96.1	93.4	100.5	99.7	94.6	93.4	95.9	95.6	91.0
	Robo ya tatu	90.6	96.5	92.9	77.8	92.3	96.4	92.9	100.6	99.7	94.9	93.4	95.9	95.7	90.6
	Robo ya nne	90.4	97.0	93.0	79.2	92.6	96.9	93.4	100.8	99.4	94.9	93.4	95.9	95.5	90.8
2018	Robo ya kwanza	94.0	97.4	94.0	81.5	93.4	97.2	94.4	100.9	99.1	96.7	94.1	96.5	95.7	92.9
	Robo ya pili	95.6	97.1	94.6	85.8	94.4	97.4	95.1	100.2	98.2	96.9	94.2	97.0	96.7	94.3
	Robo ya tatu	92.7	97.8	95.5	87.6	95.0	97.6	95.5	98.5	98.1	97.2	94.5	97.0	96.9	93.6
	Robo ya nne	91.1	98.8	96.2	89.6	95.6	97.8	97.5	98.5	98.4	97.2	95.4	98.6	97.3	93.6
2019	Robo ya kwanza	94.4	100.0	97.3	91.6	97.3	98.5	98.0	99.3	98.9	98.6	97.5	100.0	98.3	95.7
	Robo ya pili	97.3	100.6	97.8	94.2	98.3	99.4	99.0	100.0	101.6	98.8	98.7	100.0	99.1	97.6
	Robo ya tatu	96.0	100.1	98.1	93.1	98.6	99.4	98.7	99.5	99.8	98.8	98.8	100.0	99.3	96.9
	Robo ya nne	96.4	99.9	98.4	93.1	98.9	99.4	98.7	99.5	99.4	98.8	99.0	100.0	99.3	97.1
2020	Robo ya kwanza	98.8	99.5	99.5	98.1	99.4	99.4	101.1	99.1	100.5	99.9	99.5	100.0	99.6	99.2
	Robo ya pili	101.2	99.9	100.1	100.6	100.0	99.9	101.3	100.0	100.6	100.0	99.7	100.0	100.2	100.7
	Robo ya tatu	100.1	100.3	100.1	100.6	100.3	100.3	98.7	100.2	100.1	100.0	100.4	100.0	100.2	100.0
	Robo ya nne	99.9	100.3	100.3	100.8	100.3	100.4	98.9	100.7	98.8	100.1	100.5	100.0	99.9	100.1
2021	Robo ya kwanza	102.3	101.4	103.7	103.1	102.6	102.0	101.9	101.2	102.5	100.9	103.5	100.2	102.3	102.5
	Robo ya pili	106.0	102.3	104.5	104.2	103.0	102.5	103.1	101.8	102.9	101.2	105.1	100.3	102.6	104.2
	Robo ya tatu	104.3	102.5	104.8	104.5	103.3	103.1	103.9	102.0	103.0	101.2	105.3	100.3	103.0	103.9
	Robo ya nne	104.3	102.8	105.3	104.7	103.9	103.3	104.5	102.3	102.6	101.2	105.6	100.3	103.3	104.2

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Angalizo Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika 2020 = 100
Mchanganuo wa Bidhaa na Huduma umebadilishwa kutoka COICOP 1999 hadi COICOP 2018

FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA (2020=100)

Jedwali Na. 15

Mwaka	Robo ya Mwaka				Wastani wa Fahirisi	Badiliko Asilimia
	Robo ya Kwanza	Robo ya Pili	Robo ya Tatu	Robo ya Nne		
2004	32.5	32.5	32.6	33.7	32.8	4.7
2005	33.9	34.3	34.4	35.4	34.5	5.0
2006	36.5	37.5	36.5	37.6	37.0	7.3
2007	39.1	39.6	39.5	40.2	39.6	7.0
2008	42.6	43.3	43.6	45.2	43.7	10.3
2009	48.1	48.2	48.7	50.9	49.0	12.1
2010	51.2	51.8	51.6	52.0	51.7	5.5
2011	54.9	56.8	59.2	61.9	58.2	12.7
2012	65.52	67.14	67.90	69.53	67.52	16.0
2013	72.30	72.81	72.50	73.73	72.84	7.9
2014	76.67	77.47	77.30	77.78	77.30	6.1
2015	79.84	81.58	82.17	82.91	81.62	5.6
2016	84.52	85.87	86.12	86.87	85.85	5.2
2017	89.32	91.01	90.56	90.77	90.41	5.3
2018	92.88	94.30	93.56	93.61	93.59	3.5
2019	95.69	97.59	96.88	97.10	96.81	3.4
2020*	99.16	100.72	100.04	100.08	100.00	3.3
2021	102.46	104.16	103.94	104.20	103.69	3.7

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Jan-Dec. 2020 = 100

*Mchanganuo wa Bidhaa na Huduma umebadilishwa kutoka COICOP 1999 hadi COICOP 2018

FAHIRISI ZA BEI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI-TANZANIA BARA (2020=100)

Jedwali Na. 16

Mwaka	FAHIRISI			WAKAZI MIJINI TANZ. BARA	BADILIKO %			WAKAZI MIJINI TANZ. BARA
	KIPATO CHA				KIPATO CHA			
	CHINI	KATI	JUU		CHINI	KATI	JUU	
2004	26.88	28.53	27.09	32.85	6.4	8.2	6.2	4.7
2005	29.10	30.80	29.41	34.50	8.3	7.9	8.6	5.0
2006	32.47	33.62	32.87	37.00	11.5	9.2	11.8	7.3
2007	35.49	37.47	37.24	39.60	9.3	11.5	13.3	7.0
2008	41.64	43.21	44.06	43.67	17.3	15.3	18.3	10.3
2009	48.64	50.32	50.96	48.97	16.8	16.4	15.7	12.1
2010*	55.07	55.35	55.08	51.65	13.2	10.0	8.1	5.5
2011	59.15	59.70	60.91	58.21	7.4	7.9	10.6	12.7
2012	70.25	69.63	67.71	67.52	18.8	16.6	11.2	16.0
2013	76.82	75.41	73.10	72.84	9.3	8.3	8.0	7.9
2014	82.71	80.09	77.49	77.30	7.7	6.2	6.0	6.1
2015	87.17	84.60	82.52	81.62	5.4	5.6	6.5	5.6
2016	90.94	88.43	86.45	85.85	4.3	4.5	4.8	5.2
2017	92.63	90.75	90.11	90.41	1.9	2.6	4.2	5.3
2018	94.44	92.44	94.31	93.59	2.0	1.9	4.7	3.5
2019	97.99	96.61	97.66	96.81	3.8	4.5	3.6	3.4
2020*	100.00	100.00	100.00	100.00	2.1	3.5	2.4	3.3
2021	102.37	102.40	103.02	103.69	2.4	2.4	3.0	3.7

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Jan-Dec. 2020 = 100

*Mchanganuo wa Bidhaa na Huduma umebadilishwa kutoka COICOP 1999 hadi COICOP 2018

SURA YA 2

FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA

Ujazi wa Fedha

31. Mwaka 2021, ujazi wa fedha uliendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha sambamba na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kuendelea kupambana na athari za janga la UVIKO - 19. Hatua hizi za kisera zililenga kukuza uchumi na kuimarisha sekta ya fedha na utendaji wa masoko ya fedha. Utekelezaji huu wa sera ya fedha ulichagizwa na uwepo wa mfumuko mdogo wa bei ulioendelea kubaki ndani ya wigo wa kati ya asilimia 3 - 5. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania ilitumia nyenzo mbalimbali za kisera ili kuongeza kiwango cha ukwasi katika sekta ya benki ikiwemo utoaji wa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara, ununuzi wa fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni na uingiaji wa mikataba ya kubadilishana fedha za kigeni na mabenki.

32. Kutokana na utekelezaji huu wa sera wezeshi ya fedha, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kwa asilimia 15.5 na kufikia shilingi bilioni 34,558.0 mwaka 2021 kutoka shilingi bilioni 29,920.6 mwaka 2020. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 17.6 kutoka kiasi cha shilingi bilioni 23,032.6 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 27,088.4 mwaka 2021. Aidha, ujazi wa fedha kwa tasfiri finyu (M1) nao pia uliongezeka kwa asilimia 23.1 na kufikia shilingi bilioni 17,625.5 mwaka 2021 kutoka shilingi bilioni 14,321.7 mwaka 2020. Hali hii inaashiria kuongezeka kwa mzunguko wa fedha katika uchumi kufuatia juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kulipa madeni na madai yaliyohakikiwa na kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, mzunguko wa fedha katika uchumi uliongezeka kwa asilimia 11.4 na kufikia shilingi bilioni 5,012.0 mwaka 2021.

Kielelezo Na. 2.1: Ukuaji wa Ugavi wa Fedha



	Dec-18	Mar-19	Jun-19	Sep-19	Dec-19	Mac-20	Jun-20	Sep-20	Dec-20	Mac-21	Jun-21	Sep-21	Dec-21
M3	4.5	5.0	7.7	9.4	9.6	9.9	9.5	6.5	5.7	6.8	11.7	12.7	15.5
M2	3.8	4.4	10.8	9.8	11.8	10.8	10.5	9.1	8.2	9.3	10.5	15.0	17.6

Mikopo kwa Sekta Binafsi

33. Mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kuimarika na kuongezeka kutoka shilingi bilioni 20,308.3 mwaka 2020 hadi kufikia shilingi bilioni 22,344.1 mwaka 2021 sawa na ukuaji wa asilimia 10.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.1 mwaka 2020. Ongezeko la kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi lilichangiwa zaidi na utekelezaji endelevu wa sera wezeshi ya fedha pamoja na jitihada za Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara sambamba na kuendelea kuimarika kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi zilizokuwa zimeathiriwa zaidi na janga la UVIKO-19. Aidha, sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kuelekezwa kwenye shughuli binafsi kwa asilimia 36.0, ikifuatiwa na shughuli za biashara na viwanda kwa asilimia 16.4 na asilimia 9.4 mtawalia.

34. Mwaka 2021, Benki Kuu ya Tanzania ilichukua hatua za ziada za kisera ili kuongeza chachu ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kupunguza viwango vya riba za mikopo. Hatua hizo ni pamoja na: kuanzishwa kwa mfuko maalum wenye thamani ya shilingi trilioni moja ambao unatumika kukopesha mabenki na taasisi nyingine za fedha kwa riba ya asilimia 3 ili kutoa mikopo ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10; kupunguza kiwango cha sehemu ya amana za mabenki kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na mabenki yatakayotoa mikopo kwa sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10 kwa mwaka; kuondoa sharti la uzoefu wa kufanya biashara kwa angalau miezi 18 kwa waombaji wa biashara ya wakala wa benki, badala yake, waombaji watatakiwa kuwa na kitambulisho cha Taifa au namba ya kitambulisho cha Taifa; kuweka ukomo wa kiwango cha riba kinachotolewa na benki za biashara kwenye akaunti za makampuni ya simu yanayotoa huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi; na kupunguza kiwango cha mtaji kinachotakiwa kuwekwa na benki za biashara kwa ajili ya kutoa mikopo.

Jedwali Na. 2.1: Mikopo iliyotolewa na benki za biashara kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi

									Ukuaji (%)		Mchango (%)	
	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021	2020	2021	2020	2021
Uzalishaji katika Kilimo	1,057.3	1,174.2	1,107.6	1,134.8	952.9	1,824.3	1,725.6	1,592.5	-5.4	-7.7	8.5	7.1
Madini na Uchimbaji Mawe	166.3	275.2	328.6	292.6	375.2	424.5	429.4	474.0	1.1	10.4	2.1	2.1
Viwanda	1,386.2	1,695.8	1,627.8	1,777.6	2,087.9	2,086.8	1,878.4	2,111.1	-10.0	12.4	9.2	9.4
Majengo na Ujenzi	660.1	741.4	740.7	837.2	643.3	1,129.9	1,072.3	998.4	-5.1	-6.9	5.3	4.5
Uchukuzi na Mawasiliano	925.7	1,231.8	1,180.9	975.6	918.0	1,059.6	1,142.4	1,053.9	7.8	-7.8	5.6	4.7
Biashara	2,652.1	3,077.7	3,349.3	3,306.9	3,228.9	3,379.5	3,054.9	3,657.3	-9.6	19.7	15.0	16.4
Mahoteli na Migahawa	436.1	514.6	526.4	595.0	587.3	555.0	549.5	542.7	-1.0	-1.2	2.7	2.4
Umeme	440.9	439.8	429.9	335.2	358.1	225.3	114.7	143.9	-49.1	25.4	0.6	0.6
Watu Binafsi	2,104.5	2,731.7	2,981.7	3,258.7	5,019.5	5,485.5	6,793.9	8,047.7	23.9	18.5	33.5	36.0
Sekta Nyinginezo	2,583.0	3,610.4	4,335.8	4,381.9	3,555.7	3,525.0	3,547.2	3,722.5	0.6	4.9	17.5	16.7
Jumla	12,412.3	15,492.7	16,608.9	16,895.4	17,726.8	19,695.4	20,308.3	22,344.1	3.1	10.0	100.0	100.0

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo Na. 2.2: Mchango wa Mikopo iliyotolewa na Benki za biashara kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi



Amana katika Benki za Biashara

35. Mwaka 2021, amana za benki za biashara ziliendelea kuongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 26,813.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 23,813.2 mwaka 2020, sawa na ukuaji wa asilimia 13.0. Kati ya hizo amana za sekta binafsi zilifikia shilingi bilioni 26,390.7, sawa na asilimia 98.4 ya amana zote. Ongezeko la amana lilitokana na jitihada za benki za biashara kutoa vivutio mbalimbali na kuhimiza wananchi kuweka akiba ya fedha benki ikiwa ni pamoja na kuongeza utoaji wa huduma bora za fedha nchini, ongezeko la matawi ya benki za biashara na matumizi ya wakala wa benki na huduma za kidigitali katika kutoa huduma za fedha. Amana za sekta binafsi zilifikia shilingi bilioni 26,390.7, sawa na asilimia 98.4 ya amana zote. Aidha, uwiano wa amana za fedha za kigeni kwa jumla ya amana ulikuwa asilimia 26.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 27.1 mwaka 2020.

Mwenendo wa Viwango vya Riba

36. Mwaka 2021, wastani wa viwango vya riba uliendelea kupungua katika masoko ya fedha kutokana na utekelezaji wa sera wezeshi ya fedha. Katika kipindi hicho, wastani wa riba ya jumla katika soko la fedha baina ya mabenki ulipungua hadi asilimia 4.44 kutoka asilimia 4.50 mwaka 2020. Aidha, riba ya jumla ya dhamana za Serikali za muda mfupi zimeendelea kubakia katika wastani wa asilimia 4. Kwa upande mwingine, viwango vya riba za mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi vimeendelea kupungua japo kwa kasi ndogo ambapo mwaka 2021 viwango vya riba za mikopo kiujumla vilipungua hadi wastani wa asilimia 16.59 kutoka asilimia 16.66 mwaka 2020. Aidha, viwango vya riba za mikopo ya mwaka mmoja vilikua hadi wastani wa asilimia 16.43 mwaka 2021 kutoka asilimia 15.73 mwaka 2020. Utekelezaji wa sera wezeshi ya fedha pamoja na hatua za

ziada za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania zinatarajiwa kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya kupunguza gharama ya mikopo nchini, na hivyo kuchangia kupungua kwa viwango vya riba za mikopo na kuongeza ukuaji wa mikopo ya sekta binafsi. Aidha, wastani wa viwango vya riba za amana za muda maalum na za mwaka mmoja uliongezeka hadi asilimia 6.85 na asilimia 8.32 mwaka 2021 kutoka asilimia 6.70 na asilimia 8.28 mwaka 2020 mtawalia.

MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA

Huduma za Benki

37. Mwaka 2021, utoaji wa huduma za benki uliongezeka kama inavyojidhihirisha kutokana na ongezeko la matawi na ukuaji wa amana na mikopo. Hadi kufikia Desemba 2021 kulikuwa na jumla ya benki 46 sawa na idadi ya benki zilizokuwepo hadi mwishoni mwa mwaka 2020 kutokana na kutokuwa na benki mpya iliyoanzishwa ndani ya mwaka huo. Hata hivyo, matawi ya benki yaliongezeka hadi kufikia 990 ikilinganishwa na matawi 969 yaliyokuwepo mwaka 2020. Kwa upande mwingine, amana za wateja na mikopo kwa wateja iliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 22,112.15 na shilingi bilioni 28,502.22 mwaka 2021 kutoka shilingi bilioni 18,765.13 na shilingi bilioni 24,765.94 mwaka 2020 mtawalia, sawa na ongezeko la asilimia 15.09 kwa amana za wateja na asilimia 17.84 kwa mikopo iliyotolewa kwa wateja.

Huduma za Mawakala wa Benki

38. Katika kuhakikisha huduma za fedha zinawafikia watu wengi zaidi, benki zimeongeza idadi ya mawakala ambao hutoa huduma za kibenki jirani na maeneo wanayoishi wateja. Hadi kufikia Desemba 2021, jumla ya benki 26 zilikuwa zinatoa huduma za kibenki kwa njia ya uwakala ikilinganishwa na benki 23 zilizokuwa zikifanya hivyo mwaka 2020. Ongezeko la benki zinazotoa huduma kupitia mawakala limechangiwa na benki kuendelea kutambua faida zitokanazo na utoaji huduma kwa njia ya uwakala ikiwemo kuwafikia wateja wengi zaidi, kuongeza ukuaji wa amana za benki na kupunguza gharama za riba kutokana na ongezeko la amana zenye gharama nafuu. Aidha, mwaka 2021 idadi ya mawakala wa benki iliongezeka kufikia 48,923 kutoka mawakala 40,410 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 21.07. Ongezeko hilo lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na hatua ya Benki Kuu ya Tanzania kulegeza masharti ya usajili wa mawakala wa benki.

39. Mwaka 2021, idadi ya miamala ya kuweka amana kupitia mawakala ilikuwa 17,253,498 yenye thamani ya shilingi bilioni 13,601.55 ikilinganishwa na miamala 9,860,061 yenye thamani ya shilingi bilioni 6,763.9 mwaka 2020, sawa na ongezeko la miamala kwa asilimia 74.98. Aidha, idadi ya miamala ya kutoa fedha ilikuwa 10,593,253 yenye thamani ya shilingi bilioni 4,480.81 mwaka 2021 ikilinganishwa na miamala 6,704,709 yenye thamani ya shilingi bilioni 2,548.28 mwaka 2020, sawa na ongezeko la miamala kwa asilimia 56.0. Ongezeko hilo lilichangiwa na ongezeko la idadi ya mawakala pamoja na uelewa wa wateja kuhusu huduma zinazotolewa na mawakala wa benki.

Mwenendo wa Viashiria vya Sekta ya Benki

40. Mwaka 2021, hali ya kifedha ya sekta ndogo ya benki ilikuwa ya kuridhisha kwa kuangalia vigezo vya mtaji, mapato, ubora wa mali na ukwasi. Katika kipindi hicho, uwiano wa mtaji halisi na mtaji mkuu na mali hatarishi ulikuwa asilimia 19.49 na asilimia 20.17 mtawalia ikilinganishwa na asilimia 19.07 na asilimia 19.87 mtawalia katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ongezeko la uwiano wa mtaji lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la faida katika sekta ndogo ya benki ambapo faida baada ya kodi (kabla ya ukaguzi wa fedha) iliongezeka kwa asilimia 77.9 na kufikia shilingi bilioni 678.1 mwaka 2021 kutoka shilingi billion 381.1 mwaka 2020. Aidha, uwiano wa ukwasi katika benki ulipungua mpaka kufikia asilimia 29.38 ikilinganishwa na asilimia 30.72 mwaka 2020

41. Kwa upande mwingine, ubora wa mali uliongezeka kwa kuangalia kiwango cha mikopo chechefu ambacho kilipungua hadi asilimia 8.5 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 9.8 mwaka 2020. Kupungua kwa mikopo chechefu kulitokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali kwa kuongeza ukwasi katika uchumi uliowezesha wateja kulipa mikopo kwa wakati na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Benki Kuu ikiwemo: kuongeza ufuatiliaji wa utoaji mikopo; kuwaondoa katika sekta ya benki wafanyakazi wa benki wasio waaminifu; kuamuru benki kutumia taarifa za mikopo kutoka kwenye makampuni ya kuchakata na kutunza kumbukumbu za mikopo; utekelezaji wa kanuni za kuwalinda walaji wa huduma za kibenki kwa kuhakikisha utunzaji wa haki na usawa wa walaji pamoja na wakopaji; kuhakikisha kunakuwa na uwazi wa habari pamoja na kutoa elimu ya fedha na ufahamu kwa walaji; kuziamuru benki ziwe na mifumo ya udhibiti na utawala bora kwa kupitia upya mifumo iliyopo ili kukidhi mabadiliko na maendeleo katika sekta ya benki; na kuzitaka benki na taasisi za fedha kuimarisha taratibu zao za utoaji wa mikopo na ufuatiliaji.

Maboresho katika Sekta ya Benki

42. Mwaka 2021, Benki Kuu iliendelea kutoa kanuni na miongozo mbalimbali katika kusimamia benki na taasisi za fedha ili kuhakikisha sekta ya benki inabaki thabiti, imara na himilivu. Kwa msingi huo, Benki Kuu ilitoa kanuni, miongozo na nyaraka mbalimbali zifuatazo: kanuni za utawala bora ili kuweka viwango vya utawala bora kwa benki na taasisi za fedha; kanuni za taasisi za fedha za maendeleo zenye lengo la kutoa mwongozo katika shughuli mbalimbali za taasisi hizo; mwongozo wa kupata watoa huduma kutoka nje, benki na taasisi za fedha; muongozo wa namna kazi zitaendelea iwapo janga lolote litatokea kwa benki na taasisi za fedha; waraka uliokusudia kuwaondoa katika sekta ya benki wafanyakazi wa benki wasio waaminifu; waraka ulioamuru benki na taasisi za fedha kutolipa gawio iwapo uwiano wa gharama na mapato pamoja na kiwango cha mikopo chechefu vinazidi asilimia 55 na asilimia 5 mtawalia; na waraka unaohusu utekelezaji wa makubaliano ya pili na ya tatu kuhusu usimamizi wa benki na taasisi za fedha (Basel II na III).

43. Mwaka 2021, Benki Kuu pia ilitoa waraka kuhusu hatua mbalimbali za kukuza mikopo kwa sekta binafsi na kupunguza viwango vya riba ikiwemo: kupunguza kiwango

cha sehemu ya amana za mabenki kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na mabenki yatakayotoa mikopo katika sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10 kwa mwaka; kulegeza masharti ya kuwa wakala wa benki ikiwemo kuondoa kigezo kuhusu uzoefu wa miezi 18 ya biashara na badala yake waombaji wa biashara ya wakala wa benki watatakiwa kuwa na kitambulisho cha Taifa au namba ya kitambulisho cha Taifa; kuweka ukomo wa kiwango cha riba kinachotolewa na benki za biashara kwenye akaunti za makampuni yanayotoa huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi ambapo riba itakayotolewa kwenye akaunti hizi haitazidi riba itolewayo na benki husika katika amana za akiba; kuanzisha mfuko maalum wenye thamani ya shilingi trilioni moja (1) ambao utatumika kukopesha mabenki na taasisi za fedha kwa riba ya asilimia 3 ili taasisi hizo zikopeshe sekta binafsi zinazojihusisha na shughuli za kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10 kwa mwaka; na kupunguza kiwango cha mtaji kinachotakiwa kuwekwa na benki za biashara kwa ajili ya kuweza kutoa mikopo.

Huduma Jumuishi za Fedha

44. Mwaka 2021, Serikali ilisajili vituo 110,553 vya kutoa huduma za fedha vikiwa na jumla ya huduma mbalimbali za fedha 279,994 katika kanzidata ya huduma za fedha baada ya kuzifikia asilimia 92 ya kata zote nchini. Kukamilika kwa usajili wa watoa huduma za fedha kote nchini kutawezesha kubainisha maeneo ambayo bado yana changamoto ya kufikiwa na huduma rasmi za fedha ndani ya kipenyo cha kilometa tano.

45. Mfumo wa malipo ya rejareja wa papo kwa hapo ulifikia hatua ya majaribio baada ya kukamilika kwa hatua ya kwanza ya uundaji ambapo benki za biashara tatu (3) pamoja na kampuni za simu mbili (2) ziliunganishwa mwaka 2021. Mfumo huo una lengo la kuongeza ufanisi na mwingiliano kati ya watoa huduma za fedha nchini.

46. Mwaka 2021, Serikali iliendelea na utekelezaji wa mikakati ya Mpango wa Huduma Jumuishi za Fedha 2018 - 2022 ambapo Kamati ya Wanawake ya Huduma Jumuishi za Fedha iliundwa. Kamati hiyo iliundwa kwa lengo la kufuatilia, kuchochea na kupendekeza mikakati itakayoongeza idadi ya wanawake watakaofikiwa na kutumia huduma rasmi za fedha kutoka asilimia 60 mwaka 2017 hadi asilimia 70 mwaka 2022.

47. Matumizi ya huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi ikiwa ni moja ya mikakati muhimu ya huduma jumuishi za fedha yaliongezeka na kufikia akaunti 33,142,118 mwaka 2021 kutoka akaunti 30,325,019 mwaka 2020. Aidha miamala ya huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi ilipungua na kufikia 272,634,498 yenye thamani ya shilingi trilioni 9.2 mwaka 2021 kutoka miamala 285,432,978 yenye thamani ya shilingi trilioni 11.1 mwaka 2020.

Huduma Ndogo za Fedha

48. Hadi Desemba 2021, idadi ya maombi ya leseni za watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la pili iliyopokelewa na Benki Kuu ya Tanzania ilikuwa 1,159 ambapo watoa huduma 692 walipata leseni ikilinganisha na maombi 698 na leseni 215 zilizotolewa mwaka 2020. Aidha, hadi kufikia Desemba 2021, idadi ya maombi ya leseni za watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la tatu iliyopokelewa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika - TCDC ilikuwa 1,114 ambapo leseni 580 zilitolewa ikilinganishwa na maombi 241 na leseni 56 zilizotolewa mwaka 2020. Vilevile, katika kipindi hicho, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) ilipokea maombi 27,177 ya usajili wa watoa huduma ndogo za fedha daraja la nne ambapo vikundi 24,123 vilisajiliwa.

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana

49. Mwaka 2021, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana iliendelea kuchambua na kuidhinisha miamala ya uuzaji wa dhamana mbalimbali kwa lengo la kuongeza idadi ya bidhaa katika masoko ya mitaji. Katika kipindi hicho, bidhaa zilizoidhinishwa ni pamoja na: hatifungani inayokidhi matakwa ya maadili ya kiislam - Sukuk Bond; hatifungani ya benki ya NMB - Jasiri Bond; hatifungani kwa ajili ya kuendeleza sekta ya nyumba na makazi kupitia TMRC; na hatifungani ya Kampuni ya Afrisian Gining Limited kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo cha pamba.

50. Hadi Desemba 2021, Mamlaka ilitoa leseni 154 ikilinganishwa na leseni 144 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 6.9. Leseni hizo zilizotolewa kwa: Soko la Hisa la Dar es Salaam (1); soko la bidhaa (1); hifadhi kuu ya dhamana (1); kampuni za utendaji katika soko la hisa (13); watendaji katika soko la bidhaa (5); watendaji katika soko la hatifungani (6); washauri wateule (6); washauri wa uwekezaji (14); mifuko ya uwekezaji wa pamoja (10); mameneja wa mifuko ya uwekezaji wa pamoja (9); watunza dhamana (6); na wawakilishi wa taasisi zinazotoa huduma katika masoko ya mitaji (82).

51. Hadi Desemba 2021, mtaji wa Soko la Hisa la Dar es Salaam - DSE kwa kampuni za ndani uliongezeka kwa asilimia 2.2 na kufikia shilingi trilioni 9.4 ikilinganishwa na shilingi trilioni 9.2 kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, mtaji wa jumla wa Soko la Hisa ulikuwa shilingi trilioni 15.8 Desemba 2021 ikilinganishwa na shilingi trilioni 15.1 kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 4.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa katika soko la hisa ikiwemo kampuni za CRDB Plc, Jatu Plc, na Tanga Cement.

52. Mwaka 2021, fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni za ndani iliongezeka kwa alama 80.7 na kufikia alama 3,565.2 kutoka alama 3,484.5 mwaka 2020. Aidha, fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni zote iliongezeka kwa alama 79.8 na kufikia alama 1,896.7 kutoka alama 1,816.9 mwaka 2020. Kuongezeka kwa alama za fahirisi kunaashiria ufanisi wa soko

hususan kuongezeka kwa bei za hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

53. Mauzo ya hisa katika soko la hisa yalipungua na kufikia shilingi bilioni 104.4 mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 591.2 mwaka 2020. Kupungua kwa mauzo kulichangiwa na kupungua kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na athari za UVIKO - 19 ambapo wawekezaji wengi walihamishia uwekezaji katika hatifungani za Serikali.

54. Mwaka 2021, mauzo ya hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam yalikuwa shilingi trilioni 2.6 ikilinganishwa na mauzo ya shilingi trilioni 2.1 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 23.8. Hii ilitokana na wawekezaji kuhamishia uwekezaji kwenye hatifungani za Serikali ambazo ni salama zaidi. Kwa upande mwingine, mauzo ya hatifungani za kampuni zilizoorodheshwa DSE yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 3.5 mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.3 mwaka 2020. Kuongezeka kwa mauzo ya hatifungani za kampuni kulitokana na kuimarika kwa biashara katika soko la hatifungani za kampuni.

55. Mwaka 2021, Kampuni ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS ilisimamia uwekezaji katika mifuko ya Umoja, Wekeza Maisha, Watoto, Jikimu, Ukwasi na Hatifungani. Hadi Desemba 2021, thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja ilikuwa shilingi bilioni 744.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 476.9 kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 56.2. Katika kipindi hicho, thamani ya mifuko yote iliongezeka isipokuwa Mfuko wa Jikimu ambao thamani yake ilipungua na kufikia shilingi bilioni 17.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 18.0 kipindi kama hicho mwaka 2020. Kupungua kwa thamani kulitokana na Mfuko kulipa baadhi ya wawekezaji kufuatia kuiva kwa uwekezaji na baadae kuwekeza kwenye Mifuko ya Hatifungani na Ukwasi.

Jedwali Na. 2.2: Thamani ya mfuko katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja

Jina la Mfuko	**2020**	**2021**	**Ongezeko la thamani (Asilimia)**
	Thamani ya Mfuko (Shilingi Milioni)	**Thamani ya Mfuko (Shilingi Milioni)**	
Mfuko wa Umoja	237,355.4	269,464.7	13.5
Mfuko wa Wekeza Maisha	1,431.0	2,536.6	77.3
Mfuko wa Watoto	3,686.1	4,599.0	24.8
Mfuko wa Jikimu	17,964.4	17,321.6	-3.6
Mfuko wa Ukwasi	152,620.4	304,337.4	99.4
Mfuko wa Hatifungani	63,929.9	146,666.6	129.4
Jumla	**476,987.2**	**744,925.9**	**56.17**

Chanzo: Kampuni ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma

56. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma - PSSSF ulisajili wanachama wapya 27,120 mwaka 2021 ikilinganishwa na wanachama 14,615 mwaka 2020. Aidha, Mfuko ulikusanya shilingi trilioni 3.6 kutokana na michango ya wanachama mwaka 2020/21 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.4 mwaka 2019/20. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kulipa malimbikizo ya michango ya wanachama kwa njia ya hatifungani maalum yenye thamani ya shilingi trilioni 2.2. Katika kipindi hicho, Mfuko ulilipa mafao yenye thamani ya shilingi trilioni 1.9 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.2 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 58.3.

57. Mwaka 2020/21, uwekezaji wa Mfuko ulifikia kiasi cha shilingi bilioni 7,443.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 5,753.0 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 29.4. Vilevile, mapato ya Mfuko yatokanayo na uwekezaji yalifikia shilingi bilioni 612.4 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na shilingi bilioni 428.1 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 43.1. Aidha, mwaka 2020/21 thamani ya Mfuko iliongezeka kwa asilimia 25.3 na kufikia shilingi bilioni 7,341.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 5,861.3 mwaka 2019/20. Ongezeko hilo lilitokana na ulipaji wa malimbikizo ya michango ya wanachama kwa mfumo wa hatifungani maalumu.

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii

58. Mwaka 2020/21, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii - NSSF ulikuwa na wanachama wachangiaji 921,865 ikilinganishwa na wanachama 797,564 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 15.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa utolewaji wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa hifadhi ya jamii pamoja na kuimarika kwa usajili wa wanachama. Aidha, wastaafu wa Mfuko walikuwa 23,164 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na wastaafu 22,042 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 5.1. Vilevile, Mfuko ulikusanya michango ya wanachama kiasi cha shilingi trilioni 1.2 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.1 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 9.1. Hii ilitokana na juhudi za Mfuko katika kukusanya michango na kuwaelimisha waajiri umuhimu wa kulipa michango ya waajiriwa kwa wakati. Kwa upande mwingine, mafao yaliyolipwa kwa wanachama yaliongezeka kwa asilimia 28.7 na kufikia shilingi bilioni 594.3 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na shilingi bilioni 461.9 mwaka 2019/20.

59. Mwaka 2020/21, mapato ya Mfuko yatokanayo na uwekezaji yalifikia shilingi bilioni 454.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 337.8 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 34.4. Hii ilitokana na ongezeko la uwekezaji katika hatifungani za Serikali. Aidha, thamani ya uwekezaji katika vitega uchumi vya Mfuko iliongezeka kwa asilimia 30.3 kufikia shilingi bilioni 4,140.3 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na shilingi bilioni 3,177.8 mwaka 2019/20. Katika kipindi hicho, thamani ya Mfuko iliongezeka kwa asilimia 15.9 na kufikia shilingi trilioni 5.1 kutoka shilingi trilioni 4.4 mwaka 2019/20. Hii ilitokana na ongezeko la mapato ya uwekezaji na michango ya wanachama.

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi

60. Mwaka 2020/21, idadi ya waajiri waliosajiliwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi - WCF iliongezeka na kufikia waajiri 25,085 kutoka waajiri 22,471 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 11.6. Katika kipindi hicho, idadi ya wafanyakazi waliochangiwa ilipungua na kufikia 1,134,806 kutoka wafanyakazi 1,146,718 mwaka 2019/20. Upungufu huo ulitokana na athari za ugonjwa wa UVIKO-19 uliosababisha baadhi ya waajiri kufunga biashara zao na kupunguza idadi ya wafanyakazi. Aidha, michango kutoka kwa waajiri ilikuwa shilingi bilioni 106.9 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na shilingi bilioni 106.4 mwaka 2019/20.

61. Mwaka 2020/21, mapato yatokanayo na uwekezaji wa Mfuko yalikuwa shilingi bilioni 69.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 42.3 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 65.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika hatifungani za Serikali za muda mrefu. Aidha, Mfuko uliwekeza katika amana za Serikali shilingi bilioni 343.8, amana za benki shilingi bilioni 14.7, amana za kampuni shilingi bilioni 3.6, Mfuko wa Umoja UTT shilingi bilioni 45.0, hisa za kampuni shilingi bilioni 21.9 na thamani ya mali isiyohamishika milioni 192. Vile vile, mapato yaliyotokana na shughuli nyingine za kiuchumi yalikuwa shilingi milioni 103.0 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na shilingi milioni 445.6 mwaka 2019/20.

62. Mwaka 2020/21, Mfuko ulitumia shilingi bilioni 13.2 kulipa matibabu na fidia kwa wafanyakazi walioumia au kufariki wakiwa kazini ikilinganishwa na shilingi bilioni 9.1 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asimilia 45.1. Hii ilitokana na kutolewa kwa elimu kwa umma kuhusu masuala ya fidia kwa wafanyakazi na taratibu za kudai mafao kulikosababisha kuongezeka kwa madai ya wafanyakazi walioumia, kuugua au kufariki wakiwa kazini. Kwa upande mwingine, thamani halisi ya mali za Mfuko iliongezeka kwa asilimia 33.5 na kufikia shilingi bilioni 445.3 mwaka 2020/21 kutoka shilingi bilioni 333.5 mwaka 2019/20. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato ya uwekezaji na makusanyo ya michango ya waajiri.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

63. Wanachama wachangiaji katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya - NHIF waliongezeka kwa asilimia 14.9 na kufikia wanachama 1,212,519 mwaka 2020/21 kutoka wanachama 1,055,555 mwaka 2019/20. Aidha, Mfuko ulihudumia wanufaika 4,550,207 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na wanufaika 4,403,581 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 3.3. Hii ilitokana na utoaji wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa bima ya afya na huduma zinazotolewa pamoja na kuongezeka kwa usajili wa makundi mbalimbali kutoka sekta isiyo rasmi.

Jedwali Na.2.3: Wanachama Wachangiaji na Wanufaika wa Mfuko

Mwaka	Idadi ya wanachama	Wanufaika waliohudumiwa
2016/17	753,832	3,491,400
2017/18	858,446	3,918,999
2018/19	966,792	4,025,693
2019/20	1,055,555	4,403,581
2020/21	1,212,519	4,550,207

Chanzo: Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

64. Mwaka 2020/21, idadi ya vituo vya afya vilivyosajiliwa na Mfuko vilifikia 8,483 ikilinganishwa na vituo 8970 mwaka 2019/20, sawa na upungufu wa asilimia 5.4. Upungufu huo ulisababishwa na baadhi ya vituo kutofanya usajili kwa wakati baada ya ukomo wa mkataba. Kati ya vituo vilivyosajiliwa; vituo 6,088 vilikuwa vya Serikali (asilimia 71.8), vituo 770 madhehebu ya dini (asilimia 9.1) na vituo vya binafsi 1,625 (asilimia 19.1).

Jedwali Na. 2.4: Vituo vya Kutolea Huduma za Afya Vilivyosajiliwa na Mfuko

Vituo vya Kutolea Huduma ya Afya	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	Badiliko (Asilimia)
Zahanati	5,401	5,753	6,485	6,252	-3.6
Vituo vya Afya	713	766	853	832	-2.5
Hospitali	286	298	346	381	10.1
Maduka ya dawa	349	449	597	560	-6.2
Maduka ya dawa maalumu	202	200	461	179	-61.2
Cliniki Maalum	73	130	211	265	25.6
Vituo vya Uchunguzi	6	9	16	13	-18.8
Vituo vya Uokozi	1	1	1	1	0
Jumla	**7,031**	**7,606**	**8,970**	**8,483**	**-5.4**

Chanzo: Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

65. Mwaka 2020/2021, mapato ya Mfuko yalikua kwa asilimia 3.5 na kufikia shilingi bilioni 569.7 kutoka shilingi bilioni 550.4 mwaka 2019/2020. Ukuaji wa mapato ulitokana na ongezeko la usajili wa wanachama kutoka sekta rasmi na isiyo rasmi pamoja na jitihada za ukusanyaji na ufuatiliaji wa michango kutoka kwa wanachama. Aidha, thamani ya Mfuko ilipungua kwa asilimia 6.2 na kufikia shilingi bilioni 1,175.4 mwaka 2020/21 kutoka shilingi bilioni 1,253.0 mwaka 2019/20. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa malipo ya madai na kupungua kwa mapato yatokanayo na uwekezaji.

Jedwali Na. 2.5: Mchanganuo wa Mapato ya Mfuko kwa aina ya Chanzo

Mwaka wa Fedha	Shilingi Bilioni			Jumla ya Mapato
	Mapato ya Michango	Mapato ya Vitega Uchumi	Mapato Mengineyo	
2016/17	367.6	109.5	1.9	479
2017/18	394.9	107.4	1.5	503.8
2018/19	431	84.8	3.1	518.9
2019/20	467.8	80.7	1.9	550.4
2020/21	489.5	77.1	3.1	569.7
Badiliko (Asilimia) 2020/21 - 2019/20	**4.6**	**-4.5**	**63.2**	**3.5**

Chanzo: Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa

66. Mwaka 2020/21, wanachama wachangiaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa - iCHF waliongezeka na kufikia wanachama 2,945,893 kutoka wanachama 1,359,063 waliojiunga mwaka 2019/20. Katika kipindi hicho, shilingi milioni 12,159 zilikusanywa kutokana na michango ya wanachama ikilinganishwa na shilingi milioni 6,327 mwaka 2019/20. Ongezeko la wanachama wa Mfuko pamoja na kiwango cha fedha kilichokusanywa na kurejeshwa katika vituo vya kutolea huduma za afya lilitokana na utolewaji wa elimu ya dhana ya bima ya afya kwa wananchi na watoa huduma za afya kuhusu Mfuko huo.

Jedwali Na. 2.6: Wanachama Wachangiaji, kiasi cha fedha kilichokusanywa na kilichorejeshwa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mwaka	Idadi ya Wanachama	Fedha zilizokusanywa	Fedha zilizorejeshwa katika vituo vya kutolea huduma za afya
2018/19	374,019	2,230,050,000	369,391,222.6
2019/20	1,359,063	6,327,300,000	3,291,383,184.5
2020/21	2,945,893	12,158,921,000	7,940,817,643.1

Chanzo: Ofisi ya Rais, TAMISEMI

Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania

67. Mwaka 2021, Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania - TIRA iliendelea kusimamia kampuni 32 za bima kama ilivyokuwa mwaka 2020. Kati ya hizo, kampuni 10 zinamilikiwa na watanzania na kampuni 22 zinamilikiwa kwa ubia kati ya watanzania na wageni. Aidha, idadi hiyo inajumuisha kampuni 24 za bima ya kawaida, kampuni tano (5) za bima ya maisha, kampuni mbili (2) za bima mtawanyo na kampuni moja (1) inayotoa huduma za bima ya kawaida na bima ya maisha.

68. Mwaka 2021, Mamlaka ilisajili kampuni za udalali wa bima 73, madalali wa bima mtawanyo 5, mawakala wa bima 938, benki wakala wa bima 20 na wakadiriaji hasara 52

ikilinganishwa na kampuni za udalali wa bima 77, udalali wa bima mtawanyo nne (4), wakala wa bima 756, benki wakala wa bima 14 na wakadiriaji hasara 60 mwaka 2020. Aidha, kampuni nne (4) za sayansi ya uthaminishaji zilisajiliwa mwaka 2021 ikilinganishwa na kampuni tatu (3) mwaka 2020. Vile vile, kampuni mbili (2) za uchunguzi binafsi zilisajiliwa mwaka 2021.

69. Mwaka 2021, watumiaji wa huduma za bima walikuwa 6,913,514 ikilinganishwa na watumiaji 6,686,267 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Hii ilitokana na jitihada za Mamlaka kuendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa bima kwa wananchi na ulipaji wa madai ya bima kwa wakati. Aidha, madai ya bima za kawaida yaliyolipwa yaliongezeka kwa asilimia 17.6 na kufikia shilingi milioni 339,622 mwaka 2021 kutoka shilingi milioni 288,916 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa madai katika bima za uhandisi, afya, moto na vyombo vya moto. Kwa upande mwingine, malipo ya madai ya bima za maisha yalikuwa shilingi milioni 85,145 mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi milioni 64,227 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 32.6.

70. Mwaka 2021, mauzo katika soko la bima yaliongezeka kwa asilimia 10.4 na kufikia shilingi bilioni 910.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 824.3 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Bima inayotaka mizigo yote inayoingia nchini ikatiwe bima na kampuni za ndani na kuongezeka kwa uelewa wa umma kuhusu faida za bima. Katika kipindi hicho, mauzo ya bima za kawaida yalikuwa shilingi bilioni 745.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 688.6 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 8.3. Aidha, mauzo ya bima za maisha yaliongezeka kwa asilimia 21.1 na kufikia shilingi bilioni 164.3 mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 135.7 mwaka 2020. Vilevile, bima za kawaida zilichangia asilimia 82.0 ya mauzo na bima za maisha zilichangia asilimia 18.0. Mchango wa aina za bima za kawaida katika mauzo ulikua kama ifuatavyo: bima za vyombo vya moto asilimia 33.4, moto (asilimia 21.5), afya (asilimia 18.4), ajali (asilimia 7.1), majini (asilimia 4.5), anga (asilimia 4.9) uhandisi (asilimia 3.7) mafuta na gesi (asilimia 0.1) na aina zingine za bima kwa ujumla (asilimia 6.2).

71. Mwaka 2021, thamani ya mali za kampuni za bima ilifikia shilingi bilioni 1,075.5 kutoka shilingi bilioni 1,181.0 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 8.9. Uwekezaji wa kampuni za bima ulikuwa na thamani ya shilingi bilioni 790.9 mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 858.7 mwaka 2020. Uwekezaji huo unajumuisha: amana katika taasisi za fedha na fedha taslimu asilimia 50.6; dhamana za Serikali asilimia 36.8; hisa asilimia 5.2; mali zisizohamishika asilimia 4.3; na uwekezaji kwenye maeneo mengine asilimia 3.0. Aidha, madeni ya kampuni za bima yalipungua kwa asilimia 10.4 na kufikia shilingi bilioni 685.0 mwaka 2021 kutoka shilingi bilioni 764.9 mwaka 2020. Tofauti kati ya mali na madeni ya kampuni hizo ilikuwa shilingi bilioni 390.5 mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 416.1 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 6.1.

72. Mwaka 2021, mapato yaliyotokana na uwekezaji wa bima za kawaida yalikuwa shilingi bilioni 54.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 52.5 mwaka 2020. Aidha, faida iliyotokana na bima za kawaida ilikuwa shilingi bilioni 53.2 mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 50.1 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 6.2.

Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania

73. Mwaka 2021, amana za Benki ya Maendeleo ya Kilimo - TADB zilipungua na kufikia shilingi bilioni 360.5 kutoka shilingi bilioni 376.9 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 4.4. Aidha, mtaji wa Benki uliongezeka na kufikia shilingi bilioni 294.9 kutoka shilingi bilioni 77.4 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na hatua ya Serikali ya kubadili mkopo wa shilingi bilioni 208 ambao TADB ilikopa kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika - AfDB na kuwa mtaji ili kuiwezesha Benki kufikia wakulima, wavuvi na wafugaji wengi zaidi.

74. Mwaka 2021, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 122.1 ilitolewa na TADB ikilinganishwa na shilingi bilioni 86.7 zilizotolewa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 40.8. Kati ya mikopo hiyo, shilingi bilioni 19.2 zilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo, shilingi bilioni 31.1 kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa mazao na shilingi bilioni 71.8 kwa ajili ya miradi ya uchakataji wa mazao. Katika kipindi hicho, Benki kupitia mfuko wa dhamana kwa wakulima wadogo kwa kushirikiana na benki washirika 9 ilitoa dhamana kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 61.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 27.7 zilizotolewa mwaka 2020. Aidha, mikopo iliyotolewa iliwanufaisha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa 12,676 kupitia mikopo ya moja kwa moja na wakulima 11,987 kupitia mfuko wa dhamana kwa wakulima wadogo mwaka 2021 ikilinganishwa na wakulima 9,476 kupitia mikopo ya moja kwa moja na wakulima 11,231 kupitia mfuko wa dhamana kwa wakulima wadogo mwaka 2020.

75. Benki ilipata faida ya shilingi bilioni 10.2 mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 8.2 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 24.4. Hii ilichangiwa na jitihada za benki katika kufuatilia urejeshaji wa mikopo, kupunguza gharama za uendeshaji pamoja na kuongezeka kwa kiasi cha mikopo iliyotolewa. Aidha, kiwango cha mikopo chechefu kilikuwa asilimia 5.5 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2020.

Benki ya Biashara Tanzania

76. Mwaka 2021, benki ya TPB ilibadilishwa jina na kuwa Benki ya Biashara Tanzania - TCB na kuendelea kutoa huduma kupitia matawi 48 na matawi madogo 36. Katika kipindi hicho, amana za wateja ziliongezeka kwa asilimia 13.1 na kufikia shilingi milioni 908,115 kutoka shilingi milioni 803,100 mwaka 2020. Hii ilitokana na ongezeko la idadi ya wateja kufikia wateja 536,544 mwaka 2021 kutoka wateja 480,888 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 11.6. Aidha, TCB ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 718,600 mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi milioni 616,512 mwaka 2020, sawa na

ongezeko la asilimia 16.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vyanzo vya amana na mahitaji katika soko. Hadi Desemba 2021, mikopo chechefu ilikuwa shilingi milioni 107,790 kutoka shilingi milioni 86,867 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 24.1. Ongezeko hilo kwa kiasi kikubwa lilitokana na iliyokuwa benki ya TPB kuungana na benki ya TIB Corporate na kurithi mikopo chechefu.

77. Mwaka 2021, uwekezaji wa benki katika dhamana za Serikali uliongezeka kwa asilimia 32.6 na kufikia shilingi bilioni 133.2 kutoka shilingi bilioni 100.5 mwaka 2020. Aidha, pato ghafi la Benki lilikuwa shilingi bilioni 169.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 152.1 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 11.6. Thamani ya mali za benki iliongezeka kwa asilimia 14.3 na kufikia shilingi bilioni 1,184.5 mwaka 2021 kutoka shilingi bilioni 1,036.4 mwaka 2020.

Soko la Bidhaa Tanzania

78. Mwaka 2020/21, Soko la Bidhaa Tanzania - TMX liliandaa miongozo ya mauzo ya bidhaa mbalimbali ambayo ni: ufuta; choroko; kakao; mifugo hai; ngozi; nyanya na vitunguu; ndizi; mbaazi; na mkonge. Miongozo hiyo huboreshwa kila msimu wa mauzo kulingana na mazingira na changamoto zinazojitokeza. Aidha, TMX iliendelea kuboresha mfumo wa mauzo kwa njia ya kielektroniki na kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wadau zaidi ya 190,954 kuhusu matumizi ya mfumo. Wadau hao ni pamoja na wakulima, wafugaji, wanunuzi wa bidhaa na viongozi wa Serikali katika mikoa ya Mtwara, Kilimanjaro, Arusha, Tabora, Ruvuma, Njombe, Mwanza, Lindi, Mbeya, Manyara, Katavi, Songwe, Iringa, Dodoma, Kagera, Singida, Simiyu, Geita, Morogoro, Pwani na Rukwa.

79. Mwaka 2020/21, wakulima wa zao la kakao katika mkoa wa Morogoro waliwezeshwa kufanya mauzo kupitia TMX ambapo tani 260.1 za kakao ziliuzwa na kiasi cha shilingi milioni 1,292.6 kililipwa kwa wadau walioshiriki katika mkoa huo. Katika kipindi hicho, tani 310.9 za ufuta ziliuzwa na kiasi cha shilingi milioni 754.2 kililipwa kwa washiriki wa mkoa wa Manyara na Songwe. Aidha, tani 14,112.1 za choroko ziliuzwa na shilingi bilioni 22.6 zililipwa kwa washiriki mkoa wa Shinyanga, Mwanza, Tabora, Simiyu na Singida.

Jedwali 2.7: Kiasi na Thamani ya Bidhaa Zilizouzwa

Bidhaa (Mazao)	2020		2021	
	Kiasi (Tani)	Thamani (Shilingi)	Kiasi (Tani)	Thamani (Shilingi)
Ufuta	20,068.3	37,651,622,377	310.9	754,218,551
Choroko	1,124.4	1,485,419,176	14,112.1	22,603,319,507
Dengu	104.0	122,720,000	-	-
Korosho	19,867.8	42,524,659,859	-	-
Cocoa	-	-	260.1	1,292,578,070
Jumla	**41,164.5**	**81,784,421,412**	**14,683.1**	**24,650,116,128**

Chanzo: Soko la Bidhaa Tanzania

MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA – TANZANIA BARA

Jedwali Na. 17

	Kipindi Kinachoishia Mwezi Desemba (Shiling Bilioni)								
								Badiliko 2020-2021	
	2015	**2016**	**2017**	**2018**	**2019**	**2020**	**2,021**	**Kiasi**	**Asilimia**
Fedha ya msingi (M0)	6,833.1	6,854.4	6,954.4	6,992.9	7,466.4	7,169.3	8,407.3	1,238.0	17.3
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	9,575.7	10,083.8	11,155.3	11,723.7	13,325.1	14,321.7	17,625.5	996.6	23.1
Amana za Akiba na za muda maalum	6,204.4	6,536.5	7,194.6	7,316.7	7,955.1	8,711.0	9,462.8	755.9	8.6
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)	15,780.1	16,620.3	18,349.9	19,040.4	21,280.3	23,032.6	27,088.8	1,752.3	17.6
Amana za fedha za kigeni	6,335.2	6,257.5	6,364.4	6,783.1	7,032.9	6,887.9	7,469.7	-145	8.4
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	22,115.3	22,877.8	24,714.3	25,823.5	28,313.1	29,918.2	34,558.0	1,605.1	15.5
Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)	**8,244.0**	**8,186.3**	**11,596.1**	**10,629.8**	**12,034.5**	**10,722.5**	13,966.0	**-1,312.0**	30.2
Rasilimali halisi katika fedha za kigeni Benki Kuu	7,528.2	8,281.4	12,149.9	10,692.3	12,063.1	10,308.8	**13,219.1**	-1,754.3	28.2
Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye mabenki	715.9	-95.1	-553.8	-62.5	-28.5	413.8	746.8	442.3	-
Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)	**13,871.3**	**14,691.6**	**13,118.2**	**15,193.7**	**16,278.6**	**19,198.0**	20,592.1	**2,919.4**	7.3
Madai rasmi ya ndani	22,505.5	23,775.8	24,977.2	26,249.3	28,103.3	26,139.6	30,030.5	-1,963.7	14.9
Madai halisi kwa serikali kuu	4,881.6	4,282.0	3,275.7	4,481.6	3,893.9	5,831.3	7,686.4	1,937.4	31.8
Mikopo kwa sekta binafsi	15,492.7	16,608.9	16,895.4	17,726.8	19,695.4	20,308.3	22,344.1	612.9	10.0
Rasilimali nyinginezo (Other Items Net)	-6,503.1	-6,199.3	-7,052.9	-7,014.7	-7,310.7	-6,941.6	-9,438.4	369.1	36.0

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

VIWANGO VYA UKUAJI WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

Jedwali Na. 18

	Kipindi kinachoishia mwezi Desemba (Asilimia)						
	2015	**2016**	**2017**	**2018**	**2019**	**2020**	**2021**
Fedha ya msingi (M0)	15.6	0.3	1.5	0.6	6.8	…..	.....
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	15.6	5.3	10.6	5.1	13.7	7.5	-0.7
Amana za Akiba na za muda maalum	10.1	5.4	10.1	1.7	8.7	9.5	-2.0
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)	13.4	5.3	10.4	3.8	11.8	8.2	-1.2
Amana za fedha za kigeni	34.9	-1.2	1.7	6.6	3.7	-2.1	4.1
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	18.8	3.4	8.0	4.5	9.6	5.7	0.0
Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)	**25.8**	**-0.7**	**41.7**	**-8.3**	**13.2**	**-10.9**	**10.6**
Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)	**15.0**	**5.9**	**-10.7**	**15.8**	**7.1**	**17.9**	**-5.9**
Madai rasmi ya ndani	26.8	2.5	-3.4	10.1	6.2	10.8	-3.7
Madai halisi kwa serikali kuu	33.7	-12.3	-23.5	36.8	-13.1	49.8	-17.0
Mikopo kwa sekta Binafsi	24.8	7.2	1.7	4.9	11.1	3.1	0.1
Rasilimali nyinginezo (Other Items Net)	62.5	-4.7	13.8	-0.5	4.2	-5.0	2.3

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI FEDHA KATI YA SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI

Jedwali Na. 19

	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Shs/Dola (mwisho wa mwaka)	2,181.3	2,242.2	2,291.3	2,300.0	2,309.8	2,307.4
Badiliko la thamani ya shilingi (%)	1.3	2.8	2.2	0.4	0.4	-0.1
Shs/Dola (wastani wa mwaka)	2,188.0	2,240.8	2,275.4	2,299.8	2,305.6	2,309.2
Badiliko la wastani wa thamani ya shilingi (%)	9	2.4	1.5	1.1	0.3	0.2

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA

Jedwali Na. 20 **Shilingi Bilioni**

	Mwaka						Badiliko (Asilimia)	
	2016	2017	2018	2019	2020	2021	2020	2021
Amana za Sekta binafsi								
Amana za Hundi Zinazaohamishika	5,941.5	6,685.3	7,031.7	7,866.5	8,121.4	9,894.0	3.2	21.8
Amana za Akiba na za Muda Maalum	6,415.6	7,052.2	7,154.7	7,750.4	8,519.4	9,350.8	9.9	9.8
Amana za fedha za kigeni	5,831.5	6,087.1	6,376.3	6,160.6	6,427.1	7,146.0	4.3	11.2
Jumla	**18,188.7**	**19,824.6**	**20,562.8**	**21,777.5**	**23,067.9**	**26,390.7**	**5.9**	**14.4**
Amana za Serikali	577.8	560.6	358.5	981.3	652.9	422.5	-33.5	-35.3
Jumla za Amana zote	**18,766.5**	**20,385.1**	**20,921.3**	**22,758.9**	**23,720.7**	**26,813.2**	**4.2**	**13**

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

VIWANGO VYA WASTANI WA RIBA

Jedwali Na. 21 **Asilimia**

Aina ya Riba	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Riba ya Benki kuu (Discount rate)	16.0	16.0	16.0	7.0	7.0	5.0	5.00
Riba katika soko la fedha kati ya benki za biashara kwa ujumla	11.23	13.47	6.0	2.21	5.13	4.5	4.44
Riba za dhamana za serikali kwa ujumla	12.91	16.17	11.1	6.43	7.71	4.42	4.78
Siku 35	5.92	7.27	5.54	2.51	3.47	2.37	2.60
Siku 91	8.8	7.85	5.49	2.89	4.17	2.37	2.74
Siku 182	13.04	15.84	10.01	4.13	5.07	2.88	3.2
Siku 364	13.92	16.56	11.79	7.08	8.04	2.32	4.85
Riba za hati fungani							
Miaka miwili	14.78	17.44	14.52	9.42	11.45	8.14	7.67
Miaka mitano	15.15	17.79	15.78	11.64	12.56	11.24	9.19
Miaka saba	16.6	17.69	16.31	12.62	13.09	11.48	10.09
Miaka kumi	17.14	18.11	16.79	14.39	15.04	12.51	11.59
Miaka kumi na tano	17.71	18.85	17.54	14.69	15.52	14.05	13.59
Miaka ishirini				17.7	17.35	15.79	15.27
Miaka ishirini na tano							16.06
Riba za amana							
Amana za akiba	3.45	3.35	3.03	2.52	2.44	2.34	1.95
Amana za muda maalum kwa ujumla	8.89	9.19	10.04	8.24	7.25	6.7	6.85
Mwaka mmoja	10.8	11.47	11.66	8.78	8.8	8.28	8.32
Riba za mikopo							
Mikopo kwa ujumla	16.1	15.96	17.77	17.43	16.97	16.66	16.59
Mikopo ya muda mfupi hadi mwaka mmoja	14.25	13.66	18.3	18.25	16.69	15.73	16.43

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

SURA YA 3

FEDHA ZA SERIKALI

Utangulizi

80. Katika mwaka 2021/22, bajeti ilizingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 wenye dhima ya **"*Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*"**. Aidha, bajeti ilizingatia utekelezaji wa shughuli mbalimbali kama zilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26. Hivyo, bajeti ya mwaka 2021/22 ilijielekeza katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika maeneo matano (5) ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22. Maeneo hayo ni: Kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo; kukuza uwekezaji na biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu. Kadhalika, bajeti hii iliendelea kugharamia utekelezaji wa miradi ya kitaifa ya kimkakati inayoendelea ikiwemo ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (*Standard Gauge Railway - SGR*), Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115 na kuboresha Shirika la Ndege Tanzania.

81. Katika mwaka 2021/22, shabaha za uchumi jumla na bajeti zililenga: kuwa na ukuaji wa Pato halisi la Taifa wa asilimia 5.0 mwaka 2021; kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei kuwa katika wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia 3.0 hadi 4.5 katika kipindi cha muda wa kati; mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya halmashauri kuwa asilimia 15.9 ya Pato la Taifa; mapato ya kodi kufikia asilimia 13.5 ya Pato la Taifa; kuhakikisha nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) haizidi asilimia 3.0 kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

82. Mwaka 2021/22, Serikali ilitarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 37,980.6 kutoka vyanzo vya ndani na nje. Jumla ya mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yalitarajiwa kuwa shilingi bilioni 25,691.7, sawa na asilimia 67.6 ya bajeti yote. Kati ya mapato ya ndani, mapato ya kodi yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 21,778.1, sawa na asilimia 84.8 ya mapato ya ndani. Mapato yasiyo ya kodi yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 3,049.8 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri shilingi bilioni 863.9. Misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilikadiriwa kuwa shilingi bilioni 4,254.6, sawa na asilimia 11.2 ya bajeti yote. Aidha, Serikali ilitarajia kukopa shilingi bilioni 4,989.1 kutoka soko la ndani na shilingi bilioni 3,045.1 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara.

Mwenendo wa Mapato

Mapato ya Ndani

83. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Serikali ilitarajia kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi bilioni 19,548.9. Katika kipindi hicho, makusanyo ya mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 18,129.2 sawa na asilimia 92.7 ya lengo na ukuaji wa asilimia 17.3 ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Kati ya mapato hayo; mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yalifikia shilingi bilioni 15,630.7, sawa na asilimia 93.9 ya lengo la shilingi bilioni 16,646.1; makusanyo ya maduhuli yalifikia shilingi bilioni 1,822.6 sawa na asilimia 81.1 ya lengo la shilingi bilioni 2,248.5; na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 675.9, sawa na asilimia 103.3 ya lengo la shilingi bilioni 654.3. Sababu za kutofikiwa kwa lengo la makusanyo ya mapato ya ndani ni pamoja na kushuka kwa mauzo ya baadhi ya bidhaa na huduma katika soko la ndani na nje kutokana na athari za UVIKO - 19; ukwepaji kodi; uelewa mdogo wa wananchi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi na kupungua kwa baadhi ya vyanzo vya mapato kutokana na kukua au kushamiri kwa biashara za mtandaoni.

Misaada na Mikopo Nafuu

84. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, misaada na mikopo nafuu iliyopokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 3,655.1, sawa na asilimia 107.6 ya lengo la kipindi hicho. Sababu za kuvuka lengo la misaada na mikopo nafuu ni pamoja na watekelezaji wa miradi ya maendeleo kutimiza matakwa ya kimkataba kwa wakati, ikijumuisha kasi ya utekelezaji wa miradi. Kati ya kiasi kilichopokelewa, misaada na mikopo nafuu ya kibajeti ilikuwa shilingi bilioni 1,362.8 ikiwa ni asilimia 104.0 ya matarajio ya kipindi hicho; mifuko ya kisekta shilingi bilioni 57.2, sawa na asilimia 25.6 ya matarajio katika kipindi hicho; na miradi ya maendeleo shilingi bilioni 2,236.0, sawa na asilimia 120.0 ya matarajio ya kipindi hicho. Kutofikiwa kwa lengo la misaada na mikopo nafuu ya Mifuko ya Pamoja ya Kisekta kumetokana na mabadiliko ya sera za misaada na mikopo nafuu za Washirika wa Maendeleo ambapo baadhi yao wameonesha kuwa hawataweza kutoa fedha kama walivyoahidi kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo athari hasi za UVIKO - 19.

85. Kufuatia mlipuko wa UVIKO - 19, Serikali iliandaa Mpango mahususi wa Kukabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi za UVIKO - 19 (Tanzania COVID - 19 Socio - Economic Response and Recovery Plan - TCRP). Mpango huo ulizinduliwa rasmi tarehe 10 Oktoba, 2021 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan jijini Dodoma ambapo pamoja na mambo mengine, alihimiza utekelezaji wa kizalendo wa Mpango huo ili kuwakinga watanzania dhidi ya maambukizi ya UVIKO - 19 na kuleta mapinduzi makubwa katika uchumi na maendeleo ya wananchi kwa haraka zaidi. Mchakato mzima wa uandaaji wa Mpango husika uliiwezesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupata mkopo usio na riba kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (International Monetary Fund - IMF) wenye thamani ya shilingi bilioni 1,310.65

(dola za Marekani milioni 567.3) kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO - 19 katika sekta za kiuchumi na kijamii. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 230.2 (dola za Marekani milioni 100) zilielekezwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo sehemu kubwa ya uchumi wake uliathiriwa na UVIKO - 19.

86. Kufuatia upatikanaji wa fedha hizo ambazo hazikuwa sehemu ya bajeti iliyoidhinishwa awali, Serikali iliwasilisha katika Bunge la Februari 2022 mapendekezo ya kujumisha mkopo huo kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/22 kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Sura 439 Kifungu cha 43 ambapo yaliridhiwa na Bunge tarehe 18 Februari 2022.

Mikopo ya Ndani

87. Hadi Machi 2022, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 3,860.0 kutoka soko la ndani, sawa na asilimia 78.7 ya shilingi bilioni 4,904.2 zilizopangwa kukopwa mwaka 2021/22. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 2,185.5 zilikopwa kwa ajili ya kulipia hati fungani na dhamana za Serikali zilizoiva na shilingi bilioni 1,674.5 zilikopwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mikopo ya Nje yenye Masharti ya Kibiashara

88. Katika mwaka 2021/22, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 3,045.1 kutoka katika vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 1,639.7, sawa na asilimia 53.8 ya lengo la mwaka.

Mwenendo wa Matumizi

89. Katika mwaka 2021/22, Sera za matumizi zililenga: kuendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima; kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi; kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya miradi mipya; kudhibiti ulimbikizaji wa madai; na kuongeza kasi ya matumizi ya TEHAMA katika miamala na shughuli za Serikali.

90. Serikali ilikadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 37,980.6 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo katika mwaka 2021/22. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 23,003.0 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni asilimia 60.6 ya bajeti yote na shilingi bilioni 14,977.6 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, sawa na asilimia 39.4 ya bajeti yote. Aidha, bajeti ya maendeleo inajumuisha shilingi bilioni 12,033.7 ambazo ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,944.0 fedha za nje.

91. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, ridhaa ya matumizi iliyotolewa ilikuwa shilingi bilioni 26,433.2, sawa na asilimia 95.2 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 16,835.4 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 9,597.8 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, ambapo shilingi bilioni 8,444.4 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1,153.4 ni fedha za nje. Kati ya kiasi kilichotolewa kwa

ajili ya matumizi ya kawaida kilijumuisha shilingi bilioni 6,481.2 za kugharamia malipo ya deni la Serikali ambapo malipo ya riba kwa madeni ya ndani na nje yalikuwa shilingi bilioni 2,107.4, sawa na asilimia 99.7 ya makadirio. Aidha, malipo ya mtaji kwa deni la ndani na nje yalikuwa shilingi bilioni 4,373.8, sawa na asilimia 99.9 ya lengo.

92. Matumizi ya kawaida yalijumuisha malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali kiasi cha shilingi bilioni 6,033.6, sawa na asilimia 98.7 ya lengo la kipindi hicho la shilingi bilioni 6,113.4. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 2,076.6 zililipwa kwa watumishi wa Serikali Kuu, shilingi bilioni 51.0 kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na shilingi bilioni 2,963.2 kwa watumishi wa Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya. Aidha, Serikali ililipa mishahara yenye jumla ya shilingi bilioni 942.7 kwa Taasisi na Mashirika ya Umma.

93. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, ridhaa ya matumizi ya fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 9,597.8 ilitolewa, sawa na asilimia 91.8 ya makadirio. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 8,444.4 zilikuwa fedha za ndani na shilingi bilioni 1,153.4 fedha za nje ikijumuisha shilingi bilioni 887.2 za kugharamia mradi wa Mpango wa Kukabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi zitokanazo na UVIKO - 19. Kutofikiwa kwa malengo ya utoaji wa fedha za maendeleo kulitokana na kutofikiwa kwa malengo ya upatikanaji wa mapato ya ndani, misaada na mikopo kutoka nje.

Deni la Serikali

94. Hadi Machi 2022, Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 69,261.2 sawa na ongezeko la asilimia 15.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 59,852.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 21,778.0 na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 47,483.2. Ongezeko la deni lilitokana na kupokelewa kwa fedha za mikopo kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji. Kwa upande mwingine ongezeko hilo lilichangiwa na kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani pamoja na Serikali kutoa hatifungani maalumu yenye thamani ya shilingi trilioni 2.2 kwa ajili ya kulipa madai ya PSSSF ya kabla ya mwaka 1999. **Kielelezo Na. 3.1** kinaonesha mwenendo wa Deni la Serikali.

Kielelezo Na. 3.1: Mwenendo wa Deni la Serikali kwa kipindi cha Machi 2012 - Machi 2022



Deni la Nje

95. Hadi Machi 2022, deni la Serikali la nje liliongezeka kwa asilimia 9.11 na kufikia dola za Marekani milioni 20,658.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 18,933.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ongezeko hilo lilitokana na kupokelewa kwa fedha za mikopo kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Deni la Nje kwa Wakopeshaji

96. Hadi Machi 2022, mashirika ya fedha ya kimataifa yalichangia asilimia 60.1 ya deni la nje ikilinganishwa na asilimia 58.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Benki za biashara zilichangia asilimia 29.0 na Washirika wa Maendeleo walichangia asilimia 10.9 ya deni lote la nje. **Jedwali Na. 3.1** linaonesha mchanganuo wa deni la nje kwa wakopeshaji. Aidha, kati ya deni lote la nje, mikopo kutoka vyanzo nafuu ilichangia dola za Marekani milioni 14,671.8 sawa na asilimia 71.0 na mikopo yenye masharti ya kibiashara ilichangia dola za Marekani milioni 5,986.40 sawa asilimia 29.0.

Jedwali Na. 3.1: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Wakopeshaji (Dola za Marekani Milioni)

Taasisi	Machi 2019	Mchango kwa asilimia	Machi 2020	Mchango kwa asilimia	Machi 2021	Mchango kwa asilimia	Machi 2022	Mchango kwa asilimia
Mashirika ya Fedha	9,561.9	58.2	10,091.5	57.7	11,121.7	58.7	12,416.4	60.1
Washirika wa Maendeleo	1,930.8	11.9	2,038.5	11.7	2,194.7	11.6	2,255.4	10.9
Benki za kibiashara	4,865.8	29.9	5,358.2	30.6	5,617.3	29.7	5,986.4	29.0
Jumla	**16,358.6**	**100**	**17,488.2**	**100**	**18,933.7**	**100**	**20,658.2**	**100**

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Deni la Ndani

97. Hadi Machi 2022, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 21,778.0 ikilinganishwa na shilingi bilioni 16,116.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 26.0. Ongezeko hilo lilitokana na hatifungani maalumu iliyotolewa na Serikali yenye thamani ya shilingi trilioni 2.2 kwa ajili ya kulipa madeni ya PSSSF ya kabla 1999, kukopa kutoka kwenye soko la ndani ili kupata fedha za kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na kulipa mikopo ya ndani iliyoiva.

98. Sehemu kubwa ya deni la ndani ilikuwa ni mikopo ya hati fungani ambayo ilikuwa ni asilimia 70.0 ya deni lote la ndani ikifuatiwa na dhamana za Serikali za muda mfupi asilimia 8.0, hati fungani maalum asilimia 15.0 na madeni mengine asilimia 7.0. **Kielelezo Na. 3.2** kinaonesha mwenendo wa deni la ndani.

Kielelezo Na. 3.2: Mwenendo wa Deni la Ndani



Deni la Ndani kwa Wakopeshaji

99. Hadi Machi 2022, benki za biashara ziliongoza kwa kuhodhi asilimia 35.2 ya deni la ndani ikilinganishwa na asilimia 39.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Aidha, mifuko ya hifadhi ya jamii ilihodhi asilimia 39.6 ikifuatiwa na kampuni za bima asilimia 7.6. **Jedwali Na. 3.2** linaonesha mchanganuo wa deni la ndani kwa wakopeshaji.

Jedwali Na. 3.2: Mchanganuo wa Deni la Ndani kwa Wakopeshaji hadi Machi 2022 (Shilingi Bilioni)

Taasisi	Machi 2019	Mchango kwa asilimia	Machi 2020	Mchango kwa asilimia	Machi 2021	Mchango kwa asilimia	Machi 2022	Mchango kwa asilimia
Benki za Biashara	4,866.3	42.4	5,346.5	40.7	5,600.7	39.2	6,606.6	35.2
Taasisi za Fedha	139.0	1.2	189.5	1.4	79.8	0.6	187.9	1.0
Mifuko ya Jamii	3,782.1	32.9	4,318.3	32.9	4,908.9	34.3	7,429.4	39.6
Kampuni za Bima	1,310.6	11.4	1,305.3	10.0	1,383.3	9.7	1,425.3	7.6
Taasisi za Kigeni	502.4	4.4	877.2	6.7	967.7	6.8	1,051.8	5.6
Mashirika Madogo	230.3	2.0	296.6	2.3	429.7	3.0	686.6	3.7
Watu binafsi	656.9	5.7	790.7	6.0	926.2	6.5	1,386.8	7.4
Jumla	**11,487.6**	**100**	**13,278.6**	**100**	**14,296.4**	**100**	**18,774.4**	**100**

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Tathmini ya Uhimilivu wa Deni

100. Tathmini ya Uhimilivu wa Deni iliyofanyika Novemba 2021 inaonesha kuwa deni ni himilivu kwa kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Katika tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa kwa mwaka 2021/22: Thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 18.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 132.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180 na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani ni asilimia 14.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 18. **Jedwali Na. 3.3** linaonesha viashiria vya uhimilivu wa deni la Serikali.

Jedwali Na. 3.3: Tathmini ya Viashiria vya Deni la Taifa

Viashiria vya deni la nje	2021/22	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26	2026/27	2031/32	Ukomo
Deni (PV(1))/Pato la Taifa	18.8	18.7	18.8	18.8	18.5	18.4	20.2	40
Deni (PV)/uuzaji wa bidhaa nje	132.9	117.4	108.5	102.8	96.9	93.7	95.7	180
Ulipaji wa deni la nje/Uuuzaji wa bidhaa nje	14.9	11.5	9.4	9.2	9.2	7.7	9.4	15
Ulipaji wa deni /Mapato ya ndani	14.2	12.1	10.6	10.9	11.3	9.6	12.1	18
Viashiria vya deni la nje na ndani	**2021/22**	**2022/23**	**2023/24**	**2024/25**	**2025/26**	**2026/27**	**2031/32**	**Ukomo**
Deni (PV)/ Pato la Taifa	31.8	31.8	31.5	30.7	29.4	29.0	20.2	55
Deni (PV)/ Mapato ya ndani	206.2	201.9	198.3	191.8	181.8	179.4	95.7	-
Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani	32.4	31.2	27.4	25.6	23.0	20.6	26.3	-

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipa

MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI

Jedwali Na. 22 **Shilingi milioni**

	2018/19 Halisi	2019/20 Halisi	2020/21 Halisi	2021/22 Bajeti	2021/22 Matokeo hadi Machi 2022	Matarajio hadi Juni 2022
A. MAPATO YA NDANI (yakijumuisha Halmashauri)	18,529,558.0	21,069,956.8	20,562,328.4	25,691,700.3	18,129,207.7	23,368,466.3
MAPATO YA NDANI	17,868,195.0	20,352,708.1	19,837,680.3	24,827,842.3	17,453,344.7	22,512,373.2
1. Mapato yayayokusanywa na TRA	15,511,330.1	17,622,822.1	17,624,454.4	21,778,068.5	15,630,736.9	20,036,056.7
Ushuru wa Forodha na Excise Duty	3,585,509.0	3,781,641.1	4,042,533.8	4,623,250.2	3,280,962.3	4,374,616.4
Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)	4,781,633.0	5,184,322.0	5,217,889.3	6,208,062.7	4,643,865.6	5,892,494.6
Bidhaa toka nje	2,259,827.4	2,421,392.8	2,584,453.5	3,039,437.9	2,494,385.5	3,026,521.1
Bidhaa za ndani	2,521,805.6	2,762,929.2	2,633,435.8	3,168,624.7	2,149,480.1	2,865,973.5
Kodi ya Mapato	5,148,191.5	6,523,795.2	6,015,898.2	6,846,549.3	5,738,905.3	7,039,723.8
Mapato mengine	2,130,594.5	2,379,568.6	2,570,987.9	4,362,255.9	2,766,130.9	3,688,174.6
Marejesho (Refunds Accounts)	(134,597.9)	(246,504.8)	(222,854.8)	(262,049.6)	(799,127.2)	(958,952.6)
2. Maduhuli	2,356,864.9	2,729,886.0	2,213,225.8	3,049,773.8	1,822,607.8	2,476,316.5
3. Mapato ya Halmashauri	661,363.0	717,248.7	724,648.2	863,858.0	675,863.0	856,093.1
B. JUMLA YA MATUMIZI	22,300,627.4	23,509,931.6	26,545,124.7	31,778,875.5	23,199,166.8	29,266,833.6
1. Matumizi ya Kawaida	13,806,788.9	14,201,147.8	14,883,722.6	16,801,260.4	12,461,600.0	16,297,222.6
2. Matumizi ya Maendeleo	8,493,838.5	9,308,783.8	11,661,402.2	14,977,615.1	10,737,566.8	12,969,611.0
Fedha za ndani	6,535,879.2	6,840,103.8	9,238,505.0	12,033,639.0	8,444,400.0	10,039,453.3
Fedha za nje	1,957,959.3	2,468,679.9	2,422,897.2	2,943,976.1	2,293,166.8	2,930,157.6
C. NAKISI/ SALIO (A-B)	(3,771,069.4)	(2,439,974.8)	(5,982,796.3)	(6,087,175.2)	(5,069,959.1)	(5,898,367.3)
D. KUZIBA NAKISI	20,169,133.4	12,927,807.7	5,982,796.3	6,087,175.2	5,069,959.1	6,872,341.0
1. Fedha kutoka nje	18,141,626.6	13,841,819.9	3,327,302.6	4,248,379.0	3,533,960.4	4,900,570.0
Ruzuku	4,767,182.0	17,759,598.0	520,635.8	915,506.3	476,049.6	634,732.8
Basket support	6,015,898.2	-	175,363.7	222,570.0	50,404.8	67,206.3
Mikopo ya uagizaji bidhaa/OGL	7,788,877.2	(3,711,564.0)	287,345.5	1,358,439.0	1,317,410.3	1,756,547.1
Mikopo ya miradi	-	-	1,649,790.8	1,758,111.0	1,812,138.8	2,416,185.1
Mikopo ya masharti ya kibiashara	1,144,822.3	1,822,093.1	3,121,190.2	3,045,106.9	1,639,657.8	2,492,279.9
Kulipia madeni ya nje (Amortization Foreign)	(1,575,153.1)	(2,028,307.3)	(2,427,023.4)	(3,051,354.3)	(1,761,700.9)	(2,466,381.2)
2. Fedha za Ndani	2,027,506.8	(914,012.1)	2,655,493.7	1,838,796.2	1,535,998.7	1,971,771.0
Mikopo isiyo ya mabenki	653,774.1	781,780.6	1,550,288.0	200,000.1	692,418.2	199,416.4
Mikopo ya mabenki	2,383,403.3	(404,856.6)	1,808,932.4	1,638,796.2	609,000.3	1,631,308.7
Mikopo ya ndani (Rollover)	3,718,008.3	3,976,811.2	3,262,551.9	3,150,336.7	2,612,099.1	3,482,798.9
Marekebisho (Adjustment to Cash)	(1,009,670.7)	(1,275,185.8)	(696,408.7)	-	234,582.4	141,048.0
Kulipia madeni ya ndani (amortization)	(3,718,008.3)	(3,976,811.2)	(3,262,551.9)	(3,150,336.7)	(2,612,099.1)	(3,482,798.9)
Expenditure float	-	(15,750.3)	(7,318.0)	-	(2.2)	(2.2)

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Kielelezo Na. 3.3: MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI



MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI

Jedwali Na. 23 **Shilingi Milioni**

Fungu	Maelezo	2020/21 (Halisi)			2021/22 (Bajeti)			2022/23 (Makadirio)		
		Matumizi ya Kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya Kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya Kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla
701	**Huduma za Kawaida**	**9,923,535.4**	**3,542,661.0**	**13,466,196.4**	**14,222,806.9**	**6,722,497.5**	**20,945,304.5**	**14,403,507.3**	**7,738,908.6**	**22,142,415.9**
70111	Utawala na Shughuli za Bunge	670,014.4	91,956.6	761,970.9	927,823.9	104,934.5	1,032,758.4	8,529,344.4	654,587.6	9,183,932.0
70112	Fedha na Masuala ya Kodi	656,063.4	683,214.0	1,339,277.4	939,618.3	2,241,513.9	3,181,132.2	1,217,361.0	1,431,831.6	2,649,192.6
70113	Mambo ya Nje	97,379.9	0.0	97,379.9	160,207.8	0.0	160,207.8	151,234.4	0.0	151,234.4
70121	Misaada ya Kiuchumi kutoka Nje	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70122	Misaada ya Kiuchumi kupitia Mashirika ya Kimataifa	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70131	Huduma za Umma	109,102.6	37,205.6	146,308.1	52,363.0	17,292.0	69,655.0	50,927.3	10,858.9	61,786.2
70132	Huduma za Mipango na Takwimu	336,003.0	1,012,843.2	1,348,846.2	439,621.9	2,497,367.3	2,936,989.3	422,442.1	1,904,750.2	2,327,192.3
70133	Huduma nyingine za Kawaida	93,281.5	1,000,379.9	1,093,661.3	120,250.7	1,715,341.3	1,835,592.0	115,723.8	3,508,577.6	3,624,301.4
70140	Utafiti wa Msingi	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70150	Utafiti na Maendeleo Huduma za Umma	320.5	20,729.4	21,049.9	270.4	35,013.3	35,283.7	291.4	17,984.1	18,275.5
70160	Huduma za Umma zisizotajwa hapo Juu	11,654.8	594,620.3	606,275.0	15,549.9	23,472.6	39,022.5	13,751.5	6,146.9	19,898.4
70170	Deni la Taifa	7,455,051.2	0.0	7,455,051.2	10,699,720.4	0.0	10,699,720.4	1,851,275.6	0.0	1,851,275.6
70180	Uhamishaji Fedha Ndani ya Serikali	494,664.1	101,712.2	596,376.3	867,380.7	87,562.5	954,943.2	2,051,155.8	204,171.6	2,255,327.4
702	**Ulinzi**	**1,652,667.8**	**902,029.5**	**2,554,697.3**	**2,166,148.9**	**306,488.5**	**2,472,637.4**	**2,046,522.3**	**154,643.0**	**2,201,165.3**
70210	Huduma za Ulinzi wa Kijeshi	1,652,454.2	555,924.7	2,208,378.9	2,165,840.2	83,707.9	2,249,548.0	2,045,766.4	57,494.6	2,103,261.0
70220	Huduma za Ulinzi wa Kiraia	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70230	Misaada ya Nje ya Ulinzi	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70240	Utafiti na Maendeleo ya Ulinzi	213.6	346,104.8	346,318.4	308.8	222,780.6	223,089.4	755.9	97,148.4	97,904.3
70250	Huduma za Ulinzi zisizotajwa hapo Juu	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
703	**Usalama wa Raia**	**706,325.8**	**307,140.0**	**1,013,465.8**	**834,534.4**	**132,555.3**	**967,089.7**	**837,354.7**	**108,136.3**	**945,491.0**
70310	Huduma za Polisi	503,138.2	53,047.9	556,186.1	319,855.0	4,576.9	324,431.9	304,477.3	26,077.0	330,554.3
70320	Huduma za Zimamoto	25,447.4	18,295.8	43,743.1	36,693.5	8,009.6	44,703.1	35,416.1	8,117.4	43,533.5
70330	Mahakama	116,169.4	152,455.3	268,624.7	191,882.9	102,027.4	293,910.2	182,887.5	55,982.6	238,870.1
70340	Magereza	47,187.9	83,340.9	130,528.8	43,107.0	17,941.4	61,048.4	95,547.0	17,468.8	113,015.8
70350	Huduma za utafiti na Maendeleo Usalama wa Raia	21.6	0.0	21.6	79.3	0.0	79.3	75.6	0.0	75.6
70360	Huduma Usalama wa Raia zisizotajwa hapo juu	14,361.5	0.0	14,361.5	242,916.8	0.0	242,916.8	218,951.3	490.5	219,441.8
704	**Shughuli za Kiuchumi**	**340,330.3**	**6,969,948.0**	**7,310,278.3**	**870,236.1**	**5,890,241.6**	**6,760,477.7**	**986,007.9**	**5,020,893.6**	**6,006,901.6**
70411	Shughuli za Kiuchumi na Biashara	24,235.4	76,579.1	100,814.5	39,141.6	39,137.6	78,279.2	106,093.6	13,830.1	119,923.7
70412	Masuala ya Kazi	5,917.7	29,079.2	34,996.9	9,259.6	24,147.3	33,406.9	9,202.5	66,326.6	75,529.1
70421	Kilimo	125,207.1	235,748.1	360,955.2	228,123.8	340,176.9	568,300.8	311,908.4	339,713.6	651,622.0
70422	Misitu	14,448.2	0.0	14,448.2	23,056.0	343.3	23,399.3	30,134.4	6,105.6	36,240.1
70423	Uvuvi na Uwindaji	28,105.3	16,551.4	44,656.6	362,772.7	438,199.4	800,972.1	309,444.5	184,044.1	493,488.6
70431	Makaa ya Mawe na Nishati nyingine	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70432	Petroli na Gesi Asilia	14,432.7	0.0	14,432.7	19,299.0	0.0	19,299.0	17,764.7	0.0	17,764.7
70433	Nishati ya Nyukilia	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70434	Nishati nyingine	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70435	Umeme	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70436	Nishati isiyo ya umeme	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70441	Uchimbaji Madini yasiyo Nishati	0.0	62,223.6	62,223.6	0.0	34,326.7	34,326.7	0.0	2,203,047.6	2,203,047.6
70442	Uzalishaji Viwandani	8,994.4	25,921.4	34,915.7	11,888.0	44,712.7	56,600.7	14,645.6	39,663.2	54,308.8
70443	Ujenzi	10,489.2	134,865.6	145,354.8	15,019.6	199,073.0	214,092.7	14,196.3	61,084.5	75,280.8
70451	Usafiri wa Barabara	14,012.3	0.0	14,012.3	19,802.0	0.0	19,802.0	18,811.6	0.0	18,811.6
70452	Usafiri wa Majini	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70453	Usafiri wa Reli	63,890.3	6,182,249.6	6,246,139.9	83,005.6	4,146,860.9	4,229,866.6	71,038.2	1,785,059.9	1,856,098.1
70454	Usafiri wa Anga	28.2	0.0	28.2	255.9	0.0	255.9	267.0	0.0	267.0
70455	Usafirishaji kwa njia ya Bomba na njia nyingine za usafiri	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70460	Mawasiliano	2,050.6	50,804.1	52,854.7	2,736.4	552,431.2	555,167.6	19,455.6	208,319.6	227,775.2
70471	Huduma za Biashara na Utunzaji Mizigo	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0

Jedwali Na. 23 Linaendelea

70472	Hoteli na Migahawa	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70473	Utalii	10,076.0	0.0	10,076.0	19,607.0	1,601.9	21,208.9	16,706.3	67,274.0	83,980.3
70474	Miradi ya Maendeleo	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70481	Utafiti katika shughuli za Kiuchumi, Biashara na Kazi	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70482	Utafiti na Maendeleo ya Kilimo, Misitu, Uvuvi na	28.5	0.0	28.5	285.8	0.0	285.8	182.2	0.0	182.2
70483	Utafiti na Maendeleo ya Mafuta na Nishati	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70484	Utafiti na Maendeleo ya Uchimbaji Madini, Uzalishaji Viwandani na Ujenzi	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70485	Utafiti na Maendeleo ya Usafiri	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70486	Utafiti na Maendeleo ya Mawasiliano	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70487	Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Vingine	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70490	Shughuli nyingine za Kiuchumi zisizotajwa hapo juu	18,414.4	155,925.9	174,340.3	35,983.0	69,230.5	105,213.5	46,157.1	46,424.8	92,581.9
705	**Hifadhi ya Mazingira**	**6,467.4**	**341.0**	**6,808.4**	**11,905.8**	**1,144.2**	**13,050.0**	**18,245.6**	**3,896.0**	**22,141.6**
70510	Hifadhi ya Taka	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70520	Hifadhi ya Maji Taka	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70530	Kupunguza Uharibifu wa Mazingira	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70540	Hifadhi ya Viumbehai na Mazingira	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70550	Utafiti na Maendeleo ya Hifadhi ya Mazingira	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70560	Huduma nyingine za Hifadhi ya Mazingira zisizotajwa hapo juu	6,467.4	341.0	6,808.4	11,905.8	1,144.2	13,050.0	18,245.6	3,896.0	22,141.6
706	**Nyumba na Huduma za Jamii**	**119,066.8**	**109,167.2**	**228,234.0**	**109,692.3**	**373,592.0**	**483,284.3**	**162,652.4**	**533,986.2**	**696,638.7**
70610	Maendeleo ya Nyumba	81,553.1	28,623.3	110,176.3	59,236.2	67,624.4	126,860.6	60,336.2	21,403.8	81,740.0
70620	Maendeleo ya Jamii	10,485.3	11,290.4	21,775.7	5,052.0	198,396.0	203,448.0	51,712.1	79,002.8	130,714.9
70630	Usambazaji Maji	25,034.1	69,253.5	94,287.6	42,785.0	107,571.6	150,356.6	47,660.0	433,579.6	481,239.6
70640	Taa za Barabarani	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70650	Utafiti wa Nyumba na Maendeleo ya Jamii	101.2	0.0	101.2	133.3	0.0	133.3	88.3	0.0	88.3
70660	Nyumba na Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu	1,893.1	0.0	1,893.1	2,485.9	0.0	2,485.9	2,855.9	0.0	2,855.9
707	**Afya**	**804,455.0**	**1,044,928.7**	**1,849,383.7**	**1,220,318.3**	**969,865.8**	**2,190,184.1**	**1,628,843.4**	**646,501.9**	**2,275,345.3**
70711	Madawa	283.0	775,650.4	775,933.4	1,117.3	499,110.9	500,228.2	932.4	163,608.8	164,541.2
70712	Bidhaa nyingine za madawa	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70713	Huduma za Tiba na Vifaa vya Tiba	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70721	Huduma za Tiba za Jumla	248,402.5	85,299.1	333,701.6	362,848.6	162,820.9	525,669.5	283,272.2	57,084.3	340,356.5
70722	Huduma Maalumu za Tiba	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70723	Huduma za Meno	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70724	Huduma za Wakunga Wasaidizi	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70731	Huduma za Hospitali	159,000.3	2,548.1	161,548.5	69,626.6	12,918.3	82,544.8	70,355.6	6,169.8	76,525.4
70732	Huduma za Hospitali Maalumu	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70733	Huduma za Vifaa vya Kujifungulia Wajawazito	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70734	Huduma za Wakunga na Wakunga wa Jadi	259.7	0.0	259.7	662.4	0.0	662.4	559.8	0.0	559.8
70740	Huduma za Afya	174,345.8	119,111.1	293,456.9	262,612.3	294,215.2	556,827.4	844,176.6	122,912.1	967,088.6
70750	Utafiti na Maendeleo ya Huduma za Afya	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70760	Huduma za Afya zisizotajwa hapo juu	222,163.7	62,319.9	284,483.6	523,451.2	800.6	524,251.8	429,546.9	296,726.9	726,273.7
708	**Burudani, Utamaduni na Dini**	**20,674.0**	**22,391.2**	**43,065.2**	**31,161.1**	**46,833.1**	**77,994.2**	**12,416.1**	**14,494.5**	**26,910.7**
70810	Huduma za Burudani na Michezo	1,629.8	2,458.6	4,088.3	2,709.7	28,488.9	31,198.6	2,558.3	9,863.6	12,421.9
70820	Huduma za Utamaduni	6,316.1	1,541.3	7,857.3	10,420.4	4,611.2	15,031.6	9,631.5	4,630.9	14,262.4
70830	Huduma za Utangazaji na Uchapishaji	12,585.6	18,391.4	30,977.0	17,787.2	13,733.0	31,520.2	0.0	0.0	0.0
70840	Dini na Huduma nyingine za Kijamii	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70850	Utafiti na Maendeleo katika Burudani, Utamaduni na Dini	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70860	Huduma nyingine za Burudani, Utamaduni na Dini zisizotajwa hapo juu	142.6	0.0	142.6	243.9	0.0	243.9	226.3	0.0	226.3
709	**Elimu**	**2,656,469.5**	**371,142.3**	**3,027,611.8**	**3,322,036.1**	**539,768.5**	**3,861,804.6**	**5,581,998.4**	**858,727.1**	**6,440,725.6**
70911	Elimu ya Awali	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70912	Elimu ya Msingi	1,432,796.9	213,654.5	1,646,451.4	1,803,562.6	271,272.9	2,074,835.5	3,252,315.2	793,456.0	4,045,771.2
70921	Elimu ya Sekondari (Kidato cha I - IV)	844,502.8	18,982.2	863,484.9	1,027,418.5	66,444.5	1,093,863.0	1,901,883.3	14,684.8	1,916,568.1
70922	Elimu ya Sekondari (Kidato cha V - VI)	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70930	Elimu baada ya Sekondari isiyo ya Chuo Kikuu	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70941	Daraja la Awali Elimu ya Chuo Kikuu	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70942	Daraja linalofuata Elimu ya Chuo Kikuu	15,840.6	35,782.5	51,623.1	21,205.5	80,085.4	101,290.9	19,204.9	27,996.4	47,201.3
70950	Elimu isiyopambanuliwa	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70960	Huduma za Ziada kwa Elimu	363,329.3	102,723.1	466,052.4	469,849.5	121,965.6	591,815.1	408,595.0	22,589.9	431,185.0
70970	Utafiti na Maendeleo ya Elimu	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
70980	Huduma za Elimu zisizotajwa hapo juu	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
710	**Kinga ya Jamii**	**115,306.8**	**950,408.2**	**1,065,715.0**	**161,988.9**	**6,391.8**	**168,380.8**	**96,956.7**	**158,071.6**	**255,028.4**
71011	Ugonjwa	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
71012	Ulemavu	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
71020	Wazee	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
71030	Waathirika	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
71040	Familia na Watoto	108,042.8	3,047.3	111,090.1	150,214.2	3,416.9	153,631.1	87,049.1	150,431.6	237,480.8
71050	Ukosefu wa Ajira	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
71060	Nyumba	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
71070	Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
71080	Utafiti na Maendeleo ya Kinga ya Jamii	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
71090	Huduma za Kinga ya Jamii zisizotajwa hapo juu	7,264.0	947,360.9	954,624.9	11,774.7	2,975.0	14,749.7	9,907.6	7,640.0	17,547.6
7	**Jumla**	**16,345,298.8**	**14,220,157.1**	**30,565,455.9**	**22,950,828.9**	**14,989,378.3**	**37,940,207.3**	**25,774,505.0**	**15,238,258.9**	**41,012,763.9**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

SURA YA 4

SEKTA YA NJE

Bidhaa Zilizouzwa Nje

101. Mwaka 2021, thamani ya mauzo ya bidhaa nje iliongezeka kwa asilimia 6.0 na kufikia dola za Marekani milioni 6,755.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6,371.7 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa zisizo asilia hususani bidhaa za viwandani, mazao ya mbogamboga na bidhaa nyinginezo zikijumuisha mahindi na mpunga. Aidha, mauzo ya bidhaa zisizo asilia yalichangia asilimia 85.3 ya mauzo yote nje ya nchi.

Bidhaa Asilia

102. Mwaka 2021, thamani ya mauzo ya bidhaa asilia ilipungua kwa asilimia 22.3 na kufikia dola za Marekani milioni 627.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 808.1 mwaka 2020. Hii ilitokana na kupungua kwa thamani ya mauzo ya mazao ya tumbaku na korosho.

Korosho

103. Mwaka 2021, thamani ya mauzo ya korosho nje ilipungua kwa asilimia 55.8 hadi dola za Marekani milioni 159.0 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 359.6 mwaka 2020. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha korosho kilichouzwa nje kutoka tani 320,900 mwaka 2020 hadi tani 154,400 mwaka 2021. Hata hivyo, wastani wa bei ya korosho katika soko la dunia uliongezeka kwa asilimia 0.2 na kufikia dola za Marekani 1,123.4 kwa tani mwaka 2021 kutoka wastani wa dola za Marekani 1,120.6 kwa tani mwaka 2020.

Kahawa

104. Mwaka 2021, thamani ya mauzo ya kahawa nje iliongezeka kwa asilimia 6.9 na kufikia dola za Marekani milioni 155.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 145.2 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha kahawa kilichouzwa nje, ambapo tani 68,000 ziliuzwa mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 64,000 zilizouzwa mwaka 2020. Aidha, wastani wa bei ya kahawa katika soko la dunia uliongezeka kwa asilimia 25.3 na kufikia dola za Marekani 2,601.8 kwa tani mwaka 2021 kutoka wastani wa dola za Marekani 2,076.4 kwa tani mwaka 2020.

Pamba

105. Mwaka 2021, thamani ya mauzo ya pamba nje ilikuwa dola za Marekani milioni 81.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 87.5 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 7.1. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa kiasi cha pamba kilichouzwa nje hadi kufikia tani 48,800 mwaka 2021 kutoka tani 72,600 mwaka 2020. Hata hivyo, wastani wa bei ya pamba katika soko la dunia uliongezeka kwa asilimia 71.9 na kufikia

dola za Marekani 1,677.7 kwa tani mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 1,206.4 kwa tani mwaka 2020.

Katani

106. Mwaka 2021, thamani ya mauzo ya katani nje iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 20.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 17.6 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 15.0. Hii ilichangiwa na kupanda kwa bei ya katani katika soko la dunia pamoja na kuongezeka kwa kiasi cha katani kilichouzwa nje. Kiasi cha katani kilichouzwa nje kiliongezeka kwa asilimia 12.5 na kufikia tani 12,600 mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 11,200 zilizouzwa mwaka 2020. Vilevile, wastani wa bei ya katani katika soko la dunia uliongezeka na kufikia dola za Marekani 1,613.5 kwa tani mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 1,566.2 kwa tani mwaka 2020.

Chai

107. Mwaka 2021, thamani ya mauzo ya chai nje ilikuwa dola za Marekani milioni 32.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 32.4 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 1.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha chai kilichouzwa nje kutoka tani 24,100 mwaka 2020 hadi tani 24,200 mwaka 2021. Hata hivyo, wastani wa bei ya chai katika soko la dunia ulishuka kwa asilimia 3.3 na kufikia dola za Marekani 1,301.4 kwa tani mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 1,345.5 kwa tani mwaka 2020.

Tumbaku

108. Mwaka 2021, thamani ya mauzo ya tumbaku nje ilipungua kwa asilimia 14.3 na kufikia dola za Marekani milioni 127.5 mwaka 2021 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 148.7 mwaka 2020. Hii ilichangiwa na kupungua kwa kiasi cha tumbaku kilichouzwa nje kutoka tani 42,600 mwaka 2020 hadi tani 37,700 mwaka 2021. Hata hivyo, wastani wa bei ya tumbaku katika soko la dunia uliongezeka kwa asilimia 1.3 hadi dola za Marekani 3,538.4 kwa tani mwaka 2021 ikilinganishwa na dola za Marekani 3,494.2 kwa tani mwaka 2020.

Bidhaa Zisizo Asilia

109. Mwaka 2021, thamani ya mauzo nje ya bidhaa zisizo asilia iliongezeka kwa asilimia 9.7 na kufikia dola za Marekani milioni 5,763.0 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,253.3 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za viwandani, mbogamboga na bidhaa nyinginezo zinazojumuisha nafaka.

Madini

110. Mwaka 2021, thamani ya mauzo ya madini nje ilipungua kwa asilimia 7.9 hadi dola za Marekani milioni 3,103.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,369.1 mwaka 2020. Hii ilitokana na kupungua kwa mauzo ya dhahabu na madini mengine.

Thamani ya mauzo ya dhahabu ilipungua kwa asilimia 7.2 na kufikia dola za Marekani milioni 2,743.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,957.5 mwaka 2020. Hii ilitokana na kupungua kwa uzalishaji wa dhahabu ambapo uzalishaji katika migodi mikubwa ilipungua kutoka tani 44.8 mwaka 2020 hadi tani 39.7 mwaka 2021. Hata hivyo, bei ya dhahabu katika soko la dunia iliongezeka kutoka wastani wa dola za Marekani 1,770.3 kwa wakia moja mwaka 2020 hadi wastani wa dola za Marekani 1,799.6 kwa wakia moja mwaka 2021. Aidha, mapato ya mauzo ya madini yalichangia asilimia 53.8 ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia na mauzo ya dhahabu yalichangia asilimia 88.4 katika mauzo ya madini mwaka 2021.

Bidhaa za Viwandani

111. Mwaka 2021, thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani iliongezeka kwa asilimia 33.5 na kufikia dola za Marekani milioni 1,213.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 908.6 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za viwandani nje hususani chuma na bidhaa za chuma, saruji, vioo na bidhaa za vioo, marumaru, vipodozi na bidhaa za plastiki. Aidha, mauzo ya bidhaa za viwandani yalichangia asilimia 21.1 ya mauzo yote ya bidhaa zisizo asilia mwaka 2021.

Samaki na Mazao ya Samaki

112. Mwaka 2021, thamani ya mauzo ya samaki na mazao yake nje ilikuwa dola za Marekani milioni 164.3 ikilinganishwa na mauzo ya dola za Marekani milioni 139.6 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 17.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha samaki na mazao ya samaki kilichouzwa nje.

Mbogamboga na Maua

113. Mwaka 2021, thamani ya mauzo ya mbogamboga na maua iliongezeka kwa asilimia 36.1 na kufikia dola za Marekani milioni 373.0 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 274.1 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya matunda na mbogamboga nje hususani katika nchi jirani.

Bidhaa Nyinginezo Zilizouzwa Nje

114. Mwaka 2021, thamani ya bidhaa nyinginezo zilizouzwa nje ilikuwa dola za Marekani milioni 819.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 474.2 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 72.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya mchele nje na kufikia dola za Marekani milioni 301.9 mwaka 2021 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 143.7 mwaka 2020. Bidhaa zinazojumuishwa katika kundi hili ni pamoja na mbegu za mafuta, kakao, ngozi, maharage na nafaka kama mahindi, mchele na mtama ambapo sehemu kubwa ya bidhaa hizo ziliuzwa nchi jirani.

Jedwali Na. 4.1: Thamani, Kiasi na Bei ya Bidhaa Zilizouzwa Nje Mwaka 2017 -2021

Bidhaa	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
Bidhaa Asilia (US$ milioni)						
Kahawa						
Thamani (US$ milioni)	126.3	148.4	152.2	145.2	155.2	6.9
Kiasi ('000 tani)	41.8	56.3	76.2	64	68	6.2
Bei (US$ kwa tani)	3,019.2	2,633.0	1,996.5	2,076.4	2,601.8	14.7
Pamba						
Thamani (US$ milioni)	36.8	69.2	91.8	87.5	81.3	-7.1
Kiasi ('000 tani)	25.3	47.4	79	72.6	48.8	-32.7
Bei (US$ kwa tani)	1,450.3	1,461.1	1,162.2	1,206.4	1,677.7	39.1
Katani						
Thamani (US$ milioni)	28.7	18.8	19.3	17.6	20.2	15
Kiasi ('000 tani)	17	12.3	12.2	11.2	12.6	12.5
Bei (US$ kwa tani)	1,686.7	1,535.6	1,581.7	1,566.2	1,613.5	3
Chai						
Thamani (US$ milioni)	49.1	46.5	45.7	32.4	32.9	1.4
Kiasi ('000 tani)	27.5	26.9	31.7	24.1	24.2	0.6
Bei (US$ kwa tani)	1,783.6	1,727.4	1,444.2	1,345.5	1,301.4	-3.3
Tumbaku						
Thamani (US$ milioni)	195.8	273.5	146.5	148.7	127.5	-14.3
Kiasi ('000 tani)	48.3	75	42.6	42.6	37.7	-11.4
Bei (US$ kwa tani)	4,055.6	3,648.6	3,440.9	3,494.2	3,538.4	1.3
Korosho						
Thamani (US$ milioni)	529.7	110.8	353.1	359.6	159	-55.8
Kiasi ('000 tani)	329.5	70.1	295.6	320.9	154.4	-51.9
Bei (US$ kwa tani)	1,607.5	1,580.6	1,194.6	1,120.6	1,123.4	0.2
Karafuu						
Thamani (US$ milioni)	55.4	0.4	9.1	17.1	51.8	203.2
Kiasi ('000 tani)	7	0.1	1.8	3.6	7	96.8
Bei (US$ kwa tani)	7,865.1	4,384.6	5,047.8	4,770.0	5,493.2	15.2
Jumla (Bidhaa Asilia)	1,021.80	667.5	817.7	808.1	627.9	-22.3
Bidhaa Zisizo Asilia (US$ millioni)						
Madini	1,694.5	1,634.2	2,326.7	3,369.1	3,103.2	-7.9
Dhahabu	1,541.1	1,541.9	2,215.1	2,957.5	2,743.1	-7.2
Almasi	64.4	82.7	81.3	20.2	8.5	-57.9
Madini mengine	88.9	9.6	30.3	391.3	351.5	-10.2
Bidhaa za Viwandani	676.3	826.8	851.8	908.6	1,213.2	33.5
Nyuzi za Pamba	16.1	17	6.7	6.9	5	-27.4
Kahawa iliyozalishwa	1.2	3.3	1.4	5.2	16.3	214.9
Tumbaku iliyozalishwa	22.3	21.9	24.5	18.3	32	75.3
Mazao ya Katani	26.3	20.9	23.4	23.2	33.6	44.6
Mazao mengine ya Viwandani	610.4	763.7	795.9	855	1,126.3	31.7
Samaki na Mazao ya Samaki	193	160	168	139.6	164.3	17.7
Mazao ya Mboga na Maua	148.7	176.8	202.4	274.1	373	36.1
Bidhaa zilizouzwa tena (re-exports)	143.2	197.8	242.8	87.7	90.2	2.9
Bidhaa nyinginezo	223.3	239.3	394.3	474.2	819.1	72.7
Jumla (Bidhaa zisizo Asilia)	**3,078.9**	**3,234.9**	**4,186.0**	**5,253.3**	**5,763.0**	**9.7**
Bidhaa zisizo rekodiwa	410.1	390.2	373.8	310.4	364.8	17.5
Jumla Kuu (Bidhaa Zote)	**4,510.8**	**4,292.7**	**5,377.6**	**6,371.7**	**6,755.6**	**6.0**

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

Mapato ya Huduma

115. Mwaka 2021, mapato yatokanayo na biashara ya huduma yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 3,151.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,183.8 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 44.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma za utalii pamoja na huduma za usafirishaji. Mapato yatokanayo na huduma za safari za utalii yaliongezeka kwa asilimia 96.3 na kufikia dola za Marekani milioni 1,402.5 mwaka 2021 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni

714.5 mwaka 2020. Aidha, mapato yatokanayo na huduma ya usafirishaji yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 1,415.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,281.7 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 10.5. Hii ilitokana na kuanza kuongezeka kwa shughuli za kitalii na usafirishaji nchini kufuatia nchi mbalimbali duniani kulegeza masharti ya kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya UVIKO - 19 ikiwemo kuruhusu safari za anga na kufungua mipaka.

Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi

116. Mwaka 2021, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 10,018.7 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 7,889.1 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 27.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji, bidhaa za kati pamoja na bidhaa za matumizi ya kawaida.

Bidhaa za Kukuza Mitaji

117. Mwaka 2021, thamani ya bidhaa za kukuza mitaji zilizoingizwa nchini iliongezeka kwa asilimia 19.6 na kufikia dola za Marekani milioni 3,850.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,220.8 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya vifaa vya usafirishaji, mitambo, majengo na ujenzi vilivyoingizwa nchini kufuatia kuongezeka kwa mahitaji ya vifaa hivyo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Bidhaa za Kati

118. Mwaka 2021, thamani ya bidhaa za kukuza mitaji zilizoingizwa nchini iliongezeka kwa asilimia 19.6 na kufikia dola za Marekani milioni 3,850.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,220.8 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya vifaa vya usafirishaji, mitambo, majengo na ujenzi vilivyoingizwa nchini kufuatia kuongezeka kwa mahitaji ya vifaa hivyo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Bidhaa za Matumizi ya Kawaida

119. Mwaka 2021, thamani ya bidhaa za matumizi ya kawaida zilizoagizwa kutoka nje ilikuwa dola za Marekani milioni 2,917.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,436.5 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 19.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa nyingine hususani dawa na vifaa tiba kwa ajili mapambano ya kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya UVIKO – 19 pamoja na bidhaa za vyakula ikiwemo ngano.

Malipo ya Huduma

120. Mwaka 2021, thamani ya malipo ya huduma iliongezeka kwa asilimia 33.0 na kufikia dola za Marekani milioni 1,719.0 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni

1,292.0 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa gharama ya malipo ya huduma za usafirishaji, utalii na huduma nyinginezo.

Jedwali Na. 4.2: Thamani ya Bidhaa Zilizoagizwa kutoka Nje Mwaka 2017 – 2021 (Dola za Marekani Milioni)

Bidhaa	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
Bidhaa za Kukuza Mitaji	**2,688.4**	**3,494.1**	**3,703.9**	**3,220.7**	**3,850.9**	19.6
Vifaa vya Usafirishaji	694.2	1,218.3	1,079.9	782.8	978.4	25.0
Majengo na Ujenzi	581.8	864.0	1,006.7	936.8	1,159.5	23.8
Mitambo	1,412.5	1,411.8	1,617.4	1,501.2	1,713.0	14.1
Bidhaa za Kati	**2,704.4**	**2,624.0**	**2,682.7**	**2,231.8**	**3,250.7**	45.7
Uagizaji Mafuta	1,850.6	1,658.8	1,793.8	1,281.3	2,084.5	62.7
Mbolea	124.9	181.4	129.9	186.3	189.4	1.7
Malighafi za Viwanda	728.9	783.8	759.0	764.2	976.8	27.8
Bidhaa za Matumizi ya Kawaida	**2,158.9**	**2,364.9**	**2,406.5**	**2,436.4**	**2,917.2**	19.7
Bidhaa za Vyakula	405.3	459.0	412.1	386.7	500.9	29.6
Bidhaa Nyingine	1,753.6	1,905.9	1,994.3	2,049.8	2,416.2	17.9
Jumla (FoB)	**7,551.7**	**8,483.1**	**8,793.1**	**7,889.0**	**10,018.7**	27.0

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

Mwenendo wa Biashara Baina ya Tanzania na Nchi Mbalimbali

121. Mwaka 2021, mahusiano ya kibiashara kati ya Tanzania na nchi mbalimbali duniani ikiwemo jumuiya za kikanda na kimataifa yaliendelea kuimarika. Katika kipindi hicho, bidhaa nyingi za Tanzania ziliuzwa katika nchi za Afrika Kusini ambayo ilichangia asilimia 16.46 ya mauzo yote ikifuatiwa na Uswisi (asilimia 15.78), Umoja wa Falme za Kiarabu (asilimia 14.34), India (asilimia 8.25) na Kenya (asilimia 6.22). Aidha, mazao ya nafaka (mahindi na mchele) na mbogamboga yaliuzwa Kenya; mbegu za mafuta, tumbaku, kahawa na korosho ziliuzwa katika nchi za China, India na Umoja wa Falme za Kiarabu; na dhahabu iliuzwa Afrika kusini, India na Uswisi.

Kielelezo Na. 4.1: Mchanganuo wa Masoko ya Bidhaa za Tanzania kwenda Nje ya Nchi Mwaka 2021 (Asilimia)



122. Mwaka 2021, thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC iliongezeka kwa asilimia 42.9 na kufikia dola za Marekani milioni 1,161.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 812.5 mwaka 2020. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za chai, mahindi, ngano, alizeti, mchele, maharagwe, mbogamboga, karatasi, bidhaa za chuma, marumaru, saruji, vioo na bidhaa za vioo, sabuni na vipodozi kwenda nchi ya Kenya.

123. Mwaka 2021, thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC ilipungua kwa asilimia 10.6 na kufikia dola za Marekani milioni 1,303.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,458.3 mwaka 2020. Hii ilitokana na kupungua kwa mauzo ya madini katika soko la SADC kufuatia kuanza kutumika kwa mitambo ya kuchenjua madini hapa nchini na hivyo kupunguza kiasi cha madini yaliyokuwa yakisafirishwa nje ya nchi kwa ajili ya uchenjuaji. Aidha, sehemu kubwa ya bidhaa ikiwemo madini, pamba, chai, kahawa, vigae, vyandarua, kemikali (methly bromide), petroleum coke, saruji, sabuni, na mafuta ya kupaka ziliuzwa katika nchi za Afrika Kusini (asilimia 70.3) na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (asilimia 15.9).

124. Mwaka 2021, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda katika soko la Ulaya ilipungua kwa asilimia 40.2 hadi dola za Marekani milioni 891.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,491.7 mwaka 2020. Hii ilitokana na kupungua kwa mauzo ya bidhaa za madini, samaki, mbogamboga na maua kwenda nchi za Uswisi, Ubelgiji, Uholanzi na Ujerumani.

125. Mwaka 2021, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za Bara la Asia ilikuwa dola za Marekani milioni 2,927.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,210.8 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 32.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo kwenda nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu, India na China.

Jedwali Na. 4.3: Mauzo ya Bidhaa Kwenda Nchi Mbalimbali Duniani Mwaka 2017 – 2021

JUMUIYA/NCHI	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI	510.5	758.5	720.6	1,472.50	867.1	-41.1
NCHI NYINGINE ZA ULAYA	26.2	29	18.6	19.2	24.3	26.5
JUMLA- BARA LA ULAYA	**536.7**	**787.5**	**739.2**	**1,491.7**	**891.5**	**-40.2**
AFRIKA						
JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA - SADC						
Afrika ya Kusini	693.3	750.7	971.6	1,161.6	916.7	-21.1
Zambia	48.3	66.4	63.6	54.1	68.6	26.8
Swaziland	0.5	2	5.9	0.1	0.1	150.1
Zimbabwe	8.3	9.3	18.8	21.1	14.9	-29.6
Msumbiji	13	9.7	32.6	21	15.5	-26.4
Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo	101.4	148	164.1	144.2	207.2	43.7
Nchi nyingine za SADc	89.7	79.6	74.3	56.2	80.4	43.2
Jumla - SADC	**954.6**	**1,065.8**	**1,330.9**	**1,458.3**	**1,303.4**	**-10.6**
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI - EAC						
Burundi	50.5	59.8	87.9	179.5	163.3	-9
Kenya	174.4	224.8	269.9	230.2	397.2	72.5
Rwanda	60.1	104.1	190.9	208.2	277.8	33.5
Uganda	104.9	119.1	123.7	191.3	314	64.2
Sudan ya Kusini	1	1.3	2	3.4	8.9	161.6
JUMLA-EAC	590.9	509.1	674.4	812.5	1,161.2	42.9
Nchi nyingine za Afrika	24.8	49.6	57.3	30.5	49.5	62.6
JUMLA-AFRIKA	**1,570.3**	**1,624.5**	**2,062.7**	**2,301.3**	**2,514.2**	**9.3**
BARA LA AMERIKA						
Marekani	61.7	67.4	52.4	47	39.1	-16.9
Canada	3.6	7	3.7	3.2	3.7	14.9
Nchi nyingine za bara la Amerika	98.7	5.9	8.1	2.6	1.8	-32.1
JUMLA - BARA LA AMERIKA	**164**	**80.3**	**64.2**	**52.8**	**44.5**	**-15.7**
BARA LA ASIA						
China	141	146.9	233.7	238.9	272.9	14.3
India	974.1	744.4	867.8	528.7	1,008.7	90.8
Japan	73.9	66.8	64.2	55.8	67.4	20.8
Umoja wa falme za kiarabu	87.3	109.2	395.1	754.9	1,051.7	39.3
Honkong	42.9	40.4	49.6	128.3	61.3	-52.2
Singapore	5.4	12.9	7.6	43.7	139.2	218.4
Nchi nyingine za Asia	811.8	277.2	497.7	460.5	326.5	-29.1
JUMLA-ASIA	**2,136.5**	**1,397.8**	**2,115.6**	**2,210.8**	**2,927.8**	**32.4**
Nchi nyinginezo	783.7	12.3	22	4.7	4.9	3.6
JUMLA KUU	**5,191.2**	**4,292.7**	**5,377.6**	**6,371.7**	**6,755.6**	**6.0**

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

126. Mwaka 2021, Tanzania iliagiza kwa wingi bidhaa kutoka nchi za China, Umoja wa Falme za Kiarabu, India, Saudi Arabia, Japan, na Afrika Kusini ambapo nchi hizo zilichangia asilimia 24.75, asilimia 12.48, asilimia 11.10 asilimia 6.19, asilimia 4.74 na asilimia 3.97 ya thamani ya bidhaa zote zilizoagizwa kutoka nje ya nchi mtawalia. Aidha, bidhaa zilizoagizwa kwa kiasi kikubwa zilikuwa ni pamoja na: mitambo, matrekta na bidhaa za kielektroniki kutoka China; mafuta ya petroli kutoka Saudi Arabia na Umoja wa Falme za Kiarabu; na magari na vyuma kutoka India na Afrika Kusini.

Kielelezo Na. 4.2: Mchanganuo wa Uagizaji wa Bidhaa Nchini Mwaka 2021 (Asilimia)



127. Mwaka 2021, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki ilikuwa dola za Marekani milioni 523.4 ikilinganishwa dola za Marekani milioni 324.3 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 61.4. Aidha, bidhaa zilizoagizwa kutoka Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 616.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 470.3 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 31.2. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kuimarika kwa mahusiano ya kibiashara miongoni mwa nchi wananchama wa EAC na SADC hususani kuongezeka kwa uagizaji kutoka nchi za Afrika Kusini na Kenya.

128. Mwaka 2021, thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka nchi za Bara la Asia uliongezeka kwa asilimia 34.3 na kufikia dola za Marekani milioni 7,725.0 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,753.0 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bidhaa za kukuza mtaji na bidhaa za matumizi ya kawaida zilizoagizwa kutoka katika nchi hizo kwa ajili ya mahitaji makubwa katika sekta ya ujenzi hususan miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa hapa nchini. Kwa upande Mwingine, thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka Jumuiya ya Ulaya ulipungua kwa asilimia 10.8 na kufikia dola za Marekani milioni 915.9 mwaka 2021 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,026.4 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuendelea kuimarika kwa upatikanaji wa bidhaa

zinazozalishwa hapa nchini ikiwemo bidhaa za ujenzi kama vile marumaru na bidhaa za chuma.

Jedwali Na. 4.4: Uagizaji wa Bidhaa Kutoka Nchi Mbalimbali Duniani Mwaka 2017 - 2021 (Dola za Marekani Milioni)

JUMUIYA/NCHI	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI	1,085.60	861.9	936	1,026.40	915.9	-10.8
NCHI NYINGINE ZA ULAYA	311.5	267.2	214.7	175.3	209.2	19.3
JUMLA - BARA LA ULAYA	**1,397.1**	**1,129.1**	**1,150.7**	**1,201.8**	**1,125.1**	**-6.4**
AFRIKA						
JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA - SADC						
Afrika ya Kusini	414.7	437.4	442	345.8	432.3	25
Zambia	53.7	51	47.6	51.2	70.4	37.7
Swaziland	37.1	38.5	48.8	26.4	39.6	50.2
Zimbabwe	1.1	1.2	1	4.7	9.9	112.5
Msumbiji	9.2	24.1	8.4	2.4	4.6	92.5
Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo	1	0.6	1.3	2.1	2.6	21
Nchi nyingine za SADc	45.6	51.7	49	37.8	57.4	51.8
JUMLA-SADC	**562.5**	**604.4**	**598**	**470.3**	**616.8**	**31.1**
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI - EAC						
Burundi	0.2	1	0.4	0.3	0.6	122.6
Kenya	201	247.8	268.3	247.7	410.9	65.9
Rwanda	1.3	1.4	1.5	2.2	2.2	-2.3
Uganda	34.1	52.7	60.3	74	109.7	48.1
Sudan ya Kusini	0	0.2	0	0	0.1	7227.8
JUMLA-EAC	**236.6**	**303**	**330.5**	**324.3**	**523.4**	**61.4**
Nchi nyingine za Afrika	88.6	83.8	55.9	63.6	69.9	10
JUMLA-AFRIKA	**887.7**	**991.2**	**984.4**	**858.2**	**1,210.2**	**41**
BARA LA AMERIKA						
Marekani	201.8	238	342.2	241.2	261.1	8.3
Canada	39.5	61.1	44.9	31	45.4	46.3
Nchi nyingine za bara la Amerika	95.3	15.3	16.8	11.1	15.9	43.1
JUMLA - BARA LA AMERIKA	**336.7**	**314.4**	**403.9**	**283.3**	**322.4**	**13.8**
BARA LA ASIA						
China	1,499.6	1,764.4	2,011.5	2,155.9	2,696.2	25.1
India	1,165.0	1,222.7	1,267.8	1,089.6	1,209.5	11
Japan	410.6	398.1	490.5	377	508.4	34.9
Umoja wa Falme za Kiarabu	592.2	871.5	954.7	824.3	1,359.50	64.9
Honkong	51.3	60.3	47.8	47.7	53.1	11.2
Singapore	61.5	30.4	66.2	30.8	82.2	166.7
Nchi nyingine za Asia	961	1,513.9	1,408.0	1,227.7	1,816.1	47.9
JUMLA-ASIA	**4,741.2**	**5,861.4**	**6,246.6**	**5,753.0**	**7,725.0**	**34.3**
Nchi nyinginezo	189.1	187.1	7.5	20.3	20.5	0.9
JUMLA KUU	**7,551.7**	**8,483.1**	**8,793.1**	**7,889.0**	**10,018.7**	**27.0**

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

Mizania ya Malipo na Nchi za Nje

Urari wa Malipo Yote

129. Mwaka 2021, urari wa malipo yote nje ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,852.1 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 764.9 mwaka 2020. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa ziada katika urari wa rasilimali fedha.

Urari wa Biashara ya Bidhaa

130. Urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 3,247.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,460.0 mwaka 2020, sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 122.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje hususani mafuta ya petroli. malighafi za viwandani na bidhaa za kukuza mtaji kufuatia kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji na ujenzi nchini pamoja na kupungua kwa thamani ya madini yaliouzwa nje.

Urari wa Biashara ya Huduma

131. Mwaka 2021, urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,434.7 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 864.7 mwaka 2020, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 65.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato yaliyotokana na shughuli za utalii na usafirishaji kufuatia kuimarika kwa uchumi wa dunia baada ya nchi mbalimbali kupunguza masharti ya kudhibiti maambukizi ya UVIKO - 19.

Urari wa Biashara ya Bidhaa na Huduma

132. Urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,813.0 mwaka 2021 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 595.2 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa nakisi katika biashara ya bidhaa.

Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi

133. Urari wa mapato ya vitega uchumi ambayo yanajumuisha kiasi cha malipo yatokanayo na ajira kwa wafanyakazi, mapato ya uwekezaji na malipo ya riba ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,218.0 mwaka 2021 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,264.5 mwaka 2020, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 3.7. Hii lilichangiwa na kupungua kwa malipo ya riba.

Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida

134. Mwaka 2021, urari wa uhamisho mali wa kawaida unaojumuisha uhamisho wa fedha unaofanywa na sekta binafsi, misaada na unafuu wa kulipa deni ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 565.3 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni

399.9 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 41.4. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo iliyoelekezwa kwenye miradi mbalimbali ya kisekta.

Urari wa Malipo ya Kawaida

135. Mwaka 2021, urari wa malipo ya kawaida unaojumuisha biashara ya bidhaa, huduma, mapato ya vitega uchumi na uhamisho mali wa kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,465.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,459.9 mwaka 2020, sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 68.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa nakisi ya biashara ya bidhaa na huduma.

Urari wa Uhamisho wa Mitaji

136. Urari wa uhamisho wa mitaji unaojumuisha misaada ya vitega uchumi na misamaha ya madeni ya nje kutoka kwa mashirika ya fedha ya kimataifa na nchi wahisani ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 417.9 mwaka 2021 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 385.8 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 8.3. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa misaada kwa ajili ya kukabiliana na athari hasi za UVIKO - 19.

Urari wa Rasilimali Fedha

137. Mwaka 2021, urari wa malipo katika rasilimali fedha unaojumuisha uwekezaji wa moja kwa moja na mikopo ya fedha kutoka nje ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 2,965.0 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 884.0 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji na mapato ya huduma.

Akiba ya Fedha za Kigeni

138. Mwaka 2021, akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa katika viwango vya kuridhisha na vyenye kukidhi mahitaji ya nchi ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Hadi Desemba 2021, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 6,386.0 kutoka dola za Marekani milioni 4,767.7 kipindi kama hicho mwaka 2020. Kiasi hicho kinatosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi ikijumuisha bidhaa za uwekezaji wa nje wa moja kwa moja kwa kipindi cha miezi 6.2 ambacho ni zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi isiyopungua 4.0. Aidha, kiwango hicho ni zaidi ya lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC la miezi isiyopungua 4.5 na lengo la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika - SADC la miezi isiyopungua 6.0. Ongezeko la akiba ya fedha za kigeni lilichangiwa na upatikanaji wa mkopo nafuu na usio na riba kutoka IMF wenye thamani ya dola za Marekani milioni 567.3.

Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania

139. Mwaka 2021, thamani ya shilingi ya Tanzania iliendelea kuwa imara na tulivu dhidi ya sarafu nyingine za washirika wa kibiashara duniani. Mwaka 2021, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,309.2 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,305.6 mwaka 2020. Hii ni sawa na kupungua kwa thamani kwa asilimia 0.16 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 0.25 mwaka 2020. Hii ilichangiwa na: mfumuko mdogo wa bei nchini; utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti; usimamizi imara katika kuhakikisha uwazi na utaratibu mzuri katika soko la kubadilisha fedha za kigeni; akiba ya kutosha ya fedha za kigeni; na mwendelezo wa nakisi ndogo ya urari wa biashara ya bidhaa na huduma. Kiwango hicho cha badiliko la thamani ya shilingi kilikuwa kidogo na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache duniani zilizoweza kuwa na utulivu wa kiwango cha ubadilishaji wa fedha za kigeni licha ya athari za UVIKO - 19.

THAMANI YA BIDHAA ZA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 24 **Shilingi Milioni**

Aina ya Bidhaa	2016	2017	2018	2019	2020r	2021
Zilizouzwa Nje	10,610,721	10,053,844	10,064,249.0	11,378,808.0	13,882,712.0	14,384,873.8
Bidhaa Halisi	9,303,457	8,779,726	8,307,170.0	10,824,002.0	13,673,643.3	14,178,681.4
Zilizouzwa Tena	422,502	319,086	422,733.0	554,806.0	209,068.6	206,192.4
Zilizoagizwa	18,425,925	16,831,696	18,789,124.0	20,939,079.0	19,631,817.9	24,916,297.0
Jumla	29,036,647	26,885,540	28,853,373.0	32,317,886.0	33,514,529.9	39,301,170.8
Urari	-7,815,204	-6,777,852	-8,724,875.0	-9,560,271.0	-5,749,106.0	-10,531,423.2

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
r -Takwimu zimeboreshwa

KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE YA NCHI

Jedwali Na. 25

Bidhaa	Kiasi (000" Tani)						Thamani (shilingi Milioni)					
	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko (2021/20) Asilimia	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko (2021/20) Asilimia
Kahawa	42.1	58.0	78.1	64.0	68.0	6.2	282,427	337,459	349,423	331,453	354,768	7.0
Pamba	25.0	50.7	82.3	72.6	48.8	-32.7	80,259	157,151	212,310	199,823	185,917	-7.0
Katani	16.3	12.0	13.8	11.2	12.6	12.5	57,703	46,925	53,829	40,071	46,126	15.1
Chai	27.5	26.9	31.7	24.1	24.2	0.6	108,990	103,341	104,044	73,987	75,173	1.6
Tumbaku	48.3	72.2	46.3	42.6	37.7	-11.4	434,456	609,677	389,502	339,428	291,367	-14.2
Korosho	331.1	77.1	296.8	320.9	154.4	-51.9	1,200,450	287,891	821,945	824,634	363,012	-56.0
Karafuu	6.9	0.1	1.8	3.6	7.0	96.8	121,237	684	20,807.4	38,915.6	118,412.6	204.3
Almasi (Carat)	282,032.1	408,655.9	590,000.0	154,331.1	47,430.0	-69.3	142,998	184,233	184,967	46,080	19,443	-57.8
Dhahabu (gms)	54,660,377	60,784,383	81,098,466	66,871,114.9	59,392,496.2	-11.2	3,418,902	3,435,639	5,043,077	6,752,407	6,257,279	-7.3

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mapato Tanzania

KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NJE YA NCHI

Jedwali Na. 26

Bidhaa	Kiasi (000" Tani)						Badiliko 2020/21 Asilimia	Thamani (Milioni US$)						Badiliko 2020/21 Asilimia
	2016	2017	2018	2019	2020r	2021		2016	2017	2018	2019	2020r	2021	
Bidhaa Asilia:														
Kahawa	58.7	41.8	56.6	76.2	64	68.0	6.2	153.7	126.3	147.9	152.2	145.2	155.2	6.9
Pamba	33	25.3	47.4	79	72.6	48.8	-32.7	46.8	36.8	68.4	91.8	87.5	81.3	-7.1
Katani	8.6	17	20.3	12.2	11.2	12.6	12.6	17.2	28.7	32.5	19.3	17.6	20.2	14.6
Chai	26.3	27.5	26.9	31.7	24.1	24.2	0.6	44.8	49.1	45.9	45.7	32.4	32.9	1.5
Tumbaku	74.3	48.3	72.2	42.6	42.6	37.7	-11.5	339.2	195.8	270.3	146.5	148.7	127.5	-14.3
Korosho	217.5	329.4	120.2	295.6	320.9	154.4	-51.9	320.2	529.6	196.5	353.1	359.6	159.0	-55.8
Karafuu	4.9	6.9	1.3	1.8	3.6	7.0	95.8	39.3	54.4	10.5	9.1	17.1	51.8	202.8
Jumla								**961.2**	**1,020.7**	**772.1**	**817.7**	**808.1**	**627.9**	**-22.3**
Bidhaa zisizo asilia:														
Madini								1,930.0	1,694.5	1,615.3	2,326.7	3,369.1	3,103.17	-7.9
Bidhaa za Viwanda								714.2	693.7	794.6	851.8	908.6	1,213.2	33.5
Samaki na Mazao ya Samaki								143.7	193	158.4	168	139.6	164.3	17.7
Mazao ya Mboga na Maua								24.8	27.2	33	202.4	274.1	373.0	36.1
Bidhaa zilizouzwa tena								187.7	126.5	175.6	242.8	87.7	90.2	2.8
Bidhaa nyinginezo								538.1	357.1	432.5	394.3	474.2	819.1	72.7
Jumla								**3,538.5**	**3,091.9**	**3,209.3**	**4,186.0**	**5,253.3**	**5,762.95**	**9.7**
Bidhaa Zisizorekodiwa								450	411.3	398.1	373.8	310.4	364.8	**17.5**
Jumla Kubwa								**4,949.7**	**4,523.9**	**4,379.6**	**5,377.6**	**6,371.7**	**6,755.64**	**6.0**

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na Mamlaka ya Mapato Tanzania

Kielelezo Na. 4.3: MWENENDO WA THAMANI YA BIDHAA ASILIA NA ZISIZO ASILIA ZILIZOUZWA NJE YA NCHI



Kielelezo Na. 4.4: BIDHAA ASILIA NA ZISIZO ASILIA ZILIZOUZWA NJE YA NCHI MWAKA 2021



WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE YA NCHI

Jedwali Na. 27

Shilingi/Tani*

Bidhaa	2015	2016	2017	2018	2019	2020r	2021	Badiliko (Asilimia)
kahawa	6,084,327	5,563,694	6,703,080	5,818,259	4,585,610	5,178,939	5,217,177	0.7
Pamba	2,164,592	3,080,982	3,210,269	3,099,625	2,690,875	2,753,527	3,806,866	38.3
Katani	3,554,124	2,473,086	3,539,730	3,910,417	3,901,618	3,575,866	3,657,568	2.3
Chai	3,139,968	3,543,747	3,956,329	3,841,673	3,292,541	3,070,579	3,101,340	1.0
Tumbaku	8,576,002	10,259,213	8,998,738	8,444,280	9,143,243	7,975,654	7,727,540	-3.1
Korosho	2,503,867	3,422,830	3,625,943	3,733,995	2,759,651	2,570,147	2,351,759	-8.5
Karafuu	17,576,080	30,707,266	17,570,634	6,840,000	16,005,679	10,868,651	16,801,625	54.6
Almasi (carat)	353,123	789,375	507,027	205,594	313,503	298,578	409,930	37.3
Dhahabu (gramu)	56,146	37,674	62,548	56,522	62,185	100,976	105,355	4.3

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania
* isipokuwa kwa almasi na dhahabu
r – Takwimu zimeboreshwa

WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE YA NCHI

Jedwali Na. 28 **USD/Tani**

Bidhaa	2016	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko 2021/20 Asilimia
Kahawa	2,557	3,019	2,584	2,017	2,269	2,602	14.7
Pamba	1,416	1,438	1,371	1,147	1,206	1,678	39.1
Katani	2,002	1,579	1,733	2,109	1,566	1,614	3.0
Chai	1,696	1,777	1,706	1,446	1,346	1,301	-3.3
Tumbaku	4,732	4,056	3,744	3,441	3,494	3,538	1.3
Korosho	1,599	1,636	1,674	1,193	1,121	1,123	0.2
Karafuu	7,976	7,884	3,000	7,000	4,770	5,493	15.2
Almasi (kwa carat)	361	228	200	138	131	180	37.1
Dhahabu (kwa gramu)	17	28	25	27	44	46	4.5

Chanzo: Mamalaka ya Mapato Tanzania
*Isipokuwa kwa almasi na dhahabu

Kielelezo Na. 4.5: MWENENDO WA BEI YA PAMBA NA KAHAWA ILIYOUZWA NJE YA NCHI



MIZANIA YA MALIPO MWAKA 2017 - 2021

Jedwali Na. 29 **Dola za Marekani**

	2017r	2018r	2019r	2020r	2021p
Urari wa Biashara	**- 2,782.3**	**- 4,227.0**	**-3,237.6**	**-1,460.0**	**-3,247.7**
Zilizouzwa nje (fob)	4,510.8	4,292.7	5,377.6	6,371.7	6,755.6
Zilizonunuliwa toka nje (fob)*	7,293.0	8,519.7	8,615.2	7,831.7	10,003.4
Urari wa Huduma	**1,830.5**	**2,088.9**	**2,492.5**	**864.7**	**1,434.7**
Mapato	3,831.9	4,014.7	4,281.0	2,183.8	3,152.3
Malipo	2,001.4	1,925.7	1,788.4	1,319.0	1,717.7
Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi	**- 935.7**	**- 639.2**	**- 1,013.7**	**- 1,264.5**	**-1,218.0**
Yaliyoingia	125.3	155.9	212.4	111.2	103.2
Yaliyotoka	1,061.0	795.2	1,226.2	1,375.7	1,321.3
Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida	402.0	468.5	418.5	399.9	565.3
Iliyoingia	485.2	535.8	474.9	452.6	650.7
Serikalini	121.8	170.3	103.5	139.9	104.4
Sekta nyingine	363.4	365.5	371.4	312.7	546.3
Iliyotoka	83.2	67.3	56.4	52.7	85.4
Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali	**- 1,485.5**	**- 2,308.7**	**-1,340.2**	**-1,459.9**	**-2,465.8**
Urari wa Uhamisho wa Mitaji	**376.8**	**464.1**	**481.2**	**385.8**	**417.9**
Iliyoingia	376.8	464.1	481.2	385.8	417.9
Iliyotoka	-	-	-	-	-
Urari katika uwekezaji	**2,147.7**	**1,621.2**	**2,505.8**	**884.0**	**2,965.0**
Uwekezaji katika miradi	- 937.7	- 971.6	-1,217.2	-943.8	-1,032.9
Uwekezaji katika hisa	2.9	- 3.7	36.8	-2.1	-7.7
Uwekezaji aina nyingine	1,207.0	653.3	1,251.8	-57.7	1,939.8
Makosa na Masahihisho	630.7	- 560.6	-1,059.8	-574.8	935.1
Urari wa Malipo yote	**1,669.6**	**- 784.0**	**587.0**	**-764.9**	**1,852.1**

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo Na. 4.6: MWENENDO WA URARI KATIKA MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE MWAKA 2021



SURA YA 5

HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

HALI YA UCHUMI WA DUNIA

Ukuaji wa Uchumi

140. Mwaka 2021, uchumi wa dunia uliimarika na kufikia ukuaji chanya wa asilimia 6.1 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 3.1 mwaka 2020. Kasi ya ukuaji wa uchumi iliimarika kutokana na nchi mbalimbali duniani kutekeleza sera za kukabiliana na athari za kiuchumi zitokanazo na janga la UVIKO - 19. Sera hizo ni pamoja na kuongeza ukwasi kwa kampuni na kaya zilizoathirika na kupunguza masharti mbalimbali yaliyowekwa ili kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo.

141. Mwaka 2021, kasi ya ukuaji wa Pato la nchi zilizoendelea uliimarika na kufikia asilimia 5.2 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 4.5 mwaka 2020. Hii ilitokana na nchi nyingi kutoa chanjo ya kudhibiti ugonjwa wa UVIKO - 19 hivyo kuiwezesha jamii kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi bila vikwazo. Aidha, kurejea kwa shughuli za biashara na usafirishaji kulichangia Pato la nchi hizo kuongezeka.

142. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoendelea ilikuwa asilimia 6.8 mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 2.0 mwaka 2020. Ukuaji huu ulichangiwa na nchi hizo kupunguza masharti yaliyowekwa kwa ajili ya kudhibiti maambukizi ya UVIKO - 19 kwa kufungua mipaka, kurejesha safari za ndege za kimataifa na kuruhusu kuendelea kwa shughuli za kiuchumi zinazohusisha mikusanyiko zilizokuwa zimesitishwa. Kasi ya ukuaji wa Pato la nchi za Asia zinazoendelea ikijumuisha China na India ilikuwa asilimia 7.3 mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 0.8 mwaka 2020.

143. Mwaka 2021, ukuaji wa Pato la nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikuwa asilimia 4.5 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.7 mwaka 2020. Ukuaji huu ulichangiwa na kuimarika kwa bei za bidhaa zinazouzwa nje ya ukanda huo pamoja na kuondolewa kwa vikwazo vilivyowekwa ili kudhibiti kuenea kwa UVIKO - 19. Aidha, ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa shughuli za utalii katika nchi zinazotegemea kwa kiasi kikubwa sekta ya utalii katika uchumi ikiwemo Madagaska, Mauritius, Namibia na Seychelles ambazo zote zilikuwa na ukuaji hasi mwaka 2020.

Jedwali Na. 5.1: Pato la Dunia Mwaka 2017 - 2021

	2017	2018	2019	2020	2021
	Ukuaji (Asilimia)				
Pato la dunia	3.7	3.6	2.9	-3.1	6.1
Nchi zilizoendelea	2.5	2.3	1.7	-4.5	5.2
Nchi Zinazoendelea	4.7	4.6	3.7	-2.0	6.8
Nchi za Asia Zinazoendelea	6.6	6.4	5.3	-0.8	7.3
Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara	3.0	3.3	3.1	-1.7	4.5

Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), WEO Aprili 2022

144. Mwaka 2021, ukuaji wa Pato la nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Africa ulikuwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 4.3 mwaka 2020. Aidha, ukuaji wa Pato la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa asilimia 5.9 mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.1 mwaka 2020. Ukuaji chanya kwa jumuiya hizo ulitokana na kulegezwa kwa masharti yaliyowekwa kwa ajili ya kudhibiti maambukizi ya UVIKO - 19 pamoja na hatua mbalimbali za sera na kibajeti zilizochukuliwa kwa ajili ya kuchochea shughuli za kiuchumi katika sekta zilizoathirika na ugonjwa huo.

Jedwali Na. 5.2: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi Mwaka 2020 - 2021

Ukuaji wa Uchumi kwa nchi za SADC		
Nchi	**2020**	**2021**
Angola	-5.6	0.7
Botswana	-8.7	12.5
Comoros	-0.3	2.2
Tanzania	4.8	4.9
DRC	1.7	5.7
Eswatin	-1.9	3.1
Lesotho	-6	2.1
Madagascar	-7.1	3.5
Malawi	0.9	2.2
Maurtius	-14.9	3.9
Msumbiji	-1.2	2.2
Namibia	-8.5	0.9
Seychelles	-7.7	8
Sudani Kusini	-6.4	4.9
Zambia	-2.8	4.3
Zimbabwe	-5.3	6.3
Wastani	**-4.3**	**4.2**
Ukuaji wa Uchumi kwa nchi za EAC		
Burundi	0.3	2.4
Kenya	-0.3	7.2
Rwanda	-3.4	10.2
Sudan Kusini	-6.6	5.3
Tanzania	4.8	4.9
Uganda	-1.4	5.1
Wastani	**-1.1**	**5.9**

Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), WEO Aprili 2022

Mwenendo wa Bei

145. Mwaka 2021, mfumuko wa bei wa dunia uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.7 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bei za nishati na vyakula kulikosababishwa na kuvurugika kwa mnyororo wa thamani kutokana na kusitishwa kwa baadhi ya shughuli za uchumi katika jitihada za kudhibiti UVIKO - 19. Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 0.7 mwaka 2020. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Ulaya ulikuwa wa wastani wa asilimia 9.5 mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2020. Sababu za kuongezeka kwa kasi ya mfumuko wa bei wa dunia zinawiana na zile za nchi zinazoendelea za Ulaya. Mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia ulipungua hadi wastani wa asilimia 2.2 mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2020. Kupungua kwa mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia kulitokana na kupungua kwa bei ya vyakula hususan mchele.

146. Mwaka 2021, mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 11.0 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 10.2 mwaka 2020. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo kupanda kwa bei za vyakula na mafuta kwa baadhi ya nchi hizo. Nchi zilizokuwa na mfumuko wa bei wa juu ni pamoja na Zimbabwe (asilimia 98.5), Ethiopia (asilimia 26.8), Angola (asilimia 25.8), Zambia (asilimia 20.5) na Nigeria (asilimia 17). Mfumuko wa bei kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa asilimia 4.4 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2020. Katika kipindi hicho, nchi ya Burundi ilikuwa na kiwango kikubwa cha mfumuko wa bei wa asilimia 8.3 na Rwanda ilikuwa na kiwango kidogo cha mfumuko wa bei wa asilimia 0.8.

Jedwali Na. 5.3: Viwango vya Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki Mwaka 2020 - 2021

Nchi	**2020**	**2021**
	Mfumuko wa Bei (Asilimia)	
Tanzania	3.3	3.7
Uganda	2.8	2.2
Kenya	5.3	6.1
Rwanda	7.7	0.8
Burundi	7.3	8.3
Sudani ya Kusini	24.0	5.3
Wastani kwa Afrika Mashariki	**8.4**	**4.4**

Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), WEO Aprili 2022

Mwenendo wa Biashara Duniani

147. Mwaka 2021, biashara ya bidhaa duniani ilikuwa na ukuaji chanya wa asilimia 10.9 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 4.9 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji baada ya kupungua kwa masharti ya udhibiti wa

UVIKO - 19. Aidha, kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Biashara Duniani - WTO, Trade Statistics and Outlook - Aprili 2022, uuzaji wa bidhaa nje ya Bara la Afrika ulikuwa na ukuaji chanya wa asilimia 5.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 7.5 mwaka 2020. Aidha, uagizaji wa bidhaa nje ya Bara la Afrika ulikuwa na ukuaji chanya wa asilimia 4.2 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 11.8 mwaka 2020.

Ushirikiano wa Uchumi Kimataifa

148. Mwaka 2021, Tanzania iliendelea kushirikiana na jumuiya za kimataifa kupitia Umoja wa Mataifa, mashirika ya fedha na biashara ya kimataifa na majukwaa mengine ya kimataifa. Katika kipindi hicho, Tanzania ilishiriki Kikao cha 76 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ambapo pamoja na mambo mengine, iliieleza Jumuiya ya Kimataifa kuhusu jitihada za Serikali katika kupambana na athari za UVIKO - 19 pamoja na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa sera, mipango na miradi ya maendeleo. Aidha, Tanzania iliihakikishia Jumuiya ya Kimataifa kuhusu utayari wa kutumia majukwaa ya diplomasia majumui (multilateral diplomacy) katika kukabiliana na changamoto za kiuchumi, kijamii na kisiasa zinazoikabili dunia. Kutokana na ushirikiano na jumuiya za kimataifa, Tanzania ilichaguliwa kuwa mjumbe wa: Bodi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization - UNESCO) kwa kipindi cha miaka minne (2021-2025); Baraza la Utawala na Baraza la Uendeshaji la Umoja wa Posta Duniani kwa kipindi cha miaka minne (2021-2025); Baraza la Uchumi na Jamii la Umoja wa Mataifa (Economic and Social Council - ECOSOC) kwa kipindi cha mwaka 2022-2024. Baraza hili husimamia miradi yote ya maendeleo ya Umoja wa Mataifa na baadhi ya mashirika ya Umoja huo ikiwemo United Nations Development Programme - NDP, United Nations Population Fund - UNFPA na United Nations High Commissioner for Refugees - UNHCR.

149. Mwaka 2021, Tanzania ilishiriki katika Jukwaa la Viongozi la Mabadiliko ya Tabianchi na Mkutano wa 26 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (The 26th Conference of the Parties - COP26). Katika jukwaa hilo Tanzania ilieleza kuhusu utekelezaji wa sera, mikakati na programu za kuhifadhi mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo lengo la kupanda miti takriban milioni 270 kila mwaka ili kupunguza kiwango cha uzalishaji wa hewa ukaa kwa asilimia 30 hadi 35 ifikapo mwaka 2030. Aidha, Tanzania iliungana na nchi nyingine duniani kuzitaka nchi zilizoendelea kutimiza ahadi ya kuchangia dola za Marekani bilioni 100 kila mwaka kwa nchi zinazoendelea kwa lengo la kuziwezesha kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kulingana na matakwa ya Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Paris wa mwaka 2015 na kuzitaka nchi vinara wa uchafuzi wa mazingira kutekeleza kwa vitendo makubaliano ya kupunguza kiwango cha hewa ukaa wanachozalisha.

Ushirikiano wa Kiuchumi Barani Afrika

150. Mwaka 2021, mikutano miwili (2) ya Tume za Kudumu za Pamoja kati ya Tanzania na nchi za Kenya na Rwanda ilifanyika ambapo kupitia mikutano hiyo Tanzania ilifanikiwa kudumisha uhusiano wa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Aidha, nchi hizo zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika sekta mbalimbali zikiwemo afya, biashara na uwekezaji, ujenzi na uchukuzi, nishati, elimu, na ulinzi na usalama. Vilevile, Tanzania na Kenya zilikubaliana kuondoa kwa awamu vikwazo 70 vya muda mrefu visivyo vya kiforodha ambapo hadi Desemba 2021 vikwazo 56 vilikuwa vimepatiwa ufumbuzi na vikwazo 14 vipo katika hatua ya majadiliano ya kuviondoa. Baadhi ya vikwazo vilivyopatiwa ufumbuzi ni pamoja na: kudhibiti upandishwaji wa bei ya vinywaji baridi kutoka Tanzania kwenda Kenya ili ziwe na ushindani sawa na zile zinazozalishwa nchini Kenya (preferential treatment); kubadilisha mfumo wa ukaguzi wa shehena ambapo kwa sasa ukaguzi unahusisha mamlaka za pande mbili kwa pamoja (joint inspection); kufanya ukaguzi wa shehena ya aina moja kwa pamoja badala ya ukaguzi wa kila shehena kwa kusudi la kupunguza muda wa malori kusubiri ukaguzi mpakani (bulk clearance); kuondolewa kwa gharama za tozo ya ukaguzi; kuondolewa kwa tozo ya asilimia moja ya thamani ya kahawa inayotoka Kenya kuja Tanzania; na kuondoa zuio la mpaka wa kuingiza kemikali za kulinda mazao. Hatua hiyo ilichochea ukuaji wa biashara na uwekezaji kati ya nchi hizo mbili. Kufuatia kukua kwa biashara, nakisi ya urari wa biashara baina ya Tanzania na Kenya ilipungua na kufikia dola za Marekani milioni 13.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 17.5 mwaka 2020.

151. Mwaka 2021, Tanzania iliridhia mkataba wa kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (African Continental Free Trade Area - AfCFTA) na hivyo kuwa mwanachama wa 41 kati ya 55 wa Umoja wa Afrika kuridhia mkataba huo. Kuridhiwa kwa Mkataba huo kuliongeza ushawishi wa Tanzania katika mtangamano wa Afrika na hivyo kuwa sehemu ya soko la Afrika ambapo bidhaa na huduma zitaingizwa baina ya nchi wanachama bila kutozwa ushuru wa forodha. Aidha, nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zimekubaliana kufunguliana biashara ya bidhaa kwa kuzingatia utaratibu maalum (modalities). Utaratibu huo unaelekeza asilimia 97 ya bidhaa zifunguliwe kwa kuondoa ushuru wa forodha hatua kwa hatua ambapo bidhaa za kundi A (asilimia 90) zitafunguliwa baada ya kuanza utekelezaji wa Mkataba na Kundi B (asilimia 7) zitafunguliwa baada ya miaka 5 tangu kuanza kwa utekelezaji wa Mkataba na asilimia 3 (exclusion list) ya bidhaa hazitaondolewa ushuru wa forodha. Vilevile, kwa Nchi ambazo zinatekeleza Umoja wa Forodha (Customs Union) kama vile nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC zinatakiwa kuwasilisha tariff offer moja itakayokubaliwa na nchi wanachama bila kuathiri taratibu za Umoja wa Forodha.

Ushirikiano wa Kiuchumi katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

152. Mwaka 2021, mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC ulifanyika mwezi Agosti, ambapo Mpango Mkakati wa Maendeleo wa SADC 2020 - 2030 (SADC Regional Indicative Strategic Develpment Plan - RISDP) uliidhinishwa. Mpango Mkakati huo umezingatia sekta zote za kijamii, kisiasa na kiuchumi na umeainisha mipango ya namna ya kushirikisha sekta binafsi katika kutekeleza vipaumbele vya Jumuiya ili kuwezesha kufikia Dira ya Jumuiya ya mwaka 2050. Aidha, Mpango huo umezingatia vipaumbele vilivyopo katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 hususani katika maendeleo ya miundombinu, viwanda, uchumi wa buluu na uvumbuzi wa aina mbalimbali za nishati. Vilevile, Mkutano uliazimia kuwa bajeti ya Sekretarieti ya SADC ya mwaka 2022/23 isiwe na ongezeko (no budget increament) na ukomo (budget ceilling) uwe kama mwaka wa fedha uliopita ili kuepuka kuwa na ongezeko la michango ya nchi wanachama na kusaidia kupunguza makali ya athari za kiuchumi zilizotokana na janga la UVIKO - 19.

Ushirikiano wa Kiuchumi Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

Utekelezaji wa Himaya Moja ya Forodha

153. Mwaka 2021, Tanzania iliendelea kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inayolenga kukuza biashara; kuongeza ufanisi katika uzalishaji; kukuza uwekezaji wa ndani baina ya nchi wanachama; na kuendeleza viwanda. Katika kipindi hicho, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliongezeka kwa asilimia 42.9 na kufikia dola za Marekani milioni 1,161.2 mwaka 2021 ikilinganishwa na dola za Marekani 812.5 mwaka 2020. Hii ilitokana na juhudi za Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Aidha, bidhaa zilizonunuliwa kutoka nchi wanachama wa EAC zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 523.4 mwaka 2021 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 324.3 zilizonunuliwa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 61.4. Kutokana na mwenendo huo, urari wa biashara baina ya Tanzania na nchi nyingine za EAC ulikuwa wa ziada ya dola za Marekani milioni 637.8 mwaka 2021 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 488.2 mwaka 2020.

154. Mwaka 2021, Tanzania iliridhia Itifaki ya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuridhiwa kwa Itifaki hiyo kutaiwezesha Tanzania kuuza kwa wingi bidhaa zitokanazo na mimea, wanyama na samaki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki bila vikwazo.

Sekta za Miundombinu na Huduma za Jamii katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

155. Mwaka 2021, Tanzania iliendelea kushirikiana na nchi nyingine wanachama wa EAC kujenga na kuendelea kuboresha Vituo vya Kutoa Huduma Pamoja Mpakani - One Stop Border Post - OSBPs kwa lengo la kurahisisha biashara ndani ya Jumuiya. Katika

kipindi hicho, hatua za awali za utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kituo kipya cha OSBP Manyovu/Mugina kati ya Tanzania na Burundi zilianza ambazo zilihusisha uhakiki wa nyaraka muhimu za mradi na eneo kitakapojengwa kituo hicho. Mradi huo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa barabara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kabingo - Kasulu - Manyovu/ Rumonge - Gitaza.

156. Mwaka 2021, nchi wanachama wa EAC ziliendelea kushirikiana katika kudhibiti maambukizi na athari za UVIKO - 19. Katika kipindi hicho, nchi wanachama zilijadiliana namna ya kuanzisha Hati ya Pamoja ya Jumuiya itakayorahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji ndani na nje ya Jumuiya. Aidha, nchi wanachama zilikubaliana namna bora ya kutambua vyeti vya UVIKO - 19 vinavyotolewa na maabara za nchi hizo. Hadi Desemba 2021, maabara 66 kati ya 77 zilifanyiwa tathmini na kuthibitishwa kukidhi viwango vya kutoa huduma ya upimaji wa UVIKO - 19 kwa wasafiri kulingana na vigezo vya Shirika la Afya Duniani.

SURA YA 6

RASILIMALI WATU

Idadi ya Watu

157. Mwaka 2021, idadi ya watu ilikadiriwa kuwa 59,441,988 ikilinganishwa na watu 57,637,628 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Tanzania bara ilikadiriwa kuwa na watu 57,724,380, sawa na asilimia 97.1 ya watu wote na Tanzania Zanzibar ilikadiriwa kuwa na watu 1,717,608. Aidha, wanawake walikadiriwa kuwa 30,309,750 sawa na asilimia 51.0 ya watu wote na wanaume walikadiriwa kuwa 29,132,238. Makadirio hayo yalitokana na maoteo ya idadi ya watu kwa kutumia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 pamoja na viashiria muhimu vya mabadiliko ya idadi ya watu ikiwemo uzazi, vifo na uhamiaji.

Mgawanyiko wa Watu Kimkoa

158. Mwaka 2021, Mkoa wa Dar es Salaam ulikadiriwa kuwa na idadi kubwa ya watu wapatao 5,526,638 sawa na asilimia 9.6 ya watu wote Tanzania Bara ikifuatiwa na Mkoa wa Mwanza uliokadiriwa kuwa na watu 3,983,793, sawa na asilimia 6.9. Idadi kubwa ya watu katika mkoa wa Dar es Salaam ilichangiwa na upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii na fursa za kiuchumi zilizovutia watu kuhamia kutoka mikoa mingine. Aidha, Mkoa wa Katavi ulikuwa na idadi ndogo ya watu wapatao 842,200, sawa na asilimia 1.5 ya watu wote Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na idadi kubwa ya watu wapatao 750,033, sawa na asilimia 43.7 ya watu wote Tanzania Zanzibar. Mkoa wa Kusini Unguja ulikadiriwa kuwa na idadi ndogo ya watu wapatao 140,821, sawa na asilimia 8.2 ya watu wote Tanzania Zanzibar.

159. Mwaka 2021, msongamano wa watu kwa Tanzania ulikuwa wastani wa watu 67 kwa kila kilometa ya mraba ikilinganishwa na wastani wa watu 65 mwaka 2020. Aidha, msongamano wa watu Tanzania Bara ulikuwa wastani wa watu 65 kwa kila kilometa ya mraba ikilinganishwa na wastani wa watu 63 mwaka 2020. Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na msongamano mkubwa wa wastani wa watu 3,967 kwa kila kilometa ya mraba, ukifuatiwa na Mwanza uliokuwa na wastani wa watu 420 kwa kilomita ya mraba. Kwa upande mwingine, Mkoa wa Lindi ulikuwa na msongamano mdogo ukiwa na wastani wa watu 16 kwa kila kilometa ya mraba, ukifuatiwa na Mkoa wa Katavi wastani wa watu 18 kwa kila kilometa ya mraba. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na msongamano mkubwa wa wastani wa watu 3,261 kwa kila kilometa ya mraba ukifuatiwa na Mkoa wa Kusini Pemba uliokuwa na wastani wa watu 853 kwa kila kilometa ya mraba. Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na msongamano mdogo ukiwa na wastani wa watu 165 kwa kila kilometa ya mraba.

160. Mwaka 2021, idadi ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano ilikuwa 10,080,305, sawa na asilimia 17.0 ya watu wote Tanzania. Aidha, idadi ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 35 walikuwa 20,125,724 sawa na asilimia 34.9 ya watu wote; watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 ilikuwa 31,124,653 sawa na asilimia 53.9 na watu wenye umri wa miaka 65 na zaidi walikuwa 1,662,774 sawa na asilimia 2.9. Vilevile, jumla ya watu wenye umri wa miaka 65 na zaidi na wenye umri chini ya miaka 15 walikuwa 26,599,727 sawa na asilimia 46.1 ya watu wote.

Jedwali Na. 6.1. Mchanganuo wa Idadi ya Watu kwa Makundi ya Umri na Jinsi Tanzania Bara Mwaka 2021

Umri	Jinsia		Jumla	Asilimia
	Wanawake	Wanaume		
0 - 4	4,952,084	4,858,540	9,810,624	17.0
5 - 14	7,598,669	7,527,660	15,126,329	26.2
15 - 35	9,741,490	10,384,234	20,125,724	34.9
36 - 64	5,233,283	5,765,646	10,998,929	19.0
65+	769,678	893,096	1,662,774	2.9
Jumla	**28,295,204**	**29,429,176**	**57,724,380**	**100**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Sensa ya watu na Makazi

161. Mwaka 2021, Serikali iliendelea na maandalizi ya zoezi la Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika mwezi Agosti 2022 kwa lengo la kukusanya, kuchakata, kuchambua na kusambaza taarifa za kidemografia, kiuchumi, mazingira na kijamii za watu wote na makazi nchini kwa kipindi maalumu. Aidha, Mkakati wa Uhamasishaji na Uelimishaji wa Sensa ya Watu na Makazi ulizinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan tarehe 14 Septemba 2021. Hadi Desemba 2021, sensa ya majaribio ilikuwa imefanyika katika mikoa 13 ya Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, kazi nyingine za maandalizi ya sensa zilizotekelezwa ni pamoja na: kuhuisha mipaka ya vitongoji vyote vya Tanzania Bara na mitaa na uandaaji wa madodoso ya sensa zote tatu (Sensa ya Watu na Makazi, Sensa ya Majengo na Sensa ya Anwani za Makazi).

Nguvu Kazi na Ajira

162. Mwaka 2021, asilimia 75.8 ya watu wenye umri wa zaidi ya miaka 15 walikuwa katika ajira, asilimia 9.0 walikuwa hawana ajira lakini walikuwa wanatafuta kazi na asilimia 16.7 walikuwa hawana kazi lakini hawakuwa tayari kufanya kazi kutokana na ugonjwa, walikuwa masomoni au kwa sababu nyingine.

Jedwali Na. 6.2: Mchanganuo wa Uwiano wa Ajira kwa Idadi ya Watu Mwaka 2021

Umri	**Jinsi**		**Jumla**
	Wanawake	**Wanaume**	
Idadi ya Watu (15+)	16,229,848	14,818,047	31,047,894
Wenye Ajira (15+)	11,477,354	12,058,781	23,536,135
Wasiokuwa na ajira lakini wanatafuta kazi	1,599,791	725,096	2,324,887
Wasiokuwa na ajira lakini hawakuwa tayari kufanya kazi	3,152,703	2,034,169	5,186,872
Uwiano wa ajira kwa idadi ya watu (Asilimia)	**81.4**	**70.7**	**75.8**

Chanzo: Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu

163. Mwaka 2021, jumla ya watu 25,861,023 walikuwa katika soko la ajira ambapo watu 23,536,135 (wanaume 12,058,781 na wanawake 11,477,354) walikuwa wameajiriwa katika sekta mbalimbali za kiuchumi ikilinganishwa na watu 23,029,954 waliokuwa wameajiriwa mwaka 2020. Aidha, ajira za watu wenye ulemavu zilikuwa asilimia 8.6 ya ajira zote. Katika kipindi hicho, sekta ya kilimo ilichangia asilimia 65.6 ya ajira zote ikifuatiwa na sekta ya biashara iliyochangia asilimia 12.2. Kati ya watu waliokuwa wameajiriwa, watu 22,922,749 sawa na asilimia 97.4 walikuwa wameajiriwa katika sekta binafsi na watu 613,387 waliajiriwa katika sekta ya umma.

Jedwali Na. 6.3: Mchanganuo wa Ajira kwa Sekta Mwaka 2021

Sekta	Wanaume	Wanawake	Jumla	Mchango wa Sekta (Asilimia)
Kilimo, misitu na uvuvi	7,761,893	7,686,198	15,448,091	65.6
Uchimbaji wa madini na mawe	176,815	41,538	218,353	0.9
Viwanda	606,382	435,147	1,041,529	4.4
Umeme, Gesi, usambazaji wa mifumo ya upozaji	19,394	2,088	21,482	0.1
Usambazaji na usimamizi wa maji safi na taka	17,896	10,802	28,698	0.1
Ujenzi	550,167	18,607	568,774	2.4
Biashara ya jumla na rejareja, matengenezo ya magari na pikipiki	1,138,218	1,726,548	2,864,767	12.2
Uchukuzi na uhifadhi bidhaa/mizigo	688,724	19,447	708,171	3.0
Malazi na huduma ya chakula	117,232	565,211	682,443	2.9
Habari na mawasilisno	32,208	8,405	40,613	0.2
Huduma ya fedha na bima	42,768	35,844	78,613	0.3
Upangishaji, ununuzi na uuzaji majengo	9,760	4,620	14,380	0.1
Shughuli za kitaaluma, kisayansi na ufundi	47,673	22,602	70,275	0.3
Huduma za masuala ya kiutawala	237,022	148,624	385,646	1.6
Utawala, ulinzi na huduma za hifadhi ya jamii;	81,800	25,624	107,425	0.5
Elimu	207,570	172,941	380,510	1.6
Afya na huduma za kijamii	66,955	86,403	153,357	0.7
Sanaa na burudani	25,452	6,261	31,713	0.1
Huduma nyingine	172,544	190,108	362,652	1.5
Shughuli za kaya, huduma na uzalishaji katika kaya	58,003	269,702	327,705	1.4
Shughuli nyingine katika taasisi na mamlaka za kigeni	306	632	938	0.0
Jumla	**12,058,781**	**11,477,354**	**23,536,135**	**100**

Chanzo: Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu

164. Mwaka 2021, kiwango cha ukosefu wa ajira nchini kilipungua na kufikia asilimia 9.0 sawa na watu 2,324,887 waliokuwa katika soko la ajira kutoka kiwango cha asilimia 9.5 sawa na watu 2,406,950 mwaka 2020. Aidha, kiwango cha ukosefu wa ajira kwa wanawake kilikuwa asilimia 12.2 ikilinganishwa na wanaume wanaume asilimia 5.7.

Jedwali Na. 6.4: Mwenendo wa Kiwango cha Ukosefu wa Ajira Mwaka 2021

	Jinsi		Jumla
	Wanawake	Wanaume	
Walio katika soko la ajira (15+)	13,077,145	12,783,878	25,861,023
Walioajiriwa (15+)	11,477,354	12,058,781	23,536,135
Wasioajiriwa (15+)	1,599,791	725,096	2,324,887
Kiwango cha ukosefu wa ajira (Asilimia)	**12.2**	**5.7**	**9.0**

Chanzo: Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu

165. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kutekeleza Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi kwa Vijana kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira. Katika kipindi hicho, vijana 22,899 walipata mafunzo ya ujuzi unaohitajika katika soko la ajira ili waweze kuajiriwa na kujiajiri ikilinganishwa na vijana 18,956 waliopata mafunzo mwaka

2020. Kati ya hao, vijana 14,440 walipata mafunzo ya uanagenzi, wahitimu 2,215 walipata mafunzo kwa vitendo mahala pa kazi na vijana 2,644 walipata mafunzo ya ufundi stadi na kurasimisha ujuzi walioupata nje ya mfumo rasmi na vijana 3,600 waliwezeshwa kupata mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba.

166. Mwaka 2021, Serikali kupitia Kitengo cha Huduma za Ajira ilisajili watafutakazi 8,849 na kuwapatia ushauri nasihi kuhusu uchaguzi wa kazi ikilinganishwa na watafutakazi 12,230 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 27.6. Kati ya watafutakazi hao, wanawake walikuwa 4,015 na wanaume walikuwa 4,834 ikilinganishwa na wanaume 6,524 na wanawake 5,706 mwaka 2020. Katika kipindi hicho, watafutakazi 6,344 (wanaume 3,311 na wanawake 3,033) walipata mafunzo ikilinganishwa na watafutakazi 2,861 (wanaume 1,456 na wanawake 1,405) waliopata mafunzo mwaka 2020. Aidha, mafunzo hayo yalitolewa kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kutafuta kazi, kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi pamoja na mafunzo ya kujenga maadili ya kazi yanayohitajika na waajiri mbalimbali. Vilevile, vijana 592 (wanaume 348 na wanawake 244) waliunganishwa na fursa za kazi kwa waajiri mbalimbali nchini ikilinganishwa na vijana 923 (wanaume 504 na wanawake 419) mwaka 2020.

IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA MWAKA 2012 - 2021

Jedwali Na. 30

Mkoa	2012**	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Dodoma	2,083,588	2,172,165	2,217,856	2,264,508	2,419,941	2,492,989	2,568,514	2,647,410	2,729,668
Arusha	1,694,310	1,789,791	1,839,531	1,890,653	1,948,219	1,999,907	2,051,852	2,104,074	2,156,511
Kilimanjaro	1,640,087	1,698,526	1,728,522	1,759,048	1,823,151	1,864,329	1,906,978	1,951,252	1,996,952
Tanga	2,045,205	2,138,517	2,186,757	2,236,086	2,284,712	2,337,053	2,391,791	2,449,235	2,509,439
Morogoro	2,218,492	2,325,386	2,380,750	2,437,431	2,531,268	2,596,287	2,662,468	2,730,058	2,799,260
Pwani	1,098,668	1,147,227	1,172,306	1,197,933	1,236,481	1,265,504	1,295,267	1,325,852	1,357,271
Dar es Salaam	4,364,541	4,884,061	5,166,570	5,465,420	5,017,294	5,147,070	5,275,315	5,401,814	5,526,638
Lindi	864,652	880,939	889,197	897,533	963,465	983,738	1,004,439	1,025,800	1,047,783
Mtwara	1,270,854	1,302,340	1,318,374	1,334,606	1,397,723	1,424,083	1,451,078	1,478,874	1,507,426
Ruvuma	1,376,891	1,436,563	1,467,362	1,498,821	1,543,869	1,579,811	1,616,991	1,655,443	1,695,057
Iringa	941,238	962,813	973,784	984,882	1,068,695	1,095,172	1,122,131	1,149,481	1,177,327
Mbeya	2,707,410	2,858,585	2,937,310	1,883,024	2,006,072	2,070,412	2,136,614	2,204,543	2,274,236
Singida	1,370,637	1,435,758	1,469,469	1,503,972	1,569,304	1,612,854	1,658,086	1,705,182	1,754,370
Tabora	2,291,623	2,429,679	2,501,796	2,576,053	2,769,093	2,870,522	2,974,427	3,081,263	3,191,194
Rukwa	1,004,539	1,071,044	1,105,931	1,141,953	1,160,568	1,195,550	1,231,959	1,270,049	1,310,007
Kigoma	2,127,930	2,232,520	2,286,727	2,342,250	2,528,708	2,616,200	2,706,831	2,800,919	2,898,568
Shinyanga	1,534,808	1,599,325	1,632,593	1,666,554	1,816,316	1,874,709	1,933,768	1,993,589	2,054,229
Kagera	2,458,023	2,618,558	2,702,715	2,789,577	2,919,942	3,022,037	3,127,908	3,238,347	3,353,241
Mwanza	2,772,509	2,942,537	3,031,422	3,122,992	3,393,620	3,532,378	3,676,300	3,826,573	3,983,793
Mara	1,743,830	1,831,810	1,877,451	1,924,230	2,123,683	2,209,143	2,298,317	2,391,845	2,490,155
Manyara	1,425,131	1,518,516	1,567,479	1,618,020	1,692,667	1,750,864	1,810,929	1,873,105	1,937,450
Njombe	702,097	713,345	719,036	724,772	786,347	803,299	820,355	837,557	854,932
Katavi	564,604	602,325	622,121	642,567	706,472	738,237	771,287	805,887	842,200
Simiyu	1,584,157	1,643,549	1,674,075	1,705,168	1,998,224	2,094,798	2,196,449	2,304,228	2,418,495
Geita	1,739,530	1,833,350	1,882,141	1,932,230	2,148,409	2,239,949	2,335,134	2,434,800	2,539,114
Songwe				1,136,415	1,166,094	1,202,419	1,239,970	1,278,850	1,319,064
Tanzania Mainland	**43,625,354**	**46,069,230**	**47,351,275**	**48,676,698**	**51,020,337**	**52,619,314**	**54,265,158**	**55,966,030**	**57,724,380**
Kaskazini Unguja	187,455	199,844	206,343	213,053	216,697	222,066	227,317	232,480	237,505
Kusini Unguja	115,588	120,305	122,736	125,215	131,162	133,767	136,235	138,589	140,821
Mjini Magharibi	593,678	645,701	673,398	702,283	683,833	700,791	717,468	733,914	750,033
Kaskazini Pemba	211,732	217,309	220,153	223,033	260,884	271,594	282,716	294,267	306,173
Kusini Pemba	195,116	199,456	201,662	203,893	241,715	251,631	261,853	272,348	283,076
Zanzibar	**1,303,569**	**1,382,616**	**1,424,292**	**1,467,477**	**1,534,291**	**1,579,849**	**1,625,589**	**1,671,598**	**1,717,608**
Tanzania	**44,928,923**	**47,451,847**	**48,775,567**	**50,144,175**	**52,554,628**	**54,199,163**	**55,890,747**	**57,637,628**	**59,441,988**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Takwimu za matokeo ya sensa mwaka 2012

SEHEMU YA PILI

UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

SURA YA 7

UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

Usajili wa Miradi ya Uwekezaji

167. Mwaka 2021, Kituo cha Uwekezaji Tanzania - TIC kilisajili miradi 256 ikilinganishwa na miradi 203 iliyosajiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 26.1. Kati ya hiyo, miradi 75 ilikuwa ya watanzania, miradi 114 ya wageni na miradi 67 ya ubia kati ya watanzania na wageni ikilinganishwa na miradi 64 ya watanzania, miradi 74 ya wageni na miradi 65 ya ubia kati ya watanzania na wageni mwaka 2020. Katika kipindi hicho, thamani ya miradi iliyosajiliwa ilikuwa dola za Marekani bilioni 3.8 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 1.1 mwaka 2020. Ongezeko la thamani na idadi ya miradi iliyosajiliwa lilichangiwa na jitihada za Serikali katika: kuitangaza nchi kuwa sehemu sahihi na salama kwa uwekezaji; kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini; na kuboreshwa kwa mfumo wa tathmini ya maombi ya usajili wa miradi kulikorahisisha taratibu za kuhudumia wawekezaji. Aidha, miradi iliyosajiliwa mwaka 2021 inatarajiwa kutoa fursa za ajira 53,025 ikilinganishwa na fursa za ajira 17,084 mwaka 2020.

Mgawanyiko wa Usajili wa Miradi Kisekta

168. Mwaka 2021, sekta ya ujenzi wa majengo ya biashara iliongoza kwa kusajili miradi yenye thamani ya dola za Marekani milioni 1,318.3, sawa na asilimia 35.2 ya thamani ya miradi iliyosajiliwa ikifuatiwa na uzalishaji viwandani dola za Marekani milioni 953.0, sekta ya huduma za kifedha dola za Marekani milioni 574.4, utalii dola za Marekani milioni 354.1 na kilimo dola za Marekani milioni 251.1. Katika kipindi hicho, sekta ya uzalishaji viwandani iliongoza kwa kusajili miradi 135, sawa na asilimia 52.7 ya miradi iliyosajiliwa ikifuatiwa na usafirishaji mizigo miradi 25, ujenzi wa majengo ya biashara miradi 24, utalii miradi 21, kilimo miradi 19 na sekta ya huduma za biashara miradi 16.

Jedwali Na. 7.1: Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa Mwaka 2021

Na.	Sekta	Miradi Iliyosajiliwa				Fursa za ajira	Thamani (Dola za Marekani Milioni)
		Wazawa	Wageni	Ubia	Jumla		
1	Kilimo	6	8	5	19	2,516	251.1
2	Maliasili	0	1	0	1	20	0.7
3	Utalii	5	12	4	21	1,786	354.1
4	Uzalishaji viwandani	37	64	34	135	20,865	953.0
5	Ujenzi majengo ya biashara	8	12	4	24	3,344	1,318.3
6	Usafirishaji mizigo	14	6	5	25	2,989	149.3
7	Huduma za biashara	4	6	6	16	1,148	71.9
8	Huduma za kifedha	0	3	1	4	2,869	574.4
9	Rasilimali Watu	1	1	6	8	396	10.0
10	Nishati	0	0	1	1	92	4.1
11	Miundombinu ya kiuchumi	0	1	1	2	17,000	62.5
	Jumla	**75**	**114**	**67**	**256**	**53,025**	**3,749.3**

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

Mgawanyiko wa Miradi Kimkoa

169. Mwaka 2021, Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kwa kuvutia miradi ya uwekezaji 93, sawa na asilimia 36.3 ya miradi yote iliyosajiliwa ikifuatiwa na Mkoa wa Pwani miradi 36, Mwanza miradi 20, Dodoma miradi 15, Arusha miradi 13 na Tanga miradi 11. Mkoa wa Dar es Salaam uliendelea kuongoza kwa kusajili miradi mingi kutokana na uwepo wa mazingira wezeshi ya uwekezaji hususani miundombinu bora ikilinganishwa na mikoa mingine.

Jedwali Na. 7.2: Mgawanyiko wa Miradi Iliyosajiliwa Kimkoa Mwaka 2021

Mkoa	Sekta											Jumla
	Kilimo	Majengo ya Biashara	Miundo mbinu	Nishati	Taasisi za kifedha	Rasilimali watu	Uzalishaji viwandani	Maliasili	Huduma	Utalii	Usafirishaji mizigo	
Arusha	1	1	0	0	0	0	4	0	1	6	0	13
Dar es Salaam	0	10	1	0	4	5	41	0	8	6	18	93
Dodoma	1	1	0	0	0	0	11	0	1	0	1	15
Geita	0	0	0	0	0	0	5	0	2	0	0	7
Iringa	0	0	0	0	0	0	4	1	0	2	0	7
Kagera	0	0	0	0	0	0	2	0	0	0	0	2
Katavi	1	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	1
Kigoma	2	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	2
Kilimanjaro	0	0	0	0	0	0	2	0	0	0	0	2
Lindi	3	0	0	0	0	1	1	0	0	0	0	5
Mara	0	0	0	0	0	0	5	0	0	3	0	8
Manyara	0	0	0	0	0	0	3	0	0	1	0	4
Mbeya	1	0	0	1	0	0	1	0	0	0	0	3
Morogoro	4	0	0	0	0	0	4	0	1	0	0	9
Mtwara	0	1	0	0	0	0	0	0	0	0	0	1
Mwanza	1	3	0	0	0	1	10	0	2	2	1	20
Njombe	1	0	0	0	0	0	3	0	0	0	0	4
Pwani	2	7	1	0	0	0	22	0	0	1	3	36
Rukwa	0	0	0	0	0	1	0	0	0	0	0	1
Ruvuma	1	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	1
Shinyanga	0	1	0	0	0	0	5	0	0	0	2	8
Singida	0	0	0	0	0	0	2	0	0	0	0	2
Songwe	0	0	0	0	0	0	0	0	1	0	0	1
Tanga	1	0	0	0	0	0	10	0	0	0	0	11
Jumla	**19**	**24**	**2**	**1**	**4**	**8**	**135**	**1**	**16**	**21**	**25**	**256**

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje

170. Kwa mujibu wa Taarifa ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2021, uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje kwa ujumla uliongezeka kwa asilimia 4.4 na kufikia dola za Marekani milioni 18,461.9 mwaka 2020 kutoka dola za Marekani milioni 17,677.5 mwaka 2019. Kati ya uwekezaji huo, uwekezaji wa moja kwa moja ulifikia dola za Marekani milioni 15,612.6, sawa na asilimia 84.6 ya uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje, uwekezaji wa hisa ulifikia dola za Marekani 124.8 (asilimia 0.6) na uwekezaji mwingine dola za marekani 2,724.5 (asilimia 14.8). Aidha, mitaji iliyowekezwa kwenye sekta binafsi kutoka nje ya nchi kwa bei za miaka husika ilikuwa na thamani ya dola za

Marekani milioni 860.1 mwaka 2020 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,240 zilizowekezwa mwaka 2019. Kwa upande mwingine, uwekezaji wa moja kwa moja ulitoa ajira kwa watu 184,552 mwaka 2020 ikilinganishwa na watu 140,415 walioajiriwa mwaka 2019. Kati ya hao, wafanyakazi wataalamu walikuwa 68,778 sawa na asilimia 37 ya waajiriwa wote na wasiokuwa wataalamu walikuwa 115,774.

Jedwali Na.7.3: Uwekezaji kwenye Sekta Binafsi kutoka Nje ya Nchi (Dola za Marekani Milioni) Mwaka 2017 - 2020

Aina ya Uwekezaji	Kiasi Kilichowekezwa				Limbikizo Lililowekezwa			
	2017	2018	2019	2020	2017	2018	2019	2020
Uwekezaji wa moja kwa moja kutoka Nje	937.7	971.6	1,217.2	943.8	13,274.4	14,092	14,762.9	15,612.6
Uwekezaji wa Hisa	0.8	1.6	5.5	1.8	176.6	30.6	104.6	124.8
Uwekezaji mwingine	113.2	241.3	17.3	-85.5	2,058.7	5,233.7	2810	2,724.5
Jumla	**1,051.7**	**1214.4**	**1,240**	**860.1**	**15,392.7**	**19356.3**	**17,677.5**	**18,461.9**

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Mazingira ya Biashara na Uwekezaji

171. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara na Uwekezaji nchini - *BluePrint* kwa lengo la kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Katika kipindi hicho, utekelezaji wa *Blueprint* ulikuwa na mafanikio mbalimbali ikiwemo: kufutwa au kupunguzwa kwa jumla ya tozo na ada 14; kuboreshwa kwa Miundo ya Taasisi za Umma 57 zinazohusika na uwekezaji; na kuanzishwa kwa Idara ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Mfumo wa Kieletroniki wa Malipo ya Serikali (GePG) uliboreshwa ambapo hadi Desemba 2021 watoa huduma 726 walikuwa wameunganishwa katika mfumo huo.

172. Mwaka, 2021 Serikali ilifanya uchambuzi na mapitio ya tozo za Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania - TASAC zilizokuwa zikilalamikiwa na wadau wa usafirishaji majini ambapo tozo hizo zilipunguzwa kupitia Tangazo la Serikali Na.181 lililotolewa tarehe 5 Februari, 2021. Kwa upande mwingine, Serikali ilihuisha kanuni za sheria ya mawasiliano ya kielektroniki na posta zinazohusu maudhui ya utangazaji katika redio na runinga na utoaji wa leseni za utangazaji wa redio na runinga. Pamoja na mambo mengine uhuishwaji wa kanuni hizo umewezesha kufutwa kwa leseni ya kuuza vifaa vya mawasiliano na kupunguza gharama za baadhi ya leseni za utangazaji wa redio na runinga.

173. Mwaka 2021, Serikali ilifanya mapitio ya Kanuni za Misitu ambazo zimetoa fursa kwa sekta binafsi kuwekeza kwenye hifadhi za misitu asilia pamoja na kuweka viwango rafiki vya tozo katika biashara ya mazao ya misitu. Aidha, mapitio ya kanuni hizo yalitoa

fursa ya uwekezaji katika maeneo ya kufugia wanyama hai (zoo) katika hifadhi za misitu zilizopo maeneo ya jirani na miji ili kukuza utalii wa ndani na ajira kwa watanzania.

174. Mwaka 2021, Shirika la Viwango Tanzania - TBS lilisaini Hati ya Makubaliano na Wakala wa Chakula na Dawa Zanzibar - ZFDA ambapo pamoja na mambo mengine iliwezesha bidhaa za chakula zilizosajiliwa na ZFDA au TBS kutambuliwa na taasisi hizo kwa lengo la kupunguza gharama za usajili na usumbufu kwa wafanyabiashara. Aidha, Serikali iliendelea kuboresha Kituo cha Huduma ya Mahala Pamoja (One Stop Facilitation Center) katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania ambapo imeendelea kujumuisha taasisi za Serikali zikiwemo Idara ya Kazi, Idara ya Uhamiaji, Idara ya Ardhi, NEMC, TBS, OSHA, TMDA na NIDA ambazo zinazotoa vibali na leseni kwa lengo la kupunguza usumbufu na kurahisisha utoaji huduma kwa wawekezaji.

Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

175. Mwaka 2021, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iliendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Katika kipindi hicho, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 903.0 ilitolewa na mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa wajasiriamali wadogo 5,932,668 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 898.1 iliyotolewa kwa wajasiriamali 3,614,857 mwaka 2020. Kati ya mikopo hiyo, shilingi bilioni 415.4 zilitolewa kwa wanawake 3,737,581, sawa na asilimia 63.0 ya wanufaika wote na shilingi bilioni 487.6 zilitolewa kwa wanaume 2,195,087. Aidha, kiasi hicho cha mkopo kinajumuisha shilingi bilioni 81.3 zilitolewa kwa watu 640,723 wenye ulemavu, sawa na asilimia 10.8 ya wanufaika wote. Ongezeko la idadi ya wanufaika wa mikopo lilitokana na kuongezeka kwa wajasiriamali wenye sifa za kukopesheka. Mikopo iliyotolewa ilitengeneza fursa za ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa watu 7,712,468 ikijumuisha ajira 5,090,229 kwa wanawake, sawa na asilimia 66.0 na ajira 2,622,239 kwa wanaume. Mikopo iliyotolewa ilitokana na vyanzo mbalimbali ikiwemo mapato yanayotokana na miradi iliyofadhiliwa na kusimamiwa na Mifuko, misaada, michango pamoja na fedha zilizochangwa na watu binafsi, mashirika, mifuko na asasi za kitaifa na kimataifa.

176. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na vya Kati. Kupitia Mpango huo, mikopo yenye thamani ya shillingi bilioni 1.75 ilitolewa kwa kampuni 32 mwaka 2021 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shillingi milioni 934.5 iliyotolewa kwa kampuni 13 mwaka 2020. Mikopo hiyo ilitolewa kwa kampuni katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Dar Es Salaam, Dodoma, Mbeya, Kilimanjaro, Shinyanga na Geita. Ongezeko la mikopo na kampuni zilizokopeshwa lilitokana na juhudi za Serikali katika kuhamasisha kujenga uchumi shindani na viwanda kulikochangia watanzania kuhamasika kuanzisha viwanda katika sekta mbalimbali za kiuchumi. Chanzo cha fedha hizi ni Serikali kupitia Mfuko wa Hifadhi za Jamii wa NSSF.

177. Mwaka, 2021 Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ilitoa mafunzo kwa wajasiriamali na wananchi 4,787,622. Kati ya hao, wanawake walikuwa 2,824,696 sawa na asilimia 59 na wanaume walikuwa 1,962,926. Kati ya wanufaika wa mafunzo hayo, watu wenye ulemavu walikuwa 502,701 sawa na asilimia 10.5 ya wanufaika wote. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wajasiriamali ili waweze kuendesha shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo uandishi wa maandiko ya biashara, utunzaji wa vitabu vya biashara na utunzaji wa fedha.

178. Mwaka 2021, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi liliendelea kutekeleza Mkakati Jumuishi wa Taifa wa Ujasiriamali wa Mwaka 2017. Katika kipindi hicho, Baraza liliratibu utoaji wa mafunzo kwa wajasiriamali 200,988 (wanawake 129,473 na wanaume 71,515) ikilinganishwa na wajasiriamali 191,418 waliopata mafunzo mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 5.0. Ongezeko la wajasiriamali waliopata mafunzo lilichangiwa na kuhamasika kwa wananchi wanaojihusisha na shughuli mbalimbali za ujasiriamali kushiriki mafunzo hayo. Mafunzo hayo yalilenga: kuongeza ujuzi kwa wajasiriamali katika kuanzisha na kuendeleza shughuli za kiuchumi; kuwaunganisha na fursa za mitaji kutoka mifuko ya uwezeshaji, benki na taasisi za fedha; kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kurasimisha biashara na kuunda vikundi pamoja na mbinu za utafutaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi.

179. Mwaka 2021, Serikali kupitia Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iliendelea kuratibu uanzishwaji wa vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika mikoa mbalimbali kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa huduma za uwezeshaji kwa wananchi. Hadi Desemba 2021, vituo vya uwezeshaji vilivyoanzishwa viliongezeka na kufikia 17 kutoka vituo 10 vilivyoanzishwa kipindi kama hicho mwaka 2020. Kati ya hivyo, Mkoa wa Dodoma una vituo saba (7); Kigoma vituo sita (6); na Shinyanga, Singida, Geita na Rukwa kituo kimoja kila mkoa. Katika kipindi hicho, vituo vya uwezeshaji vilitoa huduma kwa wananchi 18,441 (wanaume 11,646 na wanawake 6795) ikilinganishwa na wananchi 28,541(wanaume 18,411 na wanawake 10,130) waliopata huduma mwaka 2020. Aidha, vituo vya uwezeshaji viliwezesha upatikanaji wa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 5.4 kwa wajasiriamali 2,012 kutoka katika taasisi mbalimbali za fedha na mifuko ya uwezeshaji mwaka 2021 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.74 iliyotolewa kwa wajasiriamali 6,147 mwaka 2020.

180. Mwaka 2021, Majukwaa 928 ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi yalianzishwa ikilinganishwa na Majukwaa 500 yaliyoanzishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 85.6. Ongezeko hilo lilitokana na juhudi za Serikali za kufufua Mfuko wa Rais wa Kujitegemea ili utumike katika kuimarisha majukwaa hayo kwa ajili ya kuwawezesha wanawake kupata mafunzo ya ujasiriamali na mikopo. Kati ya majukwaa yaliyoanzishwa, majukwaa 25 yapo katika ngazi ya mikoa, majukwaa 123 ngazi ya halmashauri, majukwaa 280 ngazi ya kata na majukwaa 500 ngazi ya vijiji.

Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati

181. Mwaka 2021, miradi ya kimkakati na uwekezaji ilizalisha ajira 72,395 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja ikilinganishwa na ajira 60,329 zilizozalishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 20.0. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali. Kati ya ajira zilizozalishwa, ajira 68,305 zilikuwa za wazawa sawa na asilimia 94.4 na ajira 4,090 za wageni ikilinganishwa na ajira 56,921 za wazawa na ajira 3,408 za wageni mwaka 2020. Ongezeko la wazawa waliopata ajira lilichangiwa na kuendelea kutekelezwa kwa Mwongozo wa Ushiriki wa Watanzania katika Uwekezaji na Miradi ya Kimkakati. Aidha, makandarasi wa miradi ya kimkakati waliingia mikataba na kampuni 2,019 za watanzania kwa ajili ya huduma za chakula, ulinzi, usafiri, bima na bidhaa za ujenzi mwaka 2021 ikilinganishwa na makampuni 1,015 yaliyopewa kandarasi mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 98.9. Hii ilitokana na juhudi za Serikali katika kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Ushiriki wa Watanzania katika Uwekezaji na Miradi ya Kimkakati.

Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

182. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kupokea na kuchambua miradi inayotarajiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi - PPP. Katika kipindi hicho, miradi iliyopokelewa na kuchambuliwa ilikuwa: Mradi wa Ujenzi wa Boya la Kuegesha Meli katika Bandari ya Dar es Salaam na Tanga; Miradi mitatu (3) ya Ujenzi wa Mifumo ya Uhifadhi wa Mazao ya Uvuvi wa Bahari pamoja na Ujenzi wa Kiwanda cha Kutengeneza Barafu kutoka TAFICO; Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Mazoezi Tiba kutoka Taasisi ya MOI; Miradi minne (4) ya Upanuzi wa Chuo Cha Afya na Sayansi Shirikishi; Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Awali na Msingi yenye Mchepuo wa Lugha ya Kiingereza; Mradi wa Kufufua Shamba la Ng'ombe wa Maziwa kutoka Taasisi ya Elimu Kibaha; na Mradi wa Kuanzisha Sehemu ya Vivutio vya Wanyama. Aidha, miradi hiyo ilikidhi vigezo vya kutekelezwa kwa utaratibu wa Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

183. Hadi Desemba 2021, maandiko ya miradi 54 yalikuwa katika hatua mbalimbali za uchambuzi ambapo miradi 24 ilikuwa katika hatua ya andiko dhana, miradi 8 hatua ya upembuzi yakinifu wa awali, miradi 17 hatua ya upembuzi yakinifu na miradi 5 hatua ya ununuzi wa mbia. Aidha, miradi iliyokuwa katika hatua ya ununuzi wa mbia ilikuwa: Mradi wa Ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na Ujenzi wa Kituo cha Biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; Mradi wa Kuzalisha Dawa Muhimu na Vifaa Tiba wa Bohari Kuu ya Dawa; Mradi wa Kujenga na Kuendesha Kiwanda cha Kutengeneza Simu za Kiganjani; na Mradi wa Uendeshaji wa Mabasi Yaendayo Haraka - DART awamu ya kwanza. Kwa upande mwingine, Serikali iliendelea kujenga uwezo kwa mamlaka za Serikali, sekta binafsi na taasisi za fedha katika kuibua, kuandaa, kugharamia na kutekeleza miradi ya PPP ambapo wadau 247 walipata mafunzo kuhusu dhana ya PPP, sheria na kanuni za PPP mwaka 2021.

KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA: MIRADI YA UWEKEZAJI ILIYOSAJILIWA

Jedwali Na. 31

	2020								2021							
Sekta	**A**	**B**	**C**	**D**	**E**	**F**	**G**	**H**	**A**	**B**	**C**	**D**	**E**	**F**	**G**	**H**
Kilimo	12	-	-	4	5	3	802	46	19	19	-	6	8	5	2,516	251
Maliasili	2	-	-	-	-	2	185	6	1	1	-	-	1	-	20	1
Utalii	12	-	-	3	5	4	834	47	21	21	-	5	12	4	1,786	354
Uzalishaji Viwandani	130	-	-	41	47	42	11,303	636	135	135	-	37	64	34	20,865	953
Madini	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Majengo ya biashara	10	-	-	2	6	2	789	45	24	24	-	8	12	4	3,344	1,318
Usafirishaji Mizigo	17	-	-	6	5	6	2,004	94	25	25	-	14	6	5	2,989	149
Huduma za Biashara	10	-	-	4	4	2	656	36	16	16	-	4	6	6	1,148	72
Kompyuta	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Huduma za Kifedha	-	-	-	-	-	-	-	-	4	4	-	-	3	1	2,869	574
Rasilimali watu	5	-	-	3	1	1	206	4	8	8	-	1	1	6	396	10
Mawasiliano	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Nishati	4	-	-	-	1	3	285	159	1	1	-	-	-	1	92	4
Miundombinu ya Kiuchumi	-	-	-	-	-	-	-	-	2	2	-	-	1	1	17,000	63
Utangazaji	1	-	-	1	-	-	20	1	-	-	-	-	-	-	-	-
Jumla	203	-	-	64	74	65	17,084.0	1,073.0	256	256	-	75	114	67	53,025.0	3,749.3

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

A Jumla ya Miradi Iliyosajiliwa
B Miradi Mipya
C Miradi ya Maendeleo
D Miradi ya Wazawa
E Miradi ya Wageni
F Miradi ya Ubia
G Jumla ya Ajira
H Jumla ya Thamani ya Uwekezaji (USD. Milioni)
- Takwimu Hazikupatikana

SURA YA 8

MASUALA MTAMBUKA

Mapambano Dhidi ya UKIMWI

184. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ya kupambana na UKIMWI ili kuweza kufikia malengo yaliyoainishwa katika Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI 2018/19-2022/23. Hadi Desemba 2021, Tanzania ilikadiriwa kuwa na watu milioni 1.7 waliokuwa wanaishi na Virusi vya UKIMWI kama ilivyokuwa mwaka 2020. Kati ya hao, watu milioni 1.5 sawa na asilimia 88.2 walikuwa wanatambua hali zao ikilinganishwa na watu milioni 1.4 waliokuwa wanatambua hali zao mwaka 2020. Aidha, kati ya watu wanaotambua hali zao, asilimia 98.6 wako katika tiba endelevu ya dawa za ARV na asilimia 91.0 ya wanaotumia ARV walikuwa wamefubaza virusi vya UKIMWI.

185. Mwaka 2021, Serikali iliongeza mashine za kupima wingi wa virusi vya UKIMWI na kufikia mashine 172 kutoka mashine 77 mwaka 2020. Aidha, mashine tatu (3) zenye uwezo wa kuchakata sampuli nyingi zilifungwa kwenye Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya, Hospitali ya Rufaa Temeke na Hospitali ya Bugando kwa lengo la kupunguza muda wa kusubiri majibu.

Mazingira

186. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuhimiza wawekezaji kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi ya uwekezaji kwa mujibu ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 19. Katika kipindi hicho, miradi 950 ilipata hati za Tathmini ya Athari kwa Mazingira ikilinganishwa na miradi 780 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 21.8. Hii ilichangiwa na: kuendelea kwa uhamasishaji kuhusu umuhimu wa kufanya tathmini ya athari kwa mazingira kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi; na kuzingatiwa kwa maelekezo yaliyotolewa kwa taasisi za fedha ya kutoidhinisha mikopo kwa miradi isiyokuwa na vyeti vya TAM pamoja na mamlaka za udhibiti za Serikali zinazohusika na utoaji wa vibali kutokutoa vibali kwa miradi isiyokuwa na vyeti vya TAM. Aidha, hati moja (1) ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira Kimkakati ilitolewa mwaka 2021 kama ilivyokuwa mwaka 2020 kwa lengo la kuhakikisha sera, mikakati na programu mbalimbali zinatekelezwa kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi.

187. Mwaka 2021, Serikali kupitia utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji na Utunzaji wa Miti iliwezesha upandaji wa miti 197,623,843 kwa lengo la kukabiliana na uharibifu wa ardhi na misitu ambapo miti 159,282,897 sawa na asilimia 80.6 ilistawi. Kwa upande mwingine, Serikali iliendelea kuhamasisha urejelezaji wa taka nchini kwa kutoa elimu kwa wadau mbalimbali wakiwemo wamiliki wa viwanda na

wafanyabiashara ili kupunguza taka zinazotupwa kwenye mazingira ambapo vibali 323 vilitolewa kwa ajili ya kukusanya, kuhifadhi na kusafirisha taka hatarishi ikilinganishwa na vibali 212 vilivyotolewa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 50.2. Hii ilitokana na kufanyiwa mapitio ya Kanuni ya Udhibiti wa Taka Hatarishi ya mwaka 2019.

Jedwali Na. 8.1: Vibali vya Taka Hatarishi Vilivyotolewa, Mwaka 2020-2021

Na.	Aina ya taka hatarishi	2020	2021
1.	Vyuma Chakavu	127	175
2.	Betri Chakavu	26	39
3.	Mafuta Machafu	23	50
4.	Taka za kielektroniki	20	38
5.	Mipira Chakavu	8	9
6.	Plastiki Chakavu	1	8
7	Vibali vya kusafirisha taka nje ya nchi	7	4
	Jumla	**212**	**323**

Chanzo: Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira

188. Bioanuai na ikolojia nchini huathiriwa na ongezeko la viumbe vamizi vinavyojumuisha mimea na wanyama pamoja na shughuli za binadamu zisizo endelevu ikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi. Tathmini ya viumbe vamizi ya mwaka 2021 ilionesha kuwa kulikuwa na aina 220 za viumbe vamizi wa jamii ya mimea, wanyama na wadudu. Aidha, Serikali iliendelea na utekelezaji wa mkakati wa kukabiliana na viumbe vamizi nchini kwa lengo la kupunguza athari za kiuchumi zitokanazo na kusambaa kwa viumbe hawa katika maeneo muhimu ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na hifadhi za wanyamapori.

Ulinzi na Usalama wa Raia

189. Mwaka 2021, makosa ya jinai yaliyotolewa taarifa yalipungua na kufikia 50,452 ikilinganishwa na makosa 50,689 yaliyotolewa taarifa mwaka 2020. Hii ilichangiwa na kuimarika kwa ushirikiano kati ya vyombo vya ulinzi na usalama, wananchi na wadau wengine pamoja na kuimarika kwa doria. Kati ya makosa yaliyotolewa taarifa, makosa dhidi ya binadamu yalikuwa 10,127, makosa ya kuwania mali 20,466, makosa ya uhalifu wa kifedha 752 na makosa dhidi ya maadili ya jamii 19,107.

190. Mwaka 2021, matukio makubwa 1,864 ya ajali za barabarani yaliyotolewa taarifa ikilinganishwa na matukio 1,933 yaliyotolewa taarifa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 3.6. Kati ya hayo, matukio ya ajali 1,038 yalisababisha vifo vya watu 1,368 na majeruhi 2,452. Kwa upande mwingine, matukio madogo 1,745,917 ya usalama barabarani yalitolewa taarifa ikilinganishwa na matukio 2,152,533 yaliyotolewa taarifa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 18.9. Upungufu huo ulichangiwa na utii wa sheria bila shuruti na Serikali kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya barabara.

191. Mwaka 2021, idadi ya wafungwa na mahabusu katika magereza yote nchini ilikuwa 31,005 (wafungwa 15,650 na mahabusu 15,355) ikilinganishwa na wafungwa na mahabusu 32,398 mwaka 2020. Idadi hiyo inazidi uwezo wa magereza wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,902 hivyo kusababisha msongamano. Katika kipindi hicho, Serikali ilichukua hatua mbalimbali kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu katika magereza hayo. Hatua hizo zilijumuisha kuachiliwa huru wafungwa 73 na kutoa vifungo vya nje kwa wafungwa 1,343 kupitia vikao vya Bodi ya Parole pamoja na kuachiliwa huru kwa wafungwa 10,705 kupitia msamaha wa Mheshimiwa Rais mwaka 2021 ikilinganishwa na wafungwa 73 walioachiliwa huru kwa mpango wa Parole, wafungwa 984 waliopewa vifungo vya nje na wafungwa 3,973 walioachiliwa huru kwa msamaha wa Mheshimiwa Rais mwaka 2020.

192. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kutekeleza Programu ya Huduma kwa Jamii na Huduma za Uangalizi iliyolenga kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani. Katika kipindi hicho, wafungwa 4,065 walitumikia adhabu chini ya programu hiyo ikilinganishwa na wafungwa 3,228 waliotumikia mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 25.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uelewa kuhusu adhabu mbadala miongoni mwa wadau ikiwemo Mahakama, Magereza na wadau wengine wa haki jinai.

193. Mwaka 2021, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilipokea idadi ya miito 1,941 ya matukio ya moto ikilinganishwa na miito 2,001 iliyopokelewa mwaka 2020. Kupungua kwa miito ya matukio ya moto kulichangiwa na Jeshi kutoa elimu kwa umma kuhusu kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya moto kupitia vyombo vya habari ikiwemo vipindi 47 vya televisheni na vipindi 207 vya redio. Aidha, Jeshi lilifanya ukaguzi wa kinga na tahadhari dhidi ya moto katika maeneo 62,542 mwaka 2021 ikilinganishwa na maeneo 47,818 yaliyokaguliwa mwaka 2020. Kwa upande mwingine, miito ya maokozi iliyopokelewa na Jeshi ilipungua na kufikia 706 mwaka 2021 ikilinganishwa na miito 876 iliyopokelewa mwaka 2020. Kupungua kwa miito ya maokozi kulitokana na kuendelea kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu matumizi sahihi ya namba ya dharura 114 pindi tukio linalohusu Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linapotokea.

194. Mwaka 2021, Idara ya Uhamiaji ilitoa hati za kusafiria 66,390 ikilinganishwa na hati 123,113 zilizotolewa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 46.1. Upungufu huo ulichangiwa na hatua zilizochukuliwa na mataifa mengine katika kujikinga dhidi ya maambukizi ya UVIKO-19 ikiwemo kuweka vikwazo vya kusafiri. Aidha, wageni 954,286 waliingia nchini kwa vibali halali mwaka 2021 ikilinganishwa na wageni 614,838 walioingia nchini mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 55.2. Hii ilitokana na Tanzania kuweka mkakati madhubuti wa kukabiliana na maambukizi ya UVIKO - 19 na hivyo kuvutia wageni kuingia nchini. Vilevile, wageni 892,915 walitoka nchini ikilinganishwa na wageni 563,230 waliotoka nchini mwaka 2020.

195. Mwaka 2021, Serikali ilitoa hati za ukaazi 23,490 ikilinganishwa na hati za ukaazi 16,282 zilizotolewa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 44.3. Aidha, wageni 81 walipewa uraia wa Tanzania mwaka 2021 ikilinganishwa na wageni 88 waliopewa uraia mwaka 2020. Kwa upande mwingine, Idara ya Uhamiaji ilikamata wahamiaji haramu 21,027 ikilinganishwa na wahamiaji haramu 15,266 waliokamatwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 37.7. Hii ilitokana na jitihada za Serikali katika kudhibiti wahamiaji haramu ikiwemo kufanya oparesheni za misako na doria.

196. Mwaka 2021, waomba hifadhi walikuwa 83 ikilinganishwa na waomba hifadhi na wakimbizi 275,430 mwaka 2020. Waomba hifadhi hao walitoka katika nchi za Uganda, Comoro, Somalia, Liberia, Afghanistani, Marekani, Burundi, Uingereza, Ethiopia, Bahrain, Kenya, Syria, Sudani Kusini, Yemeni na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, wakimbizi 2,163 walihamishiwa nchi ya tatu mwaka 2021 ikilinganishwa na wakimbizi 1,365 waliohamishiwa nchi ya tatu mwaka 2020. Kati ya hao, wakimbizi waliohamishiwa Australia walikuwa 10, Canada wakimbizi 269, Sweden wakimbizi 371, Marekani wakimbizi 1,512 na Uingereza mkimbizi mmoja. Vilevile, wakimbizi 30,073 walirejeshwa katika nchi zao za asili kwa hiari yao ikilinganishwa na wakimbizi 30,644 mwaka 2020.

Utambuzi na Usajili wa Watu

197. Hadi Desemba 2021, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ilitambua na kusajili wananchi 22,778,905 kutoka wananchi 22,280,625 waliotambuliwa na kusajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 2.2. Katika kipindi hicho, wageni wakaazi 34,003 na wakimbizi 234,879 walisajiliwa ikilinganishwa na wageni wakaazi 32,062 na wakimbizi 212,608 waliokuwa wamesajiliwa kipindi kama hicho mwaka 2020. Wakimbizi waliosajiliwa walitoka katika kambi za Mtendeli, Nduta na Nyarugusu (Kigoma), makazi ya Katumba na Mishamo (Katavi), kambi ya Ulyankulu (Tabora), Mtambaswala (Mtwara) pamoja na wakimbizi wenye vibali vya kuishi katika Jiji la Dar es Salaam.

198. Hadi Desemba 2021, Mamlaka ilikuwa imezalisha namba za utambulisho 19,205,774 kutoka namba za utambulisho 18,543,158 zilizokuwa zimezalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Aidha, vitambulisho vilivyotolewa na Mamlaka viliongezeka kwa asilimia 68.1 na kufikia 10,583,735 mwaka 2021 kutoka vitambulisho 6,296,037 vilivyotolewa mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na Mamlaka kuendelea kutumia mashine za kuzalisha vitambulisho zenye uwezo mkubwa.

199. Mwaka 2021, Mamlaka iliendelea kuunganisha vituo vya usajili na huduma ya mtandao wa mawasiliano ili kurahisisha usafirishaji wa taarifa baina ya vituo na makao makuu ya Mamlaka. Katika kipindi hicho, vituo 129 vya usajili viliunganishwa na

huduma ya mawasiliano ikilinganishwa na vituo 137 vilivyounganishwa mwaka 2020. Kwa upande mwingine, taasisi 57 ziliunganishwa katika mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa kwa lengo la kuziwezesha taasisi hizo kuhakiki taarifa za wananchi wanaopata huduma na hivyo kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa jamii pamoja na kuimarisha ulinzi na usalama wa wananchi.

Udhibiti wa Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu

200. Mwaka 2021, wahanga 126 wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu waliokolewa na kutafutiwa hifadhi kwenye nyumba salama na baadhi yao kuunganishwa na familia zao ikilinganishwa na wahanga 213 waliookolewa mwaka 2020. Aidha, kesi zilizofunguliwa kuhusu biashara ya binadamu zilipungua hadi kesi saba (7) mwaka 2021 kutoka kesi tisa (9) zilizofunguliwa mwaka 2020. Hii ilitokana na juhudi za Serikali za kupinga biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu kwa kutoa elimu kwa jamii na kufunga makampuni yote yaliyokuwa yanawatafutia ajira nje ya nchi watanzania wasio na ujuzi. Katika kipindi hicho, kesi sita (6) za usafirishaji binadamu zilitolewa hukumu ikilinganishwa na kesi nne (4) zilizotolewa hukumu mwaka 2020.

Msajili wa Jumuiya

201. Mwaka 2021, Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya iliendelea na jukumu la kusajili jumuiya za kidini na zisizo za kidini kwa lengo la kufuatilia utendaji na uendeshaji ili kuhakikisha jumuiya zilizosajiliwa zinazingatia sheria. Katika kipindi hicho, jumuiya 273 zilisajiliwa ikilinganishwa na jumuiya 160 zilizosajiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 70.6. Ongezeko hilo lilitokana na elimu iliyoendelea kutolewa kuhusu umuhimu wa kujisajili.

Usajili, Ufilisi na Udhamini

202. Mwaka 2021, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini ilisajili vizazi 1,789,383 ikilinganishwa na vizazi 1,434,279 vilivyosajiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 24.8. Katika kipindi hicho, vizazi vilivyosajiliwa vilihusisha watoto 1,188,677 waliosajiliwa kupitia Mpango wa Usajili kwa Watoto Walio Chini ya Umri wa Miaka Mitano. Ongezeko la usajili wa vizazi lilitokana na maboresho ya mfumo unaotumika kusajili watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano (5) katika mikoa 12 pamoja na kuanza kutumika kwa mfumo huo katika mikoa ya Arusha, Manyara, Rukwa na Katavi. Aidha, vifo 34,502 vilisajiliwa ikilinganishwa na vifo 28,531 vilivyosajiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 20.9. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuanza kutumika kwa mfumo wa usajili wa matukio ya vifo katika Mkoa wa Songwe na Mbeya. Kwa upande mwingine, Wakala uliendelea kupokea maombi kupitia mfumo wa usajili wa vizazi na vifo na uhakiki wa nyaraka kwa njia ya mtandao (E-Huduma) ambapo maombi 116,829 yalipokelewa mwaka 2021 ikilinganishwa na maombi 117,923 yaliyopokelewa mwaka 2020. Maombi hayo yalihusisha: maombi mapya ya vyeti vya

vizazi na vifo; uhakiki wa vyeti vya vizazi na vifo; na maombi ya kubadili vyeti vya kuzaliwa na vifo.

203. Mwaka 2021, Wakala ulisajili hati za viapo vya ndoa 36,645 ikilinganishwa na hati 48,193 zilizosajiliwa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 24.0. Hii ilitokana na marejesho hafifu ya hati hizo kutoka katika Mamlaka zinazofungisha ndoa kwa ajili ya kuzisajili katika Daftari la Msajili Mkuu wa Ndoa. Aidha, hati za talaka zilizosajiliwa ziliongezeka na kufikia 512 mwaka 2021 ikilinganishwa na hati za talaka 210 zilizosajiliwa mwaka 2020. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuunganishwa kwa mifumo ya RITA na mahakama ambayo ilirahisisha upatikanaji na uhakiki wa taarifa za talaka zilizotolewa hukumu. Vilevile, Wakala ilisajili hati za watoto wa kuasili 32 mwaka 2021 ikilinganishwa na hati za watoto wa kuasili 33 zilizosajiliwa mwaka 2020.

204. Mwaka 2021, Wakala ulitoa hati 77 za miunganisho ya wadhamini ikilinganishwa na hati 79 zilizotolewa mwaka 2020. Aidha, idadi ya wosia zilizoandikwa na kuhifadhiwa ziliongezeka kwa asilimia 31.9 na kufikia 149 mwaka 2021 ikilinganishwa na wosia 113 zilizoandikwa na kuhifadhiwa mwaka 2020. Hii ilichangiwa na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuandika na kutunza wosia kama sehemu ya kuepusha migogoro ya wanafamilia pindi mwenye mali anapofariki. Kwa upande mwingine, mfumo wa kielektroniki wa usajili wa bodi za wadhamini ulikamilika na kuanza kutumika ambapo jumla ya bodi 82 zilisajiliwa mwaka 2021.

Utawala Bora

205. Mwaka 2021, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilifanya chambuzi 660 za mifumo ya utendaji kazi na utoaji huduma katika sekta mbalimbali ikilinganishwa na chambuzi 863 zilizofanyika mwaka 2020. Aidha, TAKUKURU ilikagua miradi 1,257 ya maendeleo katika sekta ya maji, afya, elimu na ujenzi (barabara) mwaka 2021 ikilinganishwa na miradi 1,356 iliyokaguliwa mwaka 2020. Kutokana na ukaguzi huo, miradi 235 ilibainika kuwa na viashiria vya rushwa ambapo TAKUKURU ilianzisha uchunguzi.

206. Mwaka 2021, TAKUKURU ilikamilisha uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa 826 na kufungua kesi za rushwa 482 katika mahakama mbalimbali nchini ikilinganishwa na majalada 914 yaliyochunguzwa na kesi 484 zilizofunguliwa mwaka 2020. Katika kipindi hicho, kesi 483 zilitolewa maamuzi mahakamani na Jamhuri ilishinda kesi 293 ikilinganishwa na kesi 587 zilizotolewa maamuzi ambapo Jamhuri ilishinda kesi 446 mwaka 2020.

SURA YA 9

HALI YA UMASKINI NA MAENDELEO YA WATU

Utangulizi

207. Mwaka 2021, Serikali kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26) - FYDP III iliendelea kutekeleza Sera na Mikakati mbalimbali inayolenga kuongeza kasi ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Aidha, katika kuhakikisha kuwa nchi inafikia malengo ya Dira, Serikali iliendelea kuweka msukumo katika kujenga uchumi jumuishi wa viwanda wenye lengo la kuongeza fursa za ajira na kupunguza umaskini. Hivyo, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa unalenga kutekeleza mipango na mikakati ya kisekta pamoja na mipango mikakati ya kikanda na kimataifa ikiwemo utekelezaji wa Ajenda 2030 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii hususani katika kuinua ubora wa maisha, ustawi wa jamii na kupunguza umaskini

Hali ya Umaskini

208. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano unalenga kupunguza uwiano wa idadi ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi ya dola moja kwa siku kutoka asilimia 26.4 mwaka 2018 hadi asilimia 22 mwaka 2025/26. Aidha, uwiano huo kwa upande wa vijijini unatarajiwa kupungua kutoka asilimia 31.4 mwaka 2018 hadi asilimia 28.4 mwaka 2025/26 na upande wa mijini kutoka asilimia 15.8 mwaka 2018 hadi asilimia 13.2 mwaka 2025/26. Umaskini wa mahitaji ya msingi kwa ujumla umepungua kwa nukta ya asilimia 1.8 na kufikia asilimia 26.4 mwaka 2021 kutoka asilimia 28.2 mwaka 2012.

Kielelezo Na. 9.1: Mwenendo wa Kiwango cha Umaskini wa Mahitaji ya Msingi Vijijini na Mijini kuanzia Mwaka 2007 - 2018



209. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano unalenga kupunguza uwiano wa idadi ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini wa chakula kutoka asilimia 8.0 mwaka 2018 hadi asilimia 5.8 mwaka 2025/26. Aidha, uwiano huo kwa upande wa vijijini unatarajiwa kupungua kutoka asilimia 9.7 mwaka 2018 hadi asilimia 8.0 mwaka 2025/26 na upande wa mijini kutoka asilimia 4.4 mwaka 2018 hadi asilimia 3.1 mwaka 2025/26. Umaskini wa chakula kwa ujumla ulipungua kwa nukta ya asilimia 1.7 na kufikia asilimia 8.0 mwaka 2021 kutoka asilimia 9.7 mwaka 2012. Kupungua kwa viwango vya umaskini kulitokana na jitihada mbalimbali za Serikali ikiwemo kuendelea kuziwezesha kaya maskini kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini – TASAF pamoja na kuimarika kwa sekta ya kilimo inayotegemewa na wananchi wengi wa kipato cha chini.

Kielelezo Na. 9.2: Mwenendo wa Kiwango cha Umaskini wa Chakula Vijijini na Mijini kuanzia Mwaka 2007 - 2018



210. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuboresha hali za maisha ya watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri kupitia programu mbalimbali ikiwemo Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini. Mpango huo unatekelezwa kupitia maeneo matatu ambayo ni: kuhawilisha fedha kwa kaya maskini ili ziweze kukidhi matumizi ya kaya; kutoa ajira za muda kwa kaya za walengwa ili kuongeza kipato; na kuhamasisha uundaji wa vikundi vya kuweka akiba, kukopeshana na kuwekeza kwenye miradi ya uzalishaji mali kupitia vikundi hivyo.

211. Hadi Desemba 2021, kaya 1,279,433 zenye jumla ya wanufaika 6,396,620 zilinufaika na Mpango huo ikilinganishwa na kaya 1,087,622 zenye wanufaika 5,641,008 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ongezeko la kaya lilitokana na kuingizwa kwa kaya mpya kutoka vijiji 7,217 ambazo hazikufikiwa kipindi cha kwanza cha mpango.

Aidha, Kaya 1,992 zilizoboreka kimaisha na kuamua kujiondoa zenyewe kutoka kwenye Mpango na kaya 211,674 ambazo baada ya tathmini zimeonekana kuboreka kiuchumi hivyo kupewa muda kujiandaa kutoka katika Mpango kama taratibu zinavyoelekeza. Kati ya wanufaika hao, wanawake walikuwa 3,246,434 sawa na asilimia 50.8 na wanaume walikuwa 3,150,186. Aidha, watoto wenye umri chini ya miaka mitano wanaotakiwa kuhudhuria kliniki walikuwa 537,654 sawa na asilimia 8.4 ya wanufaika wote. Vilevile, wanufaika waliokuwa shule za msingi na sekondari wenye umri kati ya miaka 6 hadi 18 walikuwa 2,639,852, sawa na asilimia 41.3 ya wanufaika wote na wanufaika wenye umri kati ya miaka 19 hadi 60 walikuwa 2,195,971 sawa na asilimia 34.3 ya wanufaika wote. Kadhalika, wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60 walikuwa 1,023,143, sawa na asilimia 16.0 ya wanufaika wote.

Jedwali Na. 9.1: Wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Mwaka 2020 - 2021

Jinsia	Idadi ya Wanufaika		Umri				
	2020	2021	0-2	03 - 05	06-18	19-60	zaidi ya 60
Wanaume	2,778,065	3,150,186	98,461	193,155	1,447,090	1,021,249	390,231
Wanawake	2,862,943	3,246,434	83,005	163,033	1,192,762	1,174,722	632,912
Jumla	5,641,008	6,396,620	181,466	356,188	2,639,852	2,195,971	1,023,143
Asilimia ya wanufaika wote			**2.8**	**5.6**	**41.3**	**34.3**	**16**

Chanzo: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii

212. Hadi Desemba 2021, shilingi bilioni 1,047.7 zilitolewa kupitia uhawilishaji fedha kwa wanufaika wote ikilinganishwa na shilingi bilioni 858.4 zilizotolewa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 22.1. Hii ilitokana na ongezeko la kaya mpya kutoka katika vijiji 7,217 ambazo hazikuwa zimefikiwa katika kipindi cha kwanza cha Mpango. Kwa upande mwingine, vikundi 30,648 kutoka katika kaya maskini vyenye wanachama 421,353 viliundwa na kuweka akiba ya shilingi bilioni 6.2 mwaka 2021 ikilinganishwa na vikundi 23,618 vyenye wanachama 319,940 na akiba ya shilingi bilioni 5.9 mwaka 2020, sawa na ongezeko la vikundi kwa asilimia 29.8. Ongezeko hilo lilitokana na wananchi kuhamasika kuunda vikundi vya kuweka akiba na kukopeshana pamoja na kutambua umuhimu wa kuweka akiba kwa ajili ya maendeleo ya shughuli za uzalishaji mali zinazofanywa na walengwa.

213. Mwaka 2021, jumla ya shilingi bilioni 2.9 zilikopeshwa kwa wanachama wa vikundi kwa ajili ya kuanzisha au kuendeleza shughuli za uzalishaji mali ikilinganishwa na mikopo ya shilingi bilioni 2.5 mwaka 2020. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa wanachama wa vikundi kuhusu namna ya kuanzisha au kuendeleza shughuli za uzalishaji ili kuongeza tija katika shughuli za kiuchumi wanazofanya. Kupitia ruzuku zilizotolewa kwa wanufaika na mikopo ya vikundi, walengwa wameweza kuboresha maisha kwa kuanzisha shughuli za kiuchumi ikiwemo kilimo na biashara ndogondogo. Hadi

Desemba 2021, kaya 573,227 zilianzisha miradi ya kilimo, kaya 38,600 miradi ya ufugaji na kaya 210,850 biashara ndogondogo. Katika miradi ya ufugaji kulikuwa na jumla ya ng'ombe 51,300, mbuzi 2,757,000, kuku 12,150,000, nguruwe 785,700, kondoo 194,610 na bata 217,200.

Maendeleo ya Watu

214. Mwaka 2021, Serikali iliendelea na juhudi za kuboresha maendeleo ya watu kwa lengo la kuinua viwango vya maisha. Maendeleo ya watu ni kipimo muhimu cha maendeleo na ustawi wa nchi kwa ujumla na huboreshwa kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma muhimu ikiwemo maji, elimu na afya. Aidha, maendeleo ya watu huathiriwa na masuala mbalimbali ikijumuisha wastani wa idadi ya watu kwa kaya, uwiano wa utegemezi na rushwa.

215. Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18, wastani wa idadi ya watu kwa kaya kwa Tanzania Bara ulipungua na kufikia watu 4.6 kwa kaya mwaka 2018 kutoka wastani wa watu 5.0 kwa kaya mwaka 2012. Katika maeneo ya vijijini, wastani wa idadi ya watu kwa kaya ulipungua kutoka watu 5.3 kwa kaya mwaka 2012 hadi watu 4.9 kwa kaya mwaka 2018. Aidha, wastani wa idadi ya watu kwa kaya kwa jiji la Dar es Salaam uliendelea kuwa asilimia 4.0 kama ilivyokuwa mwaka 2012 na maeneo mengine ya mijini, wastani wa idadi ya watu kwa kaya ulipungua kutoka watu 4.7 kwa kaya mwaka 2012 hadi watu 4.3 kwa kaya mwaka 2018. Vilevile, Mkoa wa Simiyu ulikuwa na wastani mkubwa wa watu 6.7 kwa kaya na Mkoa wa Mbeya ulikuwa na wastani mdogo wa watu 3.7 kwa kaya. Kupungua kwa idadi ya watu kwa kaya kunatoa fursa kwa mkuu wa kaya kuweza kumudu mahitaji ya msingi ya kaya na Serikali kuweza kusogeza karibu zaidi huduma za msingi kwa jamii hizo hususani elimu na afya katika viwango stahiki.

Jedwali 9.2: Wastani wa Idadi ya Watu kwa Kaya Kuanzia Mwaka 1992 – 2018

Mwaka	Dar es salaam	Maeneo mengine ya Mijini	Maeneo ya Vijijini	Tanzania Bara
1992	4.8	4.9	5.9	5.7
2001	4.3	4.5	5.1	4.9
2007	3.7	4.4	5.1	4.8
2012	4.0	4.7	5.3	5.0
2018	4.0	4.3	4.9	4.6

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Kielelezo 9.3: Wastani wa Idadi ya Watu kwa Kaya katika Ngazi ya Mikoa Mwaka 2017/18



216. Wastani wa uwiano wa utegemezi huonesha idadi ya wategemezi wenye umri wa miaka 0-14 pamoja na wazee wenye umri wa miaka 65 au zaidi ikilinganishwa na nguvu kazi ya Taifa inayojumuisha watu wenye umri wa miaka 15 - 64. Matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi ya Mwaka 2017/18 yanaonesha kuwa uwiano wa utegemezi ulikuwa 0.48 mwaka 2018 kama ilivyokuwa mwaka 2012. Aidha, uwiano wa watu tegemezi katika maeneo ya vijijini ulikuwa 0.51 ikilinganishwa na uwiano wa 0.43 katika maeneo mengine ya mijini. Vilevile, mikoa ya Simiyu na Mara ilikuwa na uwiano mkubwa wa utegemezi wa 0.55 kila mmoja na Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na uwiano mdogo wa utegemezi wa 0.35. Mikoa 14 ilikuwa na uwiano wa juu zaidi ya uwiano wa kitaifa wa 0.48 ikiashiria kuwa mikoa hiyo ina wategemezi wengi zaidi. Aidha, uwiano huo, haujazingatia wanafunzi wenye zaidi ya miaka 14 na walemavu wasioweza kufanya kazi.

Kielelezo 9.4: Uwiano wa Utegemezi Mwaka 1992 – 2018



Kielelezo 9.5: Uwiano wa Utegemezi Katika Ngazi ya Mikoa Mwaka 2017/18



217. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kudhibiti vitendo vya rushwa katika sekta na mashirika ya umma ili kuimarisha upatikanaji wa huduma muhimu pamoja na ustawi wa jamii. Katika kipindi hicho, Taarifa ya Transparency International (TI) ya mwaka 2021 ilionesha kuwa Tanzania ilipata alama 39 kati ya alama 100 ya fahirisi ya rushwa ikilinganishwa na alama 38 mwaka 2020. Alama hiyo ipo juu ya wastani wa alama 36 zilizopata Nchi za Ulaya Mashariki na Asia ya Kati pamoja na wastani wa alama 33 zilizopata Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hii inaashiria kuendelea kuimarika kwa jitihada za kupambana na vitendo vya rushwa nchini. Aidha, Tanzania imeshika nafasi ya 87 kati ya nchi 180 katika kupambana na vitendo vya rushwa ikiwa imepanda kwa nafasi saba (7) kutoka nafasi ya 94 mwaka 2020. Mikakati inayochukuliwa na Serikali kupambana na rushwa ina lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma za msingi kwa wananchi ikiwemo elimu, maji na afya.

SEHEMU YA TATU

SUALA MAALUMU KIMAENDELEO

SURA YA 10

TATHMINI YA ATHARI ZA KIUCHUMI NA KIJAMII ZA UVIKO - 19

Utangulizi

218. Ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya korona ujulikanao kama UVIKO - 19 ulianzia nchini China mwishoni mwa mwaka 2019 na kusambaa kwa kasi katika nchi mbalimbali duniani. Mwezi Machi 2020, Shirika la Afya la Kimataifa - WHO lilitangaza UVIKO - 19 kuwa janga la dunia linaloathiri afya na uchumi kwa ujumla kutokana na kuvurugika kwa mfumo wa uzalishaji na uhitaji wa huduma na bidhaa (disruption in supply and demand chain). Hadi Desemba 2021, dunia ilikumbwa na mawimbi matatu ya UVIKO - 19 ambapo maambukizi kwa ujumla yalifikia 290,681,556 na vifo 5,450,282 kwa mujibu wa takwimu za WHO. Katika kipindi hicho, shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii duniani ziliathiriwa ikiwemo huduma za fedha, bidhaa, huduma, usafiri na usafirishaji, biashara, utalii na viwanda. Hali hiyo ilitokana na hatua kadhaa za awali zilizochukuliwa na nchi mbalimbali duniani ikiwemo kulazimisha wananchi kubaki majumbani (lockdown) pamoja na kuzuia mikusanyiko ya watu ambazo zilisababisha kusitishwa kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Kutokana na hayo, uchumi wa dunia uliporomoka na kukua kwa kiwango hasi cha asilimia 3.6 mwaka 2020 ikiwa ni miaka kumi na mbili (12) tangu hali kama hiyo ya kuporomoka kwa uchumi ilipojitokeza tena mara ya mwisho mwaka 2009 ambapo uchumi wa dunia ulikua kwa asilimia hasi 1.7 kufuatia mdororo wa sekta ya fedha duniani.

219. Tanzania kama nchi nyingine iliathirika na UVIKO - 19 ambapo Machi 2020, Serikali ilitangaza rasmi uwepo wa mgonjwa wa kwanza mwenye maambukizi ya ugonjwa huo katika Jiji la Arusha. Hadi Desemba 2021, jumla ya sampuli 325,728 zilipimwa ambapo sampuli 26,115 zilithibitika kuwa na maambukizi na jumla ya watu 725 walipoteza maisha. Hata hivyo, Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi 11 kati ya 45 za Kusini mwa Jangwa la Sahara zilizokuwa na ukuaji chanya wa uchumi wa asilimia 4.8 mwaka 2020. Mwenendo huo ulitokana na nchi kutochukua sera ya kulazimisha wananchi kubaki majumbani (lockdown) na hivyo wananchi kuendelea na shughuli za kiuchumi pamoja na kutofunga mipaka ya nchi wakati wakiendelea kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya ya namna ya kujikinga na UVIKO - 19. Pamoja na ustahimilivu (resilience) wa uchumi wa Tanzania ikilinganishwa na nchi nyingine, hatua zilizochukuliwa na nchi nyingine duniani katika kukabiliana na athari za UVIKO - 19 zilianza kuathiri uchumi wa Tanzania.

220. Pamoja na athari za kiafya zinazojumuisha vifo, ongezeko la gharama za madaktari na watumishi wa afya, vifaa na vifaa tiba, dawa, vitendanishi na vituo vya kuhudumia wagonjwa, tathmini ya kiuchumi ilionesha kuwa kuna maeneo mengine yaliyoathirika na UVIKO -19. Maeneo hayo ni pamoja na kupungua kwa ukuaji wa

uchumi, kupungua kwa mikopo kwa sekta binafsi, kudorora kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi hususan biashara, utalii na huduma kama usafirishaji, malazi, chakula, vinywaji na burudani.

MWENENDO WA VIASHIRIA MBALIMBALI

221. Sehemu hii inaonesha mwenendo wa baadhi ya maeneo yaliyoathirika kutokana na UVIKO - 19. Maeneo hayo ni pamoja na:

Ukuaji wa Uchumi

222. Kabla ya kuingia kwa UVIKO - 19, uchumi wa Tanzania ulikuwa unakua kwa wastani wa asilimia 6.5 hadi 7.0. Baada ya UVIKO - 19 kuingia, kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 4.8 kati ya mwaka 2020 na 2021. Hii ilisababishwa na athari ya hatua zilizochukuliwa na mataifa mbalimbali duniani katika kupambana na UVIKO - 19 ikiwemo kuzuia safari za anga. Hata hivyo, hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali ikiwemo kuruhusu wananchi kuendelea na shughuli za kiuchumi, utekelezaji wa Mpango wa kukabiliana na athari za UVIKO - 19 na miradi mbalimbali ya maendeleo zilinusuru uchumi wa nchi kutoporomoka kwa kiwango kikubwa. Pamoja na kuporomoka, Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi 11 za Kusini mwa Jangwa la Sahara zilizokuwa na ukuaji chanya mwaka 2020 kati ya nchi 45.

Biashara ya Bidhaa na Huduma Nje

223. Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yalipungua kwa asilimia 11.4 kufikia dola za Marekani milioni 8,555.5 mwaka 2020 kutoka dola za Marekani milioni 9,658.6 mwaka 2019 kabla ya UVIKO - 19. Athari kubwa ilitokana na kufungwa kwa mipaka na kupungua kwa idadi ya watalii kufuatia katazo la kutosafiri lililowekwa na mataifa wabia wakubwa wa biashara ya utalii kwa Tanzania. Hata hivyo, baada ya kuondolewa kwa vikwazo hivyo na uhamasishaji wa elimu ya chanjo, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 15.8 na kufikia dola za Marekani milioni 9,907.40 mwaka 2021.

Mikopo kwa Sekta Binafsi

224. Sekta ya huduma za fedha ilipungua kasi ya ukuaji kutoka asilimia 4.5 mwaka 2019 hadi asilimia 3.1 mwaka 2020 kabla ya kuanza kuimarika tena na kufikia asilimia 5.3 mwaka 2021. Mikopo kwa sekta binafsi ilipungua kutoka wastani wa asilimia 11.1 mwaka 2019 kabla ya UVIKO - 19 hadi asilimia 3.1 mwaka 2020 kutokana na athari za UVIKO - 19 kwenye baadhi ya biashara hususan za wajasiriamali wadogo na shughuli za uwekezaji katika sekta za usafiri na mawasiliano. Aidha, kufuatia kuyumba kwa shughuli za kiuchumi ikiwemo biashara, mikopo chechefu iliongezeka hadi asilimia 9.8 mwaka 2020.

225. Mwaka 2021, mikopo chechefu ilipungua hadi asilimia 8.5 na kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 10.0. Ongezeko la

mikopo kwa sekta binafsi lilitokana na hatua mbalimbali za kisera zilizochukuliwa na Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ili kuchochea shughuli za kiuchumi. Hatua hizo ni pamoja na kuanzishwa kwa mfuko maalum wenye thamani ya shilingi trilioni moja ambao unatumika kukopesha mabenki na taasisi nyingine za fedha kwa riba ya asilimia 3 ili kutoa mikopo ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10; kuondoa sharti la uzoefu wa kufanya biashara kwa angalau miezi 18 kwa waombaji wa biashara ya uwakala wa benki, badala yake, waombaji watatakiwa kuwa na kitambulisho cha Taifa au namba ya kitambulisho cha Taifa; kuweka ukomo wa kiwango cha riba kinachotolewa na benki za biashara kwenye akaunti za kampuni za simu zinazotoa huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi; na kupunguza kiwango cha mtaji kinachotakiwa kuwekwa na benki za biashara kwa ajili ya kutoa mikopo.

Mapato ya Ndani

226. Mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya kodi, mapato yasiyo ya kodi na mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalipungua kwa asilimia 2.2 kufikia shilingi bilioni 20,594.7 mwaka 2020/21 kutoka shilingi bilioni 21,051.8 mwaka 2019/20. Hii ilitokana na athari hasi za UVIKO - 19 zilizosababisha ukusanyaji wa baadhi ya kodi kutofikia malengo ikiwemo kodi zinazotozwa kwenye sekta ya utalii na bidhaa kutoka nje, tozo/ada za visa, kodi zinazolipwa na hoteli, ada za viingilio kwenye viwanja vya michezo na maeneo ya sanaa na burudani. Hata hivyo, hadi mwezi Machi 2021/22, mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yaliongezeka kwa asilimia 17.2 kufikia shilingi bilioni 18,106.8 kutoka shilingi bilioni 15,454.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Ongezeko la makusanyo lilitokana na utekelezaji madhubuti wa Mpango wa Kukabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi Zitokanazo na UVIKO - 19 (TCRP) pamoja na hatua mbalimbali za usimamizi madhubuti wa sera za kibajeti na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato.

Usafiri wa Anga

227. Kutokana na katazo la safari za anga kufuatia mlipuko wa UVIKO-19, jumla ya mashirika 21 ya kimataifa ya ndege yalifuta safari 632 zilizopangwa kufanyika kuja nchini kuanzia tarehe 20 Machi 2020. Hatua hii ilisababisha kudorora kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi hususan biashara na huduma kama usafirishaji wa chakula, vinywaji na burudani. Aidha, mapato ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga yalidorora kwa kuzingatia kuwa takribani asilimia 60 ya mapato ya sekta ya usafirishaji yanatokana na safari za kimataifa na asilimia 40 safari za ndani ya nchi. Hii ilitokana na kupungua kwa safari za ndege hadi 121,255 mwaka 2020 ikilinganishwa na safari 292,105 mwaka 2019; kupungua kwa idadi ya abiria wa usafiri wa anga nchini hadi 2,773,539 mwaka 2020 ikilinganishwa na abiria 5,487,679 mwaka 2019; na kupungua kwa miruko ya ndege nchini hadi 59,262 mwaka 2020 kutoka miruko 5, 487,679 mwaka 2019.

228. Mwaka 2021, safari za ndege ziliongezeka na kufikia 153,322 ikilinganishwa na safari 121,255 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 26.4. Katika kipindi hicho, idadi ya abiria waliosafiri kwa njia ya anga ndani na nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 38.0 na kufikia 3,827,957 mwaka 2021 ikilinganishwa na abiria 2,773,539 waliosafiri mwaka 2020. Aidha, mizigo iliyosafirishwa ilikuwa tani 30,029 mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 24,452 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 22.8. Kuongezeka kwa safari za ndege na mizigo iliyosafirishwa kulitokana na mataifa mengi kuondoa katazo la safari za anga. Vilevile, Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania - TCAA ilisajili ndege nane (8) ikilinganishwa na ndege nne (4) zilizosajiliwa mwaka 2020. Ongezeko hilo, lilitokana na baadhi ya nchi kulegeza masharti ya kijikinga na maambukizi ya UVIKO - 19.

Utalii

229. Biashara ya utalii na huduma ziliathirika kutokana na athari za UVIKO - 19 hususan kusitishwa kwa safari za anga ili kukabiliana na maambukizi ya UVIKO - 19. Mwaka 2020, idadi ya watalii waliotembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini ilipungua hadi 620,867 kutoka zaidi ya watalii 1,527,230 waliotembelea vivutio hivyo kabla ya UVIKO - 19 mwaka 2019, sawa na punguzo la asilimia 59.3. Aidha, mapato yatokanayo na sekta ya utalii yalipungua kwa asilimia 72.5 kutoka dola za marekani milioni 2,604 mwaka 2019 hadi dola za Marekani milioni 715 mwaka 2020 kutokana na kupungua kwa shughuli za utalii na idadi ya watalii nchini. Vilevile, ukusanyaji wa mapato kwenye Taasisi za utalii ikiwemo Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania - TANAPA, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro - NCAA na Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori Tanzania - TAWA uliathiriwa na UVIKO - 19 ambapo mwaka 2020 makusanyo ya mapato katika taasisi hizo yalipungua kwa asilimia 66.4 hadi shilingi bilioni 154.4 kutoka bilioni 460.4 mwaka 2019.

230. Mwaka 2021, biashara ya utalii ilianza kuimarika, ambapo idadi ya watalii waliotembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini iliongezeka kwa asilimia 48.6 na kufikia 922,692 ikilinganishwa na watalii 620,867 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na kusitishwa kwa katazo la kusafiri baada ya kupatikana kwa chanjo ya UVIKO-19 pamoja na jitihada zilizochukuliwa na Serikali katika kupambana na maambukizi ya UVIKO -19 ikiwa ni pamoja na matumizi ya *National Standard Operating Procedures (SOP)* ambazo zimesaidia kuonesha kuwa Tanzania ina mkakati madhubuti wa kupambana na ugonjwa huo na hivyo kuvutia watalii. Aidha, mapato yatokanayo na biashara ya utalii yaliongezeka kwa asilimia 74.5 na kufikia dola za Marekani milioni 1,248 mwaka 2021 kutoka dola za marekani milioni 715 mwaka 2020. Vilevile, mapato kwenye Taasisi za utalii za TANAPA, NCAA na TAWA yaliongezeka kwa asilimia 62.9 na kufikia shilingi bilioni 251.5 mwaka 2021. Kuongezeka kwa mapato kulichangiwa na sekta kuanza kuimarika kutokana na kupungua kwa athari za UVIKO - 19.

Malazi na Huduma ya Chakula

231. Sekta ya malazi na huduma ya chakula ilikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 13.7 mwaka 2020 kutoka ukuaji chanya wa asilimia 2.6 mwaka 2019. Kuporomoka kwa ukuaji ni kwa kuwa sekta hii kwa kiasi kikubwa inahusisha shughuli za utalii zilizoathiriwa na UVIKO - 19. Hata hivyo, sekta ya malazi na huduma ya chakula imeanza kuwa na ukuaji chanya wa asilimia 6.7 mwaka 2021 kufuatia kuanza kuimarika kwa shughuli za utalii. Kabla ya UVIKO - 19 sekta hii ilikuwa inakua kwa wastani wa asilimia 3.3 kwa mwaka.

Biashara

232. Biashara za jumla na rejareja zilipungua hususan zile zilizohusu bidhaa zinazoagizwa kutoka nchi kama China, India na baadhi ya nchi za Ulaya na nchi majirani ambazo zilifunga mipaka. Kasi ya ukuaji wa sekta hii ilipungua hadi asilimia 2.1 mwaka 2020 kutoka asilimia 5.5 mwaka 2019 kabla ya UVIKO - 19. Hata hivyo, hali hiyo imeanza kuimarika kufuatia kufunguka kwa shughuli za kiuchumi ambapo mwaka 2021 kiwango cha ukuaji wa sekta ya biashara kiliongezeka kufikia asilimia 3.5.

Sekta ya Afya

233. Mlipuko wa UVIKO - 19 umekuwa na athari za kiafya zinazojumuisha maambukizi na vifo vingi ambapo hadi Desemba 2021, kati ya jumla ya sampuli 325,728 zilizopimwa, sampuli 26,115 zilithibitika kuwa na maambukizi na watu 725 walipoteza maisha nchini. Katika kukabiliana na janga hili, gharama za uendeshaji wa sekta hii ziliongezeka ambapo mgao wa fedha kwenda katika sekta hii muhimu uliongezeka kutoka shilingi bilioni 1,535.4 zilizotolewa mwaka 2019/20 hadi shilingi bilioni 1,626.1 zilizotolewa mwaka 2020/21 na bajeti iliyotengwa kwa mwaka 2021/22 imeongezeka hadi shilingi bilioni 2,512. Ongezeko hilo ni kutokana na changamoto ya upungufu wa vifaa na vifaa tiba, vitendanishi, miundombinu ya kutolea huduma za afya na upungufu wa watalaam wa sekta ya afya kufuatia kuongezeka kwa wagonjwa.

234. Katika kupambana na UVIKO - 19 kupitia Mpango wa TCRP, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 466.9 kitakachotumika kwa mwaka mmoja hadi Juni 2022 kwa ajili ya kugharamia mahitaji yaliyoongezeka kutokana na upungufu uliojitokeza katika sekta ya afya. Fedha hizo zimetumika kugharamia ugomboaji na usambazaji wa chanjo (deployment cost) kwa lengo la kupunguza maambukizi; ununuzi wa vifaa na vifaa tiba, dawa, vitendanishi na vituo vya kutolea huduma za afya ikiwemo mitambo ya kuzalisha hewa ya Oksijeni; ujenzi wa nyumba na vifaa vya huduma za dharura (EMD) na vyumba vya wagonjwa mahututi (ICU); vifaa vya vipimo vya mionzi (X-RAY, CT-SCAN, MRI); na ununuzi wa magari yakiwemo ya kubebea wagonjwa (ambulance). Vilevile, fedha zilitumika kuajiri watumishi 179 wa kutoa huduma ya afya kwa muda wa miezi sita ikiwemo mtaalamu wa teknolojia ya mionzi (Radiographer), fundi sanifu vifaa tiba

(Biomedical Technician) na afisa TEHAMA (ICT) na taratibu za kuwaombea kibali cha ajira ya kudumu baada ya mradi kufika mwisho zinaendelea.

HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA ATHARI ZA UVIKO - 19

Mikakati ya Kuimarisha Sekta ya Afya

235. Hadi Desemba 2021, Serikali iliendelea kutekeleza hatua mbalimbali za kiutawala na mikakati ya kiafya katika kukabiliana na maambukizi ya UVIKO - 19 ikiwemo kuhamasisha jamii kuchukua hatua madhubuti za kujikinga na ugonjwa. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni: kuzuia mikusanyiko kama michezo na hata ibada; kudhibiti safari za ndani zisizo za lazima; kusisitiza uvaaji wa barakoa na kuosha mikono kwa vitakasa mikono; kusitisha kwa muda masomo katika ngazi zote za elimu; kutoa elimu kwa jamii juu ya dalili na namna ya kujikinga na UVIKO - 19; kujenga na kuimarisha maeneo maalum ya kutenga na kutibu wagonjwa; kuhamasisha matumizi ya tiba asili badala ya kutegemea tiba za kisasa pekee; kuimarisha taasisi za uchunguzi na utafiti wa tiba/dawa asili; na kusambaza vifaa na vifaa tiba katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo vipima joto, magari ya kubeba wagonjwa na mavazi maalum ya kujikinga yanayotumiwa na madaktari na wahudumu wa afya.

236. Serikali ilichukua hatua za muda mrefu za kujikinga na ugonjwa wa UVIKO - 19 ikiwemo: kuridhia matumizi ya chanjo za UVIKO - 19 kama moja ya afua ya kinga dhidi ya ugonjwa huo ambapo hadi Machi 2021, dozi 11,233,374 za chanjo zilipokelewa. Kati ya hizo, chanjo aina ya Janssen zilikuwa dozi 3,722,940, Sinopharm dozi 4,216,964, Pfizer dozi 2,110,680, Sinovac dozi 1,000,000 na Moderna dozi 376,320. Hadi Machi 2022, jumla ya watu milioni 3.6 walipata dozi kamili ya chanjo kati ya lengo la watu takribani milioni 30.7 wenye umri wa miaka 18 na kuendelea, sawa na asilimia 11.7 ya lengo. Kwa upande mwingine, Serikali ilinunua na kufunga mitambo saba (7) ya hewa tiba ya Oksijeni katika hospitali mbalimbali; ilifungua maabara mpya yenye mashine tano (5) zenye uwezo wa kupima sampuli 1,800 kwa siku; iliongeza idadi ya madaktari na watoa huduma wa afya ikiwemo kutoa ajira za watumishi wa sekta ya afya 1,000; na iliongeza maabara za uchunguzi wa UVIKO – 19 na kufikia maabara 10 mwaka 2021 kutoka maabara tatu (3) mwaka 2020.

Mikakati ya Kuimarisha Uchumi

237. Mbali ya hatua za kiafya, Serikali ilitekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha uchumi. Hatua hizo ni pamoja na:

i. Kutoa unafuu wa kodi kwa kupunguza ushuru wa forodha hadi asilimia 0 kutoka viwango vya awali vya asilimia 10 na asilimia 25 kwenye malighafi zinazopatikana nchini ili kuwezesha upatikanaji wa vifaa, vifaa tiba, dawa na vitendanishi kwa gharama nafuu na kuhamasisha uzalishaji wa vifaa hivyo na bidhaa maalumu hapa nchini vinavyotumika katika kupambana na ugonjwa wa

homa kali ya mapafu UVIKO - 19 ikiwemo barakoa (masks), kipukusi (sanitizer), mashine za kusaidia kupumua (ventilators), na mavazi maalum ya kujikinga yanayotumiwa na madaktari na wahudumu wa afya (PPE);

ii. Kugharamia mahitaji ya Taasisi za sekta ya utalii za TANAPA, NCAA na TAWA zilizoathiriwa na UVIKO - 19 ikiwemo mishahara ya watumishi, matumizi mengineyo na matumizi ya maendeleo yaliyokuwa yakigharamiwa na mapato ya ndani ya taasisi hizo. Mwaka 2020/21, jumla ya shilingi bilioni 350.63 zilifanyiwa uhamisho kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji katika taasisi husika. Aidha, mahitaji ya bajeti ya taasisi hizo yaliingizwa kwenye mfumo wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22, ambapo shilingi bilioni 441.1 zilitengwa na hadi Machi 2022 shilingi bilioni 283 zilitolewa. Mchanganuo wa fedha zilizotengwa na kutolewa ni kama zinavyoonekana katika **Jedwali Na. 10.1**

Jedwali Na.10.1: Matumizi ya Fedha za Taasisi za Utalii (Shilingi Bilioni)

	2020/21 (Halisi)				**2021/22 (Bajeti)**	**Machi 2021/22 (Fedha zilizotolewa)**
Taasisi	**Matumizi ya maendeleo**	**Matumizi ya kawaida**	**Mishahara**	**Jumla**		
TANAPA	26.51	104.50	74.01	**205.03**	246.4	151.7
NCAA	9.72	65.79	21.95	**97.47**	121	82.9
TAWA	4.03	39.62	4.42	**48.13**	73.7	48.4
Jumla	**40.33**	**209.92**	**100.38**	**350.63**	**441.1**	**283**

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

iii. Kupunguza kiwango cha riba kinachotozwa kwa benki kukopa Benki Kuu (discount rate) kutoka asilimia 7 hadi asilimia 5 ili kupunguza gharama za upatikanaji wa mikopo na kuongeza wigo wa benki za kibiashara kukopa kwa riba nafuu kwa lengo la kupunguza riba ya mikopo kwa wateja;

iv. Kupunguza kiwango cha chini cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu ya Tanzania (Statutory Minimum Reserve Requirement) kutoka asilimia 7 hadi asilimia 6 ili kuongeza ukwasi katika sekta ya benki na hivyo kuwezesha benki kutoa mikopo kwa sekta binafsi.

v. Taasisi za umma kutumia mifumo ya kielektroniki katika kufanya shughuli mbalimbali kama vile mikutano kwa njia ya mtandao; ukusanyaji wa takwimu; mafunzo; miamala ya fedha; na mifumo ya huduma za afya;

vi. Kuimarisha zaidi Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF na kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo ya gharama nafuu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati (SME financing) pamoja na kuhakikisha halmashauri zinatenga fedha asilimia 10

ya mapato kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kama Sheria inavyotaka;

vii. Benki na taasisi za fedha zilitoa unafuu katika urejeshwaji wa mikopo (loan rescheduling) ikiwemo kuongeza muda wa urejeshaji wa mikopo ili kusaidia wateja wao katika sekta ambazo biashara zao zimeathiriwa na UVIKO - 19;

viii. Kufanya mazungumzo na wakopeshaji ili kunufaika na hatua ya unafuu wa madeni (*debt relief from external creditors*) kwa mataifa maskini duniani ikiwemo Tanzania. Mpango huo ulihusisha kuahirisha malipo ya madeni yanayoiva kwa kipindi kilichoanzia Mei 2020 hadi Desemba 2021. Katika kipindi hicho, kiasi cha shilingi bilioni 301.9 sawa na dola za Marekani milioni 131.3 kiliahirishwa ili ahueni hiyo itumike kukabiliana na athari za UVIKO - 19 na kunusuru uchumi. Aidha, Serikali ilikamilisha mazungumzo ya kupatiwa msamaha wa madeni kutoka Shirika la Fedha la Kimatifa - IMF kupitia dirisha la Catastrophe Containment Relief Trust (CCRT) wenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 60.5 sawa na dola za Marekani milioni 25.5 uliotolewa kwa awamu mbili za mwezi Agosti 2020 na Februari 2021. Msamaha huo ulisaidia kuongeza nguvu za kukabiliana na athari za UVIKO - 19 katika sekta za huduma za jamii na utalii; na

ix. Kutekeleza Mpango wa kukabiliana na athari za kijamii na kiuchumi zitokanazo na UVIKO-19 - TCRP kupitia fedha za mkopo wenye masharti nafuu kutoka IMF ili kuimarisha sekta zilizoathirika zaidi ikiwemo maji, afya, elimu na utalii.

MPANGO WA KUKABILIANA NA ATHARI ZA KIJAMII NA KIUCHUMI ZITOKANAZO NA UVIKO - 19

238. Kufuatia mlipuko wa UVIKO-19, Serikali iliandaa na kuanza utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO - 19 (TCRP) uliozinduliwa rasmi mnamo tarehe 10 Oktoba 2021 na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mpango huo unatekelezwa kupitia mkopo nafuu usio na riba wenye thamani ya shilingi bilioni 1,310.7 sawa na dola za Marekani milioni 567.25 kutoka IMF. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1,079.6 ni kwa ajili ya Tanzania Bara, sawa na dola za Marekani milioni 467.3 na shilingi bilioni 231.0, sawa na dola za Marekani milioni 100 kwa ajili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

239. Lengo la Mpango huo ni kupambana na maambukizi ya UVIKO - 19 pamoja na kuimarisha sekta za kiuchumi na kijamii zilizoathiriwa na UVIKO - 19. Fedha hizo zilielekezwa katika ujenzi wa madarasa ili kupunguza msongamano; ugharamiaji wa huduma za chanjo; elimu kwa umma; huduma za afya (kukinga na kutibu); upatikanaji wa maji tiririka safi na salama; kuwainua kiuchumi watu wa kipato cha chini na kuimarisha sekta ya utalii. Sekta zilizohusika katika Mpango kwa Tanzania Bara ni afya,

elimu, utalii, maji, biashara ndogo ndogo kupitia makundi maalum ya vijana, wanawake na wenye ulemavu na kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF. Mchanganuo wa mgawanyo wa fedha ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 10.2**.

Jedwali Na.10.2: Mgawanyo wa Fedha kwa ajili ya TCRP Kutoka IMF

Maeneo Makuu	Kiwango cha kubadilishia fedha dhidi ya dola za Marekani			**2,310.33**
	USD (Milioni)	**Shilingi Bilioni**	**Asilimia ya fedha kutoka IMF**	**Wizara/Taasisi inayohusika**
Sekya ya Maji	60.3	139.4	10.6	Wizara ya Maji
Sekta ya Afya				
o/w Wizara ya Afya	114.1	263.7	20.1	Wizara ya Afya
Afya Msingi - TAMISEMI	87.9	203.2	15.4	TAMISEMI
Sekta ya Elimu				
o/w Wizara ya Elimu	28.1	64.9	5	Wizara ya Elimu
TAMISEMI	131.6	304	23.2	TAMISEMI
Wajasiriamali wadogo (Vijana, Wanawake na Wenye Ulemavu)	2.2	5	0.4	
Kaya Maskini	2.4	5.5	0.4	TASAF
Sekta ya Utalii	39	90.2	6.9	Maliasili na Utalii
Ofisi ya Waziri Mkuu	1.5	3.469	0.3	Ofisi ya Waziri Mkuu
Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu				
Zanzibar	100	231	17.6	Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
Uratibu na Usimamizi	0.1	0.2978	0.3	Wizara ya Fedha na Mipango
Jumla	**567.3**	**1,310.7**	**100**	

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

240. Hadi mwezi Machi 2022, jumla ya shilingi bilioni 1,117.8, sawa na asilimia 85.3 ya shilingi bilioni 1,310.7 zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya UVIKO-19. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 887.2 sawa na asilimia 82.2 zilitolewa kwa upande wa Tanzania Bara kwa kuzingatia mwongozo wa maombi na utoaji wa fedha. Aidha, shilingi bilioni 230.2 zilitolewa na kupelekwa Zanzibar. Mgawanyo wa fedha zilizotolewa ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 10.3.**

Jedwali Na. 10.3: Fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa TCRP

Sekta	Fedha iliyotengwa (Shilingi Bilioni)	Kiasi kilichotolewa (Shilingi Bilioni)	Asilimia ya fedha iliyotolewa
Sekta ya Maji	139.4	139.4	100
Sekta ya Afya - Wizara ya Afya	263.7	230.7	87.5
Sekta ya Afya -TAMISEMI	203.1	51.7	25.4
Sekta ya Elimu -Wizara ya Elimu	64.9	63.7	98.2
Sekta ya Elimu - TAMISEMI	304	304	100
Wajasiriamali wadogo (Vijana, Wanawake na Wenye Ulemavu)	5.0	5.0	100
Kaya Maskini - TASAF	5.5	5.5	100
Utalii - Maliasili na Utalii	90.2	83.04	92.1
Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu	3.47	3.47	100
Zanzibar	231	231	100
Uratibu na Usimamizi	0.298	0.298	100
Jumla	**1,310.7**	**1,117.8**	**85.3**

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

241. Hadi mwezi Machi 2022, utekelezaji wa miradi kisekta kwa upande wa Tanzania Bara ulikuwa katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:

i. Sekta ya Elimu ya Msingi

a) Ujenzi wa vyumba vya madarasa 11,988 vya shule za sekondari katika halmshauri za mikoa yote ulikamilika kati ya vyumba vya madarasa 12,000 vilivyopangwa kujengwa, sawa na asilimia 99.50. Ujenzi wa madarasa hayo ulienda sambamba na ununuzi wa viti na meza (seti) 451,918. Aidha, ujenzi wa vyumba 2,996 vya madarasa kati ya vyumba 3,000 vya madarasa ya vituo shikizi vya shule za msingi ulikamilika sawa na asilimia 98.37 pamoja na madawati 47,149; na ujenzi wa mabweni 49 kati ya 50 ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ulikamilika.

b) Kukamilika kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa na mabweni kuliwezesha wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari kuanza shule kwa wakati mmoja bila kusubiri awamu nyingine kutokana na ufinyu wa madarasa uliokuwepo. Hata hivyo, ujenzi haukukamilika kwa asilimia 100 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuhamishwa kwa eneo la mradi. Mathalani, ujenzi wa vyumba vya madarasa 12 vya shule za sekondari, madarasa manne (4) ya vituo shikizi na bweni moja (1) la wanafunzi wenye mahitaji maalum vilivyopangwa kujengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro vimehamishiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kufuatia makubaliano ya kuwahamisha wakazi wa jamii ya wafugaji waliokuwa wanaishi katika hifadhi ya Ngorongoro.

ii. **Sekta ya Elimu ya Juu**: taratibu za kusaini mikataba ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi - VETA, Arusha *Technical College n*a *Teachers Vocational Training College* Morogoro zilikamilika pamoja na umaliziaji wa ujenzi wa vyuo 23. Maandalizi ya utengenezaji wa samani kwa ajili ya vyuo 25 vya wilaya uliendelea ambapo tayari uchambuzi wa mahitaji na mchakato wa ununuzi wa mbao na vifaa vingine ulikamilika. Aidha, Taasisi ya Elimu Tanzania - TIE ilikuwa katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa uchapaji wa vitabu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Vilevile, mzabuni kuwasilisha vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ambapo vyuo vyote 11 vilipokea bajaji za wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

iii. **Sekta ya Maji:** taratibu za kusaini mikataba ya ununuzi wa seti 25 za mitambo ya kuchimba visima katika mikoa yote nchini, seti tano (5) za mitambo ya ujenzi wa mabwawa na seti nne (4) za vifaa vya uchunguzi wa maji chini ya ardhi zilikamilika. Aidha, utekelezaji wa miradi 46 kwa ajili ya kuboresha huduma za maji katika maeneo ya mijini ilifikia katika hatua mbalimbali kati ya asilimia 10 na 90 na miradi 172 kwa ajili ya kuboresha huduma za maji katika maeneo ya vijijini ilifikia wastani wa asilimia 40.

iv. **Sekta ya Afya**

a) Taratibu za ununuzi wa vifaa na vifaa tiba ambavyo vitatumika katika vituo vya kutolea huduma za afya zilikamilika. Taratibu hizo zinajumuisha ununuzi wa mashine 25 za Digital za *X - Rays; CT - Scan 29, MRI* nne (4) na *Portable Echo Cardiography* saba (7). Vifaa hivyoo ni kwa ajili za Hospitali ya Taifa Muhimbili (MRI moja, CT Scan moja, Digital X - Rays mbili); Ocean Road (MRI moja); Hospitali maalum - JKCI (Echo Cardiography moja); hospitali za kanda (MRI mbili, CT Scan mbili, Digital X - Rays sita na Echo Cardiography sita); Hospitali za Rufaa za Mikoa pamoja na hospitali ya Emilio Mzena *Memorial* na Lugalo (CT Scan 16 na Digital X - Rays 16).

b) Upatikanaji wa vibali vya ununuzi wa magari na tungamo za kiufundi (specification) wa magari 407 chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na magari 96 chini ya Wizara ya Afya ulikamilika. Kati ya magari hayo, magari 233 ni kwa ajili ya kubebea wagonjwa (basic ambulance), magari 20 (Advance ambulance), magari 8 kwa ajili ya kukusanya na kusambaza damu na magari 242 kwa ajili ya kutoa elimu ya afya kwa umma, kufanya ufuatiliaji na uhamasishaji jamii kupata chanjo na huduma nyingine za kiafya.

c) Taratibu za kusaini mikataba ya ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu katika vituo vya kutolea huduma za afya zilikamilika na ujenzi ulifikia katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Miradi ya afya katika ngazi

ya msingi inayotekelezwa chini ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI ilihusisha majengo 26 ya wagonjwa mahututi (ICU), majengo 80 ya dharura (EMD) na nyumba 150 *(3 in 1)* za watumishi. Aidha, miradi inayotekelezwa moja kwa moja chini ya Wizara ya Afya ilihusisha ujenzi wa ICU 38; wodi za huduma za dharura (EMD) 20; nyumba za watumishi 26; uboreshaji wa hospitali za rufaa za mikoa 7, hospitali maalum 1 (Mirembe), kituo cha magonjwa ya kuambukiza Kisopwa - Dar es Salaam na kituo cha mfano cha utoaji elimu ya afya kwa umma Ndejengwa - Dodoma iliyopo chini ya Wizara ya Afya.

d) Mafunzo yalitolewa kwa wahandisi na waganga wakuu 476 katika ngazi ya hospitali zote za rufaa za mikoa zitakapotolewa huduma za dharura (EMD) na za wagonjwa mahututi (ICU); madaktari na wauguzi 336, wataalamu wa teknolojia ya mionzi (Riographers) 116 na madaktari bingwa wa mionzi 14 (radiologists). Vilevile, wataalamu 140 wa sekta ya afya waliajiriwa kwa muda wa miezi sita sawa na asilimia 78 ya lengo. Kada za wataalam hao ni mteknolojia mionzi 36 (Radiographer), fundi sanifu vifaa tiba 59 (Biomedical Technician) na afisa TEHAMA 42 (ICT) ambao wataendelea kutumika na kulipwa kupitia mapato ya ndani hata baada ya mradi kufika mwisho mpaka hapo kibali cha ajira ya kudumu kitakapopatikana.

v. **Uwezeshaji wa Vijana, Wanawake na wenye Ulemavu:** Ujenzi na uboreshaji wa miundombinu na mazingira ya kuwezesha wafanyabiashara wadogo/wajasiriamali/wamachinga kufanya biashara maeneo yanayokidhi kuwakinga dhidi ya maambukizo ya UVIKO - 19 umeendelea kwa kutumia Force Account katika Halmashauri za Jiji la Dodoma, Mwanza, Arusha, Tanga, Mbeya na Dar es Salaam pamoja na Halmashauri za Manispaa za Kinondoni, Temeke, Ubungo na Morogoro. Lengo la ujenzi wa miundombinu hiyo ni kupunguza msongamano wa kundi hili hususan katika maeneo yasiyopangwa rasmi na hivyo kuwainua kiuchumi.

vi. **Uwezeshaji wa Kaya masikini:** Zoezi la kutambua kaya maskini 51,290 kutoka halmashauri 35 za maeneo ya utekelezaji mijini kwenye mitaa 1,471 ambao waliingizwa kwenye mpango utakaowawezesha kupewa ruzuku kwa awamu lilikamilika. Hadi Aprili, 2022, kaya hizo zilipokea ruzuku ya fedha kiasi cha shilingi bilioni 5.49 kwa awamu tatu.

vii. **Utalii:** Taratibu za kusaini mikataba 84 kati ya miradi 120 pamoja na kukabidhi eneo la mradi (site) kwa wakandarasi kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya barabara; ukarabati wa njia za watembea kwa miguu; ujenzi wa *campsite* na bandas; ujenzi wa malango na *trails* katika hifadhi kama vile TANAPA, Nyerere National Park, Saadani National Park na Kilimanjaro (trails);

na ujenzi na ukarabati wa majengo ya kale na nyumba za kihistoria zilikamilika. Aidha, mafunzo ya waongoza watalii yalifanyika katika Hifadhi za Taifa Tarangire, Saadani, Serengeti, Ngorongoro na Manyara kwa awamu tatu ambapo jumla ya waongoza watalii 1,060 walipatiwa mafunzo ya kuimarisha udhibiti wa ubora wa huduma za utalii katika kukabiliana na UVIKO - 19.

FURSA ZITOKANAZO NA UVIKO - 19

242. Pamoja na athari zitokanazo na UVIKO - 19, fursa mbalimbali zilijitokeza ikiwemo: upatikanaji wa misamaha ya madeni; kufunguka kwa masoko ya nje ya nchi ambapo Tanzania iliweza kusafirisha bidhaa moja kwa moja badala ya kupitia nchi jirani hususani mazao ya matunda, mbogamboga na nyama; kuongezeka kwa uzalishaji katika viwanda vya ndani wa vifaa vya kujikinga na UVIKO - 19 ambapo hapo awali vilikuwa vikiagizwa kutoka nje ikiwemo barakoa, vipukusa na dawa; kuongezeka kwa ajira hususan katika sekta ya afya; na kuongezeka kwa ubunifu na utafiti wa dawa asili. Kwa upande wa sekta ya habari na mawasiliano, fursa zilizotokana na UVIKO - 19 ni pamoja na kutangaza bidhaa za habari kimtandao, kama vile magazeti ya mtandaoni kupitia *mobile application* kama *TSN e-paper*, kutumia mifumo ya masafa ya mbali katika upashanaji habari *(tele conference)* hivyo kuwezesha majadiliano au kufikisha habari kwa wananchi pasipo kuhitaji mikusanyiko ya watu.

HITIMISHO

243. Pamoja na hatua na mikakati iliyochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na athari za UVIKO - 19, janga hilo bado halijaisha. Hivyo Serikali inaendelea kuhakikisha utekelezaji madhubuti (effective implementation) wa Mpango wa Maendelo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO - 19 (TCRP) unaofikia ukomo mwezi Juni 2022 kupitia fedha za mkopo nafuu kutoka IMF. Mpango huo umepunguza changamoto ya msongamano wa wanafunzi madarasani, upatikanaji wa maji safi na tiririka, umeboresha huduma za afya, umeinua uchumi wa wananchi wa kipato cha chini na kuimarisha sekta zilizoathirika zaidi ikiwemo utalii.

244. Serikali itaendelea kuweka mikakati ya kuzuia maambukizi na vifo sambamba na kuimarisha mikakati ya kufufua uchumi ikiwemo kuendelea kuboresha huduma za afya kwa kuimarisha vitengo vinavyotoa huduma za dharura na kwa wagonjwa mahututi, kuongeza nguvukazi ya sekta ya afya sambamba na kuendelea kuhimiza wananchi kupata huduma ya chanjo ya UVIKO - 19 inayotolewa bure nchi nzima. Kuhusu mikakati ya kufufua uchumi, mkazo utawekwa kwenye sekta za uzalishaji ikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu, maliasili na nishati. Hii pia itajumuisha ujenzi wa miundombinu wezeshi ikiwemo ya umwagiliaji na nishati pamoja na kuboresha mazingira ya biashara kwa lengo la kuwezesha ushiriki wenye tija wa wajasiriamali wadogo na sekta binafsi kwa ujumla katika shughuli za kiuchumi; na kuendelea kujenga mazingira wezeshi ya kuvutia ujenzi wa viwanda hasa vile vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini kwa ajili ya soko la ndani na ziada kwa ajili ya kuuza nje.

SEHEMU YA NNE

MAENDELEO KATIKA SEKTA MBALIMBALI

SURA YA 11

KILIMO NA USHIRIKA

UZALISHAJI WA MAZAO YA KILIMO

Mazao ya Chakula

245. Mwaka 2021, uzalishaji wa mazao makuu ya chakula uliongezeka kwa asilimia 2.6 na kufikia tani 18,665,217 ikilinganishwa na tani 18,196,733 zilizozalishwa mwaka 2020. Kati ya kiasi hicho, tani 10,874,425 zilikuwa za mazao ya nafaka na tani 7,790,792 mazao yasiyo ya nafaka. Ongezeko la uzalishaji lilichangiwa na: kuwepo kwa mvua za wastani na juu ya wastani katika maeneo mengi; kuimarika kwa huduma za ugani; matumizi ya teknolojia na pembejeo bora za kilimo; na kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa mazao baada ya kuvuna.

Jedwali Na. 11.1: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Chakula (Tani '000') Mwaka 2017 - 2021

Aina ya Zao	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
Mahindi	6,681	6,273	5,652	6,711	7,039	4.9
Mchele	1,594	2,220	2,063	3,038	2,688	-11.5
Ngano	50	57	63	77	70	-9.1
Mtama, Uwele na Ulezi	1,064	988	1,117	1,043	1,077	3.3
Muhogo (mkavu)	1,342	2,791	2,728	2,427	2,486	2.4
Maharage na Mikunde	2,318	1,823	1,888	1,895	2,236	18.0
Ndizi (kavu)	845	1,132	1,135	1,358	1,443	6.2
Viazi (vitamu na mviringo) (kavu)	2,008	1,608	1,644	1,647	1,626	-1.3
Jumla	**15,902**	**16,892**	**16,290**	**18,197**	**18,665**	**2.6**

Chanzo: Wizara ya Kilimo

246. Mwaka 2021, mahitaji ya chakula yalikuwa tani 14,835,101 ambapo tani 9,448,770 zilikuwa za mazao ya nafaka na tani 5,386,331 mazao yasiyo ya nafaka ikilinganishwa na tani 14,404,171 zilizohitajika mwaka 2020. Kwa kuzingatia mahitaji na uzalishaji wa mazao ya chakula, nchi ilizalisha ziada ya tani 3,830,116 za mazao ya chakula mwaka 2021 ambapo tani 1,425,655 zilikuwa mazao ya nafaka na tani 2,404,461 mazao yasiyo ya nafaka. Kutokana na uzalishaji huo, kiwango cha utoshelevu wa chakula nchini kilikuwa asilimia 126 kama kilivyokuwa mwaka 2020.

Miundombinu ya Hifadhi ya Chakula

247. Mwaka 2021, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko - CPB ilikarabati maghala matatu (3) ambayo ni ghala la Kiteto - Manyara lenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000; Mbugani - Dodoma (tani 30,000) na Isaka - Shinyanga (tani 5,000). Aidha, Bodi ilikarabati kihenge cha Gangilonga - Iringa chenye uwezo wa kuhifadhi tani 17,500 za nafaka na Unga Limited - Arusha chenye uwezo wa kuhifadhi tani 38,100 za nafaka. Kwa upande mwingine, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula -NFRA ilijenga ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 15,000 na vihenge vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 25,000 katika Mkoa wa Manyara. Aidha, Wakala ilijenga maghala mawili (2) katika mikoa ya Rukwa na Katavi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 kila moja. Ujenzi wa maghala na vihenge uliongeza uwezo wa Wakala kuhifadhi mazao kwa asilimia 19.9 na kufikia tani 301,000 mwaka 2021 kutoka tani 251,000 mwaka 2020.

Mazao ya Biashara

248. Mwaka 2021, uzalishaji wa mazao makuu ya biashara ulikuwa tani 898,967 ikilinganishwa na tani 1,058,798 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 15.1. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa pamba ulipungua kutokana na uwepo wa mvua zilizozidi wastani katika maeneo ya uzalishaji pamoja na mazao kushambuliwa na wadudu. Aidha, uzalishaji wa chai ulipungua kutokana na uwepo wa mvua chini ya wastani katika maeneo ya uzalishaji, kushuka kwa bei katika soko la dunia, kupungua kwa matumizi ya chai pamoja na UVIKO-19 ulioathiri uendeshaji wa kampuni za chai nchini. Vilevile, uzalishaji wa zao la korosho ulipungua kutokana na mlipuko wa magonjwa na visumbufu vya mimea pamoja na matumizi madogo ya pembejeo. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa tumbaku uliongezeka kutokana na hamasa waliyopata wazalishaji ya uhakika wa soko baada ya kuongezeka kwa kampuni mpya mbili (2) za ndani za kununua zao hilo na hivyo kufikia kampuni saba (7) za ununuzi. Kadhalika, uzalishaji wa sukari uliongezeka kutokana na mafunzo yaliyotolewa kwa wakulima na viongozi kuhusu kilimo bora cha miwa na uendeshaji wa vyama vya ushirika pamoja na kuwepo kwa hali nzuri ya hewa inayofaa kwa uzalishaji wa miwa na hivyo kuongeza upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vya sukari.

Jedwali Na. 11.2: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Biashara (Tani) Mwaka 2017 - 2021

Aina ya Zao	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
Pamba	132,934	222,039	348,910	348,958	122,836	-64.8
Kahawa	48,329	45,245	68,147	60,651	73,027	20.4
Chai	26,975	34,010	37,193	28,715	27,510	-4.2
Pareto	2,150	2,400	2,014	2,510	2,412	-3.9
Tumbaku	58,639	50,522	70,824	37,546	58,508	55.8
Korosho	265,238	313,826	225,053	232,681	210,786	-9.4
Mkonge	36,533	40,635	33,271	36,379	36,170	-0.6
Sukari	330,843	303,752	359,219	311,358	367,718	18.1
Jumla	**901,641**	**1,012,429**	**1,144,631**	**1,058,798**	**898,967**	**-15.1**

Chanzo: Wizara ya Kilimo

Mazao ya Bustani

249. Mwaka 2021, uzalishaji wa mazao ya bustani ulikuwa tani 7,304,723 ikilinganishwa na tani 7,560,010 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 3.4. Hii ilichangiwa na kupungua kwa mahitaji ya mazao hayo katika soko la nje kufuatia kusitishwa kwa baadhi ya safari za mashirika ya ndege ya kimataifa ili kuepuka maambukizi ya UVIKO - 19. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau iliendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya bustani ambapo majukwaa matatu (3) ya zao la parachichi yalianzishwa ikiwa ni pamoja na kuandaa mpango mkakati wa uendelezaji wa zao hilo. Majukwaa hayo yalianzishwa katika mikoa ya Njombe na Mbeya pamoja na kongane la parachichi Meru. Vilevile, Serikali ilifanikiwa kuvutia uwekezaji katika mazao ya bustani ikiwemo ndizi, parachichi na mazao ya viungo kwa ajili ya masoko ya Kenya, India na nchi za Jumuiya ya Ulaya.

Jedwali Na. 11.3: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani) Mwaka 2017 - 2021

Aina ya Zao	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
Matunda	5,243,343	3,703,124	4,576,948	5,582,117	5,199,312	-6.9
Mboga	1,298,388	1,595,489	1,926,927	1,852,676	2,011,684	8.6
Maua	11,615	12,622	13,240	1,710	1,338	-21.8
Viungo	22,062	22,062	80,748.20	123,507	92,389	-25.2
Jumla	**6,575,408**	**5,333,297**	**6,597,863**	**7,560,010**	**7,304,723**	**-3.4**

Chanzo: Wizara ya Kilimo

Mazao ya Mbegu za mafuta

250. Mwaka 2021, uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta ulikuwa tani 1,713,178 ikilinganishwa na tani 1,583,669 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 8.2. Ongezeko hilo lilichangiwa na: uwepo wa mvua za wastani katika maeneo ya uzalishaji hususani mazao ya karanga, mawese na soya; kuendelea na matumizi ya kanuni bora za kilimo; na kuongezeka kwa mahitaji ya mafuta nchini. Hata hivyo, uzalishaji wa alizeti ulipungua kwa asilimia 26.3 kutokana na uwepo wa mvua zilizozidi wastani katika maeneo ya uzalishaji. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa mafuta ya kula mwaka 2021 ulikuwa tani 290,000 sawa na asilimia 45 ya mahitaji ya mafuta ya kula ambayo ni tani 650,000 kwa mwaka.

Jedwali Na. 11.4: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mbegu za Mafuta (Tani) Mwaka 2017 - 2021

Aina ya Zao	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
Alizeti	352,902	543,261	561,297	649,437	478,900	-26.3
Karanga	216,167	370,356	376,520	631,465	895,219	41.8
Ufuta	56,846	133,704	227,821	228,920	236,162	3.2
Mawese	42,277	40,500	42,176	42,387	58,791	38.7
Soya	6,135	21,321	22,953	31,460	44,106	40.2
Jumla	**674,327**	**1,109,142**	**1,230,767**	**1,583,669**	**1,713,178**	**8.2**

Chanzo: Wizara ya Kilimo

Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo

251. Mwaka 2021, uzalishaji wa mbegu bora uliongezeka kwa asilimia 10.9 na kufikia tani 76,725.5 ikilinganishwa na tani 69,173.2 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilichangiwa na jitihada za Serikali katika kuimarisha mazingira ya biashara ikiwemo kupunguza au kufuta baadhi ya kodi na tozo. Aidha, Wakala wa Mbegu za Kilimo - ASA kwa kushirikiana na sekta binafsi ilizalisha tani 5,634 za mbegu bora (tani 1,750 za ASA na tani 3,884 za kampuni binafsi) kwa kutumia mashamba ya ASA. Katika kuongeza uzalishaji wa mbegu bora, Serikali ilikamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye eneo la hekta 400 katika shamba la Kilangali (Kilosa) na ukarabati wa tuta la bwawa katika shamba la Mwele Wilaya ya Mkinga.

252. Mwaka 2020/21, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania iliendelea kuratibu uagizaji na usambazaji wa mbolea nchini ambapo upatikanaji wa mbolea uliongezeka na kufikia tani 766,024 ikilinganishwa na tani 413,478 zilizopatikana mwaka 2019/20. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mbolea ndani ya nchi ambapo mwaka 2020/21 mahitaji yalifikia tani 718,051 ikilinganishwa na mahitaji ya tani 586,604 mwaka 2019/20. Kwa upande mwingine, bei za mbolea ya UREA na DAP katika soko la ndani ziliongezeka na kufikia shilingi 53,869 na shilingi 66,995 kwa kilo 50 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na shilingi 52,500 na shilingi 55, 843 kwa kilo 50 mwaka 2019/20 mtawalia. Ongezeko hilo lilichangiwa na kupungua kwa uzalishajii wa mbolea zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kutokana na baadhi ya viwanda kusitisha au kupunguza uzalishaji kulikosababishwa na athari za UVIKO - 19. Aidha, mbolea aina ya DAP na UREA ndizo hutumika kwa wingi nchini kwa ajili ya kupandia na kukuzia mtawalia.

Jedwali Na. 11.5: Mahitaji, Upatikanaji na Matumizi ya Mbolea Mwaka 2017/18 - 2020/21 (Tani)

Mwaka	**2017/18**	**2018/19**	**2019/20**	**2020/21**
Makadirio ya mahitaji	485,000	514,138	586,604	718,051
Bakaa	-	-	168,397	219,206
Uzalishaji ndani ya nchi	19,233	-	33,873	42,695
Kiasi kilichoingizwa ndani ya nchi	435,178	514,725	524,972	504,122
Jumla ya upatikanaji	**419,795**	**418,355**	**413,478**	**766,023**
Kiasi kilichounzwa nje ya nchi	34,616	96,370	145,367	171,254
Matumizi ya ndani ya nchi	351,858	364,968	457,855	476,870

Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania

253. Mfuko wa Pembejeo za Kilimo - AGTIF ulitoa mikopo 44 yenye thamani ya shilingi milioni 1,643.9 mwaka 2021 ikilinganishwa na mikopo 48 yenye thamani ya shilingi milioni 2,128.4 mwaka 2020, sawa na upungufu wa thamani kwa asilimia 22.8. Hii ilitokana na wakopaji wengi kushindwa kushiriki katika shughuli za uzalishaji kulikosababishwa na athari za UVIKO - 19. Mikopo hiyo ilijumuisha: mikopo 16 ya matrekta makubwa; mikopo minne (4) kwa ajili ya matrekta ya mkono; mikopo mitatu

(3) kwa ajili ya pembejeo za kilimo na mifugo; mikopo minne (4) kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji; mkopo mmoja kwa ajili ya mashine ya kusindika; mikopo miwili (2) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya ufugaji; na shughuli za kilimo mikopo 14. Katika kipindi hicho, shilingi milioni 4,476.6 zilirejeshwa ambazo ni sawa na asilimia 72.1 ya lengo la marejesho ya shilingi milioni 6,207.9 katika kipindi husika ikilinganishwa na marejesho ya shilingi milioni 3,213.1 sawa na asilimia 58.4 ya lengo la marejesho ya shilingi milioni 5,505.3 mwaka 2020.

Mwenendo wa Bei na Masoko ya Mazao

254. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuimarisha mifumo mbalimbali ya masoko ikiwemo Soko la Bidhaa - TMX, stakabadhi za ghala, minada na kilimo cha mkataba. Matumizi ya mifumo hiyo ya masoko yalichangia kuimarika kwa bei ya baadhi ya mazao ya kilimo katika soko la ndani kama ifuatavyo: bei ya ngano iliongezeka na kufikia shilingi 1,000 kwa kilo kutoka shilingi 650 kwa kilo mwaka 2020; bei ya soya iliongezeka na kufikia shilingi 2,200 kwa kilo kutoka shilingi 1,500 kwa kilo mwaka 2020; bei ya mbaazi iliongezeka na kufikia shilingi 1,480 kwa kilo mwaka 2021 kutoka shilingi 500 kwa kilo mwaka 2020; bei ya pamba iliongezeka na kufikia shilingi 1,800 kwa kilo kutoka shilingi 810 kwa kilo mwaka 2020; na bei ya kahawa aina ya arabika iliongezeka na kufikia shilingi 7,000 kwa kilo mwaka 2021 kutoka shilingi 4,000 kwa kilo mwaka 2020.

Huduma za Ugani

255. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuimarisha huduma za ugani kwa kuanzisha vituo 29 vya huduma za kilimo vya kata na kuboresha vituo 224. Aidha, ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala ya kilimo uliendelea kutolewa kwa wakulima kupitia mfumo wa M-Kilimo. Hadi Desemba 2021, maafisa ugani kilimo 7,049 na wakulima 5,570,351 walikuwa wamesajiliwa katika mfumo huo ikilinganishwa na maafisa ugani kilimo 1,344 na wakulima 20,318 waliokuwa wamesajiliwa kipindi kama hicho mwaka 2020.

256. Mwaka 2021, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi (*Agricultural Development Market Trust* na *Care International*) ilitoa mafunzo rejea kuhusu mazao mbalimbali ikiwemo alizeti, zabibu, pamba, karanga, ufuta, soya, migomba na chikichi kwa maafisa ugani 1,557 katika mikoa 16 ya Tanzania Bara. Katika kipindi hicho, wataalamu wa kilimo 16 kutoka katika halmashauri za wilaya za Kongwa, Uyui, Ruangwa na Kilolo walipata mafunzo kuhusu namna ya kupata na kutafsiri taarifa za hali ya hewa kupitia Mradi wa Kilimo Himilivu. Aidha, wataalamu 36 kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania walipata mafunzo ya namna ya kutumia kanzidata ya hali ya hewa kupitia Mradi huo. Kwa upande mwingine, Serikali iliendelea kurasimisha ardhi ya wakulima wadogo ambapo mashamba 126 yenye ukubwa wa kuanzia ekari 50 yenye hati miliki yalihakikiwa kwa matumizi ya kilimo katika halmashauri za wilaya za Bahi, Kongwa, Mpwapwa, Chamwino, Chemba na Kondoa mkoani Dodoma.

Utafiti

257. Mwaka 2021, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo - TARI iligundua aina tano (5) za mbegu bora ikilinganishwa na aina 20 za mbegu bora zilizogunduliwa na kusambazwa mwaka 2020. Kati ya hizo, mbegu za ngano zenye kiwango kikubwa cha protini na mavuno hadi tani 4.6 kwa hekta zilikuwa aina mbili (2), mbegu za mpunga unaonukia na kukoboleka vizuri na mavuno hadi tani 6.3 kwa hekta aina moja (1) na mbegu za choroko zinazostahimili magonjwa ya yellow mosaic virus, cercospora leaf spot na anthracnose aina mbili (2).

258. Mwaka 2021, TARI ilizalisha tani 994.2 za mbegu bora za mazao ya nafaka, jamii ya mikunde na mafuta ikilinganishwa na tani 481.2 zilizozalishwa mwaka 2020. Kati ya hizo, mbegu mama zilikua tani 19.9, mbegu za awali (tani 187.6), mbegu za msingi (tani 134.6) na tani 652.1 za mbegu zilizothibitishwa. Katika kipindi hicho, TARI ilizalisha na kusambaza: miche 2,715,630 ya mkonge; mboga miche 1,953,025; minazi miche 1,250,000; michikichi miche 357,838; korosho miche 20,000; viazi vitamu miche 1,000,448; zabibu miche 120,685; na mihogo miche 27,976.

Mafunzo ya Kilimo

259. Mwaka 2021, wanafunzi 2,948 walidahiliwa katika vyuo vya mafunzo ya kilimo vya Serikali ikilinganishwa na wanafunzi 2,788 waliodahiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 5.7. Kati ya hao, wanafunzi 588 walijigharamia wenyewe na wanafunzi 2,360 walifadhiliwa na Serikali. Ongezeko la udahili lilitokana na ukarabati wa miundombinu ya kujifunza na kujifunzia ikiwemo madarasa na mabweni. Katika kipindi hicho, Serikali iliendelea kufadhili masomo kwa wakufunzi 12 katika ngazi ya shahada ya uzamili na wakufunzi sita (6) katika ngazi ya shahada ya kwanza ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa mafunzo katika vyuo vya kilimo. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania - SAT ilitoa mafunzo ya mbinu za kufundishia kwa wakufunzi kilimo 113 kutoka katika vyuo 14 vya kilimo.

Umwagiliaji

260. Mwaka 2021, eneo la umwagiliaji liliongezeka na kufikia hekta 695,045 kutoka hekta 694,715 mwaka 2020. Katika kipindi hicho, Serikali ilikarabati skimu 21 za umwagiliaji katika halmashauri 14 ikilinganishwa na skimu 15 zilizokarabatiwa mwaka 2020. Hadi Desemba 2021, vyama vya umwagiliaji vilivyosajiliwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji vilifikia 266 ikilinganishwa na vyama 196 vilivyokuwa vimesajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 35.7. Ongezeko hilo lilitokana na wakulima kuendelea kuhamasika kuanzisha vyama vya umwagiliaji.

MIFUGO

Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake

261. Mwaka 2021, idadi ya mifugo nchini ilikadiriwa kufikia ng'ombe milioni 35.3 mbuzi milioni 25.6, kondoo milioni 8.8, nguruwe milioni 3.4 na kuku milioni 92.8

ikilinganishwa na ng'ombe milioni 33.9, mbuzi milioni 24.5, kondoo milioni 8.5, nguruwe milioni 3.2 na kuku milioni 87.7 mwaka 2020. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa nyama ulikuwa tani 738,166 ikilinganishwa na tani 701,678 zilizozalisha mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Kati ya kiasi hicho, nyama ya ng'ombe ilikuwa tani 508,355, nyama ya mbuzi na kondoo tani 102,137, nyama ya kuku tani 86,206 na nyama ya nguruwe tani 41,468. Aidha, jumla ya mayai milioni 4,510.3 yalizalishwa mwaka 2021 ikilinganishwa na mayai milioni 4,051.2 yaliyozalishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 11.3. Ongezeko la idadi ya mifugo na mazao ya mifugo yaliyozalishwa lilitokana na jitihada za Serikali na wadau katika kudhibiti magonjwa ya mifugo pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya mazao ya mifugo ndani na nje ya nchi.

262. Mwaka 2021, uzalishaji wa maziwa ulikuwa lita milioni 3,101.4 ikilinganishwa na lita milioni 3,002.6 zilizozalishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 3.3. Kati ya kiasi hicho, lita milioni 2,170.5 zilizalishwa na ng'ombe wa asili na lita milioni 930.9 zilizalishwa na ng'ombe wa kisasa. Kuongezeka kwa uzalishaji wa maziwa kulichangiwa na uboreshaji wa mbari za mifugo kupitia uhimilishaji unaoendelea nchini pamoja na elimu iliyotolewa kuhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa kibiashara. Kwa upande mwingine, lita milioni 75.9 za maziwa zilisindikwa mwaka 2021 ikilinganishwa na lita milioni 74.3 zilizosindikwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa viwanda vya kusindika maziwa na kufikia viwanda 105 mwaka 2021 kutoka viwanda 91 mwaka 2020 pamoja na udhibiti wa uingizaji holela wa maziwa kutoka nje ya nchi.

Jedwali Na. 11.5: Uzalishaji wa Mazao Yanayotokana na Mifugo Mwaka 2017 - 2021

Aina ya Zao	2017	2018	2019	2020	2021
Uzalishaji Maziwa (Lita 000")					
Ng'ombe wa Asili	1,490,000	1,608,099	1,874,923	2,101,789	2,170,461
Ng'ombe wa Kisasa	626,100	792,044	803,538	900,766	930,923
Jumla	**2,087,000**	**2,400,134**	**2,678,461**	**3,002,555**	**3,101,384**
Uzalishaji Nyama (Tani)					
Ng'ombe	394,604	471,692	506,798	486,736	508,355
Mbuzi na kondoo	81,064	92,999	110,563	95,964	102,137
Nguruwe	18,899	37,191	23,140	38,377	41,468
Kuku	63,597	78,110	41,000	80,601	86,206
Jumla	**558,164**	**679,992**	**681,501**	**701,678**	**738,166**
Uzalishaji Mayai ('000')					
Mayai	2,758,000	3,156,692	3,575,621	4,051,179	4,510,345

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo)

Biashara ya Mifugo na Mazao yake

263. Mwaka 2021, ng'ombe 1,843,904, mbuzi 2,081,233, kondoo 360,745 na punda 191,656 waliuzwa katika soko la ndani ikilinganishwa na ng'ombe 1,023,200, mbuzi

987,867, kondoo 205,161 na punda 198,000 mwaka 2020. Katika kipindi hicho, thamani ya mifugo iliyouzwa ilikuwa shilingi bilioni 1,531 ikilinganishwa na shilingi bilioni 865 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 77. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mifugo hususani mbuzi katika viwanda vya kuchakata na kusindika nyama kwenda nje ya nchi pamoja na jitihada za Serikali katika kuimarisha miundombinu ya minada ya mifugo. Aidha, idadi ya mifugo hai iliyouzwa nje ya nchi ilikuwa ng'ombe 24,014 pamoja na mbuzi na kondoo 106,099 wenye thamani ya shilingi bilioni 46.6 mwaka 2021 ikilinganishwa na ng'ombe 3,574 pamoja na mbuzi na kondoo 49,184 wenye thamani ya shilingi bilioni 1.9 mwaka 2020. Ongezeko la thamani ya mauzo ya mifugo nje ya nchi lilitokana na jitihada za Serikali katika kuboresha minada na biashara za mipakani pamoja na kuimarisha ushirikiano na nchi mbalimbali zikiwemo za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

264. Mwaka 2021, tani 1,774.3 za nyama zenye thamani ya shilingi bilioni 9.9 (dola za Marekani milioni 4.3) ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 692.4 za nyama zenye thamani ya shilingi bilioni 2.99 (dola za Marekani milioni 1.3) zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2020. Kati ya kiasi hicho, nyama ya ng'ombe ilikuwa tani 365.8, mbuzi tani 551.6, kondoo tani 181.5, kuku tani 0.4 na punda tani 675. Ongezeko la kiasi cha nyama kilichouzwa nje lilitokana na kuanza kwa uzalishaji wa nyama katika viwanda vya Tan Choice Limited na Eliya Food OverSeas Company Limited pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama katika nchi za Kuwait, Oman, Qatar na Hongkong.

265. Mwaka 2021, vipande vya ngozi vyenye uzito wa tani 51,113 vilizalishwa ikilinganishwa na vipande vya ngozi vyenye uzito wa tani 39,159 vilivyozalishwa mwaka 2020. Kati ya hivyo, tani 20,340 zilikuwa za vipande vya ngozi ya ngómbe na tani 30,773 za vipande vya ngozi ya mbuzi na kondoo. Katika kipindi hicho, vipande vya ngozi ya ng'ombe, mbuzi na kondoo vyenye uzito wa tani 7,371 viliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na vipande vya ngozi vyenye tani 3,698 vilivyouzwa nje mwaka 2020. Aidha, tani 7,066.7 za ngozi ghafi zenye thamani ya shilingi milioni 9,420.8 ziliuzwa nje ya nchi mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 2,929.2 zenye thamani ya shilingi milioni 5,029.9 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2020. Vilevile, tani 145 za ngozi zilizosindikwa hadi hatua ya kati zenye thamani ya shilingi milioni 196.9 ziliuzwa nje ya nchi mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 102.7 zenye thamani ya shilingi milioni 197.3 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2020. Uzalishaji wa ngozi uliongezeka kutokana na mafunzo yaliyotolewa kuhusu mbinu bora za kuchuna ngozi, kuongezeka kwa uwezo wa kuzalisha ngozi wa kiwanda cha ACE Leather kilichopo Morogoro pamoja na kiwanda cha Kilimanjaro International Leather Company kuanza uzalishaji

Jedwali Na. 11.6: Uzalishaji wa Ngozi Mwaka 2017 - 2021

Mwaka	Ng'ozi za Ng'ombe (tani)	Ng'ozi za Mbuzi na Kondoo (tani)	Jumla (tani)
2017	13,395	21,925	35,320
2018	13,905	23,176	37,080
2019	14,449	24,503	38,952
2020	14,510	24,648	39,159
2021	20,340	30,773	51,113

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo)
*Kipimo kimebadilishwa kutoka vipande kwenda tani

Jedwali Na. 11.7: Uuzaji wa Ngozi Nje ya Nchi Mwaka 2017 - 2021

Mwaka	Ng'ozi za Ng'ombe (tani)	Ng'ozi za Mbuzi na Kondoo (tani)	Jumla (tani)
2017	5,832	3,063	7,975
2018	3,975	3,330	5,812
2019	2,951	166	3,616
2020	3,020	161	3,698
2021	7251	120	7371

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo)
*Kipimo kimebadilishwa kutoka vipande kwenda tani

Jedwali Na. 11.8: Mwenendo wa Mauzo ya Ngozi Nje ya Nchi Mwaka 2010 - 2021

Mwaka	Ngozi ghafi		Ngozi zilizosindikwa		Jumla thamani ya Ngozi ghafi na zilisindikwa (Shilingi Milioni)
	Kiasi tani (000)	Thamani Shilingi milioni	Kiasi tani (000)	Thamani (Shilingi Milioni)	
2017	4,835.0	6,592.0	6,482.0	9,452.0	16,044.0
2018	3,650.0	5,064.0	4,840.0	8,794.0	13,858.0
2019	2,871.2	4,971.4	156.0	230.0	5,201.4
2020	2,929.2	5,029.9	102.7	197.3	5,227.2
2021	7,066.7	9,420.8	145.0	196.9	9,617.7

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania

Uzalishaji wa Chanjo za Mifugo

266. Mwaka 2021, Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania - TVLA iliendelea kuzalisha chanjo kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya mifugo. Katika kipindi hicho, dozi milioni 65.1 za chanjo zilizalishwa na kusambazwa katika halmashauri zote nchini ikilinganishwa na dozi milioni 63.9 za chanjo zilizozalishwa na kusambazwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 1.9. Kati ya hizo, chanjo dhidi ya ugonjwa wa: mdondo -Temevac I-2 zilikuwa dozi 61,069,600; kimeta (dozi 739,600); chambavu (dozi 171,250); mapafu ya ng'ombe (dozi 1,968,300); kutupa mimba (dozi 7,800); mapafu ya mbuzi (dozi 32,400); na kimeta na chambavu - Tecoblax dozi 1,143,600. Ongezeko la chanjo zilizozalishwa lilichangiwa na uboreshaji wa kiwanda cha kuzalisha chanjo, Kibaha hususani ujenzi wa jengo la maabara pamoja na ununuzi wa vifaa.

Uzalishaji wa Malisho na Utengenezaji wa Vyakula vya Mifugo

267. Uzalishaji wa mbegu bora za malisho katika mashamba ya Serikali uliongezeka na kufikia kilo 3,874.5 mwaka 2021 ikilinganishwa na kilo 127.3 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea na jitihada za kuongeza mashamba ya malisho yenye jumla ya hekta 143,754.0 katika mikoa ya Arusha (hekta 111,955.9) na Manyara (hekta 31,798.1) pamoja na upatikanaji wa vitendea kazi kama matrekta. Aidha, uzalishaji wa hei katika mashamba ya Serikali ulipungua na kufikia marobota 81,188 mwaka 2021 ikilinganishwa na marobota 326,655 mwaka 2020. Hii ilitokana na kupungua kwa uzalishaji wa majani kulikosababishwa na uwepo wa mvua za chini ya wastani. Kwa upande mwingine, tani 1,200,000 za vyakula vya mifugo zilizalishwa na sekta binafsi mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 900,000 zilizozalishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 33.3. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa uzalishaji wa vifaranga vya kuku wa mayai na nyama kufuatia kuongezeka kwa mahitaji ya nyama na mayai katika soko.

268. Mwaka 2021, viwanda vya kutengeneza vyakula vya mifugo viliongezeka kwa asilimia 46.7 na kufikia 154 kutoka viwanda 105 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Serikali katika kuendelea kuhamasisha kuhusu fursa za uwekezaji hususani katika viwanda vya vyakula vya mifugo. Katika kipindi hicho, Serikali ilikagua na kusajili maeneo 45 ya kuzalisha vyakula vya mifugo, maeneo 78 ya kuuza vyakula vya mifugo na maeneo 18 ya kuhifadhi vyakula vya mifugo ikilinganishwa na maeneo 11 ya uzalishaji, maeneo 36 ya uuzaji na maeneo matano (5) ya kuhifadhi vyakula vya mifugo yaliyokaguliwa na kusajiliwa mwaka 2020. Maeneo yaliyokaguliwa na kusajiliwa yaliongezeka kutokana na uhitaji wa kuhakikisha upatikanaji wa vyakula vya mifugo vyenye ubora na viwango stahiki. Aidha, wakaguzi wa vyakula vya mifugo waliosajiliwa walifikia 176 mwaka 2021 kutoka wakaguzi 165 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 6.7.

Mafunzo ya Mifugo

269. Mwaka 2021, Wakala wa Mafunzo ya Mifugo - LITA ilidahili wanafunzi 3,972 katika ngazi ya astashahada na stashahada ikilinganishwa na wanafunzi 3,574 waliodahiliwa mwaka 2020, sawa na ongezekeo la asilimia 11.1. Ongezeko hilo lilitokana na juhudi za Serikali za kukarabati na kujenga vyumba vya madarasa katika kampasi za Mpwapwa na Morogoro. Katika kipindi hicho, Wakala ilitoa mafunzo kwa wafugaji 2,356 kuhusu mbinu bora za uzalishaji wa mifugo na malisho ikilinganishwa na wafugaji 2,078 waliopata mafunzo mwaka 2020.

Utafiti wa Mifugo

270. Mwaka 2021, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania - TALIRI iliendelea na tafiti za uzalishaji wa mifugo ambapo tafiti 58 zilifanyika ikilinganishwa na tafiti 39 zilizofanyika mwaka 2020. Kupitia tafiti hizo, ng'ombe chotara wa nyama na maziwa

217 na mbuzi chotara 84 walizalishwa mwaka 2021 ikilinganishwa na ng'ombe chotara wa nyama na maziwa 134 na mbuzi chotara 304 waliozalishwa mwaka 2020. Katika kipindi hicho, ng'ombe chotara wa nyama na maziwa 113 walisambazwa katika maeneo ya Dodoma, Morogoro na Tanga. Aidha, mbuzi bora wa mbegu 131 walisambazwa katika maeneo ya Pwani, Nyamagana, Bahi, Dodoma, Kilimanjaro, Morogoro, Tanga na Mbeya. Vilevile, vifaranga vya kuku chotara 16,076 aina ya Kuroiler na vifaranga 648 aina ya Sasso vilisambazwa katika halmashauri za Mkuranga, Mtama, Mpwapwa, Lindi, Mtwara, Tanga, Siha na Ruangwa mwaka 2021 ikilinganishwa na vifaranga vya kuku chotara 4,801 aina ya Kuroiler na vifaranga 600 aina ya Sasso vilivyosambazwa katika halmashauri za Mpwapwa na Meatu mwaka 2020. Kadhalika, mayai 648 ya kuku aina ya Sasso yalirutubishwa na kusambazwa kwa wafugaji katika eneo la Mpwapwa ikilinganishwa na mayai 240 aina ya Sasso na mayai 3,251 aina ya Kuroiler yalitorutubishwa na kusambazwa mwaka 2020.

271. Mwaka 2021, kilogramu 2,200 za mbegu bora za malisho na kilogramu 762.3 za vishina vya malisho zilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji katika maeneo ya Arusha, Tanga, Dodoma, Dar es Salaam, Mbeya, Kagera, Songwe na Pwani ikilinganishwa na kilogramu 1,041 za mbegu bora za malisho na kilogramu 758.5 za vishina vya malisho vilivyozalishwa na kusambazwa mwaka 2020. Ongezeko la uzalishaji wa mbegu za malisho lilichangiwa na majaribio ya utafiti yaliyofanyika katika kanda za kimkakati za nyanda za juu kusini, kati na mashariki kwa lengo la kurasimisha mbegu za malisho.

Huduma za Ugani katika Mifugo

272. Mwaka 2021, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Mitamba Duniani - HPI ilitoa mafunzo rejea ya ufugaji bora kwa maafisa ugani 1,231 ikilinganishwa na maafisa ugani 3,914 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 68.5. Upungufu huo ulichangiwa na mafunzo husika kutolewa kwa wakuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi waliopo katika ngazi ya wilaya ili waweze kutoa mafunzo hayo kwa maafisa ugani katika maeneo yao. Aidha, mafunzo hayo yalitolewa kwa wafugaji 54,764 katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Tanga, Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Geita, Shinyaga Lindi na Kagera. Vilevile, mafunzo hayo yalitolewa kwa washauri wa mifugo katika mikoa ya Tabora, Tanga, Shinyanga, Ruvuma, Geita, Njombe, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Simiyu, Mara, Singida, Mbeya, Iringa, Dodoma, Manyara na Morogoro.

273. Mwaka 2021, Serikali ilianzisha mashamba darasa 15 yaliyojumuisha mashamba ya malisho 11 katika wilaya za Uvinza (4), Nzega (1) na Mbozi (6) na mashamba manne (4) ya ufugaji kuku katika wilaya za Ruangwa (2) na Mkuranga (2) ikilinganishwa na mashamba darasa 12 yaliyoanzishwa mwaka 2020. Mashamba darasa yaliyoanzishwa yaliongezeka kutokana na mwitikio chanya wa wafugaji kujifunza mbinu bora za ufugaji ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi pamoja na kuongeza kipato kupitia ufugaji.

Aidha, wafugaji 94 walipata mafunzo kwa vitendo kuhusu ufugaji wa kuku na kilimo cha malisho kupitia mashamba darasa hayo ikilinganishwa na wafugaji 43 waliopata mafunzo mwaka 2020.

UVUVI

Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi

274. Mwaka 2021, Serikali iliendelea na usimamizi na ulinzi shirikishi wa rasilimali za uvuvi ikiwemo doria na operasheni maalumu zilizowezesha kukamatwa kwa vifaa na zana mbalimbali zilizotumika katika uvuvi haramu. Vifaa na zana zilizokamatwa ni pamoja na; kamba za kokoro zenye urefu wa mita 410,724, nyavu za makila vipande 8,890, ndoano 210,000, nyavu za timba 13,819, kokoro 2,566, mitumbwi 385, nyavu za dagaa 458, nyavu za mtando 454, injini za boti 88, boti 118, nyavu aina ya gonga 40, kasia 16, vyandarua 4, magari 3, pikipiki 21, katuli 4, na nyavu za kumbakumba 35. Katika kipindi hicho, samaki wachanga kilo 31,124, samaki wakubwa kilo 1,145, tani 26.8 za dagaa, jongoo bahari kilo 211, kamba koche kilo 1,823 na pweza kilo 300 zilikamatwa. Aidha, watuhumiwa 1,239 wa uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira walikamatwa ambapo kesi tatu (3) zilifikishwa mahakamani mwaka 2021 ikilinganishwa na watuhumiwa 1,400 na kesi tano (5) zilizofikishwa mahakamani mwaka 2020.

Ukuzaji Viumbe Maji

275. Mwaka 2021, idadi ya wakuzaji viumbe maji ilikuwa 30,064 ikilinganishwa na wakuzaji viumbe maji 28,009 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 7.3. Katika kipindi hicho, mabwawa ya kufugia samaki yaliongezeka kwa asilimia 7.3 na kufikia mabwawa 30,032 kutoka mabwawa 27,979 mwaka 2020. Aidha, vizimba vya kuzalishia samaki katika maziwa na malambo viliongezeka kwa asilimia 9.7 na kufikia vizimba 473 kutoka vizimba 431 mwaka 2020. Kati ya hivyo, vizimba 362 vilikuwa katika Ziwa Victoria, vizimba tisa (9) Ziwa Tanganyika, kizimba kimoja (1) Ziwa Nyasa na vizimba 101 kwenye malambo na mabwawa makubwa.

276. Mwaka 2021, vifaranga vya samaki 27,120,320 vyenye thamani ya shilingi bilioni 2.7 vilizalishwa ikilinganishwa na vifaranga 21,676, 187 vyenye thamani ya shilingi bilioni 2.2 vilivyozalishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la vifaranga vya samaki kwa asilimia 25.1. Kati ya hivyo, vifaranga 3,366,806 vilizalishwa katika vituo vitotoleshi vya Serikali na vifaranga 23,753,514 katika vituo vya sekta binafsi.

277. Mwaka 2021, uzalishaji wa samaki (sato na kambale) ulikuwa tani 20,258 zenye thamani ya shilingi bilioni 162.0 ikilinganishwa na tani 18,716.6 zilizokuwa na thamani ya shilingi bilioni 103.4 mwaka 2020, sawa na ongezeko la uzalishaji la asilimia 8.2. Katika kipindi hicho, tani 2,438 za mwani zenye thamani ya shilingi milioni 2,400 zilizalishwa ikilinganishwa na tani 1,410 zenye thamani ya shilingi milioni 705.0 zilizozalishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la uzalishaji kwa asilimia 72.9. Aidha, uzalishaji wa kambamiti ulikuwa tani 97.0 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.94

ikilinganishwa na tani 73.6 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.8 mwaka 2020, sawa na ongezeko la uzalishaji la asilimia 31.8. Kuongezeka kwa uzalishaji wa viumbe maji kulichangiwa na jitihada za Serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji ikiwemo kutoa msamaha wa kodi na ushuru kwa zana na pembejeo za ukuzaji viumbe maji zinazoagizwa kutoka nje ya nchi pamoja na elimu iliyotolewa kwa wananchi kuhusu mbinu bora za ukuzaji wa viumbe maji.

Uvunaji wa Samaki

278. Mwaka 2021, uvunaji wa samaki uliongezeka kwa asilimia 0.7 na kufikia tani 477,018 zenye thamani ya shilingi trilioni 2.7 ikilinganishwa na tani 473,592 zenye thamani ya shilingi trilioni 2.4 zilizovunwa mwaka 2020. Kati ya hizo, tani 414,104 zilivunwa katika maji baridi na tani 62,914 zilivunwa katika maji chumvi ikilinganishwa na tani 409,828 za maji baridi na tani 63,764 za maji chumvi mwaka 2020. Kuongezeka kwa uvunaji wa samaki kulitokana na kupungua kwa vitendo vya uvuvi haramu ambavyo kwa kiasi kikubwa huharibu mazalia ya samaki.

Jedwali Na. 11.9: Mwenendo wa Uvunaji wa Samaki (Tani) Mwaka 2017 - 2021

Mwaka	Maji baridi	Maji chumvi	Jumla
2017	332,373	55,170	387,543
2018	323,120	53,231	376,351
2019	409,333	60,977	470,309
2020	409,828	63,764	473,592
2021	414, 104	62,914	477,018

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi

279. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi ambapo kaguzi 7,685 zilifanyika ikilinganishwa na kaguzi 7,341 zilizofanyika mwaka 2020. Kaguzi hizo zilifanyika katika viwanda 51 vikubwa na vya kati vya kuchakata samaki, mialo 124, masoko 31, maghala 52, na vyombo 885 vya kusafirisha mazao ya uvuvi. Aidha, vibali 5,705 vilitolewa kwa wafanyabiashara wa ndani kwa ajili ya uuzaji wa tani 48,261.1 katika masoko ya ndani ikilinganishwa na vibali 3,385 vilivyotolewa kwa ajili ya uuzaji wa tani 38,221.3 mwaka 2020. Vilevile, vyeti vya afya 4,874 vilitolewa kwa wafanyabiashara wa samaki na mazao yake kwa ajili ya usafirirshaji wa tani 42,302 kwenda nje ya nchi ikilinganishwa na vyeti 2,733 vilivyotolewa kwa ajili ya usafirishaji wa tani 40,478 mwaka 2020. Kwa upande mwingine, Maabara ya Taifa ya Uvuvi iliendelea kulinda afya za walaji wa samaki na mazao ya uvuvi ambapo sampuli 3,509 zilifanyiwa uchunguzi wa kimaabara mwaka 2021 ikilinganishwa na sampuli 3,271 zilizofanyiwa uchunguzi mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 7.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuhamasika kwa wafanyabiashara wadogo wa ndani na soko la kikanda kuhusu umuhimu wa upimaji wa sampuli kwa ajili ya kudhibiti ubora wa mazao ya samaki.

Mwenendo wa Uuzaji na Uingizaji wa Mazao ya Uvuvi Nje ya Nchi

280. Mwaka 2021, tani 42,302.0 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 181,268 wenye thamani ya shilingi bilioni 414.2 waliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 40,478 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 128,316 wenye thamani ya shilingi bilioni 386.4 waliouzwa nje ya nchi mwaka 2020. Ongezeko la mauzo nje lilichangiwa na jitihada za Serikali kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi. Katika kipindi hicho, mapato yatokanayo na mrabaha wa mauzo nje ya nchi yalikuwa shilingi bilioni 18.4 ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 21.7 yaliyokusanywa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 15.2. Hii ilitokana na kupunguzwa kwa viwango vya tozo mbalimbali za kusafirisha nje mazao ya uvuvi ikilinganishwa na viwango vya tozo vilivyokuwa vikitumika mwaka 2020. Aidha, tani 371.8 za mabondo zenye thamani ya shilingi bilioni 101.3 ziliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa mapato ya shilingi bilioni 2.2 kama mrabaha ikilinganishwa na tani 706.05 za mabondo zenye thamani ya shilingi bilioni 129.9 zilizouzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa mapato ya shilingi bilioni 4.60 kama mrabaha mwaka 2020. Kupungua kwa kiasi cha mabondo yaliouzwa nje kulitokana na kuendelea kuzorota kwa soko la mabondo katika nchi za Hong Kong na China. Kwa upande mwingine, tani 4.0 za samaki zenye thamani ya shilingi milioni 168.6 ziliingizwa nchini ambapo shilingi milioni 23.6 zilikusanywa kama mrabaha mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 5.3 za samaki zenye thamani ya shilingi milioni 114.9 zilizoingizwa nchini ambapo shilingi milioni 27.2 zilikusanywa kama mrabaha mwaka 2020. Kupungua kwa kiasi cha samaki kilichoingizwa nchini kulitokana na kuendelea kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki ndani ya nchi.

Uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi

281. Serikali iliendelea kuweka mazingira wezeshi katika sekta ya uvuvi ambapo hadi Desemba 2021, kulikuwa na viwanda vikubwa 18 vya samaki, viwanda vidogo 34 vya samaki, viwanda vitatu (3) vya kati vya kutengeneza boti, viwanda vitano (5) vya kati vya kutengeneza nyavu, na maghala 90 ya kuhifadhi mazao ya uvuvi kama ilivyokuwa mwaka 2020. Aidha, Serikali kupitia Kitengo cha Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu - MPRU iliendelea kuvutia uwekezaji wa hoteli za kiikolojia ambapo hadi Desemba 2021 kulikuwa na hoteli 23 za kitalii karibu na maeneo yaliyohifadhiwa ikilinganishwa na hoteli 22 za kitalii mwaka 2020. Kati ya hizo, hoteli 13 zipo Mafia, Tanga sita (6), Dar es Salaam tatu (3) na Mtwara moja (1). Kutokana na uwekezaji kwenye maeneo yaliyohifadhiwa, idadi ya wageni waliotembelea maeneo hayo iliongezeka na kufikia wageni 34,610 mwaka 2021 ikilinganishwa na wageni 27,340 mwaka 2020. Vilevile, MPRU ilikusanya mapato ya shilingi milioni 1,339.6 kutokana na wageni waliotembelea katika maeneo hayo mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi milioni 990.1 zilizokusanywa mwaka 2020.

Mafunzo ya Uvuvi

282. Mwaka 2021, wanafunzi 1,401 walidahiliwa na Wakala wa Mafunzo ya Uvuvi - FETA ikilinganishwa na wanafunzi 1,080 mwaka 2020. Aidha, wavuvi na wakuzaji viumbe maji 16,733 walipatiwa mafunzo kuhusu uanzishwaji na uendeshaji wa vyama vya ushirika, usimamizi wa rasilimali za uvuvi, mbinu bora za ufugaji samaki na udhibiti wa magonjwa mbalimbali ikilinganishwa na wavuvi na wakuzaji viumbe maji 5,000 waliopata mafunzo mwaka 2020.

Maendeleo ya Ushirika

283. Mwaka 2021, Tume ya Maendeleo ya Ushirika - TCDC iliendelea kudhibiti, kusimamia na kuhamasisha ushirika katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi kwa lengo la kuchochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Katika kipindi hicho, vyama vya ushirika vilikuwa 9,809 ikilinganishwa na vyama 9,185 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 6.8. Kati ya hivyo, vyama vya masoko ya mazao vilikuwa 4,538, vyama vya akiba na mikopo 3,946 vyama vya aina nyingine vilikuwa 1,215, vyama vikuu 50 na vyama vya miradi ya pamoja 60. Aidha, idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika iliongezeka na kufikia wanachama 6,965,272 mwaka 2021 ikilinganishwa na wanachama 6,050,324 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilichangiwa na jitihada za Serikali za kuhamasisha wananchi kujiunga au kuanzisha ushirika kwa kutoa taarifa kuhusu mafanikio ya vyama vya ushirika.

284. Mwaka 2021, viwanda vya kuchakata mazao vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika viliongezeka na kufikia viwanda 461 ikilinganishwa na viwanda 452 mwaka 2020. Katika kipindi hicho, ajira 146,555 zilitolewa na vyama vya ushirika ikilinganishwa na ajira 100,100 zilizotolewa mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 46.4. Kati ya hizo, ajira za kudumu zilikuwa 31,819, ajira za mkataba 28,990 na ajira za msimu 85,746. Ongezeko la ajira lilitokana na kuanzishwa kwa vyama vipya vya ushirika. Kwa upande mwingine, mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 1.7 ilitolewa kwa wanachama wa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo mwaka 2021 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 1.6 iliyotolewa mwaka 2020. Aidha, thamani ya hisa na akiba za wanachama iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 898 kutoka shilingi bilioni 891 mwaka 2020. Kwa upande mwingine, Tume iliendelea kutoa elimu ya fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanachama 428 wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo - SACCOS katika mikoa ya Mwanza, Iringa, Mbeya na Kagera.

285. Mwaka 2021, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika - COASCO lilikagua hesabu za Vyama vya Ushirika 6,013 ikilinganishwa na vyama 6,021 vilivyokaguliwa mwaka 2020. Kati ya vyama vilivyokaguliwa, vyama 357 sawa na asilimia 5.9 vilipata hati inayoridhisha, vyama 2,674 sawa na asilimia 44.5 vilipata hati yenye shaka, vyama 1,253 (asilimia 20.8) vilipata hati isiyoridhisha na vyama 1,729

(asilimia 28.8) vilipata hati mbaya. Aidha, COASCO lilifanya kaguzi maalum katika vyama vya ushirika 46 wa lengo la kutathmini utendaji wake. Kupitia kaguzi hizo ilibainika kuwepo kwa mapungufu katika uendeshaji wa baadhi ya vyama na hivyo hatua stahiki kuchukuliwa ili kuimarisha utendaji kazi wa vyama husika.

UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI

Jedwali Na. 32

Msimu[1]	Miwa				Sukari*		
	Wakulima		Jumla (000 Tani)	Bei[2] (Sh./Tani)	Iliyozalishwa Tani	iliyotumika[3]	
	Umma (000 Tani)	Binafsi (000 Tani)				Jumla Tani	Kilo kwa kila mtu 4
2001/02	1,134	389	1,523	14,700	164,498	142,398	10.1
2002/03	1,402	411	1,813	15,000	190,120	167,300	10.4
2003/04	1,672	670	2,342	16,800	223,839	290,711	10.9
2004/05	1,594	752	2,346	20,568	229,617	328,005	10.9
2005/06	1,545	956	2,501	22,383	263,317	343,292	12
2006/07	1,430	611	2,041	29,000	192,095	366,708	12
2007/08	1,967	799	2,766	32,767	265,434	382,518	13
2008/09	2,056	693	2,749	32,771	279,850	396,113	13.4
2009/10	1,972	598	2,570	42,046	263,461	398,070	13.7
2010/11	2,357	661	3,018	43,865	304,135	410,259	12
2011/12	2,036	680	2,716	48,833	262,879	439,307	12
2012/13	2,242	711	2,953	52,167	296,698	468,000	12
2013/14	2,198	602	2,800	50,500	294,300	434,782	12
2014/15	2,466	697	3,163	51,333	304,007	511,680	12
2015/16	2,270	569	2,839	59,707	293,075	525,784	12
2016/17	2,504	557	3,061	72,667	324,930	456,000	12.8
2017/18	2,550	626	3,175	72,667	303,752	515,004	13.5
2018/19	2,792	797	3,589	72,667	359,219	524,772	13.5
2019/20	728	2,659	3,387	73,667	311,358	372,787	12
2020/21	1,029	2,985	4,014	79,000	367,718	372,788	12
Badiliko (Asilimia)							
2019/20 - 2020/21	41.3	12.3	18.5	7.2	18.1	0.0	0.0

Chanzo: Bodi ya Sukari Tanzania

1 Msimu ni Kati ya Julai na Juni

2 Bei ya Mimea ni ile iliyo na asilimia 10 za Sucrose

3 Ni pamoja na Sukari iliyopelekwa Zanzibar

4 Ni kwa Tanzania bara

* Sukari yote huzalishwa na wakulima/mashirika binafsi

PAMBA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 33

Msimu [1]	Pamba yenye mbegu					Pamba iliyoondolewa mbegu					
	Uzalishaji Kiasi (tani)			Bei ya wastani (Shs/Kilo)		Kiasi (tani)			Mauzo nchini		
									Kiasi (tani)	Bei ya wastani (000'Shs/tani)	
	AR	BR	Jumla	AR	BR	AR	BR	Jumla	Jumla [2]	AR	BR
2001/02	148,180	..	148,180	165	..	49,668	-	49,668	..	..	..
2002/03	187,908	781	188,689	180	50	62,983	262	63,245	..	..	..
2003/04	139,756	213	139,969	280	100	46,843	72	46,915	..	..	..
2004/05	341,589	..	341,589	250	..	114,496	..	114,496	..	..	..
2005/06	376,591	..	376,591	220	..	126,228	..	126,228	..	..	..
2006/07	130,585	..	130,585	350	..	43,770	..	43,770	..	..	..
2007/08	200,662	..	200,662	450		70,773	..	70,773	37,488	..	..
2008/09	368,697	..	368,697	480	..	123,582	..	123,582	66,554	..	..
2009/10	267,644	..	267,644	480	..	54,851	..	54,851	..	..	..
2010/11	163,518	.	163,518	900	..	54,809	-	54,809	..	..	..
2011/12	225,938	..	225,938	1,000	..	75,731	..	75,731	..	..	..
2012/13	351,156	..	351,156	660	..	117,702	..	117,702	..	..	..
2013/14	245,815	..	245,815	700	..	82,394	..	82,394	..	..	..
2014/15	202,312	..	202,312	750	..	67,812	..	67,812			..
2015/16	149,765	..	149,765	800		50,199	..	50,199	525,784	12	..
2016/17	132,934	..	132,934	1,000	..	42,203	..	42,203			
2017/18	222,790	..	222,790	1,100	..	80,575	..	80,575	39,244	3,667	..
2018/19	348,901	..	348,901	1,200	..	129,408	..	129,408	51,942	3,123	..
2019/20 r	348,977	..	348,977	1,200	..	128,660	..	128,660	25,162	3,781	..
2020/21	122,836	..	122,836	900	..	46,923	..	46,923	9,479	2,924	..
Badiliko (%) 2019/20-2020/21	-64.8		-64.8	-25.0		-63.5		-63.5	-62.3	-22.7	

Chanzo: Bodi ya Mauzo ya Pamba
1 Msimu ni kati ya Juni na Mei
2 Ni jumla ya AR na BR
r - takwimu zimeboreshwa
-Takwimu hazikupatikani
Pamba ya Tanzania hainunuliwi wala kuuzwa katika madaraja kwa sasa

ENEO LILILOPANDWA CHAI NA MAJANI MABICHI YALIYOPATIKANA

Jedwali Na. 34

Msimu [1]	Eneo lililopandwa (hekta): mashamba			Majani Mabichi yaliyopatikana (tani)						Bei kwa mkulima (Shs/Kilo)	Mauzo[2] Nchini (tani)
				Kiumilikaji: mashamba			Kikanda: mashamba				
	Makubwa	Madogo	Jumla	Makubwa	Madogo	Jumla	Kaskazini	Kusini	Jumla		
2001/02	10,811	10,364	21,175	97,297	13,999	111,296	22,794	88,502	111,296	80	2,683
2002/03	11,097	9,762	20,889	100,677	31,718	132,395	28,679	103,716	132,395	85	3,158
2003/04	11,485	10,801	22,286	95,986	31,993	127,979	26,384	101,595	127,979	86	3,225
2004/05	11,271	11,442	22,713	94,172	39,246	133,418	20,649	112,769	133,418	86	4,004
2005/06	11,310	10,977	22,287	91,337	31,881	123,218	29,046	94,172	123,218	93	3,881
2006/07	11,271	11,956	23,227	109,632	49,024	158,656	39,673	118,983	158,656	100	4,737
2007/08	11,272	11,449	22,722	97,310	51,160	148,470	33,456	115,015	148,471	111	4,253
2008/09	11,271	11,449	22,722	100,644	41,167	141,811	31,677	110,134	141,811	118	4,464
2009/10	11,272	11,449	22,722	106,021	44,716	150,737	33,309	117,428	150,737	124	5,084
2010/11	11,272	11,449	22,722	95,511	47,616	143,127	112,368	30,759	143,127	152	6,065
2011/12	11,272	11,449	22,722	88,582	52,359	140,941	27,009	113,932	140,941	200	4,839
2012/13	11,272	11,449	22,722	113,628	54,872	168,500	30,997	137,503	168,500	206	5,498
2013/14	11,272	11,449	22,722	101,489	47,001	148,490	27,935	120,555	148,490	225	5,672
2014/15	11,272	11,449	22,722	100,018	52,467	152,485	23,283	129,202	152,485	176	6,302
2015/16	11,272	11,449	22,721	96,759	44,605	141,364	25,413	115,915	141,328	230	10,257
2016/17	11,272	11,449	22,722	78,929	41,495	120,424	20,592	99,832	120,424	285	4,648
2017/18	11,322	11,705	23,028	97,428	55,620	153,048	31,599	121,449	153,048	299	5,434
2018/19	11,322	11,705	23,027	104,203	61,081	165,284	36,506	128,778	165,284	312	3,926
2019/20 r	12445	11030	23475	76028	53188	129216	22930	106286	129216	312	27128
2020/21	12445	11361	23806	72138	51655	123793	25178	98614	123792	312	28875
Badiliko (2019/2020 - 2020/2021)	-	3.0	1.4	-5.1	-2.9	-4.2	9.8	-7.2	-4.2	0.0	6.4

Chanzo: Bodi ya Chai Tanzania

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Chai iliyotengenezwa

r - takwimu zimeboreshwa

KAHAWA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 35

Msimu[1]	Iliyonunuliwa (Tani)				Bei (Sh./kilo)			Mauzo nchini+	
	ARABICA		ROBUSTA	JUMLA	ARABICA		ROBUSTA	KIASI	THAMANI
	Laini	Ngumu			Laini	Ngumu	Maganda	(Tani)	(shs'000)
2003/04	20,716	1,850	16,138	38,704	1,800.0	1,200.0	600.0	38,704.0	46,670.0
2004/05	23,870	888	9,133	33,891	2,593.5	1,976.0	1,235.0	33,891.0	62,566.0
2005/06	24,116	1,362	8,856	34,334	1,200.0	420.0	270.0	33,300.0	793,042.5
2006/07	33,345	2,417	19,076	54,838	2,840.0	1,796.0	1,616.0	548.4	129,867.5
2007/08	26,330	1,588	15,606	43,524	2,995.0	1,875.0	1,734.0	43,523.0	89,099.3
2008/09	37,207	1,727	29,643	68,577	2,887.0	2,172.0	1,836.0	68,577.0	165,615.6
2009/10	22,217	915	11,467	34,599	3,988.0	2,475.0	1,563.0	34,599.0	108,741.1
2010/11	30,309	2,013	24,348	56,670	4,500.0	1,300.0	1,200.0	56,670.0	264,143.6
2011/12	20,775	941	11,590	33,306	8,144.4	5,436.4	3,276.9	33,306.0	212,292.6
2012/13	33,204	1,655	36,150	71,009	4,850.0	3,600.0	3,200.0	71,009.0	281,781.8
2013/14	28,212	1,115	18,875	48,202	4,314.0	3,272.9	3,074.6	48,202.0	183,708.9
2014/15	26,335	810	18,788	45,933	5,848.0	4,515.0	3,848.5	-	-
2015/16	21,517	460	17,526	39,503	7,249.6	5,943.4	4,092.9	39,503.0	105,760.8
2016/17	27,023	681	19,989	47,693	7,636.0	6,164.0	4,347.0	47,693.0	129,428,710.0
2017/18	36,551	633	11,897	43,193	2,980.0	2,980.0	2,980.0	43,193.3	116,587,271.0
2018/19	30,664	2,068	27,927	66,546	2,210.0	2,210.0	2,210.0	66,546.2	123,185,587.0
2019/20	31,380	883	27,056	59,318	5,472.0	3,815.0	3,180.0	59,318.0	261,088,612.7
2020/21	28,783	2,576	41,668	73,027	6,665.0	3,749.0	3,065.0	73,027.0	329,205,776.6
Badiliko (%)	-8.3	191.7	54.0	23.1	21.8	-1.7	-3.6	23.1	26.1

Chanzo: Bodi ya Kahawa Tanzania

\+ Kahawa iliyosafishwa

2 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Ni ya muda

\- Takwimu hazikupatikana

ENEO LILILOPANDWA MKONGE NA KATANI ILIYOPATIKANA

Jedwali Na. 36

Msimu[1]	Eneo (Hekta)			Katani iliyopatikana		Mauzo nchini[+]	
	Uliokomaa	Usiokomaa	Jumla	Kiasi (tani)	Bei kwa Mkulima (shs/tani)	Kiasi (tani)	Thamani (Shilingi milioni)
2001/02	34,645	11,473	46,118	23,641	337,732	4,947	1,671
2002/03	39,462	10,611	50,073	23,280	450,000	6,300	2,835
2003/04	29,493	12,204	41,697	26,758	540,000	6,370	4,027
2004/05	45,079	14,500	59,579	27,794	617,342	8,213	5,070
2005/06	26,384	13,264	39,648	30,934	810,000	10,767	8,613
2006/07	28,273	13,608	41,882	33,327	975,000	11,010	10,152
2007/08	28,577	15,622	44,199	34,057	1,000,000	16,997	15,800
2008/09	35,751	18,023	53,774	25,996	1,000,000	11,496	10,100
2009/10	30,556	11,849	42,405	24,092	1,200,000	12,761	10,375
2010/11	31,117	12,169	43,286	25,090	1,300,000	11,617	13,154
2011/12	32,601	14,302	46,902	36,600	1,500,000	11,511	14,390
2012/13	33,649	11,994	45,643	34,874	1,600,000	11,466	16,823
2013/14	35,266	11,044	46,310	37,805	1,724,864	9,160	16
2014/15	35,946	12,494	48,440	38,872	2,071,446	8,972	17,513
2015/16	34,723	13,231	47,954	41,795	2,700,000	9,075	20,342
2016/17	41,661	12,850	54,511	36,533	2,700,000	9,559	21,541
2017/18	40,635	14,389	55,024	43,280	3,000,000	12,111	30,803
2018/19	43,406	18,567	61,973	33,271	3,300,000	13,043	39,607
2019/20r	41,757	17,044	58,801	35,341	3,500,000	12,646	38,323
2020/21	41,685	16,898	59,053	39,343	3,500,000	13,440	39,545
Badiliko (%) 2019/20-2020/21	-0.2	-0.9	0.4	11.3	0.0	6.3	3.2

Chanzo: Bodi ya Katani

+ Katani aina ya Line fibre, Tow na Flume Tow

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

- Takwimu hazikupatikana

r - Takwimu zimeboreshwa

Jedwali Na. 37

Msimu [1]	Maua yaliyonunuliwa (tani)				Mauzo Nchini: Kiasi (tani)			Mauzo Nchini: Thamani (Sh.'000)		
	Kaskazini	Kusini	Jumla	Bei[2] (Sh./kg)	Utomvu (Crude Extract)	Poda	Dawa (Dry Mack)	Utomvu Crude Extract	Poda	Dawa (Dry Mack)
2001/02	36	1699	1735	420	-	-	-	-	-	-
2002/03	111	979	1090	380	2	90	-	106920	99891	-
2003/04	85	751	842	360	-	-	-	-	-	-
2004/05	90	910	1000	360	-	-	-	-	-	-
2005/06	-	2800	2800	360	-	-	-	-	-	-
2006/07	-	1600	1600	700	-	-	-	-	-	-
2007/08	-	1470	1470	1050	-	-	-	-	-	-
2008/09	-	1600	1600	1500	36.4	105	624	-	-	-
2009/10	-	1780	1780	1500	57	69	1035	37361	1473	248
2010/11	-	1786.8	1786.8	1500	57.2	69.3	69.3	37503.7	1478.6	246.9
2011/12	0	5700	5700	1700	82	-	750	-	204	360919
2012/13	0	6100	6100	2400	84	-	2000	-	-	462000
2013/14	34	2691.8	2726.2	2000	90	60	830	6900000	160500	233000
2014/15	31	2255	2286	2500	76	30	430	133.6	116048	235612.7
2015/16	25	1987	2012.4	2100	59.9	6	480	9450000	30240	282240
2016/17	39	2111.8	2151	2050	53.2	162	727	6782016	651810	436232
2017/18	43	2355.9	2400	2500	16	204	700	13932947	869418.1	390864
2018/19	68	2050	2118	3200	-	-	-	144487	844213.9	409299.4
2019/20	68.8	2441	2510	2500	60	83	137.8	13600000	420000	353000
2020/21*	43.9	2368	2412	2600	60	158	50	13079297	728900	41035.5
Badiliko (%) 2019/20 - 2020/21	-36.2	-3.0	-3.9	4.0	0.0	90.4	-63.7	-3.8	73.5	-88.4

Chanzo: Bodi ya Pareto Tanzania

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Bei ni kwa maua ya daraja la tano

- Takwimu hazikupatikana

* Takwimu hizi hadi Desemba 2021 Msimu bado unaendelea

MUHTASARI WA KIASI CHA MAZAO MUHIMU YA BIASHARA YALIYONUNULIWA

Jedwali Na. 38 **Tani**

Mazao	2011/12	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20r	2020/21	Badiliko Asilimia 2019/20 - 2020/21
Katani	36,600	34,874	37,805	38,872	41,795	36,533	43,280	33,271	35,341	39,343	11.3
Kahawa	33,306	71,009	48,202	45,933	39,503	47,693	43,193	66,546	59,318	73,027	23.1
Pamba[1]	225,938	351,156	245,815	202,312	149,765	132,934	222,790	348,901	348,977	122,836	-64.8
Tumbaku	74,239	86,343	105,803	87,281	60,691	85,861	50,522	72,325	37,546	58,508	55.8
Pareto	5,700	6,100	2,726	2,286	2,011	2,151	2,400	2,118	2,510	2,412	-3.9
Chai[2]	140,941	168,500	148,490	152,485	141,328	120,424	153,048	61,081	129,216	123,793	-4.2
Korosho	121,946	124,924	174,695	197,933	231,864	265,238	313,826	225,116	232,682	210,786	-9.4
Miwa	2,716	2,953	2,800	3,163	2,839	556,522	625,743	797,016	3,386,928	4,014,062	18.5

Chanzo: Bodi zinazohusika
1 Yenye mbegu
2 Majani mabichi
r Takwimu zimeboreshwa

UZALISHAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI MWAKA 2010 - 2021

Jedwali Na. 39

Mwaka	Maji Baridi				Maji Chumvi				Jumla			
	Idadi ya Vyombo	Idadi ya Wavuvi	Uzito (tani)	Thamani (Shilingi)	Idadi ya Vyombo	Idadi ya Wavuvi	Uzito (tani)	Thamani (Shilingi)	Idadi ya Vyombo	Idadi ya Wavuvi	Uzito (tani)	Thamani (Shilingi)
2010	141,206	47,635	294,474.00	684,844,020.00	36,321	7,664	52,683.40	89,639,934.00	177,527	55,299	347,157.40	774,483,954.00
2011	141,206	47,635	290,473.60	1,031,883,680.90	36,321	7,664	50,592.40	166,954,953.00	177,527	55,299	341,066.00	1,198,838,633.90
2012	146,420	49,321	314,944.00	1,129,349,924.70	36,321	7,664	50,079.40	177,781,799.00	182,741	56,985	365,023.40	1,307,131,723.70
2013	147,020	49,721	315,008.00	1,248,903,393.00	36,321	7,664	52,846.00	195,529,127.00	183,431	57,385	367,854.00	1,444,432,520.00
2014	147,479	49,627	314,061.50	1,287,248,813.00	36,321	7,664	51,912.40	207,649,600.00	183,800	57,291	365,973.90	1,503,574,790.00
2015	147,479	49,627	309,922.00	1,270,856,679.90	36,321	7,664	52,723.00	210,892,897.10		57,291	362,645.00	1,481,749,577.00
2016	149,018	49,688	308,771.60	1,274,485,403.60	54,511	9,650	53,823.30	211,891,899.20	203,529	59,338	362,594.90	1,486,377,302.70
2017	149,018	49,688	309,922.10	1,270,856,679.80	54,511	9,650	52,723.20	210,892,897.10	203,529	59,338	362,645.30	1,481,749,577.00
2018	149,018	49,688	323,120.80	1,495,678,680.00	53,035	9,242	53,231.90	248,262,840.00	202,053	58,930	376,352.70	1,743,941,520.00
2019	149,018	49,688	365,104.00	1,715,988,902.70	53,035	9,242	105,205.20	494,464,497.70	202,053	58,930	470,309.20	2,210,453,400.40
2020	149,504	50,116	409,828.30	2,049,141,547.20	53,035	9,242	63,763.90	318,819,664.20	202,539	59,358	473,592.20	2,367,961,211.40
2021	141,769	48,749	414,104.80	2,418,489,585.30	53,035	9,242	62,914.00	357,308,946.00	194,804	57,991	477,018.80	2,775,798,531.30

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi)

MWENENDO WA UKUZAJI VIUMBE MAJI MWAKA 2017 - 2021

Jedwali Na. 40

Mwaka	Idadi Ya wakuzaji viumbe maji	Idadi ya mabwawa ya samaki	Idadi ya vizimba	Idadi ya vifaranga	Uzalishaji wa samaki (sato na kambale)	Uzalishaji wa mwani	Uzalishaji wa kambamiti	Uzalishaji wa kaa	Uzalishaji wa majongoo bahari	Uzalishaji wa lulu
					Tani	Tani	Tani	Kilogramu	Kilogramu	Vipande
2017	20,370	22,702	150	14,119,272	11,000.0	1,197.5	248.0	1,016.8	-	967
2018	22,598	24,302	315	15,119,757	14,800.0	1,329.7	371.7	162.0	-	180
2019	26,474	26,445	408	21,173,226	18,073.6	1,449.0	336.0	-	-	550
2020	28,009	27,979	431	21,676,187	18,716.6	1,410.0	73.6	-	-	360
2021	30,064	30,032	473	27,120,320	20,258.0	2,438.0	97.0	41	115	164

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi)
-Takwimu hazikupatikana

MWENENDO WA UUZAJI WA SAMAKI NJE YA NCHI MWAKA 2011 - 2021

Jedwali Na. 41

Mwaka	Uzito (Mt)	Samaki wa mapambo	Thamani katika dola za Marekani	Thamani katika Shilingi	Ushuru
2011	37,996.4	61,215	152,973,356.8	233,714,590,010.8	6,153,278,023.3
2012	41,394.3	45,550	163,299,365.5	254,901,017,111.3	6,819,926,007.1
2013	38,573.6	44,260	147,659,778.6	234,884,628,955.9	6,117,769,193.7
2014	43,354.4	42,100	188,101,262.0	314,489,903,877.1	7,490,632,355.2
2015	41,059.5	87,630	259,286,762.2	547,228,222,095.5	13,097,411,199.2
2016	39,691.5	65,841	257,257,100.5	526,985,019,569.3	14,302,761,906.9
2017	36,063.2	101,110	182,450,277.8	406,568,122,271.5	10,446,850,538.6
2018	44,939.8	63,978	239,680,014.6	546,993,779,393.0	13,520,367,822.3
2019	45,775.2	136,915	158,657,945.6	376,763,802,642.9	25,567,600,872.6
2020	40,478.0	128,316	169,111,837.1	386,369,197,733.3	21,678,640,820.1
2021	42,302.0	181,268	176,083,787.0	414,232,629,494.0	18,436,276,859.0

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi)

MAUZO YA SANGARA NJE YA NCHI MWAKA 2008 - 2021

Jedwali Na. 42

Mwaka	Uzito (Tan)	Thamani (USD)	Thamani (Tshs)	Ushuru (TShs)
2008	38,721	153,740,723	180,366,779,818	5,412,912,979
2009	28,722	130,644,300	168,368,910,380	4,628,409,655
2010	27,229	139,666,995	194,012,069,314	4,509,670,994
2011	25,426	127,601,694	197,899,741,508	4,299,987,312
2012	28,951	141,189,162	220,149,518,646	4,967,311,025
2013	33,733	124,551,585	197,578,220,799	5,085,642,906
2014	24,473	665,856,773	1,131,575,531,076	4,569,314,170
2015	23,001	250,279,107	528,534,413,019	11,251,591,352
2016	26,045	177,338,054	345,417,803,263	6,964,514,349
2017	26,680	168,554,019	376,572,501,425	7,057,407,121
2018	32,167	179,522,959	409,654,290,065	9,689,153,198
2019	32,609	176,894,903	400,195,293,574	17,622,314,163
2020	24,173	132,369,802	302,303,225,916	13,627,647,551
2021	21,846	143,135,053	337,103,408,189	9,704,591,513

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi)

UINGIZAJI WA MAZAO YA UVUVI KUTOKA NJE YA NCHI MWAKA 2012 - 2021

Jedwali Na. 43

Mwaka	Uzaito (Tan)	Idadi ya Samaki hai	Thamani (CIF Value)		Ushuru (TShs)
			Dola za Marekani	TShs	
2012	4,885.7		3,512,976.0	5,507,054,266.0	1,681,166,953.0
2013	6,642.4		5,718,245.6	9,027,183,853.1	2,649,611,644.0
2014	6,792.3		6,009,654.9	9,889,823,440.2	2,818,169,085.9
2015	16,743.9		15,338,684.9	32,211,238,339.3	7,247,564,250.0
2016	13,971.7		12,749,582.8	26,774,123,924.7	8,519,807,734.0
2017	22,961.8		25,065,356.0	56,121,332,048.2	12,869,006,181.4
2018	22,752.4		19,571,180.0	44,896,287,034.7	12,929,314,630.9
2019	5.9		50,693.1	116,594,174.3	37,010,742.0
2020	5.3	1,489	49,933.7	114,864,544.5	27,168,209.2
2021	3.9	895	73,018.8	168,617,559.4	23,588,310.6

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi)

SURA YA 12

MALIASILI NA UTALII

Misitu na Nyuki

286. Mwaka 2021, uzalishaji wa asali nchini uliongezeka kwa asilimia 4.7 na kufikia tani 31,442 ikilinganishwa na tani 30,037 zilizozalishwa mwaka 2020. Kati ya hizo, tani 1,988 za asali zenye thamani ya shilingi milioni 19,878.2 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 2,032.4 zenye thamani ya shilingi milioni 13,413.7 zilizouzwa nje mwaka 2020. Kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya asali kulitokana na kupanda kwa bei ya asali katika soko la dunia. Kwa upande mwingine, kiasi cha nta kilichozalishwa kiliongezeka na kufikia tani 1,901 ikilinganishwa na tani 1,894 za nta zilizozalishwa mwaka 2020. Kati ya hizo, tani 393 za nta zenye thamani ya shilingi milioni 6,490.0 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 251 zenye thamani ya shilingi milioni 3,865.4 zilizouzwa nje mwaka 2020. Kuongezeka kwa kiasi na thamani ya nta iliyouzwa nje ya nchi kulitokana na utulivu wa bei ya nta katika soko la dunia. Aidha, asali na nta iliyozalishwa nchini iliuzwa zaidi katika nchi za Marekani, Ujerumani, Japani na Umoja wa Falme za Kiarabu.

Jedwali Na 12.1: Mauzo ya Mazao ya Nyuki Nje ya Nchi Mwaka 2017 - 2021

Mwaka	Asali		Nta	
	Uzito (Tani)	Thamani (Shilingi Milioni)	Uzito (Tani)	Thamani (Shilingi)
2017	240.8	1,292,017,450	203.9	6,879,170,450
2018	1,095.9	9,342,538,000	143	1,287,099,000
2019	607.6	4,860,834,400	179.3	1,437,865,600
2020	2,032.4	13,413,721,200	251	3,865,400,000
2021	1,988	19,878,220,000	393	6,489,999,500

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

287. Mwaka 2021, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS uliotesha miche ya miti 31,295,703 ikilinganishwa na miche 20,689,369 iliyooteshwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 51.3. Miche hiyo ilipandwa katika maeneo yaliyovunwa yenye ukubwa wa hekta 3,328 na maeneo mapya ambayo miti haikuota yenye ukubwa wa hekta 2,076 ikilinganishwa na maeneo yenye ukubwa wa hekta 3,583 na hekta 3,303 mwaka 2020, mtawalia. Aidha, mashamba ya miti yenye ukubwa wa hekta 41,527 yalisafishwa ikilinganishwa na hekta 37,469 zilizosafishwa mwaka 2020. Vilevile, Wakala ulipogoa miti katika mashamba yenye ukubwa wa hekta 10,860 na kupunguzia miti katika mashamba yenye ukubwa wa hekta 4,685 ikilinganishwa na hekta 9,647 na hekta 3,317 kwa mtiririko huo mwaka 2020. Kwa upande mwingine, Wakala uliongeza mashamba mapya yenye ukubwa wa hekta 30,000 mwaka 2021 ikilinganishwa na hekta 56,500 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 46.9.

Jedwali Na.12.2: Uendelezaji wa Mashamba ya Miti Mwaka 2017 - 2021

Mwaka	Idadi ya miche iliyooteshwa	Eneo la mashamba mapya	Mashamba yaliyorudishiwa miti	Eneo lililopandwa miche baada ya miti kuvunwa	Eneo lililorudishiwa miche katika maeneo yasiyoota vizuri	Eneo la mashamba ya miti lililosafishwa	Eneo la mashamba ya miti lililopogolewa	Eneo la mashamba ya miti ambalo miti ilipunguziwa
		(Hekta)						
2017	19,181,213	9,162	2,987	4,825	2,966	41,056	7,969	1,262
2018	20,435,500	7,408	3,732	4,927	2,664	36,989	9,019	4,658
2019	21,824,600	4,438	615	1,893	251	18,101	6,244	1,293
2020	20,689,369	56,500	4,543	3,583	3,303	37,469	9,647	3,317
2021	31,295,703	30,000	4,498	3,328	2,076	41,527	10,860	4,685

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

288. Mwaka 2021, miche 960,000 ilioteshwa na kupandwa katika maeneo ya misitu ya asili, vyanzo vya maji na makazi yaliyoharibiwa kutokana na shughuli za binadamu ikilinganishwa na miche 22,270 iliyooteshwa na kupandwa mwaka 2020. Kuongezeka kwa idadi ya miche iliyooteshwa na kupandwa kulitokana na utekelezaji wa kampeni inayolenga kuifanya Tanzania kuwa ya kijani. Aidha, mipango 31 ya usimamizi wa hifadhi za misitu iliandaliwa na mipaka ya hifadhi ya misitu yenye urefu wa kilomita 1,112.0 ilisafishwa na kuwekwa maboya/vigingi 589 na mabango 204 kwa lengo la kupunguza migogoro ya mipaka kati ya hifadhi za misitu na wananchi. Vilevile, Serikali iliwezesha upandaji miti kwa jamii kwa kugawa viriba kilo 293, mbegu za miti kilo 30 na miche 3,018,477.

289. Mwaka 2021, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania iliendelea na uhifadhi na udhibiti wa uharibifu wa misitu katika kanda na mashamba ya miti nchini. Katika kipindi hicho, Wakala ilikamata na kutaifisha magunia 76,588 ya mkaa, mbao zenye mita za ujazo 5,016.7, kuni zenye meta za ujazo 1,469.7, nguzo 18,294, mita za ujazo za magogo 1,560.9 na milango na fremu 1,957 pamoja na kushikilia na kutoza faini ya pikipiki 1,469, baiskeli 3,442, magari 246, majahazi 5 na matrekta 3.

Wanyamapori

290. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kudhibiti ujangili na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa ambapo doria 583,694 zilifanyika ikilinganishwa na doria 540,553 zilizofanyika mwaka 2020. Kati ya hizo, doria 297,856 zilifanywa na Shirika la Hifadhi za Taifa; doria 37,568 zilifanywa na Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro; doria 223,490 zilifanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori; na doria 24,780 zilifanywa na Kikosi cha Taifa cha Kupambana dhidi ya Ujangili. Kutokana na doria hizo, watuhumiwa 7,264 wa makosa ya ujangili wa wanyamapori na misitu walikamatwa. Aidha, doria zilizofanyika ziliwezesha kukamatwa kwa nyara mbalimbali ikiwemo:

meno ya tembo mazima 90, vipande 274 na magego tisa (9); nyamapori vipande 1,518; meno 24 ya kiboko; kobe hai 849; kucha 130 za simba; meno 25 ya simba; magamba 37 ya kakakuona; kakakuona hai wawili (2); mbao 469; magogo 997 ya mti aina ya mninga; magunia ya mkaa 359; silaha (SMG, riffle, shotgun na gobore) 444; risasi 1,577; mitego 2,314; magari 11; pikipiki 19; na misumeno ya moto sita (6). Vilevile, kesi mpya 3,975 zilifunguliwa katika vituo mbalimbali vya polisi na kusajiliwa mahakamani kwa hatua ya usikilizwaji.

291. Mwaka 2021, sekta ndogo ya wanyamapori ilikusanya shilingi milioni 251,531.9 ikilinganishwa na shilingi milioni 154,390.1 zilizokusanywa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 62.9. Kuongezeka kwa mapato kulichangiwa na sekta kuanza kuimarika kutokana na kupungua kwa athari za UVIKO - 19. Kati ya fedha zilizokusanywa, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania lilikusanya shilingi milioni 127,028.6 (asilimia 50.5); Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro shilingi milioni 63,852.2 (asilimia 25.4); na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori shilingi milioni 60,651.3 (asilimia 24.1).

Jedwali Na. 12.3: Mapato Yatokanayo na Sekta Ndogo ya Wanyamapori Mwaka 2017 - 2021 (Shilingi)

Mwaka	Shirika la Hifadhi za Taifa	Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro	Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA)	Jumla
2017	207,587,218,000	103,090,458,000	19,202,957,607	329,880,633,607
2018	214,486,751,736	108,149,417,000	20,109,785,000	342,745,953,736
2019	292,539,502,030	147,043,375,161	20,864,030,536	460,446,907,727
2020	85,614,710,442	47,862,177,819	20,913,213,013	154,390,101,274
2021	127,028,556,252	63,852,180,870	60,651,257,787	251,531,994,909

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

Utalii

292. Mwaka 2021, watalii waliotembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini waliongezeka kwa asilimia 48.6 na kufikia 922,692 ikilinganishwa na watalii 620,867 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada zilizochukuliwa na Serikali katika kupambana na maambukizi ya UVIKO -19 ikiwa ni pamoja na matumizi ya *National Standard Operating Procedures* (SOP) ambazo zimesaidia kuonesha kuwa Tanzania ina mikakati madhubuti ya kupambana na ugonjwa huo na hivyo kuvutia watalii. Kati ya hao, watalii 836,134 (watalii 518,480 wa ndani ya nchi na watalii 317,654 kutoka nje ya nchi) walitembelea Hifadhi za Taifa ikilinganishwa na watalii 507,177 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 64.9. Aidha, idadi ya watalii waliotembelea Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ilifikia 326,112 mwaka 2021 ikilinganishwa na watalii 248,181 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 31.4. Kati ya hao, watalii 160,877 walitoka nje ya nchi na watalii 165,235 walikuwa wa ndani ikilinganishwa na watalii wa nje 122,228 na watalii wa ndani 125,953 mwaka 2020.

Kielelezo Na. 12.1: Idadi ya Watalii waliotembelea vivutio mbalimbali nchini



Jedwali Na. 12.5: Idadi ya Watalii Waliotembelea Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro Mwaka 2019 - 2021

Mwaka/Mwezi	2019		2020		2021	
	Nje ya Nchi	Ndani ya Nchi	Nje ya Nchi	Ndani ya Nchi	Nje ya Nchi	Ndani ya Nchi
Januari	32,913	21,348	35,482	22,605	11,684	13,059
Februari	41,753	22,215	44,003	23,367	9,438	8680
Machi	19,506	15,399	12,205	11,931	6,711	7478
Aprili	14,539	14,519	202	2,812	2,957	7943
Mei	17,150	14,245	184	2,447	3,812	8242
Juni	37,240	24,368	672	3,731	8,550	14520
Julai	69,211	33,100	1,971	6,410	18,721	14,536
Agosti	65,903	34,257	3,384	7,144	26,542	17593
Septemba	42,693	26,949	3,278	6,878	17,797	16331
Oktoba	43,396	25,921	5,967	8,152	19,768	15988
Novemba	24,378	19,167	4,754	7,494	15,485	14030
Desemba	36,601	27,767	10,126	22,982	19,412	26835
Jumla	**445,283**	**279,255**	**122,228**	**125,953**	**160,877**	**165,235**

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

293. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii ndani na nje ya nchi kwa: kuboresha *channel* maalum iitwayo Tanzania Safari Channel; kutumia watu maarufu, mabalozi wa hiari na Ofisi za Balozi za Tanzania; na kushiriki katika onesho la Dubai Expo 2020. Aidha, Serikali kupitia Bodi ya Utalii iliendelea kutoa elimu ya utalii kupitia matamasha, matukio ya michezo na maonesho mbalimbali yakiwemo Maonesho ya Sabasaba, Serengeti Marathon, Rock - City Marathon, East African Trade Fair, Bunda Women Marathon, Maonesho ya Nguvu Kazi Afrika Mashariki, Serengeti Cultural Festival, Kili - Summit Exhibition, Bagamoyo Festival na Sauti za Busara. Vilevile, Bodi iliandaa onesho la kwanza la kitalii ukanda wa Afrika Mashariki (East African Regional Tourism Expo 2021) lililofanyika Jijini Arusha mwaka 2021.

294. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kukagua na kupanga huduma za malazi katika viwango vya ubora wa nyota (nyota 1 hadi 5) kwa kutumia vigezo vilivyowekwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi hicho, hoteli tatu (3) za huduma za malazi ambazo zilikuwa hazitambuliki zilipangwa katika madaraja ya ubora ambapo Hoteli ya Gran Melia iliyopo Jiji la Arusha ilipangwa kuwa na hadhi ya nyota 5, Holiday Inn iliyopo jijini Dar es salaam (nyota 4) na Hill Top Hotel iliyopo mkoani Kigoma (nyota 3). Aidha, huduma za malazi zinazopaswa kukusanya tozo ya kitandasiku ziliongezeka na kufikia 8,681 mwaka 2021 kutoka huduma za malazi 1,815 mwaka 2020. Hii ilitokana na juhudi za Serikali katika kufanya utambuzi na uhakiki wa huduma za malazi katika mikoa yote nchini. Kwa upande mwingine, Serikali ilifanya ukaguzi wa mawakala wa biashara za utalii katika mikoa ya Dar es salaam, Mwanza, Iringa, Arusha pamoja na malango ya kuingilia wageni katika Hifadhi za Taifa za Ruaha, Tarangire, Mikumi na Manyara na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ambapo jumla ya shilingi milioni 994.6 zilikusanywa kama ada za leseni.

Malikale

295. Mwaka 2021, wageni wa ndani na nje ya nchi waliotembelea vivutio vya malikale waliongezeka kwa asilimia 111.9 na kufikia 94,278 ikilinganishwa na wageni 44,488 waliotembelea vivutio hivyo mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na ukarabati na uendelezaji wa lililokuwa soko la watumwa na majenzi ya kale katika mji mkongwe wa mikindani. Kati ya wageni hao, 3,341 walikua wageni kutoka nje ya nchi na wageni 90,937 walikua wa ndani ya nchi. Aidha, mapato yatokanayo na viingilio vya wageni katika vituo vya malikale yalikuwa shilingi milioni 155.3 mwaka 2021 ikilinganishwa na mapato ya shilingi milioni 128.7 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 20.7.

Jedwali Na. 12.6: **Mapato Yatokanayo na Wageni Waliotembelea Vivutio vya Malikale Mwaka 2020 - 2021**

Kituo	**2020**		**2021**	
	Wageni	Mapato (Shilingi)	Wageni	Mapato (Shilingi)
Magomeni	102	38,940	1,163	1,423,000
Kaole	12,400	25,000,000	24,765	13,086,080
Isimila	4,754	10,429,860	8,517	21,720,385
Mji Mkongwe	9,573	21,602,000	15,678	12,937,020
Kalenga	945	1,797,020	6,693	10,174,020
Kilwa	2,994	26,848,000	5,947	29,066,000
Mbozi	2,008	4,516,290	4,058	7,972,160
Amboni	5,019	17,736,827	13,666	27,971,627
Tongoni	102	400,000	164	295,641
Ujiji	2,699	7,627,340	4,194	9,296,750
Kwihara	190	251,000	181	249,800
Kolo	2,319	9,390,000	3,578	12,588,890
Caravan Serai	1,383	3,059,740	4,446	7,534,000
Kunduchi	-	-	1,228	1,030,000
Jumla	**44,488**	**128,697,017**	**94,278**	**155,345,373**

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

296. Mwaka 2021, wageni 431,396 (ndani ya nchi 426,347 na nje ya nchi 5,049) walitembelea Makumbusho ya Taifa ikilinganishwa na wageni 195,570 (ndani ya nchi 183,700 na nje ya nchi 11,870) mwaka 2020. Ongezeko la wageni wa ndani lilichangiwa na juhudi za Serikali kutangaza vivutio vya utalii ikiwemo ufunguzi wa klabu za kimakumbusho katika shule mbalimbali za msingi na sekondari, Kampeni ya Twenzetu Makumbusho na matamasha mbalimbali. Katika kipindi hicho, mapato yaliyotokana na viingilio vya wageni katika Makumbusho ya Taifa yalikuwa shilingi milioni 446.6 ikilinganishwa na shilingi milioni 269.6 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 65.7. Hii ilichangiwa na juhudi za Serikali kutangaza vivutio vya utalii na kuibua vyanzo vipya vya mapato ikiwemo kuboresha jukwaa la sanaa pamoja na ukodishaji wa huduma za viwanja, bustani na mgahawa.

Jedwali Na. 12.7: Mapato Yatokanayo na Wageni Waliotembelea Vivutio vya Makumbusho

Kituo	2020				2021			
	Nje ya nchi	Ndani ya nchi	Jumla	Mapato	Nje ya nchi	Ndani ya nchi	Jumla	Mapato
Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni	4,858	11,170	16,028	64,711,044	3,397	27,113	30,510	200,821,897
Kijiji cha Makumbusho	3,660	8,925	12,585	51,229,577	974	6,722	7,696	140,609,500
Makumbusho ya Azimio la Arusha	84	1,274	1,358	5,392,587	95	2,793	2,888	16,800,250
Makumbusho ya Elimu Viumbe	3,053	9,565	12,618	53,925,869	534	4,617	5,151	21,650,350
Makumbusho ya Mwalimu Nyerere	36	6,008	6,044	24,266,642	19	5,724	5,743	53,164,500
Makumbusho ya Vita ya Majimaji	179	17,178	17,357	70,103,631	28	3,110	3,138	12,316,000
Makumbusho ya Dkt. Rashid Kawawa	0	0	0	0	0	227	227	428,000
Mji wa Kihistoria Mikindani	0	0	0	0	2	656	658	771,500
Wageni walioingia kwa shughuli za kimakumbusho	0	129,580	129,580	0	0	375,385	375,385	0
Jumla	**11,870**	**183,700**	**195,570**	**269,629,350**	**5,049**	**426,347**	**431,396**	**446,561,997**

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

IDADI YA WATALII WALIOTEMBELEA HIFADHI ZA TAIFA KATIKA MWAKA 2010 - 2021

Jedwali Na. 44

Mwaka	Idadi ya Watalii		Jumla	Mapato (Shilingi)
	Nje	Ndani		
2010	540,440	333,294	873,734	113,856,861,145
2011	586,869	360,928	947,797	119,549,704,203
2012	537,675	364,217	901,892	137,545,109,618
2013	530,142	427,208	957,350	150,861,426,031
2014	535,140	417,220	952,360	152,977,487,000
2015	432,124	526,110	958,234	149,957,485,000
2016	439,119	518,457	957,576	175,089,696,000
2017	386,529	595,811	982,340	207,587,218,000
2018	726,003	442,543	1,168,546	214,486,751,736
2019	763,276	494,676	1,257,952	292,539,502,030
2020	218,310	288,867	507,177	85,614,710,442
2021	317,654	518,480	836,134	127,028,556,252

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

MAUZO YA BIDHAA ZA MISITU KATIKA MASOKO YA NCHI ZA NJE KWA MWAKA 2021

Jedwali Na. 45

Aina ya mazao ya misitu	Kiasi				Thamani (Shilingi)
	Ujazo (m3)	Uzito (Kg)	Idadi ya Vipande	Gallon	
Matunda		79,667.5	-	-	24,820,475.0
Vikapu			19,574.0	-	12,741,300.0
Mkaa endelevu (Briquettes)	-	413,930.0		-	8,378,000.0
Carvings	-	13,842.5	1,431.0	-	20,423,530.0
Mbao za Mpingo (Clarinets)	55.4	-	87,581.0	-	3,030,000.0
Samani		2,367.0	1,703.0	-	1,627,700.0
Wattle extract	-	2,626,745.0		-	35,256,400.0
Gum arabica	-	303,861.7		-	5,013,000.0
Vifaa vya kuchonga (Hand crafts)	-	3,000.0	770.0	-	1,212,000.0
Hardboard	2,644.7		9,900.0	-	2,448,200.0
Marine boards	100.0	-	-	-	1,218,000.0
Medicine	-	1,211.2		-	78,308,200.0
Oil	-	4,072.8		18	5,953,200.0
Mbao zilizogundishwa (Plywood)	30,883.1	-	958,501.0	-	338,451,000.0
Poles	944.5	-	63,088.0	-	5,331,000.0
Resin	-	1,049,420.0		-	13,180,000.0
Sawn timber	106,705.2	-	7,556,257.1	-	1,351,607,574.9
Small wooden item	-	1,243.9	1,311.0	-	2,118,800.0
Venia (Veneer)	44,750.3		25,795,374.0		389,352,000.0
Wild plant ornamental		9,075.6	36,686.0		42,171,200.0
Fito (Withies)	-	119,528.9	132,501.0	-	59,267,070.9
Wooden Christmas Decoration	316,452.1		-	-	606,000.0
Total					**2,402,514,650.8**

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

IDADI YA WAWINDAJI WA KITALII NA MAPATO MWAKA 2015 - 2021

Jedwali Na. 46

Mwaka	Idadi ya Watalii			Mapato (Shilingi)
	Wawindaji	Watazamaji	Jumla	
2015	608	393	1,001	28,802,391,200.0
2016	495	297	792	29,136,885,800.0
2017	473	291	764	19,202,957,607.0
2018	503	280	783	20,109,785,000.0
2019	519	483	1,002	20,864,030,536.0
2020	251	185	436	15,590,640,205.0
2021	548	101,382	101,930	35,725,991,298.5

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

MWENENDO WA BIASHARA YA UTALII MWAKA 2013 - 2021

Jedwali Na. 47

Maelezo	Kipimo	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Jumla ya Watalii	Idadi	1,095,884	1,140,156	1,137,182	1,284,279	1,327,143	1,505,702	1,527,230	620,867	922,692
Watalii wa hotelini	Idadi	1,021,766	1,005,058	1,033,555	1,155,851	1,163,752	1,404,672	1,353,279	563,779	848,936
Mapato	US $ Milion	1,853	1,983	1,902	2,132	2,200	2,433	2,604	715	1,248
Wastani wa siku za kukaa watalii hotelini	Siku	10	10	10	10	9	10	13	10	*
Wastani wa matumizi ya fedha kwa mtalii kwa siku (US $)	*Package Tour*	372	378	305	351	410	331	379	312	*
	Non - Package Tour	201	210	141	145	136	135	216	115	*

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

*Taarifa husika zipo kwenye uchakataji bado haujakamilika

WATALII WALIOTEMBELEA MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO KATIKA MWAKA 2010 HADI 2021

Jedwali Na. 48

Mwaka	Wageni Nje	Watanzania	Jumla ya watalii
2010	281,513	242,133	523,646
2011	281,513	307,086	588,599
2012	310,537	254,730	565,267
2013	350,970	296,763	647,733
2014	332,469	278,221	610,690
2015	289,061	278,922	567,983
2016	284,794	265,845	550,639
2017	391,030	249,428	640,458
2018	410,574	268,880	679,454
2019	445,283	279,255	724,538
2020	122,228	125,953	248,181
2021	160,877	165,235	326,112

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

SURA YA 13

MADINI

Leseni za Utafutaji na Uchimbaji wa Madini

297. Mwaka 2021, maombi 14,993 ya leseni mbalimbali za madini yalipokelewa ikilinganishwa na maombi 11,161 yaliyopokelewa mwaka 2020, sawa na ongezeka la asilimia 34.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji katika sekta ya madini nchini iliyochangia kuongezeka kwa uwekezaji. Kati ya maombi yaliyopokelewa, leseni 6,404 za utafutaji wa madini, uchimbaji mkubwa, uchimbaji wa kati, uchimbaji mdogo, uchenjuaji na usafishaji wa madini zilitolewa ikilinganishwa na leseni 4,978 zilizotolewa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 28.6. Ongezeko hilo lilitokana na maboresho ya Sheria ya Madini Sura 123 ambayo iliunda Tume ya Madini na hivyo kuongeza ufanisi katika usimamizi wa sekta ya hiyo ikiwemo utoaji wa leseni. Kati ya Leseni zilizotolewa, leseni 268 zilikuwa za utafutaji wa madini, leseni mbili (2) za uchimbaji mkubwa, leseni sita (6) za uchimbaji wa kati, leseni 6,066 za uchimbaji mdogo, leseni 61 za uchenjuaji wa madini na leseni moja (01) ya usafishaji wa madini.

Vibali vya Uuzaji wa Madini

298. Mwaka 2021, jumla ya vibali 5,526 vya kuuza madini nje ya nchi yenye thamani ya dola za Marekani milioni 3,046.2 vilitolewa ikilinganishwa na vibali 5,968 vya kuuza madini yenye thamani ya dola za Marekani milioni 3,310.7 vilivyotolewa mwaka 2020, sawa na upungufu wa thamani kwa asilimia 8.0. Hii ilitokana na kupungua kwa uzalishaji wa madini ya dhahabu kulikosababishwa na kufungwa kwa mgodi wa dhahabu wa Buzwagi na mgodi mmoja katika Mgodi wa dhahabu wa Geita pamoja na mgodi wa Almasi wa Mwadui kusitisha shughuli za uchimbaji katika kipindi cha mwezi Julai 2020 mpaka Oktoba 2021 kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya UVIKO -19 na hivyo kuchangia kushuka kwa bei ya Almasi katika soko la dunia.

Dhahabu

299. Uzalishaji wa dhahabu ulikuwa kilogramu 59,638 mwaka 2021 ikilinganishwa na kilogramu 55,805 zilizozalishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 6.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji katika mgodi wa Bulyanhulu kufikia kilogramu 4,864 mwaka 2021 kutoka kilogramu 1,553 mwaka 2020 na kuimarika kwa usimamizi wa wachimbaji wadogo wa dhahabu kupitia masoko na vituo vya ununuzi. Kati ya kiasi cha dhahabu kilichozalishwa, kilogramu 42,902 za dhahabu zilipata vibali vya kusafirishwa nje ya nchi ikilinganishwa na kilogramu 49,812 zilizopata vibali mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 13.9. Katika kipindi hicho, thamani ya dhahabu iliyopata vibali vya kuuzwa nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 0.5 na kufikia dola za Marekani milioni 2,831.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,844.9 mwaka 2020. Upungufu wa kiasi na thamani ya dhahabu iliyopata vibali vya kusafirishwa nje ya

nchi ulitokana na kupungua kwa biashara ya madini ya dhahabu katika soko la dunia kulikosababishwa na athari za UVIKO - 19. Aidha, wastani wa bei ya dhahabu katika soko la dunia ulikuwa dola za Marekani 1,800.2 kwa wakia moja mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 1,769.6 kwa wakia moja mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 1.7.

Almasi

300. Uzalishaji wa madini ya almasi ulikuwa karati 62,545 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 8.5 mwaka 2021 ikilinganishwa na karati 147,191 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 20.1 zilizozalishwa mwaka 2020, sawa na upungufu wa uzalishaji kwa asilimia 57.5. Upungufu huo ulitokana na kusitishwa kwa shughuli za uzalishaji katika mgodi wa almasi wa Mwadui wa Williamson Diamond Ltd ambao ndio unazalisha almasi kwa wingi nchini kuanzia mwezi Julai 2020 hadi Oktoba 2021 kutokana na UVIKO - 19. Aidha, madini yote ya Almasi yaliyozalishwa kwa mwaka 2020 na 2021 yalipata vibali vya kusafirishwa kwenda nje ya nchi kwa ajili ya mauzo.

Vito vya Thamani

301. Mwaka 2021, uzalishaji wa madini ya vito ghafi yenye ubora wa juu na chini (isipokuwa tanzanite na almasi) ulikuwa kilogramu 7,197,217 ikilinganishwa na kilogramu 23,564,525 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 69.5. Hii ilitokana na kuzorota kwa biashara ya madini ya vito ulimwenguni kufuatia mlipuko wa UVIKO - 19 kutokana na biashara ya vito kutegemea mauzo katika minada ya kimataifa kama vile Hongkong, Thailand na India. Katika kipindi hicho, minada hiyo ilisitishwa na hivyo kusababisha wafanyabiashara wa madini ya vito (dealers) kushindwa kununua madini kutoka kwa wachimbaji wadogo kwa kutokuwa na mitaji ya kutosha. Madini ya vito ghafi yaliyozalishwa ni pamoja na *ruby, saphire, almandite, garnet, spinel, sunstone na feldspar*.

Tanzanite

302. Uzalishaji wa tanzanite ghafi yenye ubora wa juu na chini uliongezeka na kufikia kilogramu 177,144.5 mwaka 2021 ikilinganishwa na kilogramu 51,542.5 mwaka 2020. Hii ilitokana na baadhi ya migodi iliyokuwa imesimama kwa kukosa mitaji kuanza uzalishaji baada ya kupata wafadhili/mitaji, kuendelea kuimarisha ukaguzi katika maeneo ya migodi pamoja na kutoa elimu ya namna bora za uchimbaji kwa wachimbaji wadogo. Aidha, karati 120,458 za madini ya tanzanite yenye thamani ya dola za Marekani milioni 276.8 yalikatwa, yalisanifiwa na kuuzwa mwaka 2021 ikilinganishwa na karati 118,773 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 10.9 mwaka 2020.

Makaa ya Mawe

303. Uzalishaji wa makaa ya mawe ulikuwa tani 976,319 mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 689,959 zilizozalishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 41.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa masoko ya makaa ya mawe nje ya nchi ikiwemo katika

nchi za Uganda, Kenya, Rwanda na China. Aidha, thamani ya makaa ya mawe iliongezeka kwa asilimia 35.7 na kufikia shilingi bilioni 277.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 204.6 mwaka 2020.

Madini Mengine

304. Mwaka 2021, uzalishaji wa madini ya fedha ulikuwa kilogramu 9,324 ikilinganishwa na kilogramu 13,187 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 29.3. Katika kipindi hicho, thamani ya madini ya fedha yaliyopata vibali vya mauzo nje iliongezeka kwa asilimia 6.9 na kufikia dola za Marekani milioni 9.3 mwaka 2021 kutoka dola za Marekani milioni 8.7 mwaka 2020. Aidha, uzalishaji wa madini ya bati ulikuwa tani 211.3 mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 47.5 mwaka 2020. Jumla ya vibali 45 kwa ajili ya mauzo ya madini ya bati nje ya nchi yenye thamani ya shilingi bilioni 10.6 vilitolewa mwaka 2021 ikilinganishwa na vibali 12 vya madini ya bati yenye thamani ya shilingi bilioni 1.1 vilivyotolewa mwaka 2020.

305. Mwaka 2021, tani 598,053 za madini ya jasi zilizalishwa ikilinganishwa na tani 443,926 zilizozalishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 34.7. Hii ilitokana na kukua kwa sekta ya viwanda nchini ambayo hutumia malighafi ya jasi kutengeneza bidhaa mbalimbali ikiwemo saruji, mbolea, karatasi na nguo. Katika kipindi hicho, jumla ya tani 9,129 za madini ya jasi yenye thamani ya dola za Marekani milioni 0.94 yalisafirishwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 4,252 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 0.45 yaliyosafirishwa mwaka 2020. Ongezeko hili lilitokana na Serikali kuruhusu uuzaji wa madini hayo nje ya nchi kwa vibali maalumu ambayo hapo awali yaliwekewa zuio la kusafirisha nje ya nchi kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani vinavotumia madini hayo kama malighafi. Aidha, vibali 42 vya kusafirisha madini ya jasi nje ya nchi vilitolewa mwaka 2021 ikilinganishwa na vibali 86 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 51.2. Upungufu huo ulitokana na kuanza utekelezaji wa mwongozo wa uongezaji thamani wa madini hao kabla ya kusafirishwa nje ya nchi.

Madini Ujenzi

306. Mwaka 2021, madini ya ujenzi yaliyozalishwa yalikuwa tani milioni 32.3 yenye thamani ya shilingi bilioni 520.8 ikilinganishwa na tani milioni 31.9 yenye thamani ya shilingi bilioni 340.93 mwaka 2020. Madini hayo hutumika katika shughuli za ujenzi ikijumuisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati ikiwemo Miradi ya Kufua Umeme wa Julius Nyerere, Reli ya kisasa ya SGR, bandari na viwanja vya ndege.

Masoko ya Madini

307. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuimarisha uendeshaji wa masoko na vituo vya ununuzi wa madini ambapo soko la madini moja (1) na vituo vya ununuzi 28 vilifunguliwa na kufanya idadi ya masoko ya madini kufikia 40 na vituo vya ununuzi 70 ikilinganishwa na masoko 39 na vituo ya ununuzi 42 mwaka 2020. Katika kipindi hicho, tani 18.3 za dhahabu zenye thamani ya shilingi trilioni 2.2 ziliuzwa katika masoko hayo

ikilinganishwa na tani 15.5 za dhahabu zenye thamani ya shilingi trilioni 1.8 zilizouzwa mwaka 2020. Aidha, karati 17,858.7 za madini ya almasi zenye thamani ya shilingi bilioni 5.9 ziliuzwa mwaka 2021 ikilinganishwa na karati 15,426.7 zenye thamani ya shilingi bilioni 6.5 zilizouzwa mwaka 2020. Vile vile, karati 148,411.32 na gramu 4,677,897,176.88 za madini ya vito zenye thamani ya shilingi bilioni 10.6 ziliuzwa mwaka 2021 ikilinganishwa na karati 137,756.93 na gramu 1,150,661,194.21 zenye thamani ya shilingi bilioni 42.6 zilizouzwa mwaka 2020. Kwa upande mwingine, jumla ya shilingi bilioni 161.1 (shilingi bilioni 132.2 mrabaha, shilingi bilioni 22.3 ada ya ukaguzi na shilingi bilioni 6.6 tozo ya huduma) zilikusanywa katika masoko na vituo hivyo mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 133.2 zilizokusanywa mwaka 2020.

UCHIMBAJI WA MADINI: KIASI KILICHOPATIKANA MWAKA 2014 - 2021

Jedwali Na. 49

Madini	Kipimo	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Almasi	Carat	252,875	216,491	237,685	304,456	381,302	416,750	147,191	62,545
Dhahabu	Kg	40,481	43,293	45,155	43,490	39,304	48,408	55,805	59,638
Tanzanite ghafi	Kg							51,542.5	177,144.5
Tanzanite(iliyochakatwa)	Carat							118,773	120,458
Madini mengine ya Vito	Kg	3,083,765	1,872,915	2,554,932	1,185,697	284,321	1,929,714	23,564,525	7,197,217
Chumvi	Tani	54,757	92,158	145,718	100,017	226,757	99,510	83,974	112,995
Phosphate	Tani	738,000	222,800	23,658	1,351	-	-	28,376	24,493
Limestone	000 Tani	873	2,945	4,170	3,301	5,805	5,527	6,788	8,506
Tin ore	Tani	79	179	138	91	8	24	47	211
Jasi	Tani	200,179	239,302	213,744	123,645	269,753	256,529	443,926	598,053
Makaa ya Mawe	Tani	246,128	257,321	276,030	563,053	627,652	712,136	689,959	976,319
Pozolana	Tani	68,925	342,628	230,045	79,085	157,406	263,064	160,078	216,934
Kaolin	Tani	3,809	1,953	656	13,816	153,506	15,343	98,454	100,950
Madini ya Fedha	Kg	14,493	15,569	17,984	10,911	10,262	12,607	13,187	9,324
Shaba	Pound	14,027,008	14,252,341	15,762,430	2,933,941	-	-	3,761,086	3,352,630
chuma	Tani							28,431	78,190
Bauxite	Tani	25,641,201	204,956	72,779	12,090	10,796	-	25,995	38,142
Madini ya Ujenzi	000 Tani	10,480	12,960	15,460	5,601	10,374	20,188	31,892	32,304
Madini mengine ya viwandani	000 Tani							2,161	1,037

Chanzo: Wizara ya Madini
Carat = 0.205 gm

THAMANI YA MADINI YALIYOTOLEWA VIBALI KWA AJILI YA KUUZWA NJE YA NCHI MWAKA 2018 - 2021

Jedwali Na. 50

Aina ya Madini	Kipimo	Kiasi cha Madini				Thamani ya Madini (000 USD)			
		2018	2019	2020	2021	2018	2019	2020	2021
Almasi (Rough)	Carats	383,391	416,750	143,471	47,337	96,066	89,335	20,065	8,473
Dhahabu	000 Gramu	35,864	48,408	49,812	42,902	1,454,878	2,123,035	2,844,960	2,831,840
Gemstones-rough	000 Gramu	284,321	761,814	128,461	4,493,669	28,006	-	-	16,501
Gemstones- cut &polished	Carats	-	-	1,435,273	166,728	-	27,314	19,215	7,426
Chumvi	Tani	36,392	99,510	-	21,095	1,207	5,576	1,927	2,360
Phosphate	Tani	-	-	14,241	15,632	-	-	1,945	3,442
Bati	Tani	8	-	41	155	-	-	420	4,603
Jasi	Tani	241,260	2,916	4,252	9,129	-	317	446	936
Graphite	Tani	27,810	9,271	2,250	2,887	2,418	4,420	1,071	1,264
Fedha	000 Gramu	12,041	12,550	13,187	10,532	6,045	6,537	8,748	9,284
Shaba	000 Lb	-	-	-	-	-	-	-	-
Makinikia ya shaba	Tani	-	-	38,683	16,679	-	-	346,673	121,871
Madini ya viwandani	Tani	783,180	336,844	7,419	206,137	35,783	23,994	374	24,697
Bauxite	Tani	7,140	-	25,995	12,570	335	-	1,349	630
Makaa ya mawe	Tani	-	-	162,648	346,779	-	-	60,212	11,838
Madini ujenzi	Tani	-	-	21,964	57,469	-	-	446	1,070
Jumla ('000 US$)						**1,624,739**	**2,280,529**	**3,307,850**	**3,046,234**

Chanzo: Wizara ya Madini

- Takwimu hazikupatikana

SURA YA 14

VIWANDA NA BIASHARA

Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani

308. Mwaka 2021, uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwandani uliongezeka kutokana na mahitaji ya bidhaa katika soko kuongezeka na mwitikio wa wananchi kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa biskuti na tambi uliongezeka kwa asilimia 35.5 kila moja, rangi (asilimia 33.9), nguo (asilimia 23.2), chibuku (asilimia 7.2), dawa za pareto (asilimia 6.5), bati (asilimia 6.1), chuma (asilimia 4.9), kamba za katani (asilimia 4.8), nyavu za uvuvi (asilimia 4.6) na saruji (asilimia 0.5). Kwa upande mwingine, uzalishaji ulipungua kwa bidhaa za bia (asilimia 1.4), unga wa ngano (asilimia 3.9), sigara (asilimia 4.1), tabaka za mbao (asilimia 12.8) na konyagi (asilimia 33.7). Aidha, gharama za uzalishaji bidhaa viwandani ziliongezeka kwa asilimia 10.0 na kufikia shilingi bilioni 10,522.4 mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 9,565.8 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bei za malighafi kutoka nje ya nchi.

Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

309. Shirika la kuhudumia viwanda vidogo - SIDO lilitoa mafunzo kwa wajasiriamali 22,945 mwaka 2021 ikilinganishwa na wajasiriamali 19,036 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 20.5. Ongezeko hilo lilitokana na kuhamasika kwa wananchi juu ya dhana ya kujiendeleza kiuchumi. Mafunzo yaliyotolewa yalihusu: usindikaji wa mafuta ya kula na vyakula vya mifugo; ubanguaji wa korosho; utengenezaji wa bidhaa za ngozi, chaki na vibuyu; mbinu na usimamizi wa biashara; uendeshaji wa miradi ya kiuchumi; utafutaji wa masoko; ubora wa bidhaa; na uongozi wa vikundi vya wajasiriamali.

310. Mwaka 2021, Vituo vya Maendeleo ya Teknolojia vilivyo chini ya SIDO vilitengeneza na kusambaza mashine 400 ikilinganishwa na mashine 509 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 21.4. Hii ilitokana na kupungua kwa uhitaji wa mashine zilizokuwa zikitumika katika kudhibiti maambukizi ya UVIKO - 19. Mashine zilizotengenezwa ni pamoja na mashine za: kusindika mazao ya kilimo na mifugo; uvunaji na uhifadhi wa mazao; kufungashia vyakula vilivyosindikwa; na kutengeneza matofali. Aidha, vituo hivyo vilibuni teknolojia za kupunguza matumizi ya miti na mazao yake kama vyanzo vya nishati.

311. Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 6.1 kwa wajasiriamali 2,584 mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.3 zilizotolewa kwa wajasiriamali 2,862 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 3.2 ya mikopo iliyotolewa. Aidha, fursa za ajira zilizozalishwa kutokana na mikopo iliyotolewa zilikuwa 6,318 mwaka 2021 ikilinganishwa na fursa 8,264 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 23.5.

Upungufu wa mikopo na fursa za ajira ulichangiwa na baadhi ya wajasiriamali kupunguza uzalishaji kutokana na athari za UVIKO - 19 katika uchumi

312. Mwaka 2021, Serikali kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara - CBE ilitoa mafunzo ya kozi 23 za muda mfupi zinazohusu elimu ya biashara katika fani mbalimbali kwa washiriki 525 ikilinganishwa na kozi 20 za muda mfupi kwa washiriki 512 mwaka 2020. Ongezeko la kozi zilizotolewa lilitokana na maboresho yaliyofanyika ikiwemo kuongeza aina za mafunzo yenye kuongeza tija na ufanisi katika kazi. Mafunzo yaliyotolewa yalihusu; uwekezaji na elimu ya fedha, biashara mitandaoni/kiganjani, uandishi wa tafiti na mapendekezo, ujuzi katika majadiliano, ukaguzi wa upimaji wa gesi na mafuta, mizani ya kieletroniki, uhakiki wa matenki ya mafuta pamoja na bomba la mafuta kati ya nchi na nchi. Aidha, Chuo kilifanya tafiti mbili (2) na kutoa machapisho ya kitaaluma 152 katika nyanja za uchumi, teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), biashara na ujasiriamali ikilinganishwa na tafiti mbili (2) na machapisho ya kitaaluma 92 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 65.2 la machapisho ya kitaaluma. Ongezeko hilo lilitokana na wanataaluma kuhamasika kuandaa machapisho.

313. Mwaka 2021, Serikali kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara - *TanTrade* iliratibu programu 10 za mafunzo kwa wafanyabiashara 3,563 ikilinganishwa na programu 13 zilizotolewa kwa wafanyabiashara 3,223 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 10.5 ya wafanyabiashara waliopata mafunzo. Hii ilichangiwa na jitihada za Mamlaka kutoa mafunzo kwa njia ya mtandao na wafanyabiashara kuhamasika kupata mafunzo ili kuongeza ufanisi na ushindani katika uendeshaji wa biashara. Mafunzo yaliyotolewa yalihusu mbinu za kukuza biashara, ubora wa bidhaa, ufungashaji na umuhimu wa utambulisho wa bidhaa (rajamu), taratibu na nyaraka muhimu zinazohitajika katika kuuza mazao ya kilimo na bidhaa nyingine nje ya nchi pamoja na uchambuzi wa masoko ya kimataifa.

314. Mwaka 2021, Serikali kupitia *TanTrade* iliendelea kuratibu utoaji wa huduma ya kliniki ya biashara ambayo huwakutanisha pamoja wataalamu wa biashara kutoka taasisi mbalimbali za umma na binafsi katika kutatua changamoto za wafanyabiashara. Katika kipindi hicho, wafanyabiashara 623 walihudumiwa ikilinganishwa na wafanyabiashara 566 waliohudumiwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 10.1. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Mamlaka katika kutangaza huduma ya kliniki kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na wafanyabiashara: 96 kupata alama ya ubora wa bidhaa; 166 kuelimishwa kuhusu matumizi sahihi ya vipimo, mashine za uzalishaji, vifungashio na masoko; 124 kuwezeshwa mitaji ya biashara kutoka Benki ya Taifa ya Biashara - NBC; 101 kusajili majina na alama za biashara; 42 kupata usajili wa utumiaji wa kemikali na taratibu za kupata vibali; 171 kupata masoko na malighafi za kutengeneza bidhaa; 75 kupata usajili wa eneo la kazi, matumizi sahihi ya vifaa kinga na taratibu za kupata cheti cha tathmini

ya athari ya mazingira; 51 kuelekezwa taratibu za kufanya biashara ya mazao ya misitu na nyuki; 46 kuelimishwa kuhusu ushindani wa kibiashara na 56 kupata maeneo ya uwekezaji.

315. Mwaka 2021, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania - TIRDO kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti - REPOA ilitoa mafunzo ya kitaalamu kwa wadau 407 wa ngozi ikilinganishwa na mafunzo kwa wadau 450 yaliyotolewa mwaka 2020. Mafunzo hayo yalitolewa katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Shinyanga, Kagera, Geita, Tabora, Iringa, Pwani, Dar es salaam na Morogoro na kuhusisha wafugaji 270, wachunaji ngozi 75, wafanyabiashara wa ngozi 25, wasindikaji ngozi 10 na watengenezaji wa bidhaa za ngozi 27. Kwa upande mwingine, TIRDO ilihaulisha tafiti tisa (9) mwaka 2021 ikilinganishwa na tafiti saba (7) mwaka 2020. Tafiti hizo zilihusu: uzalishaji wa mkaa mbadala (briketi); uboreshaji na uhifadhi wa ngozi; uongezaji thamani wa zao la mwani; uzalishaji wa vitofali lishe vinavyotumika kuzalisha uyoga; na uongezaji wa thamani katika zao la uyoga.

316. Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania - TEMDO ilitoa mafunzo kwa wahandisi wahitimu 18 mwaka 2021 ikilinganishwa na wahandisi wahitimu 10 mwaka 2020. Aidha, TEMDO ilitoa huduma za kihandisi kwa viwanda 22 ikilinganishwa na viwanda saba (7) mwaka 2020. Baadhi ya viwanda vilivyopewa huduma za kihandisi vilikuwa; STAMI Gold Mining, Kagera Sugar Industry, KADERES Coffee Industry, Mtibwa Sugar Industry, Allience Industry, Mzinga Corporation, Mamba Miamba Ginger Processing Industry, Sun Flag Tanzania Ltd, Raha Investment, Tanzania Breweries Ltd, Minjingu Mines and fertilizer Ltd, Mtambwe Trading Company Ltd. Ongezeko la viwanda vilivyopata huduma za kihandisi lilitokana na Taasisi kutanua wigo wa kutembelea na kutoa mafunzo ya kihandisi katika viwanda mbalimbali. Vilevile, TEMDO ilisanifu teknolojia 20 zilizowezesha utengenezaji wa mashine sita (6) ikilinganishwa na teknolojia 10 zilizosanifiwa na kutengeneza mashine nne (4) mwaka 2020.

317. Mwaka 2021, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - CAMARTEC kilitoa mafunzo ya ujenzi wa mitambo ya biogesi kwa vijana 675 ikilinganishwa na vijana 181 waliopatiwa mafunzo mwaka 2020. Ongezeko la vijana waliopata mafunzo lilitokana na utekelezaji madhubuti wa Programu ya Kukuza Ujuzi na Kuongeza Ajira nchini. Katika kipindi hicho, Kituo kiliwajengea uwezo wajasiriamali 65 kuhusu utengenezaji wa sufuria na majiko sanifu ikilinganishwa na wajasiriamali 59 waliojengewa uwezo mwaka 2020 ambapo ajira zaidi ya 160 za muda mfupi zilizalishwa.

318. Mwaka 2021, Serikali kupitia CAMARTEC ilifanya ukaguzi na majaribio ya aina 15 ya zana za kilimo zilizojumuisha zana sita (6) kutoka nje ya nchi na zana tisa (9) zinazozalishwa nchini ikilinganishwa na zana aina tisa (9) zilizofanyiwa ukaguzi na

majaribio mwaka 2020. Ongezeko la zana za kilimo zilizokaguliwa lilitokana na kutolewa elimu kwa wadau kuhusiana na kanuni za majaribio ya zana za kilimo na teknolojia.

Usajili wa Biashara na Viwanda

319. Mwaka 2021, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni - BRELA ilisajili kampuni 10,862 ikilinganishwa na kampuni 9,236 zilizosajiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 17.6. Aidha, majina ya biashara 21,836 yalisajiliwa mwaka 2021 ikilinganishwa na majina 18,555 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 17.7. Wakala ilitoa leseni 12,135 za biashara za kundi A mwaka 2021 ikilinganishwa na leseni 11,105 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 9.3. Ongezeko la usajili na utoaji leseni lilitokana na juhudi za Serikali za kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini ikiwemo kuweka mifumo ya kielektroniki ya usajili pamoja na utoaji wa elimu kwa umma. Vilevile, Wakala ilitoa leseni 181 za viwanda mwaka 2021 ikilinganishwa na leseni 195 zilizotolewa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 7.2. Hii ilichangiwa na kupungua kwa idadi ya wawekezaji hususani katika viwanda kulikosababishwa na athari za UVIKO - 19.

320. Mwaka 2021, alama 3,137 za biashara na huduma zilisajiliwa na Wakala ikilinganishwa na alama 3,808 zilizosajiliwa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 17.6. Upungufu huo ulisababishwa na athari za UVIKO - 19 katika uchumi na biashara za kimataifa. Aidha, Wakala ilipokea na kufanyia kazi maombi 422 ya kuwekea ulinzi uvumbuzi wa sayansi na teknolojia (hataza) mwaka 2021 ikilinganishwa na maombi 73 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Wakala katika kuboresha utoaji wa haki miliki kwa kuhamasisha uwasilishaji wa maombi kupitia kampuni, wanasheria na Shirika la Kanda la Afrika linalosimamia Haki Miliki za Kitaaluma - ARIPO.

Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa

321. Mwaka 2021, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania - *TanTrade* iliratibu maonesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ambapo kampuni 3,002 zilishiriki ikilinganishwa na kampuni 2,880 zilizoshiriki mwaka 2020. Kati ya kampuni zilizoshiriki maonesho hayo, kampuni 2,926 zilikuwa za ndani na kampuni 76 za nje ya nchi. Aidha, nchi 16 zilishiriki katika maonesho ya mwaka 2021 ikilinganishwa na nchi tano (5) zilizoshiriki mwaka 2020. Ongezeko la ushiriki katika maonesho hayo lilichangiwa na kufunguliwa kwa mipaka ya baadhi ya nchi kutokana na kupungua kwa maambukizi ya UVIKO - 19 pamoja na uwepo wa mazingira wezeshi ya biashara nchini.

322. Mafanikio yaliyopatikana katika maonesho ya 45 ni pamoja na: Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko - CPB kununua tani 100,000 za mahindi, tani 16,000 za mchele na tani 10,000 za maharage kutoka kwa wakulima wa Ruvuma, Kiteto, Dodoma, Kilindi na Singida; Kampuni ya Dar - Canton kununua tani 600 za muhogo kutoka kwa wakulima wa mkoa wa Mtwara; na kupatikana kwa ajira za muda mfupi takribani 1,200.

Kwa upande mwingine Mamlaka iliandaa na kuratibu Maonesho ya Sita (6) ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania yaliyofanyika Mjini Unguja kwa lengo la kutangaza na kuongeza hamasa ya kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini pamoja na kutoa fursa ya kuwakutanisha wazalishaji na wateja.

323. Mwaka 2021, TanTrade iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika maonesho ya Expo 2020 Dubai yaliyoanza tarehe 1 Oktoba 2021 na kumalizika tarehe 31 Machi 2022 ambapo Tanzania ni miongoni mwa nchi 192 zilizoshiriki. Maonesho hayo yalitakiwa kufanyika mwaka 2020 ambapo yalihairishwa kutokana na mlipuko wa UVIKO-19 na kupanga kufanyika tena mwaka 2021. Kupitia Maonesho hayo, Tanzania ilitangaza miradi ya kimkakati inayotekeleza ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya tehama, nishati, reli, barabara, bandari, madaraja, viwanja vya ndege, kilimo, uvuvi, mifugo na vivutio vya utalii kwa lengo la kuvutia uwekezaji, kutangaza fursa za biashara, kuvutia utalii na kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia.

324. Kampuni na taasisi za sekta binafsi zaidi ya 640 kutoka Tanzania na Jumuiya ya Watanzania waishio nje ya nchi zilishiriki katika maonesho ya Expo 2020 Dubai kwa lengo la kujitangaza na kukutana na wabia wa biashara katika Sekta mbalimbali. Aidha, mikutano 101 ilifanyika ndani ya banda la Tanzania kati ya taasisi hizo na wawekezaji na wafanyabiashara mbalimbali. Vilievile, programu 11 ziliratibiwa kwa lengo la kutangaza fursa zilizopo katika sekta za kilimo, madini, utalii, afya, ujenzi, miundombinu, usafirishaji, mifugo, uvuvi, nishati, maji, sanaa na utamaduni. Kadhalika, makongamano matatu ya utalii, uwekekezaji na kilimo yaliratibiwa. Katika kipindi hicho, watu 928,469 kutoka mataifa mbalimbali walitembelea banda la Tanzania kwa lengo la kuona fursa za utalii, uwekezaji na biashara, kujifunza mila, desturi na tamaduni za watanzania pamoja na kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia.

325. Mafanikio yaliyopatikana kupitia maonesho ya Expo 2020 Dubai ni pamoja kusainiwa kwa hati 36 za makubaliano zenye thamani ya dola za Marekani bilioni 7.5 (sawa na shilingi trilion 17.4). Kati ya hizo, hati 13 zilisainiwa baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia wizara na taasisi za umma na sekta binafsi na hati 23 zilisainiwa baina ya kampuni binafsi za Tanzania na kampuni nyingine. Aidha, sekta zinazotarajiwa kunufaika na makubaliano hayo ni pamoja na nishati, kilimo, utalii, miundombinu, viwanda, usafiri na teknolojia. Vilevile, makubaliano hayo yanatarajia kuzalisha ajira zaidi ya 200,000. Kupitia maonesho hayo bidhaa mbalimbali ikiwemo kahawa, chai, korosho, vito vya tanzanite, vipodozi vya asili (nazi, mwani na viungo), ngozi, mkonge, sanaa za mikono na ubunifu ziliuzwa katika mfumo wa soko la kimtandao la Expo 2020 Dubai uiitwao *Wolrd Souq*.

Udhibiti Ubora wa Viwango na Vipimo

326. Mwaka 2021, Shirika la Viwango Tanzania - TBS liliandaa viwango vya ubora 545 ikilinganishwa na viwango vya ubora 509 vilivyoandaliwa mwaka 2020, sawa na

ongezeko la asilimia 7.1. Katika kipindi hicho, sampuli 28,425 zilipimwa ikilinganishwa na sampuli 25,560 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 11.2. Ongezeko la uandaaji wa viwango na upimaji wa sampuli lilitokana na mwitikio wa wazalishaji na watumiaji kuzingatia ubora wa bidhaa. Aidha, vifaa 10,282 vilifanyiwa uhakiki/ugezi mwaka 2021 ikilinganishwa na vifaa 10,390 mwaka 2020.

327. Shirika lilitoa leseni 580 za ubora mwaka 2021 ikilinganishwa na leseni 526 zilizotolewa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 10.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uelewa wa watumiaji na wazalishaji kuhusu umuhimu wa kuzingatia ubora wa bidhaa. Kati ya leseni zilizotolewa, leseni 285 zilitolewa kwa wazalishaji wakubwa na wakati na leseni 295 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo. Aidha, mafunzo ya aina 87 za udhibiti ubora yalitolewa kwa washiriki 5,326 mwaka 2021 ikilinganishwa na mafunzo ya aina 128 yaliyotolewa kwa washiriki 9,618 kwa mwaka 2020.

328. Mwaka 2021, Shirika lilisajili na kutoa vibali 8,600 vya maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi ikilinganishwa na vibali 5,182 vilivyotolewa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 66.0. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutumika kwa mfumo wa kielektroniki wa maombi ya usajili wa maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi. Katika kipindi hicho, Shirika lilisajili bidhaa za chakula na vipodozi 1,591 ikilinganishwa na bidhaa 1,886 zilizosajiliwa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 15.6. Upungufu huo ulitokana na uingizaji wa bidhaa nyingi ambazo zilishapata usajili nchini ambapo usajili uhuishwa kila baada ya miaka mitano (5).

329. Shirika lilikagua magari 35,606 yaliyotumika mwaka 2021 ikilinganishwa na magari 43,172 yaliyokaguliwa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 17.5. Kati ya magari yaliyokaguliwa, magari 1,209 sawa na asilimia 3.4 hayakukidhi matakwa ya viwango vya ubora ambapo wateja walielekezwa kufanya marekebisho na kisha kuyarejesha kwa ajili ya kukaguliwa mara ya pili. Aidha, bidhaa 28,818 kutoka nje ya nchi zilikaguliwa mwaka 2021 ikilinganishwa na bidhaa 30,232 zilizokaguliwa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 4.7. Kati ya bidhaa zilizokaguliwa, bidhaa 3,239 sawa na asilimia 11.2 hazikukidhi matakwa ya viwango vya ubora ambapo wamiliki wa bidhaa hizo walielekezwa kuziharibu au kuzirejesha nchi zilipotoka. Upungufu wa magari na bidhaa zilizokaguliwa ulitokana na baadhi ya nchi washirika wa biashara kuendelea kufunga mipaka na kusitisha shughuli za kiuchumi kwa ajili ya kudhibiti maambukizi ya UVIKO-19.

330. Mwaka 2021, vipimo 804,000 vilihakikiwa na Wakala wa Vipimo - WMA ikilinganishwa na vipimo 899,975 vilivyohakikiwa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 10.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa matumizi ya umeme katika maeneo ya vijijini kulikosababisha kupungua kwa vipimo vya mafuta ya taa. Aidha, Wakala ilifanya kaguzi za kushtukiza 4,328 za vipimo mbalimbali vinavyotumika kwenye biashara, afya,

usalama na mazingira ikilinganishwa na kaguzi 5,601 zilizofanyika mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 22.7. Upungufu huo ulitokana na elimu pamoja na semina zilizotolewa kwa wadau mbalimbali kuhusu matumizi ya vipimo sahihi. Katika kipindi hicho, Wakala iliidhinisha aina mpya za vipimo 54 kutoka nje na ndani ya nchi ikilinganishwa na vipimo 56 vilivyoidhinishwa mwaka 2020.

331. Mwaka 2021, Wakala ilitoa leseni na vibali 367 kwa mafundi wanaojihusisha na urekebishaji wa vipimo ikilinganishwa na leseni na vibali 316 vilivyotolewa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 16.1. Ongezeko hilo lilitokana na elimu iliyotolewa kwa wadau mbalimbali wa vipimo kuhusu umuhimu wa vibali na leseni. Aidha, Wakala iliendelea kusimamia matumizi sahihi ya vipimo wakati wa upakuaji na upokeaji wa mafuta ya kula na petroli yanayoingizwa nchini kupitia bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Katika kipindi hicho, meli 115 zenye ujazo wa lita milioni 6,752.0 zilihakikiwa ujazo ikilinganishwa na meli 105 zenye ujazo wa lita milioni 5,881.3 zilizohakikiwa mwaka 2020.

Usawa wa Ushindani na Udhibiti wa Bidhaa Bandia

332. Mwaka 2021, makasha 4,421 ya kusafirishia mizigo yalikaguliwa na Tume ya Ushindani - FCC ikilinganishwa na makasha 5,096 yaliyokaguliwa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 13.2. Kati ya makasha yaliyokaguliwa, makasha 142 yalibainika kuwa na bidhaa bandia ambazo zilikamatwa. Bidhaa hizo ni pamoja na bidhaa za matumizi ya nyumbani, vifaa vya ujenzi, vipuri vya pikipiki na magari, shajala *(stationeries)* pamoja na vifaa vya kielektroniki. Aidha, bidhaa bandia zilizokamatwa ambazo hazikuwa na athari kwa afya za watumiaji ziligawiwa kwa jamii kupitia taasisi mbalimbali za Serikali na bidhaa zilizobainika kuwa na athari kiafya ziliteketezwa.

333. Tume ilichambua mikataba 187 ya kuwalinda walaji inayojumuisha mikataba 160 iliyopokelewa mwaka 2021 na mikataba 27 iliyorithiwa kutoka mwaka 2020. Kutokana na uchambuzi huo, mikataba 77 ilisajiliwa na mikataba 110 ilikuwa katika hatua mbalimbali za usajili. Aidha, mikataba iliyopokelewa ilitoka katika sekta ndogo za fedha na nishati ya jua. Kwa upande mwingine, FCC ilipokea maombi 85 ya kuungana kwa kampuni ambapo maombi 12 yalitoka sekta ya fedha, 14 mawasiliano, manne (4) viwanda na biashara, 24 nishati na madini, sita (6) bima, manne (4) utalii na hoteli, manne (4) dawa, 15 kilimo na mawili (2) ujenzi. Kati ya maombi hayo, Tume iliidhinisha maombi ya kuungana kwa kampuni 68, sawa na asilimia 80. Kati ya maombi yaliyoidhinishwa, maombi 67 yaliidhinishwa bila masharti na ombi 1 liliidhinishwa kwa masharti yenye lengo la kulinda ushindani, kukuza uchumi pamoja na kulinda maslahi ya umma katika soko husika. Maombi 17 hayakuidhinishwa kutokana na kutokukidhi masharti ya kuungana kwa kampuni.

Shirika la Maendeleo la Taifa

334. Shirika la Maendeleo ya Taifa - NDC kupitia Mradi wa mashamba ya mpira ya Kihuhwi (Muheza) na Kalunga (Kilombero) lilizalisha tani 146.9 za mpira mkavu mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 174.1 zilizozalishwa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 15.6. Upungufu huo ulitokana na mabadiliko ya hali ya hewa ikiwemo uwepo wa ukame na upepo mkali uliochangia kupungua kwa kiwango cha utomvu uliovunwa na kuanguka kwa miti mingi ya mpira. Kwa upande mwingine, Shirika kupitia kiwanda cha viuadudu kilizalisha lita 93,040 za viuadudu kwa ajili ya kuua viluilui vya aina mbalimbali za mbu hususani wanaoeneza malaria ikilinganishwa na lita 93,640 zilizozalishwa mwaka 2020. Aidha, lita 96,404 za viuadudu zenye thamani ya shilingi milioni 1,127.5 ziliuzwa ambapo lita 31,964 ziliuzwa katika soko la ndani na lita 64,440 katika soko la nje.

Uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Uwekezaji

335. Mwaka 2021, kampuni mpya 19 zilisajiliwa na Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji - EPZA ikilinganishwa na kampuni saba (7) zilizosajiliwa mwaka 2020. Ongezeko la usajili lilitokana na jitihada za Serikali kuendelea kuhamasisha uwekezaji kwa kuboresha mazingira ya ufanyaji wa biashara. Kampuni zilizosajiliwa zilikuwa; Kriishi Green Limited, Green Bridge Commodities Limited, Coastal Nuts Tanzania Limited, NB Industries Limited, Diamond Foods Limited, Tanzania Huafeng Agriculture Development Limited, East Africa Zhenan Group Co. Ltd, Xin Li Packaging Ltd, African Flame Logistics Ltd, Jabari Investment Limited, HongFei Investment Limited, Apex PET Plastic Limited, ZhongLian Biotecnology Limited, Agrofix Limited, Futan Mining International Limited, Kibidula Farm Limited, Sayona Chemical Limited, Red Earth Limited na Pics (esa) Tanzania Limited.

336. Mwaka 2021, mtaji wa dola za Marekani milioni 82.8 uliwekezwa katika Maeneo Maalumu ya Uwekezaji - EPZ/SEZ ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 89.7 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 7.7. Katika kipindi hicho, mauzo nje ya bidhaa zinazozalishwa katika maeneo maalumu ya uwekezaji yalikuwa dola za Marekani milioni 103.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 79.8 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 29.2. Vilevile, ajira za moja kwa moja 6,582 zilizalishwa mwaka 2021 ikilinganishwa na ajira 665 mwaka 2020. Ongezeko la mauzo ya nje na ajira kulitokana na Serikali kuimarisha ushirikiano wa kimataifa hususani katika diplomasia ya uchumi, kuendelea kuhamasisha uwekezaji na kuboresha usimamizi katika Maeneo Huru ya Uwekezaji.

MATUMIZI YA SARUJI NCHINI

Jedwali Na. 51

Mwaka	Kutoka Nje	Uuzaji nje	Uzalishaji wa ndani	Matumizi	Badiliko Asilimia
2000	7,281	30,497	833,092	809,876	
2001	56,395	53,517	900,430	903,308	11.5
2002	149,079	37,203	1,026,082	1,137,958	26.0
2003	166,446	34,396	1,186,434	1,318,484	15.9
2004	125,007	37,655	1,280,851	1,368,203	3.8
2005	120,200	40,430	1,375,222	1,454,992	6.3
2006	92,711	98	1,421,460	1,514,073	4.1
2007	101,827	52,170	1,629,890	1,679,547	10.9
2008	356,468	99,688	1,755,862	2,012,642	19.8
2009	516,182	57,569	1,940,845	2,399,458	19.2
2010	566,828	189,321	2,312,055	2,689,562	12.1
2011	768,343	217,944	2,408,765	2,959,164	10.0
2012	1,013,986	145,793	2,557,798	3,425,991	15.8
2013	1,218,453	154,481	2,369,819	3,433,791	0.2
2014	1,428,995	142,001	2,795,687	4,082,681	18.9
2015	1,257,578	126,391	3,273,000	4,404,187	7.9
2016	1,306,732	194,338	4,916,400	6,028,794	36.9
2017	188,067	226,588	4,397,684	4,359,163	(27.7)
2018	17,259	206,234	4,766,092	4,577,117	5.0
2019r	0	410,607	5,291,971	4,881,364	6.6
2020r	757,523	476,560	5,606,811	5,887,775	20.6
2021*	688,773	476,937	6,531,096	6,742,932	14.5

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na TRA
r- Takwimu zimebadilishwa

UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI

Jedwali Na. 52

Aina ya Bidhaa	Kipimo	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Biskuti & tambi	Tani	18,225	19,204	15,890	16,451	16,911	18,113	22,430	30,399
Unga wa ngano	Tani	529,797	533,257	498,940	606,432	662,967	680,393	767,476	737,652
Konyagi	000 Lita	31,963	29,491	28,754	25,555	29,335	32,366	33,287	22,066
Bia	000 Lita	379,913	386,310	383,251	396,864	412,555	391,299	385,851	380,464
Chibuku	000 Lita	20,301	23,028	26,513	22,624	20,819	20,350	21,712	23,266
Sigara	Milioni	8,028	7,837	8,091	7,412	7,921	8,369	7,320	7,021
Nguo	000 M^2	119,458	100,496	76,436	52,052	52,613	45,415	53,067	65,365
Kamba za katani	Tani	7,871	8,851	9,216	8,188	8,148	9,287	8,187	8,583
Nyavu za uvuvi	Tani	279	311	312	196	228	254	261	273
Mazulia	000 M^2	-	-	-	-	-	-	-	-
Tabaka za mbao	M^3	38,913	36,317	34,983	37,302	37,849	42,563	34,237	29,867
Dawa za pareto	Tani	136	118	126	134	139	145	154	164
Mbolea	Tani	-	-	-	-	-	-	-	-
Rangi	000 Lita	38,308	38,372	35,096	40,146	47,928	58,024	48,261	64,614
Bidhaa za petrol	000 Tani	-	-	-	-	-	-	-	-
Saruji	000 Tani	2,795	3,135	4,572	4,398	4,766	6,514	6,496	6,531
Chuma	Tani	187,199	205,575	219,765	231,591	275,267	272,531	277,785	291,311
Bati	Tani	86,825	91,385	91,421	84,541	84,132	100,963	107,836	114,421
Aluminium	Tani	27	32	14	-	-	-	-	-
Radio	000 namba	-	-	-	-	-	-	-	-
Betri	Milioni	93	87	69	122	115	120	132	-

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara ya Viwanda na Biashara

- Hakuna uzalishaji

VIWANDA: IDADI YA WATU WALIOAJIRIWA

Jedwali Na. 53

ISIC Rev.4	Shughuli	Walioajiriwa			Wengine			Jumla		
		2019*	2020*	2021*	2019*	2020*	2021*	2019*	2020*	2021*
10	Vyakula	93,072	102,379	112,619	31,285	34,414	14,991	124,357	136,793	127,610
11	Vinywaji	10,084	11,092	12,201	123	136	-1,727	10,207	11,228	10,474
12	Tumbaku na Sigara	7,437	8,182	9,000	9	10	-1,358	7,446	8,192	7,642
13,14	Ufumaji na Ushonaji	39,498	43,449	47,795	30,825	33,908	24,369	70,323	77,357	72,164
15	Ngozi Bidhaa za Ngozi	2,055	2,262	2,488	461	508	96	2,516	2,770	2,584
16	Mbao, Bidhaa za Mbao	10,506	11,556	12,712	3,219	3,541	1,372	13,725	15,097	14,084
17, 18	Karatasi, Uchapishaji	7,856	8,643	9,507	293	322	-1,144	8,149	8,965	8,363
20, 21	Utengenezaji Kemikali na Madawa ya Binadamu	10,506	11,557	12,713	331	364	-1,592	10,837	11,921	11,121
22	Bidhaa za mpira na Plastiki	6,246	6,870	7,557	82	91	-1,063	6,328	6,961	6,494
23	Bidhaa za Madini yasiyo Chuma	11,794	12,975	14,273	1,883	2,071	-237	13,677	15,046	14,036
19, 24-33	Nyinginezo	44,163	48,579	53,438	25,069	27,576	17,605	69,232	76,155	71,043
	Jumla	**243,217**	**267,544**	**294,303**	**93,580**	**102,941**	**51,312**	**336,797**	**370,485**	**345,615**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

VIWANDA: GHARAMA ZA KAZI

Jedwali Na. 54

ISIC Rev.4	Shughuli	Mishahara (Shilingi Milioni)			Malipo Mengine (Shilingi Milioni)			Jumla (Shilingi Milioni)		
		2019*	2020*	2021*	2019*	2020*	2021*	2019*	2020*	2021*
10	Vyakula	479,547	527,501	580,251	87,794	96,574	106,232	567,341	624,075	686,483
11	Vinywaji	293,895	323,284	355,612	124,905	137,396	151,136	418,800	460,680	506,748
12	Tumbaku na Sigara	130,914	144,005	158,405	36,613	40,274	44,301	167,527	184,279	202,706
13,14	Ufumaji na Ushonaji	145,871	160,458	176,504	76,994	84,693	93,162	222,865	245,151	269,666
15	Ngozi Bidhaa za Ngozi	8,289	9,118	10,030	838	922	1,014	9,127	10,040	11,044
16	Mbao, Bidhaa za Mbao	38,587	42,446	46,691	5,464	6,010	6,611	44,051	48,456	53,302
17, 18	Karatasi, Uchapishaji	70,119	77,131	84,844	15,547	17,102	18,812	85,667	94,233	103,656
20, 21	Utengenezaji Kemikali na Madawa ya Binadamu	95,192	104,711	115,182	14,876	16,364	18,000	110,068	121,075	133,182
22	Bidhaa za mpira na Plastiki	48,918	53,810	59,191	7,194	7,913	8,704	56,112	61,723	67,895
23	Bidhaa za Madini yasiyo	128,861	141,747	155,922	39,057	42,963	47,259	167,917	184,710	203,181
19, 24-33	Chuma Nyinginezo	212,580	233,838	257,222	44,239	48,663	53,529	256,819	282,501	310,751
	Jumla	**1,652,773**	**1,818,049**	**1,999,854**	**453,521**	**498,874**	**548,760**	**2,106,294**	**2,316,923**	**2,548,614**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

VIWANDA: MUHTASARI WA MATOKEO

Jedwali Na. 55

ISIC Rev.4	Shughuli	PATO (Shilingi Milioni)			GHARAMA (Shilingi Milioni)			Thamani iliyoongezeka (Value added) (Shilingi Milioni)		
		2019*	2020*	2021*	2019*	2020*	2021*	2019*	2020*	2021*
10	Vyakula	7,276,587	8,004,246	8,804,671	3,344,196	3,678,616	4,046,478	3,932,391	4,325,630	4,758,193
11	Vinywaji	3,000,852	3,300,937	3,631,031	898,561	988,417	1,087,259	2,102,290	2,312,520	2,543,772
12	Tumbaku na Sigara	1,127,667	1,240,434	1,364,477	283,013	311,314	342,445	844,654	929,120	1,022,032
13,14	Ufumaji na Ushonaji Ngozi	880,556	968,612	1,065,473	403,109	443,420	487,762	477,446	525,192	577,711
15	Bidhaa za Ngozi Mbao,	98,831	108,714	119,585	67,091	73,800	81,180	31,739	34,914	38,405
16	Bidhaa za Mbao	267,534	294,287	323,716	88,745	97,620	107,382	178,790	196,667	216,334
17, 18	Karatasi, Uchapishaji	483,649	532,014	585,215	299,476	329,424	362,366	184,173	202,590	222,849
20, 21	Utengenezaji Kemikali na Madawa ya Binadamu	1,059,335	1,165,269	1,281,796	662,883	729,171	802,088	396,452	436,098	479,708
22	Bidhaa za mpira na Plastiki	1,088,139	1,196,953	1,316,648	703,591	773,950	851,345	384,548	423,003	465,303
23	Bidhaa za Madini yasiyo Chuma	1,389,447	1,528,392	1,681,231	705,135	775,649	853,214	684,312	752,743	828,017
19, 24-33	Nyinginezo	2,136,223	2,349,845	2,584,830	1,240,384	1,364,423	1,500,865	895,839	985,422	1,083,965
	Jumla	**18,808,820**	**20,689,703**	**22,758,673**	**8,696,185**	**9,565,804**	**10,522,384**	**10,112,635**	**11,123,899**	**12,236,289**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

VIWANDA: MUHTASARI WA MATOKEO KIMKOA

Jedwali Na. 56

Jina la Mkoa	Idadi ya Wafanyakazi			Idadi ya waajiriwa			Mishahara (Shilingi Milioni)			Thamani Iliyoongezeka (Shilingi Milioni)		
	2019*	2020*	2021*	2019*	2020*	2021*	2019*	2020*	2021*	2019*	2020*	2021*
Dodoma	3,644	4,009	3,740	2,631	2,894	3,184	20,682	22,750	25,025	126,546	139,200	153,120
Arusha	28,585	31,444	29,333	20,643	22,707	24,978	70,222	77,243	84,967	429,659	472,625	519,888
Kilimanjaro	21,463	23,610	22,025	15,500	17,050	18,756	88,946	97,840	107,624	544,224	598,647	658,512
Tanga	16,202	17,823	16,627	11,701	12,871	14,159	110,838	121,922	134,114	678,176	745,994	820,593
Morogoro	50,775	55,853	52,104	36,666	40,333	44,367	47,023	51,725	56,898	287,710	316,480	348,128
Pwani	15,805	17,385	16,218	11,414	12,555	13,811	66,714	73,385	80,724	408,194	449,014	493,915
Dar es Salaam	108,672	119,542	111,517	78,477	86,325	94,959	949,027	1,043,930	1,148,323	5,806,702	6,387,375	7,026,113
Lindi	1,621	1,783	1,663	1,172	1,289	1,418	422	464	510	2,584	2,842	3,126
Mtwara	4,699	5,169	4,822	3,394	3,733	4,106	15,738	17,312	19,043	96,290	105,919	116,511
Ruvuma	3,032	3,335	3,111	2,190	2,409	2,649	3,173	3,490	3,839	19,420	21,362	23,498
Iringa	8,081	8,889	8,292	5,836	6,419	7,061	37,541	41,295	45,425	229,696	252,665	277,932
Mbeya	9,678	10,646	9,931	6,988	7,687	8,456	76,376	84,014	92,415	467,312	514,043	565,447
Singida	3,744	4,118	3,842	2,705	2,976	3,273	2,747	3,022	3,324	16,804	18,484	20,332
Tabora	1,192	1,313	1,225	860	946	1,041	15,149	16,664	18,330	92,689	101,958	112,154
Rukwa	2,494	2,744	2,560	1,801	1,981	2,179	8,750	9,625	10,588	53,538	58,892	64,781
Kigoma	3,036	3,339	3,115	2,192	2,412	2,653	1,475	1,622	1,784	9,024	9,926	10,919
Shinyanga	4,465	4,912	4,582	3,225	3,547	3,902	15,047	16,552	18,207	92,064	101,270	111,397
Kagera	5,817	6,399	5,969	4,201	4,621	5,083	7,006	7,707	8,478	42,867	47,153	51,868
Mwanza	17,812	19,594	18,279	12,863	14,149	15,565	87,974	96,771	106,448	538,276	592,104	651,314
Mara	5,707	6,277	5,856	4,121	4,533	4,987	7,687	8,456	9,302	47,030	51,733	56,906
Manyara	8,302	9,132	8,519	5,995	6,594	7,253	3,660	4,025	4,428	22,395	24,635	27,099
Njombe	4,443	4,887	4,559	3,209	3,530	3,883	6,985	7,684	8,452	42,741	47,015	51,717
Katavi	2,302	2,532	2,362	1,662	1,829	2,012	1,503	1,653	1,818	9,193	10,112	11,123
Simiyu	2,830	3,113	2,904	2,044	2,248	2,473	5,610	6,170	6,787	34,327	37,760	41,536
Geita	971	1,069	997	702	772	849	276	304	334	1,690	1,857	2,043
Songwe	1,426	1,568	1,463	1,030	1,133	1,246	2,204	2,424	2,667	13,485	14,834	16,317
Jumla	**336,798**	**370,485**	**345,615**	**243,220**	**267,544**	**294,303**	**1,652,775**	**1,818,049**	**1,999,854**	**10,112,636**	**11,123,899**	**12,236,289**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

SURA YA 15

UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI

UJENZI

Mtandao wa Barabara Nchini

337. Mtandao wa barabara nchini kwa mwaka 2021 ulifikia kilomita 180,791.7 ambapo mtandao unaosimamiwa na Wakala wa Barabara nchini - TANROADS ni kilomita 36,361.9 na mtandao unaosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini - TARURA ni kilometa 144,429.8. Mtandao wa barabara zinazosimamiwa na TANROADS ulipungua kutoka kilometa 89,204 mwaka 2020 kutokana na barabara za wilaya zinazounganisha wilaya, kata na vijiji kuhamishiwa chini ya usimamizi wa TARURA. Mtandao wa barabara zinazosimamiwa na TANROADS unajumuisha, kilometa 12,215.6 za barabara kuu zinazounganisha mikoa na nchi jirani na kilometa 24,146.4 za barabara za mikoa zinazounganisha miji mikuu ya mikoa na wilaya.

338. Barabara kuu na za mikoa zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilizofanyiwa tathmini mwaka 2021 zilikuwa na urefu wa kilometa 33,722.5 ikilinganishwa na kilometa 33,649.7 mwaka 2020. Kati ya barabara hizo, kilometa 3,614.6 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 17,431.9 hali ya wastani na kilometa 12,676.0 hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 4,256.8, kilometa 16,621.7 na kilometa 12,771.2 mwaka 2020, mtawalia. Barabara zenye hali mbaya zilipungua kutokana na baadhi ya barabara kujengwa kwa kiwango cha lami na barabara zilizokuwepo kuendelea kufanyiwa matengenezo.

339. Mwaka 2021, barabara kuu zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilizofanyiwa tathmini ziliongezeka kwa asilimia 12.7 na kufikia kilometa 11,068.7 ikilinganishwa na kilometa 9,823.1 mwaka 2020. Kati ya barabara hizo, kilometa 1,608.2 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 3,158.5 hali ya wastani na kilometa 6,302.0 hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 1,653.8, kilometa 1,997.0 na kilometa 6,172.3 mwaka 2020, mtawalia. Barabara zenye hali mbaya zilipungua kutokana na baadhi ya barabara kujengwa kwa kiwango cha lami na barabara zilizokuwepo kuendelea kufanyiwa matengenezo.

340. Mwaka 2021, kilometa 22,653.9 za barabara za mikoa zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilifanyiwa tathmini ikilinganishwa na kilometa 23,826.6 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 4.9. Hii ilitokana na matengenezo yaliyokuwa yanaendelea kwa baadhi ya barabara na hivyo kutofanyiwa tathmini. Kati ya barabara hizo, kilometa 2,006.4 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 14,273.5 hali ya wastani na kilometa 6,374.0 hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 2,603, kilometa 14,624.7 na kilometa 6,598.9 mwaka 2020, mtawalia.

Jedwali Na. 15.1: Hali ya Mtandao wa Barabara Zilizofanyiwa Tathmini Mwaka 2021

Aina ya Barabara	Hali ya Mtandao wa barabara						Jumla
	Nzuri		Wastani		Mbaya		
	Kilomita	%	Kilomita	%	Kilomita	%	Kilomita
Barabara kuu lami	5,602.5	63	1,853.5	21	1,451.0	16	8,906.9
Barabara kuu changarawe/udongo	699.6	32	1,305.0	60	157.3	7	2,161.8
Jumla Ndogo	**6302.0**	**57**	**3,158.5**	**29**	**1,608.2**	**15**	**11,068.7**
Barabara za mikoa lami	816.3	45	473.2	26	540.2	30	1,829.7
Barabara za mikoa changarawe/udongo	5,557.6	27	13,800.3	66	1,466.2	7	20,824.2
Jumla Ndogo	**6,374.0**	**28**	**14,273.5**	**63**	**2,006.4**	**9**	**22,653.8**
Jumla Kuu	**12,676.0**	**38**	**17,431.9**	**51**	**3,614.6**	**11**	**33,722.5**

Chanzo: Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi)

341. Mtandao wa barabara unaosimamiwa na TARURA una jumla ya kilomita 144,429.8 ambazo zimetangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali Na. 463 la tarehe 25 Juni 2021. Hii imeongezeka kutoka kilometa 108,946.2 mwaka 2020 kufuatia matokeo ya tathmini na uhakiki uliofanyika wa barabara zinazosimamiwa na TARURA. Kati ya barabara hizo, kilomita 2,473.55 ni barabara za lami, kilomita 30,756.51 ni barabara ya changarawe na kilomita 111,199.72 (asilimia 76.99) ni barabara za udongo ikilinganishwa na kilometa 2,205.7, kilometa 27,809.3 na kilometa 78,886.3 mwaka 2020 mtawalia. Aidha, kati ya barabara zinazosimamiwa za TARURA: kilometa 31,106.0 zilikuwa katika hali nzuri, kilometa 50,623.1 hali ya wastani na kilometa 62,700.7 zilikuwa katika hali mbaya.

Jedwali Na. 15.2: Hali ya Mtandao wa Barabara za Vijijini na Mijini Mwaka 2021

Aina ya Barabara	Hali ya Mtandao wa Barabara (Kilomita)			Jumla (Kilomita)	Asilimia
	Nzuri	Wastani	Mbaya		
Barabara za lami	1,841.9	459.7	171.9	2,473.6	1.7
Barabara za Changarawe	13,559.2	13,059.4	4,146.9	30,756.5	21.3
Barabara za udongo	15,713.9	37,104.0	58,381.8	111,199.7	77.0
Jumla (Kilometa)	**31,106.0**	**50,623.1**	**62,700.7**	**144,429.8**	**100**
Asilimia	21.5	35.1	43.4	100.0	

Chanzo: Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini

342. Hadi Desemba 2021, TARURA ilijenga na kukarabati barabara za wilaya zenye urefu wa kilometa 34,514.9 ikilinganishwa na kilometa 26,201.6 zilizojengwa na kukarabatiwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 31.7. Hii ilichangiwa na kuendelea kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa barabara ikiwemo ujenzi wa barabara za lami katika Mji wa Serikali – Dodoma. Katika kipindi hicho, barabara zenye urefu wa kilometa 284.0 zilijengwa kwa kiwango cha lami, kilometa 4,282.8 zilijengwa kwa kiwango cha changarawe na kilometa 29,948.1 zilifanyiwa ukarabati maalumu, wa kawaida pamoja na ukarabati wa maeneo korofi.

343. Mwaka 2021, Wakala ulijenga madaraja 212, makalavati 2,122, mitaro mikubwa ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 56.8 na kukarabati madaraja 236 ikilinganishwa na madaraja 19, makalavati 786, mitaro ya maji yenye urefu wa kilometa 89.4 na madaraja 102 mwaka 2020, mtawalia. Hadi Desemba 2021, Wakala kupitia miradi ya uendelezaji wa miji na majiji uliwezesha: ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 16 kwa kiwango cha lami; ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 17.9 katika halmashauri za manispaa za Kinondoni, Temeke na Ilala; na ununuzi wa magari 20 ya kubeba taka ngumu pamoja na vyombo vya kukusanyia taka.

Barabara, Madaraja, Vivuko na Magari

344. Mwaka 2021, Wakala wa Barabara Tanzania - TANROADS ulitengeneza barabara kuu na za mikoa zenye urefu wa kilometa 32,979.2 ikilinganishwa na kilometa 34,706.2 zilizotengenezwa mwaka 2020. Aidha, madaraja 2,728 yalitengenezwa ikilinganishwa na madaraja 2,482 yaliyotengenezwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 9.9. Ongezeko la madaraja yaliyotengenezwa lilitokana na jitihada za Serikali katika kuimarisha miundombinu ya barabara.

345. Mwaka 2021, Serikali ilinunua kivuko kipya cha MV Kilindoni chenye uwezo wa kubeba tani 100 kwa lengo la kuboresha huduma ya usafiri katika kisiwa cha Mafia na hivyo kufanya vivuko vinavyosimamiwa na Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania - TEMESA kufikia vivuko 34 kutoka vivuko 33 mwaka 2020. Katika kipindi hicho, abiria 34,480,252, magari 1,231,856 na mizigo yenye uzito wa tani 1,924.22 ilivushwa kwa kutumia vivuko hivyo ikilinganishwa na abiria 30,290,361, magari 1,291,974 na mizigo yenye uzito wa tani 7,159.6 mwaka 2020. Kupungua kwa magari na mizigo kulitokana na uharibifu wa miundombinu ya vivuko (maegesho ya vivuko na barabara za kuelekea kwenye vivuko) uliosababishwa na kiwango kikubwa cha mvua.

346. Mwaka 2021, TEMESA iliendelea kufanya matengenezo kinga ya vivuko vyote nchini na ukarabati mkubwa kwa vivuko vya MV Sengerema, MV Tegemeo na Boti ndogo ya Uokozi (MV Mwanza). Katika kipindi hicho, Wakala uliendelea: kukabarati karakana za magari za Mwanza, Mbeya na Arusha; kuboresha miundombinu ya maegesho ya vivuko katika mikoa ya Mwanza, Geita na Mara ; na kujenga maegesho mapya ya Kayenze - Kanyinya (Kagera), Muleba - Ikuza (Kagera), Ijinga - Kahangala

(Mwanza), Bwiro - Bukondo (Mwanza), Mafia - Nyamisati (upande wa Mafia - Pwani) na Mlimba - Malinyi (Morogoro). Aidha, magari 29,263 yalitengenezwa na TEMESA mwaka 2021 ikilinganishwa na magari 30,701 mwaka 2020.

Mfuko wa Barabara

347. Mwaka 2021, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilikusanya shilingi bilioni 926.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 820.9 zilizokusanywa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 12.9. Hii ilichangiwa na kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi zinazotumia nishati ya mafuta ikiwemo miradi ya reli ya kisasa (Standard Gauge Railway) na mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere. Aidha, miradi ya barabara 594 ilikaguliwa na Bodi mwaka 2021 ikilinganishwa na miradi 647 iliyokaguliwa mwaka 2020.

Nyumba na Majengo ya Serikali

348. Wakala wa Majengo Tanzania - TBA uliendelea kusanifu na kusimamia ujenzi wa miradi 258 ya nyumba na majengo ya Serikali mwaka 2021 ikilinganishwa na miradi 484 iliyosanifiwa na kusimamiwa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 46.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ushindani kutoka taasisi zinazotoa huduma sawa na Wakala. Aidha, Wakala ulisimamia miradi 166 ya ukarabati wa nyumba na majengo ikilinganishwa na miradi 82 mwaka 2020.

349. Mwaka 2021, nyumba 6,222 zilipangishwa kwa wapangaji wa kibiashara na watumishi wa umma ikilinganishwa na nyumba 6,649 mwaka 2020. Kati ya hizo, nyumba 1,622 zilipangishwa kwa watumishi wa umma na nyumba 4,600 kibiashara ikilinganishwa na nyumba 4,929 na 1,720 zilizopangishwa mwaka 2020, mtawalia. Kuongezeka kwa nyumba zilizopangishwa kibiashara kulitokana na kubadilishwa kwa matumizi ya nyumba za makazi kuwa za biashara.

Usajili wa Makandarasi

350. Mwaka 2021, Bodi ya Usajili wa Makandarasi ilisajili makandarasi 944 ikilinganishwa na makandarasi 907 waliosajiliwa mwaka 2020. Usajili huo uliongeza idadi ya makandarasi waliosajiliwa kufikia 12,673 Desemba 2021. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishaji uliofanywa na Bodi kwa kuwataka makandarasi kujisajili kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Makandarasi, Na. 17 ya mwaka 1997 na marekebisho yake ya mwaka 2008. Kwa upande mwingine, miradi ya ujenzi 3,878 ilisajiliwa na Bodi ikilinganishwa na miradi 3,179 iliyosajiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 22.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli mbalimbali za ujenzi zilizosajiliwa.

351. Mwaka 2021, miradi 3,518 ilikaguliwa na Bodi ikilinganishwa na miradi 3,364 iliyokaguliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 4.6. Ongezeko hilo lilitokana na utii wa sheria katika kutekeleza miradi kwa kutumia makandarasi. Kati ya miradi iliyokaguliwa, miradi 2,571 haikuwa na mapungufu na miradi 947 ilikuwa na

mapungufu. Aidha, hatua mbalimbali za kisheria zilichukuliwa kwa miradi iliyokuwa na mapungufu ikiwemo kutoza faini kwa makandarasi na kusimamisha ujenzi wa baadhi ya miradi. Vilevile, Bodi ilipeleka mahakamani mashauri 97 ya makosa mbalimbali ikiwemo kutekeleza miradi kwa kutumia kampuni au wataalam wasio makandarasi ikilinganishwa na mashauri 116 mwaka 2020.

352. Mwaka 2021, Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilisajili wahandisi 3,224 wa fani mbalimbali ikilinganishwa na wahandisi 2,841 waliosajiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 13.5. Usajili huo uliongeza idadi ya wahandisi waliosajiliwa kufikia 32,983 hadi Desemba 2021. Ongezeko la usajili wa wahandisi lilitokana na wahitimu kuendelea kujisajili kutokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi zenye mahusiano ya moja kwa moja na taaluma ya uhandisi ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya reli, barabara, madaraja, bandari na viwanja vya ndege. Kati ya wahandisi waliosajiliwa, wahandisi 2,977 sawa na asilimia 92.3 walikuwa watanzania na wahandisi 247 walitoka nje ya nchi. Aidha, Bodi ilisajili mafundi sanifu 314 mwaka 2021 ikilinganishwa na mafundi sanifu 224 waliosajiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 40.2. Usajili huo uliongeza idadi ya mafundi sanifu waliosajiliwa na Bodi na kufikia 779 hadi Desemba 2021. Ongezeko hilo lilitokana na kuanzishwa kwa mfumo wa kielektroniki wa usajili wa mafundi sanifu.

353. Mwaka 2021, Bodi ilisajili kampuni za ushauri 13 ikilinganishwa na kampuni 22 zilizosajiliwa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 40.9. Usajili huo ulifanya idadi ya kampuni zilizosajiliwa na Bodi kufikia 389 hadi Desemba 2021. Kati ya kampuni zilizosajiliwa, kampuni nane (8) zilikuwa za kitanzania na kampuni tano (5) za kigeni. Katika kipindi hicho, Bodi ilisajili wahandisi washauri 17 ikilinganishwa na wahandisi washauri 27 waliosajiliwa mwaka 2020. Usajili huo ulifanya idadi ya wahandisi washauri waliosajiliwa kufikia 622 hadi Desemba 2021. Kati ya hao, wahandisi washauri 12 walikuwa wa kitanzania na wahandisi washauri watano (5) wa kigeni. Kupungua kwa usajili wa kampuni na wahandisi washauri kulichangiwa na kutokuwepo kwa miradi mikubwa mipya ambayo utekelezaji wake unahitaji wahandisi washauri. Kwa upande mwingine, Bodi ilisajili maabara za vifaa vya ujenzi na uhandisi mbili (2) mwaka 2021 ikilinganishwa na maabara tatu (3) mwaka 2020. Usajili huo ulifanya maabara za vifaa vya ujenzi na uhandisi zilizosajiliwa na Bodi kufikia 39 hadi Desemba 2021.

354. Mwaka 2021, wahandisi waliopata mafunzo waliongezeka kwa asilimia 29.5 na kufikia 1,534 ikilinganishwa na wahandisi 1,185 waliopata mafunzo mwaka 2020. Idadi hiyo iliongeza wahandisi waliopata mafunzo kufikia 9,978 Desemba 2021. Ongezeko la wahandisi waliopata mafunzo lilitokana na kuanza kutumika kwa mfumo wa kielektroniki uliowawezesha wahandisi kuwasilisha maombi ya mafunzo. Kati ya wahandisi waliopata mafunzo, wahandisi 321 walihitimu na kusajiliwa kama wahandisi

wataalamu mwaka 2021 ikilinganishwa na wahandisi 516 waliohitimu na kusajiliwa mwaka 2020. Kwa upande mwingine, Bodi ilisajili miradi ya ujenzi 795 mwaka 2021 ikilinganishwa na miradi 567 iliyosajiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 40.2. Hii ilichangiwa na Bodi kuanza kusajili miradi ya ujenzi kwa kutumia mfumo wa kielekroniki. Aidha, Bodi ilikagua miradi 72 mwaka 2021 ikilinganishwa na miradi 77 iliyokaguliwa mwaka 2020.

Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

355. Mwaka 2021, wataalamu waliosajiliwa na Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi waliongezeka kwa asilimia 6.4 na kufikia 1,245 ikilinganishwa na wataalamu 1,170 waliosajiliwa mwaka 2020. Kati ya hao, wataalamu 1,212 walikuwa watanzania na wataalamu 33 walikuwa wageni. Kuongezeka kwa wataalamu waliosajiliwa kulichangiwa na mwitikio chanya wa wahitimu kujisajili kufuatia uhamasishaji uliofanywa na Bodi. Aidha, Bodi ilisajili kampuni 414 za wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi mwaka 2021 ikilinganishwa na kampuni 406 zilizosajiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 2.0. Kati ya hizo, kampuni 408 sawa na asilimia 98.6 zilikuwa za kitanzania na kampuni 6 za kigeni.

356. Mwaka 2021, Bodi ilisajili miradi 987 ya ujenzi wa majengo ikilinganishwa na miradi 828 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 19.2. Aidha, Bodi ilikagua miradi 2,404 ya ujenzi wa majengo ikilinganishwa na miradi 1,777 iliyokaguliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 35.3. Ongezeko la miradi iliyosajiliwa na kukaguliwa lilitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa miradi ya ujenzi na kuzingatiwa kwa Sheria Namba 4 ya Usajili ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi.

357. Mwaka 2021, wahitimu 213 walishiriki mafunzo kwa vitendo katika fani ya ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi yanayotolewa na Bodi ikilinganishwa na wahitimu 108 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 97.2. Hii ilichangiwa na ufadhili wa mafunzo uliotolewa na Serikali na kuongezeka kwa idadi ya wahitimu kutoka vyuo vikuu.

Baraza la Taifa la Ujenzi

358. Mwaka 2021, Baraza la Taifa la Ujenzi lilifanya ukaguzi wa kiufundi katika miradi 46 ya ujenzi ya barabara, madaraja na majengo ikilinganishwa na miradi 63 iliyokaguliwa mwaka 2020. Katika kipindi hicho, Baraza lilitoa ushauri wa kiufundi kwa wadau sita (6) wa sekta ya ujenzi ikilinganishwa na wadau 10 mwaka 2020. Aidha, Baraza lilisuluhisha migogoro 78 ya ujenzi ikilinganishwa na migogoro 60 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 30. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uelewa wa taratibu za usuluhishi wa migogoro uliotokana na mafunzo yaliyotolewa kwa wadau.

359. Mwaka 2021, Baraza lilitoa mafunzo kwa wadau 95 wa sekta ya ujenzi ikilinganishwa na wadau 67 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 41.8. Mafunzo hayo yalijumuisha usimamizi wa mikataba, usuluhishi wa migogoro na ukaguzi wa kiufundi wa miradi. Ongezeko hilo lilitokana na wadau kuhitaji kupata uelewa kuhusu marekebisho ya Sheria ya Usuluhishi wa Migogoro ya Mwaka 2020 pamoja na juhudi za Baraza kutangaza mafunzo hayo kwa njia mbalimbali ikiwemo mitandao ya kijamii na tovuti ya baraza. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania - TBS liliandaa viwango 54 vya ubora wa vifaa vya ujenzi mwaka 2021 ikilinganishwa na viwango 34 vilivyoandaliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 58.8. Ongezeko hilo lilitokana na mapitio ya viwango vya ubora yaliyofanyika ili kuendana na viwango vya kimataifa.

Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi

360. Mwaka 2021, Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi ilitoa mafunzo ya stashahada kwa wanafunzi 41 ikilinganishwa na wanafunzi 24 waliopata mafunzo hayo mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 70.8. Hii ilitokana na Taasisi kujitangaza na kuanza kutambulika kwenye jamii. Katika kipindi hicho, washiriki 172 walipata mafunzo ya muda mfupi ikilinganishwa na washiriki 218 waliopata mafunzo mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 21.1. Upungufu huo ulisababishwa na idadi ndogo ya maombi ya udahili kutokana na athari za UVIKO-19. Aidha, Taasisi ilitoa mafunzo kwa mafundi sanifu 13 kuhusu matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi katika kukarabati na kutengeneza barabara za changarawe mwaka 2021 ikilinganishwa na mafundi sanifu 6 waliopata mafunzo hayo mwaka 2020. Ongezeko la washiriki lilitokana na uhamasishaji uliofanywa na Taasisi kuhusu umuhimu wa mafunzo hayo.

361. Mwaka 2021, Taasisi ilihamasisha matumizi ya teknolojia ya nguvukazi kwa wadau 35 wa barabara kutoka TARURA na baadhi ya halmashauri ikilinganishwa na wadau 122 kwa mwaka 2020. Upungufu wa wadau ulitokana na uchache wa wakufunzi wa kufanya uhamasishaji kwenye halmashauri mbalimbali. Aidha, Taasisi ilishiriki katika kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo makandarasi wanawake 111 katika kazi za matengenezo na ukarabati wa barabara mwaka 2021 ikilinganishwa na makandarasi wanawake 50 waliopata mafunzo mwaka 2020. Kuongezeka kwa idadi ya washiriki kulitokana na juhudi za Serikali katika kuhamasisha makandarasi wanawake kushiriki mafunzo na fursa mbalimbali za ukandarasi.

MAENDELEO YA ARDHI

Utayarishaji wa Hatimiliki, Ukaguzi na Uhakiki Milki

362. Mwaka 2021, hatimiliki za viwanja na mashamba zilizoandaliwa kwa ajili ya usajili zilikuwa 88,810 ikilinganishwa na hatimiliki 71,972 zilizoandaliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 23.4. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa viwanja vilivyopimwa kutokana na utekelezaji wa Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha

Ardhi pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa kumiliki ardhi kisheria. Aidha, hatimiliki za kimila 76,245 zilitolewa kwa wananchi mwaka 2021 ikilinganishwa na hatimiliki 127,116 zilizotolewa mwaka 2020. Kwa upande mwingine, ilani 3,516 za ubatilisho zilitumwa kwa wapangaji waliokiuka masharti ya upangaji wa ardhi ikilinganishwa na ilani 17,199 zilizotumwa mwaka 2020. Kupungua kwa ilani za ubatilisho kulitokana na elimu iliyotolewa kwa umma kuhusu sera, sheria na miongozo mbalimbali ya umiliki wa ardhi.

Usajili wa Hatimiliki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria

363. Mwaka 2021, hatimiliki na nyaraka za kisheria zilizosajiliwa zilikuwa 141,630 ikilinganishwa na hatimiliki na nyaraka za kisheria 133,217 zilizosajiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 6.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa umiliki salama wa eneo pamoja na matumizi ya hatimiliki hizo ikiwemo dhamana ya mkopo.

Jedwali Na 15.3: Usajili wa Hatimiliki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria Mwaka 2017 - 2021

Hati zilizosajiliwa	**2017**	**2018**	**2019**	**2020**	**2021**
Hati za kumiliki ardhi zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura 334)	21,743	41,522	47,948	57,180	61,527
Hati za Sehemu ya Jengo chini ya Sheria ya Usajili wa Hati za Sehemu ya Jengo (*Unit Title Act No*.17/2008).	827	844	321	924	232
Jumla Hatimiliki	**22,570**	**42,366**	**48,269**	**58,104**	**61,759**
Nyaraka zilizosajiliwa					
Nyaraka za Kisheria zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura 334).	13,821	27,716	15,018	35,477	39,252
Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura 117).	13,027	21,807	26,096	33,938	36,354
Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya mali zinazohamishika (Sura 210).	310	1,817	3,129	5,698	4,265
Jumla Nyaraka za Kisheria	**27,158**	**51,340**	**44,243**	**75,113**	**79,871**
Jumla Kuu Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria	**49,728**	**93,706**	**92,512**	**133,217**	**141,630**

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Uthamini wa Mali

364. Mwaka 2021, Serikali iliidhinisha taarifa za uthamini 57,274 ikilinganishwa na taarifa 40,874 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 40.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa miamala ya ardhi hususan katika maeneo ya uhamisho wa milki, uhuishaji wa milki, mikopo, uthamini kwa ajili ya mizania ya kimahesabu na fidia katika miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali.

Upimaji wa Mashamba na Viwanja

365. Mwaka 2021, ramani zenye viwanja 418,831 na mashamba 671 ziliidhinishwa ikilinganishwa na ramani zenye viwanja 337,598 na mashamba 372 zilizoidhinishwa mwaka 2020. Kuongezeka kwa viwanja vilivyopimwa na kuidhinishwa kulitokana na kuongezeka kwa kasi ya upangaji na upimaji katika maeneo mbalimbali yasiyopangwa na kupimwa nchini.

Jedwali Na. 15.4: Viwanja na Mashamba Yaliyoidhinishwa Mwaka 2021

Na.	Mikoa	2020		2021	
		Viwanja	Mashamba	Viwanja	Mashamba
1	Arusha	19,051	6	34,732	13
2	Dar Es Salaam	19,033	0	37,574	
3	Dodoma	90,032	13	91,760	7
4	Geita	13,468	0	8,657	1
5	Iringa	8,674	19	9,047	17
6	Kagera	9,049	38	8,371	25
7	Katavi	1,547	7	5,895	96
8	Kigoma	9,909	12	12,690	52
9	Kilimanjaro	9,545	21	9,248	15
10	Lindi	3,725	10	5,994	31
11	Manyara	10,712	9	6,521	30
12	Mara	8,945	1	7,618	1
13	Mbeya	5,713	19	20,080	1
14	Morogoro	6,222	151	7,965	171
15	Mtwara	4,383	4	12,970	4
16	Mwanza	24,073	0	20,878	2
17	Njombe	11,041	7	4,165	2
18	Pwani	19,595	10	33,827	129
19	Rukwa	3,623	3	3,570	44
20	Ruvuma	5,472	8	8,908	6
21	Shinyanga	5,097	0	14,035	1
22	Simiyu	6,675	12	2,900	6
23	Singida	12,189	0	13,389	2
24	Songwe	3,702	10	3,034	
25	Tabora	10,210	7	14,766	5
26	Tanga	15,913	5	20,237	10
	Jumla	**337,598**	**372**	**418,831**	**671**

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mipango ya matumizi ya Ardhi

366. Mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 316 iliandaliwa katika wilaya 41 nchini mwaka 2021 ikilinganishwa na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 67 iliyoandaliwa katika wilaya 17 mwaka 2020. Ongezeko la idadi ya vijiji vilivyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi lilitokana na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na kuongezeka kwa ushiriki wa wadau katika upangaji na usimamizi wa matumizi ya ardhi.

Jedwali Na. 15.5: Orodha ya Vijiji vilivyoandaliwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Mwaka 2021

Mkoa	Wilaya	Kijiji	Idadi ya Vijiji
Kigoma	Kigoma(V)	Kasuku, Nyamoli, Pamila, Simbo, Machazo, Bigere, Nkungwe, Nyangova, Matyazo, Kizenga, Kiziba, Zashe, Mongoro, Bugamba, Chankele, Bubango, Mgaraganza, Kagongo, Mtanga, Kigalye, Mwamgongo, Milinzi	22
	Uvinza	Kalenge, Mlela, Chakulu, Malagasi, Mpeta, Mazungwe, Kazuramimba, Mwamila, Sunuka, Karago, Kanyangili, Songambele, Kangwena, Kabeba, Katete, Kandaga, Mwakizega, Kahuibili, Lyabusende, Msihezi, Sigunga, Kirando	22
Singida	Singida(V)	Malolo, Mwanyonye, Mdilu, Minyaa, Minyenye, Mpambaa, Mwasauya, Ndungwira, Mwakichenche, Kihunadi, Ikiwu, Mitonto, Mwakiti, Mudida, Ntonge, Mkimbili, Kijota, Nduu, Mughanga, Ntunduu, Itamka, Idd Simba, Makhandi, Mitula, Duamghanga, Mwighanji, Ngimu, Pohama	28
	Ikungi	Mwasutianga, Isuna A, Isuna B, Minyughe, Matogo, Mlandara, Mwaru, Ulyampiti, Mnyange, Igombwe, Dung'unyi, Mwau, Tupendane, Mlumbi, Muhintiri, Kaugeri, Mang'onyi, Iyumbu Mgungira, Mtavita, Munyu, Mnang'ana na Irisya	23
Mbeya	Mbeya (V)	Lyela, Ipinda, Tembela, Iyela Nyala, Mjele, Njelenje, Lusungo, Mwampalala, Igale, Holongo, Shisyete, Inyalailembo, Lwalanje, Idunda, Idongwa, Itaga,	21

Mkoa	Wilaya	Kijiji	Idadi ya Vijiji
		Shongo, Itimu, Innolo, Yungamapinduzi, Mlowo	
	Mbarali	Chamoto, Msesule, Mwaluma, Mbuyuni, Mpolo, Uhambule, Mantenga, Mswiswi, Ibohora, Isunura, Mkandami, Luwango, Itipingi, Malamba, Mbalino, Matebete, Ihahi, Itamboleo	18
Ruvuma	Mbinga	Barabara, Makoro, Kiwombi	3
	Namtumbo	Chengena, Kilangalanga, Njalamatata, Masuguru	4
	Songea	Matimira A	1
	Tunduru	Namsakata	1
	Nyasa	Mkali B	1
Lindi	Liwale	Chigugu, Lilombe, Luwele	3
	Nachingwea	Mjengo, Matekwe,	2
	Ruangwa	Nahangwa, Mchichili	2
	Mtama	Nteme, Mhima	2
Dodoma	Mpwapwa	Chitemo, Kimagai, Godegode, Kisisi, Gulwe, Iyoma, Msagali, Panadambii, Darajani	9
	Chamwino	Mnase, Igandu, Chimwaga, Msamalo	4
	Chemba	Kaloleni, Mrijo Chini, Mrijo juu, Cheku A, Cheku B, Makamaka	6
Tanga	Kilindi	Mzungu wa Sala, Gitu Gobore Kwekikwembe. Mtonga, Mkindi, Jungu, Lekitinge	8
	Muheza	Mianga, Makole, Kibanda, Songabatini, Pangamlima, Mamboleo, Mpakani, Nkinga, Kilulu, Tingeni, Magoda, Songakibaoni.	12
Rukwa	Sumbawanga	Mtapenda, mpete, Ilangwa, Mbwilo	4
	Nkasi	Lyele, Tambaruka, Kasapa, Kisula, Malongwe	5
	Kalambo	Kachele, Kipanga	2
Njombe	Njombe	Iyembela, Wanginyi	2
	Ludewa	Ilininda, Ilawa, Mangalanyene, Manga.	4
	Wanging'ombe	Lulanzi, Mngate, Isindagosi, Itambo, Imalinyi, Msaulwa, Sakalelenga, Itowo, Mtapa, Muhaji, Ilulu, Nyumbanilu, Itulahumba, Igima, Mlevela, Ihanzatwa, Utelewe, Kinenulo, Igodivaha, Kigudala, Gonelamafuta, Masilu,	37

Mkoa	Wilaya	Kijiji	Idadi ya Vijiji
		Masage, Samaria, Ng'anda, Igosi, Ivigo, Mafinga, Ujindile, Lulanzi, Ing'enyango, Idunda, Mdasi, Kanani, Mkeha, Mawindi, Lusisi,	
	Makete	Mwakauta, Lumage, Isapulano, Ivilikinge	4
Pwani	Kibaha	Lukenge, Kimaramsale, Mperamumbi, Magindu, Ngwale, Milalazi, Mizuguni, Gwata, Gumba	9
Mara	Serengeti	Nyichoka, Bokore, Rwamchanga, Kazi	4
Kagera	Kyerwa	Kaitabuzi, Katela	2
Katavi	Tanganyika	Bugwe, Vikonge	2
	Nsimbo	Kasisi	1
Mtwara	Rufiji	Nyamwage	1
Iringa	Mufindi	Lwing'ulo, Idetero, Nyololo Shuleni, Kitelewasi, Ipilimo, Njojo, Wangamaganga, Maduma, Tambalang'ombe, Igomtwa, Ihalimba.	11
	Kilolo	Igunda, Nyanzwa, Msosa, Mgowelo, Kitowo, Ihimbo, Ikumbi, Kitelawasi	8
Manyara	Simanjiro	Marosoit, Laangai	2
	Karatu	Rhotia Kati, Kilimatembo, Mangola juu, Malela, Endashangwet, Makhoromba	6
Tabora	Nzega	Sojo, Well II, Seki, Nindo, Selemi, Ngogoto, Mwamala, Igalula, Buhondo, Buduba, Senge, Sagida	12
	Iramba	Mgela, Kizonzo, Mukulu, Motomoto, Misigiri	5
Kilimanjaro	Same	Kizungo, Vumario	2
	Mwanga	Kalambandea	1
Jumla			**316**

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Urasimishaji wa Makazi Holela

367. Mwaka 2021, Serikali iliandaa na kuidhinisha michoro ya mipango miji 1,704 ikilinganishwa na michoro 824 iliyoidhinishwa mwaka 2020. Aidha, vipande 523,519 vya ardhi vilirasimishwa katika halmashauri mbalimbali nchini ikilinganishwa na vipande 238,538 vya ardhi vilivyorasimishwa mwaka 2020. Ongezeko la michoro ya mipango miji iliyoidhinishwa na vipande vya ardhi vilivyorasimishwa lilitokana na kuongezeka kwa kasi ya utekelezaji wa Programu ya Urasimishaji na Udhibiti wa Makazi Holela.

Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya

368. Hadi Desemba 2021, kulikuwa na mashauri 53,527 (mashauri mapya yalikuwa 29,253 na ambayo hayakufanyiwa maamuzi mwaka 2020 yalikuwa mashauri 24,274) katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ikilinganishwa na mashauri 48,191 yaliyokuwepo katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kati ya hayo, mashauri 26,810 yaliamuliwa na mashauri 26,717 yaliendelea kusikilizwa. Vilevile, migogoro 7,875 ya matumizi ya ardhi ilitatuliwa kiutawala mwaka 2021 ikilinganishwa na migogoro 8,583 mwaka 2020.

Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara

369. Shirika la Nyumba la Taifa - NHC lilikamilisha ujenzi wa nyumba 440 na kuendelea na ujenzi wa nyumba 653 katika halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya ofisi, biashara na makazi mwaka 2021 ikilinganishwa na nyumba 227 zilizokamilika na nyumba 937 zilizoendelea na ujenzi mwaka 2020. Kati ya hizo, nyumba 431 zilikuwa za bei nafuu na nyumba 662 bei ya kati na juu ikilinganishwa na nyumba 468 za bei nafuu na nyumba 696 za bei ya kati na juu mwaka 2020. Aidha, Kampuni ya Nyumba kwa Watumishi - WHC ilijenga nyumba 40 mwaka 2021 ikilinganishwa na nyumba 70 mwaka 2020.

SURA YA 16

UCHUKUZI, MAWASILIANO, SANAA NA MICHEZO

UCHUKUZI

Usafiri wa Barabara

370. Mwaka 2021, idadi ya leseni zilizotolewa kwa vyombo vya usafirishaji ziliongezeka kwa asilimia 4.1 na kufikia leseni 223,863 ikilinganishwa na leseni 215,040 zilizotolewa mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutolewa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuwa na leseni na kufanya kaguzi katika maeneo mbalimbali nchini. Hata hivyo, leseni za magari ya mizigo zilizotolewa zilipungua kwa asilimia 6.4 kutokana na baadhi ya magari kusajiliwa nchi jirani.

Jedwali Na. 16.1 Leseni za Usafirishaji Zilizotolewa Mwaka 2019 - 2021

Leseni	2019	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
Mabasi ya abiria	60,344	52,081	53,451	2.6
Magari ya mizigo	123,460	142,559	133,428	-6.4
Bajaji/Pikipiki	18,345	20,400	36,984	81.3
Jumla	**202,149**	**215,040**	**223,863**	**4.1**

Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini

371. Ajali za vyombo vya usafarishaji abiria na mizigo kwa njia ya barabara zilipungua kwa asilimia 8.7 mwaka 2021 kufikia 1,052 kutoka ajali 1,152 zilizotokea mwaka 2020. Hii ilitokana na jitihada za Serikali kuendelea kufanya kaguzi zilizoambatana na kufungiwa kwa mabasi yasiyo na ubora wa kutembea barabarani, upimaji ulevi kwa madereva, kutumia mfumo wa udhibiti mwendo wa mabasi na kuhakikisha matumizi ya madereva wawili kwa safari zilizozidi saa nane.

Jedwani Na. 16.2: Mchanganuo wa Ajali za Barabarani Mwaka 2019 - 2021

Ajali	2019	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
Mabasi ya abiria	442	330	365	10.6
Magari ya Mizigo	331	407	224	-45.0
Bajaji/Pikipiki	567	415	463	11.6
Jumla	**1,340**	**1,152**	**1,052**	**-8.7**

Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini

Usafiri kwa Njia ya Reli

Shirika la Reli Tanzania

372. Mwaka 2021, Shirika la Reli Tanzania - TRC lilisafirisha tani 370,279 za shehena ya mizigo kwa umbali wa kilometa 366,560,583 ikilinganishwa na tani 339,671 kwa umbali wa kilometa 304,826,099 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 9.0 ya tani za mizigo iliyosafirishwa. Ongezeko hilo lilitokana na kukamilika kwa ukarabati wa njia ya reli kupitia Mradi wa Kuboresha Reli ya Kati - TIRP na ukarabati wa mabehewa 240 ya mizigo.

373. Mwaka 2021, TRC ilisafirisha abiria 417,096 kwa njia kuu kwa umbali wa kilometa 316,205,354 ikilinganishwa na abiria 449,497 waliosafirishwa kwa umbali wa kilometa 343,842,068 mwaka 2020, sawa na upungufu wa abiria waliosafirishwa kwa asilimia 7.2. Hii ilitokana na kupungua kwa safari za treni kwa wiki kutoka safari nne (4) hadi safari mbili (2) kulikosababishwa na kuharibika kwa mabehewa nane (8) kufuatia ajali ya treni ya abiria. Kwa upande wa huduma ya usafiri wa treni katika Jiji la Dar es Salaam, TRC ilisafirisha abiria 2,876,199 kwa umbali wa kilometa 80,533,572 mwaka 2021 ikilinganishwa na abiria 3,069,168 kwa umbali wa kilometa 98,213,376 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 6.3. Upungufu huo ulitokana na kuhamishwa kwa kituo cha treni kutoka Stesheni kwenda Kamata-Kariakoo kwa lengo la kupisha ujenzi wa SGR kulikosababisha abiria wengi kupata adha ya kutembea umbali mrefu hadi Kamata na hivyo kuamua kupanda mabasi badala ya treni.

Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia

374. Mwaka 2021, jumla ya tani 392,081 za mizigo zilisafirishwa kupitia reli ya TAZARA ikiwa ni ongezeko la asilimia 17.7 ikilinganishwa na tani 333,097 zilizosafirishwa mwaka 2020. Kati ya hizo, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia - TAZARA ilisafirisha tani 199,129 za mizigo ikilinganishwa na tani 166,421 zilizosafirishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 19.7. Aidha, kampuni binafsi ya Callabash freight iliyoingia mkataba na TAZARA mwaka 2018 kutumia reli hiyo kusafirisha mizigo, ilisafirisha tani 192,952 za mizigo mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 166,676 zilizosafirishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la 15.8. Ongezeko la shehena ya mizigo iliyosafirishwa kupitia reli ya TAZARA lilitokana na kukarabatiwa kwa njia ya reli, kuanza kutumika kwa vichwa saba (7) vya njia kuu vilivyokarabatiwa pamoja na kampuni binafsi ya Callabash Freight kuendelea kutumia reli ya TAZARA kusafirisha mizigo.

Jedwali Na. 16.3: Shehena ya Mizigo Iliyosafirishwa (Tani) Mwaka 2020 - 2021

Aina ya Mizigo	**2020**	**2021**	**Badiliko (Asilimia)**
Kwenda nje ya nchi	71,249	75,140	5.5
Kutoka nje ya nchi	75,271	73,843	-1.9
Ndani ya Tanzania na Zambia (TAZARA)	19,901	50,146	152.0
Jumla ndogo	166,421	199,129	19.7
Kampuni binafsi *(Callabash freight)*	166,676	192,952	15.8
Jumla kuu	**333,097**	**392,081**	**17.7**

Chanzo: Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia

375. TAZARA ilisafirisha abiria 2,712,673 mwaka 2021 ikilinganishwa na abiria 2,904,492 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 6.6. Kati ya hao, abiria 432,981 walikuwa wa safari ndefu (Dar - Mbeya - Zambia), abiria 406,762 wa treni ya Udzungwa

na abiria 1,872,930 wa treni ya jiji la Dar es Salaam. Upungufu huo ulitokana na uhaba wa vitendea kazi pamoja na kuendelea kusitishwa kwa treni za abiria kuvuka mipaka kwenda Zambia na kuja Tanzania ili kuzuia maambukizi ya UVIKO - 19.

Jedwali Na.16.4: Mchanganuo wa Abiria Waliosafirishwa Mwaka 2020 - 2021

Aina ya Abiria	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
Safari ndefu	513,177	432,981	-15.6
Udzungwa	414,357	406,762	-1.8
Jiji la Dar es Salaam	1,976,958	1,872,930	-5.3
Jumla	**2,904,492**	**2,712,673**	**-6.6**

Chanzo: Mamlaka ya Reli ya Tanzania

Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania

376. Mwaka 2021, Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania - TCAA ilisajili ndege nane (8) ikilinganishwa na ndege nne (4) zilizosajiliwa mwaka 2020. Ongezeko la usajili lilitokana na baadhi ya nchi kulegeza masharti ya safari za anga kufuatia kupungua kwa maambukizi ya UVIKO - 19. Ndege zilizosajiliwa na kupewa vyeti vya awali vya ubora ni Airbus 220 - 300 mbili (2), Embraer 120ER moja (1), Hot Air Ballon mbili (2), C208B moja (1), C182 moja (1) na Microlight (1). Katika kipindi hicho, TCAA ilikagua ndege 87 na kutoa vyeti vya ubora ikilinganishwa na ndege 76 zilizokaguliwa mwaka 2020. Hadi Desemba 2021, mashirika 26 ya ndege za kimataifa yalitoa huduma kwa utaratibu wa mikataba ya usafiri wa anga baina ya Tanzania na nchi nyingine ikilinganishwa na mashirika 27 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Hii ilichangiwa na baadhi ya mikataba baina ya Tanzania na nchi nyingine kuisha muda wake na hivyo kuhitaji kuhuhishwa.

377. Idadi ya abiria waliosafiri kwa njia ya anga ndani na nje ya nchi ilikuwa 3,827,957 mwaka 2021 ikilinganishwa na abiria 2,773,539 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 38.0. Kati ya hao, abiria waliosafiri ndani ya nchi walikuwa 2,338,236 mwaka 2021 ikilinganishwa na abiria 1,830,117 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 27.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa watalii baada ya kupungua kwa athari za UVIKO - 19 na Serikali kuendelea kuchukua hatua dhidi ya kusambaa kwa ugonjwa huo.

Kielelezo Na. 16.1: Idadi ya Abiria Waliotumia Usafiri wa Anga Kimataifa na Ndani ya Nchi Mwaka 2017 - 2021



	2017	2018	2019	2020	2021
Kimataifa	2,756,372	2,593,862	2,594,978	943,422	1,489,721
Ndani ya Nchi	2,257,058	2,593,800	2,892,701	1,830,117	2,338,236
Jumla	5,013,430	5,187,662	5,487,679	2,773,539	3,827,957

378. Mwaka 2021, kulikuwa na jumla ya safari za ndege 153,322 ikilinganishwa na safari 121,255 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 26.4. Aidha, mizigo iliyosafirishwa ilikuwa tani 30,029 mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 24,452 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 22.8. Kuongezeka kwa safari za ndege na mizigo iliyosafirishwa kulitokana na mataifa mengi kuondoa katazo la safari za anga kufuatia juhudi za pamoja baina ya Serikali na mashirika ya ndege kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya UVIKO - 19.

Kielelezo Na.16.2: Idadi ya Safari za Ndege Mwaka 2017 - 2021



	2017	2018	2019	2020	2021
Kimataifa	194,405	202,402	247,803	17,885	26,414
Ndani ya Nchi	42,977	43,670	44,302	103,370	126,908
Jumla	237,382	246,072	292,105	121,255	153,322

Kielelezo Na. 16.3: Tani za Mizigo zilizosafirishwa 2017 - 2021



	2017	2018	2019	2020	2021
Kimataifa	1,967	2,003	2,230	20,333	25,321
Ndani ya Nchi	25,482	25,907	25,972	4,119	4,707
Jumla	27,449	27,910	28,202	24,452	30,028

Kampuni ya Ndege Tanzania

379. Mwaka 2021, Kampuni ya Ndege Tanzania - ATCL ilianza kutoa huduma kwa kituo kipya cha ndani cha Arusha. Hii inafanya idadi ya vituo vya ndani ambavyo kampuni ilitoa huduma kufikia 15 ikilinganishwa na vituo 14 mwaka 2020. Vituo vingine ambavyo Kampuni iliendelea kutoa huduma ni Dar es Dalaam, Dodoma, Bukoba, Geita, Kilimanjaro, Kigoma, Mbeya, Mpanda, Mtwara, Mwanza, Songea, Tabora na Zanzibar. Katika kipindi hicho, ATCL ilisimama kutoa huduma katika kituo cha Iringa ili kupisha matengenezo ya kiwanja cha ndege. Aidha, vituo vya nje vilikuwa 10 mwaka 2021 ikilinganishwa na vituo saba (7) mwaka 2020. Vituo vitatu vipya vilivyoongezeka mwaka 2021 ni Lubumbashi, Nairobi na Ndola na vituo vilivyokuwepo awali ambavyo Kampuni iliendelea kutoa huduma ni Bujumbura (Burundi), Entebbe (Uganda), Hahaya (Comoros), Guangzhou (China), Harare (Zimbabwe), Lusaka (Zambia) na Mumbai (India).

380. Kampuni ya Ndege Tanzania ilisafirisha abiria 673,311 mwaka 2021 ikilinganishwa na abiria 472,374 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 42.5. Ongezeko hilo lilitokana na ATCL kuongeza miruko mipya ya kikanda kwa vituo vya Ndola, Lubumbashi na Nairobi na miruko ya ndani kwa vituo vya Dodoma na Mtwara. Aidha, ATCL ilisafirisha tani 1,911 za mizigo ya ndani na nje ya nchi mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 1,125 zilizosafirishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 69.9. Ongezeko hilo lilitokana na kuazishwa kwa huduma za usafirishaji wa mizigo katika kituo cha Guangzhou pamoja na kurejesha safari za Mumbai (India), Hahaya (Comorro), Lusaka (Zambia) na Harare (Zimbambwe) ambazo zilikuwa zimesitishwa kutokana na tahadhari ya UVIKO - 19.

Usafiri kwa njia ya Maji

Utoaji wa Leseni

381. Mwaka 2021, Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania - TASAC lilitoa leseni 947 za uwakala wa ugomboaji shehena ipitayo katika bandari na maeneo mengine ya kiforodha ikilinganishwa na leseni 903 zilizotolewa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 4.9. Ongezeko hilo lilichangiwa na elimu iliyotolewa na Shirika kwa umma juu ya umuhimu wa kusajili kampuni pamoja na kuimarika kwa biashara. Aidha, leseni za uwakala wa meli mwaka 2021 zilikuwa 24 kama ilivyokuwa mwaka 2020. Kwa upande mwingine, TASAC ilihudumia meli 425 mwaka 2021 ikilinganishwa na meli 309 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 37.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa meli za mizigo ya jumla zilizohudumiwa kutokana na kuimarika kwa biashara.

382. Leseni za wakusanyaji wa mizigo zilizotolewa ziliongezeka na kufikia leseni 32 mwaka 2021 ikilinganishwa na leseni 31 zilizotolewa mwaka 2020. Aidha, leseni za wapimaji uzito wa makasha zilizotolewa ziliongezeka kwa asilimia 14.9 na kufikia leseni 54 mwaka 2021 ikilinganishwa na leseni 47 zilizotolewa mwaka 2020. Vilevile, idadi ya leseni za bandari kavu zilizotolewa ziliongezeka kwa asilimia 9.5 na kufikia leseni 46 mwaka 2021 ikilinganishwa na leseni 42 zilizotolewa mwaka 2020. Ongezeko la leseni za wapimaji uzito wa makasha na bandari kavu lilitokana na kuimarika kwa mazingira ya biashara na kuongezeka kwa uelewa kwa wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa kupima uzito wa mizigo.

Jedwali Na.16.5: Idadi ya Leseni kwa Watoa Huduma Mwaka 2020 - 2021

Na.	Aina ya leseni	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
1	Ugomboaji wa shehena	903	947	4.9
2	Uwakala wa meli	24	24	0
3	Wakusanyaji mizigo	31	32	3.2
4	Wapimaji makasha	47	54	14.9
5	Bandari kavu	42	46	9.5

Chanzo: Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania

Vyombo vya Usafiri Majini

383. Mwaka 2021, vyombo 3,024 vya usafiri katika maji vilipewa leseni ikilinganishwa na vyombo 4,348 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 30.5. Kati ya hivyo, vyombo vidogo chini ya mita 24 vilikuwa 2,937 na vyombo vikubwa zaidi ya mita 24 vilikuwa 87. Kupungua kwa idadi ya vyombo vilivyosajiliwa kulitokana na baadhi ya vyombo kutokidhi vigezo vya usajili. Aidha, matukio ya ajali katika maji yaliyoripotiwa katika Kituo cha Uratibu wa Uokozi na Utafutaji yalikuwa sita (6) mwaka 2021 ikilinganishwa na matukio 10 mwaka 2020. Kupungua kwa matukio ya ajali kulitokana na elimu ya usalama iliyotolewa kwa watumiaji na wamiliki wa vyombo vya usafiri katika maji na kuimarika kwa ukaguzi wa vyombo hivyo.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

384. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania - TPA ilihudumia shehena tani milioni 18.8 mwaka 2021 ikilinganishwa na tani milioni 17.0 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 10.6. Ongezeko hilo lilitokana na bandari kuhudumia shehena ya Sulphur, vifaa kwa ajili ya miradi mikubwa ya ujenzi nchini ikiwemo Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa - SGR, Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere pamoja na kuimarika kwa shughuli za uchumi na biashara nchini na nchi jirani zinazotumia bandari za Tanzania.

Jedwali Na. 16.6: Shehena Zilizohudumiwa (Tani '000') Mwaka 2017 - 2021

Bandari	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
Bandari kuu za Mwambao						
Dar es Salaam	13,761.5	15,073.8	16,023.0	15,858.0	17,025.4	7.4
Tanga	527.0	581.0	571.0	475.0	844.0	77.7
Mtwara	417.0	139.0	122.0	189.0	213.0	12.7
Jumla ndogo	**14,705.5**	**15,793.8**	**16,716.0**	**16,522.0**	**18,082.4**	**9.4**
Bandari Ndogo na Bandari za Maziwa Makuu						
Kilwa, Lindi, Mafia, Bagamoyo na Pangani	42.0	18.0	32.0	10.7	191.0	-
Mwanza	92.0	122.0	163.0	142.0	234.0	64.8
Kigoma	167.0	201.0	206.0	250.0	265.0	6.0
Kyela	7.0	9.0	1.0	17.0	11.0	-35.3
Jumla ndogo	**308.0**	**350.0**	**402.0**	**419.7**	**701.0**	**67.0**
Jumla Kuu	**15,013.5**	**16,143.8**	**17,118.0**	**16,941.7**	**18,783.4**	**10.9**

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

385. Mwaka 2021, bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga zilihudumia makasha 722,808 yenye urefu wa futi 20 (TEUs) ikilinganishwa na makasha 717,301 yaliyohudumiwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 0.8. Aidha, Kitengo cha Mizigo ya Kawaida kinachosimamiwa na Mamlaka kilihudumia makasha 110,227 yenye urefu wa futi 20 (TEUs) ikilinganishwa na makasha 108,227 mwaka 2020. Vilevile, Kampuni ya Kimataifa ya Kupakia na Kupakua Makasha Tanzania - TICTS ilihudumia makasha 606,169 yenye urefu wa futi 20 (TEUs) ikilinganishwa na makasha 601,654 mwaka 2020. Ongezeko la makasha yaliyohudumiwa lilitokana na Bandari ya Dar es Salaam kuanza kupokea na kuhudumia meli kubwa za makasha baada ya maboresho ya miundombinu hususan kuimarishwa na kuongezwa kwa kina cha gati namba 1 hadi 7 pamoja na lango la bahari kuingia na kutoka kwenye bandari.

Jedwali Na. 16.7: Shehena ya Makasha (TEUs) Iliyohudumiwa Mwaka 2017 - 2021

	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
TICTS	482,836	519,776	605,002	601,654	606,169	0.8
Shehena ya kawaida	134,430	113,455	121,429	108,227	110,732	2.3
Jumla Ndogo	**617,266**	**705,231**	**726,431**	**709,881**	**716,901**	**1.0**
Tanga	6,539	7,511	6,334	7,401	5,817	-21.4
Mtwara	40,924	12,633	3,695	19	90	373.7
Jumla Ndogo	**47,463**	**20,144**	**10,029**	**7,420**	**5,907**	**-20.4**
Jumla Kuu	**664,729**	**725,375**	**736,460**	**717,301**	**722,808**	**0.8**

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

386. Mamlaka ilihudumia abiria 3,875,190 mwaka 2021 ikilinganishwa na abiria 2,879,455 waliohudumiwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 34.6. Hii ilichangiwa na: kuongezeka kwa huduma za meli kati ya bandari za mwambao wa pwani na visiwa vya Unguja na Pemba; Bandari za Kagunga, Kibirizi, Kirando na Kipili kuanza kutoa huduma ya kusafirisha abiria tofauti na awali ambapo vituo hivi vilitumika kusafirisha mizigo tu; kuimarika kwa utoaji wa huduma za usafirishaji kupitia meli ya Mv. Victoria; kuanza kutumika kwa meli mpya ya Mv. Mbeya II katika bandari za Ziwa Nyasa; na meli mpya ya abiria ya MV. Amani ya nchi ya Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC) kuanza kutoa huduma ya kusafirisha abiria katika Ziwa Tanganyika.

Jedwali Na. 16.8: Idadi ya Abiria Waliohudumiwa Mwaka 2017 - 2021

Bandari	2017	2018	2019	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
Dar es Salaam	1,662,730	1,501,648	1,994,809	1,639,683	2,303,471	40.5
Tanga	43,184	43,613	67,699	55,403	49,246	-11.1
Mwanza	0	423,749	541,121	1,176,918	1,461,900	24.2
Kigoma	11,844	3,643	2,148	1,781	43,364	2,334.8
Kyela	890	1,598	3,790	5,670	17,209	203.5
Jumla	**1,718,648**	**1,974,251**	**2,609,567**	**2,879,455**	**3,875,190**	**34.6**

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

Muda wa Meli Kukaa Bandarini

387. Muda wa meli kukaa bandarini ulikuwa wastani wa siku 4.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa siku 4.0 mwaka 2020. Aidha, muda wa meli kukaa bandarini kwa meli za makasha na shehena ya kawaida ulikuwa siku 3.8 na 3.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na siku 3.3 na 3.1 mwaka 2020 mtawalia. Katika kitengo cha mafuta, muda wa meli kukaa bandarini uliongezeka na kufikia siku 6.5 mwaka 2021 ikilinganishwa na siku 5.6 mwaka 2020. Kuongezeka kwa muda wa meli kukaa bandarini kulitokana na upungufu wa vifaa vya kuhudumia shehena na meli ambapo

bandari ya Dar es Salaam ilikuwa na wastani wa asilimia 62 ya vifaa vyote vinavyohitajika kutoka angalau wastani wa asilimia 85 (kiwango cha chini cha idadi ya vifaa) pamoja na shughuli za ujenzi zinazoendelea katika eneo la Bandari ya Dar es Salaam.

Jedwali Na.16.9: **Muda wa Meli Kukaa Bandarini (Siku) Mwaka 2017 - 2021**

Kitengo	2017	2018	2019	2020	2021
Makasha	2.0	2.2	3.5	3.3	3.8
Shehena ya kawaida	2.8	3.2	3.6	3.1	3.7
Mafuta	5.5	6.6	5.8	5.6	6.5
Wastani	**3.4**	**4.0**	**4.3**	**4.0**	**4.7**

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

Shehena za Nchi Jirani

388. Mwaka 2021, tani 6,421,598 za shehena ya mizigo kwenda nchi jirani zilihudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na tani 5,340,287 zilizohudumiwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 20.2. Hii ilitokana na jitihada za Mamlaka katika kupanua wigo wa masoko hasa katika nchi za Zambia na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo. Hata hivyo, shehena ya nchi ya Uganda ilipungua kutokana na upungufu wa meli katika Ziwa Viktoria kulikosababishwa na meli ya mizigo ya Mv. Umoja kuwa katika matengenezo.

Jedwali Na. 16.10: Shehena za Kwenda Nchi Jirani (Tani) Mwaka 2017 - 2021

Nchi	2017	2018	2019	2020	2021	Asilimia Badiliko
Zambia	2,021,089	1,504,014	1,763,052	1,159,013	1,507,746	30.1
J.D. Kongo	1,176,764	1,779,617	1,914,138	1,840,657	2,357,867	28.1
Burundi	415,993	379,704	453,280	476,809	507,017	6.3
Rwanda	1,061,193	911,870	1,238,540	1,239,238	1,366,290	10.3
Malawi	276,039	311,138	336,714	407,472	471,385	15.7
Uganda	271,957	188,591	140,960	153,995	138,805	-9.9
Nyingenezo	85,340	98,542	25,203	63,104	72,488	14.9
Jumla	**5,308,372**	**5,173,477**	**5,871,887**	**5,340,287**	**6,421,598**	**20.2**

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

Uchukuzi Kwenye Maziwa

Kampuni ya Huduma za Meli

389. Kampuni ya Huduma za Meli ilisafirisha abiria 284,738 mwaka 2021 ikilinganishwa na abiria 173,859 waliosafirishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 63.8. Katika kipindi hicho, Kampuni ilisafirisha tani 20,584.4 za mizigo ikilinganishwa na tani 19,391 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 6.0. Kuongezeka kwa abiria na mizigo iliyosafirishwa kulitokana na kuboreshwa kwa kitengo cha masoko na biashara na kuendelea kutoa huduma kwa meli za New Victoria na New Butiama katika Ziwa Victoria baada ya kufanyiwa matengenezo makubwa.

Kampuni ya Meli ya China na Tanzania

390. Mwaka 2021, Kampuni ya Meli ya China na Tanzania - SINOTASHIP ilisafirisha shehena ya mizigo tani 613,112 ikilinganishwa na tani 609,010 zilizosafirishwa mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na uhakika wa upatikanaji wa shehena baada ya meli ya MV *Changshun II* kukodishwa kwa Kampuni ya *COSCO Bulk Refines* yenye uzoefu na uwezo mkubwa katika maswala ya usafirishaji wa shehena duniani. Katika kipindi hicho, Kampuni ilihudumia makasha 56,198 katika bandari ya Da-es salaam ikilinganishwa na makasha 49,990 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 12.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa biashara ya uwakala wa meli katika bandari ya Dar es salaam na kuimarika kwa mikakati ya kutafuta mizigo inayosafirishwa kwenda nje ya nchi.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

391. Mwaka 2021, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania iliendelea kutekeleza mfumo wa udhibiti wa ubora wa huduma za hali ya hewa zinazotolewa kwa sekta mbalimbali zikiwemo usafiri wa anga na maji. Katika kipindi hicho, Mamlaka ilihudumia ndege 35,511 ikilinganishwa na ndege 27,348 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 29.8. Ongezeko hilo lilitokana na kupungua kwa athari za maambukizi ya UVIKO-19 pamoja na Serikali kuendelea na jitihada za kuhamasisha mashirika ya ndege ya kimataifa kufanya safari za kuja nchini.

392. Mamlaka ilihudumia meli na boti 31,736 mwaka 2021 ikilinganishwa na meli na boti 7,248 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na elimu iliyotolewa kwa wadau kuhusu umuhimu wa kutumia taarifa za hali ya hewa. Aidha, idadi ya wateja wa huduma mahsusi waliohudumiwa na Mamlaka iliongezeka kwa asilimia 3.9 na kufikia wateja 2,683 ikilinganishwa na wateja 2,582 mwaka 2020. Katika kipindi hicho, kiwango cha usahihi wa utabiri wa hali ya hewa kilikuwa asilimia 88.3 ikilinganishwa na asilimia 87.9 mwaka 2020, ambacho ni zaidi ya kiwango cha asilimia 70 kinachokubalika kimataifa.

Jedwali 16.11: Viashiria vya Ufanisi Katika Sekta ya Hali ya Hewa Mwaka 2020 - 2021

Na.	Viashiria vya Ufanisi	Maelezo	Mwaka	
			2020	2021
1	Kiwango cha usahihi wa utabiri wa siku na msimu (asilimia)	Usahihi wa utabiri	87.9	88.3
2	Idadi ya wateja wa huduma za hali ya hewa	Sekta ya usafiri wa anga	27,348	35,511
		Meli na boti	7,248	31,736
		Huduma mahsusi	2,582	2,683
3	Kiwango cha watumiaji na wateja wanaoridhika na huduma za hali ya hewa (asilimia)	Kiwango cha kuridhika	91	91

Chanzo: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

MAWASILIANO

Huduma za Posta

393. Shirika la Posta Tanzania lilisafirisha barua 2,210,487 ndani ya nchi mwaka 2021 ikilinganishwa na barua 3,705,183 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 40.3. Aidha, barua 497,525 zilisafirishwa nje ya nchi mwaka 2021 ikilinganishwa na barua 1,173,732 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 57.6. Upungufu huo ulitokana na matumizi makubwa ya njia za kidigitali katika mawasiliano.

394. Mwaka 2021, vifurushi vilivyosafirishwa ndani ya nchi viliongezeka na kufikia 7,120 ikilinganishwa na vifurushi 2,828 mwaka 2020. Aidha, vifurushi vilivyosafirishwa nje ya nchi vilikuwa 1,423 mwaka 2021 ikilinganishwa na vifurushi 1,064 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 33.7. Ongezeko la usafirishaji wa vifurushi ndani na nje ya nchi lilitokana na ukuaji wa biashara mtandao (*Posta Shop Tz*) ambapo wateja huagiza vifurushi kwa njia ya mtandao na Shirika kuwapelekea mahali walipo.

395. Shirika la Posta Tanzania lilisafirisha rejesta 40,596 nchini mwaka 2021 ikilinganishwa na rejesta 74,639 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 45.6. Aidha, rejesta 3,473 zilisafirishwa nje ya nchi mwaka 2021 ikilinganishwa na rejesta 6,112 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 43.2. Idadi ya rejesta zilizosafirishwa ndani na nje ya nchi zilipungua kutokana na wateja kutumia zaidi huduma nyingine za posta kama rejesta vipeto (small packets). Katika kipindi hicho, rejesta vipeto 63,626 zilisafirishwa ndani ya nchi na rejesta vipeto 59,836 zilisafirishwa nje ya nchi.

396. Mwaka 2021, nyaraka na vipeto 516,725 vilitumwa kwa njia ya haraka - EMS ndani ya nchi ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 520,217 zilivyotumwa mwaka 2020. Kupungua kwa nyaraka na vipeto vilivyotumwa kulitokana na ongezeko la ushindani kutoka kwa wasafirishaji wengine hususani mabasi ya abiria. Aidha, nyaraka na vipeto 10,675 vilitumwa nje ya nchi kwa njia ya haraka mwaka 2021 ikilinganishwa na nyaraka

na vipeto 6,774 vilivyotumwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 57.6. Ongezeko hilo lilichangiwa na ukuaji wa biashara mtandao ndani na nje ya nchi. Kwa upande mwingine, barua na nyaraka 31,039 zilipokelewa na kusambazwa kwa njia ya huduma ya haraka ya usambazaji wa barua ndani ya miji mwaka 2021 ikilinganishwa na barua na nyaraka 44,065 zilizopokelewa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 29.6. Hii ilitokana na ongezeko la usambazaji wa barua za haraka usio rasmi ndani ya miji kwa kutumia pikipiki.

397. Mwaka 2021, miamala ya fedha 2,905 ya *money gram* ilihaulishwa kwa njia ya kielektroniki ikilinganishwa na miamala 5,518 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 47.4. Upungufu huo ulitokana na kusitishwa kwa huduma ya kuhaulisha fedha kwa kipindi cha miezi saba kutokana na Shirika la Posta kutokidhi masharti ya *Money gram*. Kwa upande mwingine, wateja 311 walihudumiwa kupitia huduma ya kufanya malipo kwa njia ya uwakala wa *Post Giro* ndani ya nchi mwaka 2021 ikilinganishwa na wateja 230 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 35.2. Ongezeko hilo lilitokana na kampuni za TCC, UTT, Swissport na Vodacom kufanya malipo ya gawio kwa njia ya *Post Giro*.

Huduma za Simu

398. Idadi ya kadi za simu za kiganjani iliongezeka kwa asilimia 5.5 na kufikia kadi 54,044,384 mwaka 2021 kutoka kadi 51,220,233 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarika kwa miundombinu ya mawasiliano iliyosababisha kukua kwa huduma za habari na mawasiliano kwa kutumia mitandao ya kijamii na matumizi ya simu za kiganjani katika kufanya miamala ya fedha. Katika kipindi hicho, kadi za simu za mezani zilipungua na kufikia kadi 71,834 kutoka kadi 72,469 mwaka 2020 kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya simu za kiganjani.

399. Mwaka 2021, gharama za kupiga simu ndani ya mtandao zilikuwa shilingi 32 kwa dakika ikilinganishwa na shilingi 72 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 55.6. Katika kipindi hicho, gharama za kupiga simu nje ya mtandao zilikuwa shilingi 32 kwa dakika ikilinganishwa na shilingi 73 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 56.2. Kupungua kwa gharama kulitokana na kuendelea kuongezeka kwa ushindani kwa watoa huduma za mawasiliano.

400. Mwaka 2021, gharama za kupiga simu ndani ya Afrika Mashariki zilipungua kwa asilimia 2.3 na kufikia shilingi 1,173 kwa dakika ikilinganishwa na shilingi 1,201 kwa dakika mwaka 2020. Aidha, gharama za kupiga simu mataifa mengine zilipungua kwa asilimia 1.8 na kufikia shilingi 1,908 kwa dakika mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi 1,942 kwa dakika mwaka 2020. Kupungua kwa gharama hizo kulitokana na kuongezeka kwa ushindani kwa watoa huduma za mawasiliano ya kimataifa.

Huduma za Intaneti

401. Watumiaji wa huduma za intaneti walikuwa milioni 29.8 mwaka 2021 ikilinganishwa na watumiaji milioni 28.5 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 4.6. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya huduma za mtandao wa intaneti ikiwemo minara.

Jedwali Na. 16.12: Watumiaji wa Intaneti Nchini Mwaka 2020 - 2021

Aina ya Huduma	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
Fixed Wireless	510,683	1,034,958	102.7
Mobile Wireless	27,371,350	25,176,367	-8.0
Fixed Wired	588,472	3,647,434	519.8
Jumla	**28,470,506**	**29,858,759**	**4.9**

Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

Huduma za Utangazaji

402. Mwaka 2021, watumiaji wa huduma za utangazaji kupitia satellite waliongezeka kwa asilimia 17.6 na kufikia 1,577,315 kutoka watumiaji 1,341,686 mwaka 2020. Aidha, watumiaji wa huduma za utangazaji kupitia mitambo iliyosimikwa ardhini waliongezeka kwa asilimia 9.6 na kufikia 1,613,031 mwaka 2021 kutoka watumiaji 1,472,317 mwaka 2020. Ongezeko la watumiaji wa huduma za utangazaji ulitokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na haja ya mahitaji ya upashanaji habari.

Jedwali Na. 16.13: Watumiaji wa Huduma za Utangazaji Mwaka 2020 - 2021

Aina ya Huduma	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
Mitambo iliyosimikwa ardhini *(Digital Terrestrial Television – DTT)*	1,472,317	1,613,031	9.6
Satellite - DTH	1,341,686	1,577,315	17.6
Cable	158,224	29,403	-81.4
Jumla	**2,972,227**	**3,219,749**	**8.3**

Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

Utoaji wa Leseni za Mawasiliano

403. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilitoa leseni 546 za huduma mbalimbali za mawasiliano mwaka 2021 ikilinganishwa na leseni 1,125 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 51.5. Hii ilichangiwa na kupungua kwa waombaji wa leseni za kuuza vifaa vya mawasiliano vya kieletroniki kulikosababishwa na kupungua kwa shughuli za uchumi pamoja na ugumu wa usafirishaji wa vifaa hivyo kutoka nchi zinazozalisha kutokana na athari za UVIKO - 19 ikiwemo kusitishwa kwa shughuli za kiuchumi na kufungwa kwa mipaka.

Jedwali Na. 16.14: Leseni zilizotolewa Mwaka 2020 - 2021

Na.	Aina ya Leseni	2020	2021	Badiliko (Asilimia)
1	Huduma za mawasiliano daraja B	6	0	-100.0
2	Maudhui ya redio	15	13	-13.3
3	Maudhui ya luninga	7	9	28.6
4	Ufungaji na utengenezaji wa vifaa vya mawasiliano vya kieletroniki	33	50	51.5
5	Kuingiza nchini vifaa vya mawasiliano vya kieletroniki	30	44	46.7
6	Kusambaza nchini vifaa vya mawasiliano vya kieletroniki	12	16	33.3
7	Kuuza vifaa vya mawasiliano vya kieletroniki	606	201	-66.8
8	Huduma za kusafirisha vifurushi na vipeto	39	20	-48.7
9	V-sat	57	21	-63.2
10	Maudhui ya mtandaoni	305	151	-50.5
11	Maudhui kutokana na matumizi	15	21	40.0
	Jumla	**1,125**	**546**	**-51.5**

Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

404. Hadi Desemba 2021, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ulikuwa na urefu wa kilomita 8,319 zilizounganishwa kwenye mikoa 26 nchini ikilinganishwa na kilomita 7,910 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Aidha, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano uliunganishwa na mikongo ya baharini ya SEACOM na EASSY pamoja na mikongo ya nchi jirani za Burundi, Kenya, Rwanda, Uganda, Malawi, Zambia na Msumbiji.

Sekta ya Habari

405. Hadi Desemba 2021, kulikuwa na jumla ya magazeti 276, vituo vya redio 207 na vituo vya runinga 54 vilivyosajiliwa na kupewa leseni ikilinganishwa na magazeti 250, vituo vya redio 198 na vituo vya runinga 44 vilivyosajiliwa hadi Desemba 2020. Ongezeko la lesseni za magazeti, vituo vya radio na runinga lilitokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia katika sekta ya habari na utangazaji hususani uwepo wa magazeti/majarida, runinga na redio mtandao. Mchanganuo wa usajili mpya unaonesha kuwa, magazeti na majarida yaliyosajiliwa/kupewa leseni yaliongezeka na kufikia 26 mwaka 2021 ikilinganishwa na magazeti na majarida 24 mwaka 2020. Aidha, idadi ya vituo vya redio vilivyosajiliwa vilikuwa 9 mwaka 2021 ikilinganishwa na vituo vya redio 15 mwaka 2020. Vilevile, idadi ya vituo vya runinga vilivyosajiliwa vilikuwa 10 mwaka 2021 ikilinganishwa na kituo kimoja (1) kilichosajiliwa mwaka 2020. Kwa upande mwingine, blogu zilizosajiliwa mwaka 2021 zilikuwa 15 ikilinganishwa na blogu 40 zilizosajiliwa mwaka 2020.

Jedwali 16.15: Magazeti, Vituo vya Redio na Runinga, na Blogu Vilivyosajiliwa

Mwaka	Idadi ya Magazeti/Majarida	Idadi ya Vituo vya Redio	Idadi ya Vituo vya Runinga	Idadi ya Blogu
2015	39	22	1	0
2016	26	23	6	0
2017	161	6	3	0
2018	42	8	3	0
2019	23	21	8	106
2020	24	15	1	40
2021	26	9	10	15

Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Utamaduni

Maendeleo ya Kiswahili

406. Mwaka 2021, Baraza la Kiswahili la Taifa - BAKITA liliendelea kufanya jitihada za kupanua wigo wa matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi. Katika kipindi hicho, BAKITA iliandaa na kurusha hewani vipindi 1,008 kuhusu teknolojia ya lugha, sarufi na fasihi ya Kiswahili kupitia redio na runinga ikilinganishwa na vipindi 1,020 mwaka 2020. Aidha, vitabu vya miswada ya ithibati ya lugha vinavyokusudiwa kutumika shuleni vilipungua kwa asilimia 4.7 mwaka 2021 na kufikia 203 ikilinganishwa na miswada 213 mwaka 2020. Upungufu huo ulitokana na kampuni binafsi za uchapishaji kupunguza kuchapisha vitabu vya kiada ambavyo hutumika katika mfumo wa elimu. Kwa upande mwingine, BAKITA ilisajili wataalamu wa kiswahili 77 katika kanzidata mwaka 2021 ikilinganishwa na wataalamu 64 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 20.3. Kuongezeka kwa usajili wa wataalamu kulitokana na BAKITA kuendelea kuhamasisha kuhusu faida na fursa za kujisajili.

Maendeleo ya Kiswahili Kimataifa

407. Mwaka 2021, Baraza la Kiswahili la Taifa lilisajili na kutoa ithibati kwa vituo 18 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni. Lengo la usajili huu ni kuhakikisha ubora wa mafunzo yanayotolewa. Vituo vitano kati ya vilivyosajiliwa viko nje ya Tanzania ambavyo ni Afrika Kusini, Italia, Ethiopia, Ubalozi wa Tanzania nchini Nigeria na Ubalozi wa Tanzania nchini Korea Kusini. Aidha, Baraza kupitia balozi limekusanya takwimu za Watanzania 73 wanaofundisha Kiswahili nje ya nchi/waliojiajiri kupitia taaluma husianifu za Kiswahili.

Uhariri na Tafsiri ya Nyaraka

408. Mwaka 2021, BAKITA ilitafsiri jumla ya nyaraka 1,148 ikilinganishwa na nyaraka 869 zilizotafsiriwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 32.1. Kati ya hizo, nyaraka 477 zilitafsiriwa kutoka lugha ya kiarabu kwenda lugha ya kiingereza, nyaraka 305 kutoka lugha ya kifaransa kwenda lugha ya kiingereza, nyaraka 204 kutoka

lugha ya kiingereza kwenda lugha ya kiswahili na nyaraka 162 kutoka lugha ya kiswahili kwenda lugha ya kiingereza. Ongezeko hilo lilitokana na juhudi za Baraza katika kutangaza na kuhamasisha matumizi ya huduma zinazotolewa. Aidha, Baraza lilihariri nyaraka 23 mwaka 2021 ikilinganishwa na nyaraka 41 zilizoharirirwa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 43.9. Upungufu huo ulichangiwa na kuongezeka kwa matumizi ya kampuni za uchapishaji katika kuhariri kazi za waandishi. Kwa upande mwingine, BAKITA ilibaini makosa 1,205 matumizi sahihi na sanifu ya lugha ya mwaka 2021 ikilinganishwa na makosa 1,380 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 12.7. Upungufu huu ulitokana na Baraza kuongeza vipindi vya kiswahili vya kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kama vile redio na televisheni pamoja na kuandika makala mbalimbali katika magazeti. Hii iliwezesha wanahabari wengi kuzingatia weledi wa matumizi sahihi na sanifu ya lugha ya Kiswahili.

Jedwali Na. 16.16: Huduma Zilizotolewa na BAKITA Mwaka 2015 - 2021

Mwaka	Vipindi vya Redio na Runinga	Huduma ya Ithibati	Huduma ya Tafsiri	Huduma ya Ukalimani	Huduma ya Uhariri	Makosa Yaliyobainika Kutumiwa Katika Vyombo vya Habari
2015	118	121	320	3	8	1,200
2016	110	60	350	2	20	1,048
2017	87	61	268	3	10	805
2018	847	63	1,607	3	39	848
2019	780	38	5,061	2	7	1,081
2020	1,020	213	869	0	41	1,380
2021	1,008	203	1,148	0	23	1,205

Chanzo: Baraza la Kiswahili la Taifa

Maendeleo ya Sanaa

Vibali vya Utayarishaji wa Filamu

409. Mwaka 2021, Bodi ya Filamu Tanzania ilitoa vibali 128 vya utayarishaji wa filamu ikilinganishwa na vibali 88 vilivyotolewa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 45.5. Kati ya hivyo, vibali 60 vilitolewa kwa watayarishaji filamu watanzania na vibali 68 vilitolewa kwa wageni ikilinganishwa na vibali 54 kwa watayarishaji filamu watanzania na vibali 34 kwa wageni mwaka 2020. Ongezeko la vibali lilitokana na kuondolewa kwa tozo ya uhakiki wa filamu ya kila mwaka na kupunguzwa kwa ada za vibali, uhakiki na usambazaji filamu pamoja na elimu iliyotolewa kwa wadau kuhusu umuhimu wa kuzingatia taratibu za utengenezaji wa filamu.

Usajili wa Wabunifu na Kazi za Sanaa

410. Serikali kupitia Taasisi ya Hakimiliki Tanzania - COSOTA ilisajili wabunifu wa kazi za sanaa 2,066 mwaka 2021 ikilinganishwa na wabunifu 1,436 waliosajiliwa mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 43.9. Aidha, kazi za sanaa zilizosajiliwa na COSOTA ziliongezeka na kufikia 3,827 mwaka 2021 ikilinganishwa na kazi 1,431

mwaka 2020. Ongezeko la usajili lilitokana na jitihada za COSOTA katika kulinda hakimiliki za sanaa na ubunifu nchini ikiwemo kukusanya na kugawa mirabaha kwa wadau wa kazi hizo na kuimarika kwa matumizi ya usajili wa wanachama na kazi za sanaa kwa njia ya mtandao.

411. Mwaka 2021, COSOTA ilitoa vyeti 3,835 vya uthibitisho wa umiliki wa hakimiliki ikilinganishwa na vyeti 1,431 vilivyotolewa mwaka 2020. Aidha, leseni 370 za watumiaji wa kazi zenye hakimiliki zilitolewa mwaka 2021 ikilinganishwa na leseni 354 zilizotolewa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishaji uliofanywa na Serikali kwa kutoa elimu kuhusu umuhimu na manufaa ya wadau kusajili kazi zao pamoja na ugawaji wa mirabaha pale kazi za wasanii zinapochezwa kupitia redio, runinga na mitandao ya kijamii.

Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo

412. Mwaka 2021, jumla ya vikundi 40 vya sanaa na utamaduni kutoka ndani na nje ya nchi vilishiriki katika Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ikilinganishwa na vikundi 47 vilivyoshiriki mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 14.9. Kati ya vikundi vilivyoshiriki mwaka 2021, vikundi 37 vilitoka nchini na vikundi 3 vilitoka nje ya nchi. Ushiriki wa vikundi vya ndani na nje ulipungua kutokana na mlipuko wa UVIKO - 19.

Jedwali Na. 16.17: Idadi ya Vikundi vya Sanaa na Utamaduni Vilivyoshiriki Katika Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo

Mwaka	Vikundi vya Utamaduni		Jumla
	Vikundi vya Ndani ya Nchi	Vikundi kutoka Nje ya Nchi	
2015	48	4	52
2016	83	4	87
2017	101	3	104
2018	119	5	124
2019	83	5	88
2020	47	-	47
2021	37	3	40

Chanzo: Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo

Usajili wa Wasanii katika Fani za Sanaa

413. Mwaka 2021, Baraza la Sanaa la Taifa - BASATA liliendelea kurasimisha kazi za wasanii nchini ambapo wasanii binafsi 466 walisajiliwa ikilinganishwa na wasanii 377 waliosajiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 23.6. Kati ya hao, wasanii wa ufundi walikuwa 68 (asilimia 14.6), maonesho 197 (asilimia 42.3) na muziki 201 (asilimia 43.1). Ongezeko hilo lilitokana na hamasa na elimu iliyotolewa na Baraza kuhusu umuhimu wa kujisajili.

Jedwali Na.16.18: Wasanii wa Sanaa Waliosajiliwa Mwaka 2017- 2021

Mwaka	Ufundi	Maonesho	Muziki	Jumla
2017	7	40	205	252
2018	44	172	181	397
2019	64	446	500	1010
2020	34	172	171	377
2021	68	197	201	466

Chanzo: Baraza la Sanaa la Taifa

Utoaji wa Tuzo za Kazi za Sanaa

414. Mwaka 2020/2021 jumla ya tuzo 28 za ndani na nje ya nchi zilitolewa kwa wasanii wa muziki wa Kitanzania kutokana na ubora wa kazi zao ikilinganishwa na tuzo 10 zilizotolewa mwaka 2019/2020. Kati ya tuzo zilizotolewa mwaka 2020/2021, tuzo 15 zilikuwa za ndani ya nchi na tuzo 13 zilikuwa za nje ya nchi. Kuongezeka kwa tuzo zilizotolewa kulitokana na jitihada zilizofanywa na Serikali kuwashirikisha wadau katika uendeshaji wa matukio ya sanaa na kuweka mazingira wezeshi ya utoaji wa vibali na matumizi ya mitandao ya kijamii kwa wasanii na kupata fursa ya kupata taarifa za tuzo zinazotolewa kimataifa na hatimaye kuweza kushiriki. Mwenendo wa tuzo zilizotolewa kwa wasanii wa muziki wa Kitanzania ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 16.19.**

Jedwali Na.16.19: Tuzo za Muziki Walizoshinda Wasanii wa Kitanzania

Mwaka	Idadi ya Tuzo za Ndani	Idadi ya Tuzo za Nje	Jumla
2014/15	46	8	54
2015/16	30	5	35
2016/17	28	4	32
2017/18	32	5	37
2018/19	10	4	14
2019/20	8	2	10
2020/21	15	13	28

Chanzo : Baraza la Sanaa la Taifa

415. Mwaka 2021, jumla ya tuzo 36 zilitolewa kwa wadau wa filamu kutoka ndani na nje ya nchi ikilinganishwa na tuzo 4 zilizotolewa mwaka 2020. Kati ya tuzo zilizotolewa mwaka 2021, tuzo 33 zilikuwa za ndani ya nchi na tuzo 3 zilikuwa za nje ya nchi. Kuongezeka kwa tuzo zilizotolewa ndani ya nchi kulitokana na kuwepo kwa tuzo za kitaifa zilizoandaliwa na Serikali kupitia Bodi ya Filamu Tanzania.

Jedwali Na. 16.20: Tuzo za Filamu Zilizotolewa kwa Wasanii Ndani na Nje ya Nchi

Tuzo	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Tuzo za Ndani	12	11	6	30	22	2	33
Tuzo za Nje	1	4	1	10	2	2	3
Jumla	**13**	**15**	**7**	**40**	**24**	**4**	**36**

Chanzo: Bodi ya Filamu Tanzania

Maendeleo ya Michezo

416. Mwaka 2021, Baraza la Michezo la Taifa - BMT lilisajili vilabu vya michezo 216 ikilinganishwa na vilabu 110 vilivyosajiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 96.4. Hii inafanya jumla ya vilabu vya michezo vilivyosajiliwa kufikia 9,491 kutoka vilabu 9,275 mwaka 2020. Aidha, vyama vya michezo vilivyosajiliwa mwaka 2021 vilikuwa 15 na hivyo kufanya jumla ya vyama vilivyosajiliwa kufikia 503 kutoka vyama 488 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Vilevile, wakuzaji/mawakala 60 walisajiliwa mwaka 2021 hivyo kufanya jumla yao kufikia 148 kutoka wakuzaji/mawakala 88 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 68.2. Ongezeko la usajili lilitokana na elimu na hamasa iliyotolewa na Baraza kuhusu kanuni na taratibu za usajili wa vyama na vilabu vya michezo nchini.

417. Mwaka 2021, taasisi za michezo 9 zilisajiliwa ikilinganishwa na taasisi 10 zilizosajiliwa mwaka 2020. Aidha, vituo/shule za michezo 22 zilisajiliwa mwaka 2021 ikilinganishwa na vituo/shule 5 zilizosajiliwa mwaka 2020. Ongezeko la vituo/shule lilitokana na elimu inayotolewa kwa wadau wa michezo kuhusu fursa zinazotokana na vituo/shule zilizosajiliwa ikiwemo upatikanaji wa ajira, kuaminika katika masuala ya biashara na kuandaa matukio ya michezo ya kulipwa mfano kama vile ngumi za kulipwa.

Jedwali Na. 16.21: Usajili wa Vilabu, Vyama, Vituo/Shule, Wakuzaji/Mawakala wa Michezo na Taasisi za Michezo Mwaka 2017 - 2021

Mwaka	Vilabu vya Michezo	Vyama vya Michezo	Vituo/shule za Michezo	Wakuzaji /Mawakala wa Michezo	Taasisi za michezo	Jumla
2017	288	29	13	14	0	344
2018	212	23	18	29	0	282
2019	231	18	21	19	0	289
2020	110	12	5	26	10	163
2021	216	15	22	60	9	322

Chanzo: Baraza la Michezo la Taifa

SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jedwali Na. 57

Maelezo	Kipimo	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Urefu wa Reli	Km	2,707	2,707	2,707	2,707	2,707	2,707	2,707	2,707	2,707
Magari ya Moshi:	Namba	45	45	30	44	44	30	30	30	30
(Serviceable Fleet)										
Mvuke	Namba	0	0	0	0	0	0	0	0	1
Dizeli:	Namba	45	45	30	44	44	30	30	30	30
Mainline	Namba	38	38	21	40	40	28	28	28	28
Shunting	Namba	7	7	9	4	4	2	2	2	2
Jumla ya mabehewa:	Namba	1,200	1,214	1155	426	426	327	329	380	360
Abiria	Namba	91	91	56	56	56	71	71	115	99
Mizigo ya kawaida	Namba	681	590	561	22	22	18	22	22	22
Mafuta	Namba	178	203	196	123	123	95	93	147	136
Mifugo	Namba	39	64	64	27	27	27	27	91	77
Mengineyo	Namba	211	266	278	198	198	116	116	27	18
Uchukuzi										
Abiria	,000	373	170	196.4	1,707	2,150	6,012	3,449	3,069	1,958
Mizigo	tani '000	185	127	282.6	102	170	357	374	340	380

Chanzo: Shirika la Reli Tanzania

RELI YA UHURU TANZANIA

Jedwali Na. 58

Maelezo	Kipimo	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Urefu wa Reli Kuu	Km	1,860	1,860	1,860	1,860	1,860	1,860	1,860	1,860	1,860
Magari ya Moshi	Namba	14.8	16	17.2	21	21	18	18	17	17
Reli Kuu	Namba	10.8	12.8	11.7	14	12	13	13	13	14
Ya kujongeza	Namba	4	3.2	5.5	7	7	5	5	4	3
Mabehewa ya abiria	Namba	52	50	51	56	49	60	61	47	45
Abiria	Namba	45	44	43	48	40	51	52	35	35
Chakula	Namba	3	3	3	4	4	4	4	5	3
Vifurushi	Namba	4	3	5	4	5	5	5	7	7
Mabehewa ya mizigo	Namba	1,391	1,101	1,142	1,221	1,033	1,118	1,113	803	803
Mizigo ya kawaida	Namba	1,229	966	1,007	1,077	972	998	992	659	659
Mifugo	Namba	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Mafuta	Namba	104	82	82	89	26	70	72	94	94
Barafu	Namba	5	5	5	5	-	-	-	-	-
Mengineyo	Namba	1	1	1	1	1	1	1	2	2
Breki	Namba	35	30	30	32	30	34	34	34	34
Ballast	Namba	17	17	17	17	4	15	14	14	14
Uchukuzi mizigo (Tani)										
Freight (tani)	tani' 000	245	33	81	96	171	268	155.2	224	257
Abiria	0'00	654	287	327	440	443	154	509.6	534	254

Chanzo: Mamlaka ya Reli ya Uhuru

USAFIRISHAJI KWA MELI: DAR ES SALAAM

Jedwali Na. 59A

Maelezo	Kipimo	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Jumla ya meli	Namba	1,600	1,617	1,684	1,688	1,744	1,516	1,407	1,610
Uwezo wa kubeba mizigo	000 Tani	31,936	31,614	31,278	31,287	32,513	31,200	28,532	32,293
Jumla ya abiria	000 Namba	1,433	1,612	1,735	1,874	1,901	2,035	1,307	1,610
Jumla ya bidhaa zote	000 Dwt	14,476	14,601	13,580	13,761	14,401	16,385	15,280	17,068
Bidhaa zilizopakuliwa	000 Dwt	**11,763**	**11,901**	**11,260**	**11,460**	**11,682**	**13,836**	**12,473**	**13,914**
Za kawaida	000 Dwt	7,100	6,657	6,087	6,376	6,199	7,876	7,113	8,185
Mafuta (Petroleum)	000 Dwt	4,357	4,882	4,772	4,740	5,483	5,959	5,360	5,729
Mengineyo1	000 Dwt	306	362	401	344	-	-	-	-
Bidhaa zilizopakiwa	000 Dwt	**2,713**	**2,700**	**2,320**	**2,301**	**2,719**	**2,550**	**2,807**	**3,154**
Za kawaida	000 Dwt	2,232	2,137	1,915	1,986	2,353	2,422	2,680	3,091
Mafuta (Petroleum)	000 Dwt	66	362	116	59	99	82	127	63
Mengineyo1	000 Dwt	-	-	-	-	-	-	-	-
Mabadilishano(Transhipment)	000 Dwt	415	201	289	256	267	46	-	-

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

USAFIRISHAJI KWA MELI: TANGA

Jedwali Na. 59B

Maelezo	Kipimo	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Jumla ya meli	Namba	68	63	87	72	144	120	108	156
Uwezo wa kubeba mizigo	000 Tani	1,403	1,018	1,258	1,041	780	568	633	984
Jumla ya abiria	000 Namba	-	-	-	-	45,820	68	49	92
Jumla ya bidhaa zote	000Dwt	368	645	677	486	646	619	621	839
Bidhaa zilizopakuliwa	**000Dwt**	**265**	**561**	**614**	**436**	**502**	**511**	**519**	**683**
Za kawaida	000Dwt	259	483	398	141	183	181	285	232
Mafuta (Petroleum)	000Dwt	6	78	216	295	319	331	234	451
Bidhaa zilizopakiwa	**000Dwt**	**103**	**83**	**63**	**50**	**144**	**108**	**102**	**156**
Za kawaida	000Dwt	103	83	63	50	144	108	102	156
Mafuta (Petroleum)	000Dwt	-	-	-	-	-	-	-	-

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

USAFIRISHAJI KWA MELI: MTWARA

Jedwali Na. 59C

Maelezo	Kipimo	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Jumla ya meli	Namba	65	46	113	105	69	132	72	125
Uwezo wa kubeba mizigo	0	841	593	460	457	589	598	304	607
Jumla ya abiria	000 Namba	0	0	0	0	0	0	0	0
Jumla ya bidhaa zote	000 DWt	365	248	375	378	363	270	155	204
Bidhaa zilizopakuliwa	000 DWt	**249**	**109**	**158**	**91**	**69**	**40**	**21**	**35**
Za kawaida	000 DWt	249	108	147	91	69	2	10	23
Mafuta (Petroleum)	000 DWt	-	1	10	-	-	37	11	12
Bidhaa zilizopakiwa	000 DWt	**116**	**139**	**218**	**286**	**294**	**230**	**134**	**169**
Za kawaida	000 DWt	116	139	218	286	294	230	134	169
Mafuta (Petroleum)	000 DWt	-	-	-	-	-	-	-	-

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania
- Takwimu hazikupatikana

HUDUMA ZA POSTA

Jedwali Na. 60

Maelezo	Kipimo	2014	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Ofisi Ndogo Posta	Namba	74	65	65	66	57	46	40	29
Franchised Post Offices	Namba	89	90	90	87	87	79	72	70
Ofisi Kubwa	Namba	160	158	158	154	157	139	132	144
Jumla	Namba	**323**	**313**	**313**	**307**	**301**	**264**	**244**	**243**
Masanduku Binafsi	000	142	160	160	161	161	145	126	126
Masanduku Yaliokodishwa	000	128	138	138	143	157	126	125	125
Maombi Yasiotimizwa	000	18	4	1	1	3	1	1	2
Mifuko Pekee Iliyokodishwa	Namba	260	180	180	342	675	442	291	240
Barua Zilizotumwa bila Vifurushi	Mill.	**15**	**10.3**	**4**	**5**	**9**	**11**	6	4
Regista na Barua za Amana	000	455	402	297	269	280	186	65	45
Vifurushi Nchini	000	12	17	36	51	63	32	4	6
Vifurushi Nje	000	5	9	2	3	4	3	2	2
Leseni za kuuza stamp	Namba	3,715	-	-	4,635	6,027	5,570	2,803	1,726
Huduma za Haraka, barua na vifurushi									
Ndani ya Nchi	Namba	406,732	416,007	452,827	560,710	655,927	511,274	466,029	627,822
Nje ya Nchi	Namba	20,564	308,288	6,364	9,534	14,346	13,742	7,080	11,642
EMS Money Fax	Namba	745	748	272	18	-	-	52	-
EMS Fax (Fax message received)	Namba	1,194	3,844	2,518	129	-	-	-	-
Overnight Mail Services	Namba	-	-	-	-	-	-	-	-
Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa	Namba	46,652	53,639	57,605	24,966	14,553	19,598	46,093	30,339
Vifurushi vya magazeti vilivyosafirishwa	Namba	**8,700**	**9,130**	**113,448**	**2,120**	**5,346**	**7,800**	-	-
Huduma za gari ndogo									
Idadi ya Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa	Namba	714	9,576	-	-	2,919	2,518	5,651	3,293
Amna za Haraka Zilizotolewa	Namba	845	58,423	272	127	104	109	52	
Amana za Haraka Zilizolipwa	Namba	**-**	**-**	**-**	**-**	-	-	-	-
Amana za Haraka za Nje ya Nchi									
Zilizotumwa	Namba	325	221	220	8	11	26	-	-
Zilizopokelewa	Namba	227	283	116	43	37	-	-	-
Amana za Posta zilizouzwa	Namba	261	251	107	45	2	-	-	-
Amana za Posta Zilizolipwa	Namba	67	25	18	8	-	-	-	-
Benki ya Akiba (Transaction)									
Uwekaji Amana (Deposit)	Namba	12,732	21,541	261,423	59,249	108,972	91,567	56,064	94,689
Uchukuaji Amana (Withdrawal)	Namba	12,807	18,098	45,449	76,926	133,531	103,958	75,065	69,203

Chanzo: Shirika la Posta
Takwimu hazikupatikana

IDADI YA WANAOTUMIA SIMU ZA MEZANI NA VIGANJANI

Jedwali Na. 61

Simu	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Mobitel/Tigo	10,639,610	11,677,344	11,044,520	12,583,640	12,572,826	13,032,073	13,369,276
Vodacom	12,520,645	12,419,425	12,714,297	14,143,657	15,672,390	15,621,457	15,913,553
Airtel	10,887,742	10,456,117	10,571,110	10,954,621	12,722,224	13,823,756	14,700,426
Zantel	1,563,503	1,083,157	934991	1,153,623	1,170,085	1,021,409	1,107,504
Benson/Smart	528	803,251	131,501	132,292	-	-	-
TTCL Mobile	165,460	166,383	175717	587,191	981,072	963,384	1,813,719
Smile	-	-	-	-	1,222	12,395	11,600
Hallotel	-	3,438,509	3,799,691	3,942,237	4,641,701	6,818,228	7,200,140
Jumla	**35,777,488**	**40,044,186**	**39,371,827**	**43,497,261**	**47,761,520**	**51,292,702**	**54,116,218**
Mobile Network							54,044,384
Fixed Network							71,834
Jumla							**54,116,218**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

-Takwimu hazikupatikana

SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA (ATCL)+

Jedwali Na. 62

Maelezo	Unit	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Tani - Kilometa:								
Zilizokuwepo	0	60,042	3,937	863,107	32,095	32,927	65,968	68,806
Zilizotumika	0	30,889	1,756	89,092	17,526	18,944	33,655	38,930
Matumizi	%	54	47	10	55	58	51	56.6
Viti - kilometa:								
Vilivyokuwepo	0	21,693	37,877	225,259	231,943	321,771	557,216	552,682
Vilivyotumika	0	11,472	20,692	122,532	158,203	220,433	347,101	417,706
Matumizi	%	53	56	54	68	69	62	75
Abiria	0	31	28	129	279	627	434	657
Mizigo ya ziada	Ton	53	1	41	55	96	86	75
Mizigo mingine	Ton	42	7	50	220	696	438	526
Shehena za Posta	Ton	4	-	32	119	295	61	21

Chanzo: Shirika la Ndege Tanzania

SURA YA 17

NISHATI

Ufuaji wa Umeme

418. Mwaka 2021, uwezo wa uzalishaji wa umeme ulifikia megawati 1,733.4 ikilinganishwa na megawati 1,605.8 mwaka 2020. Katika kipindi hicho, umeme uliozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali ulikuwa saa za gigawati 8,580.8 ikilinganishwa na saa za gigawati 7,862.9 zilizozalishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 9.1. Kati ya umeme uliozalishwa, saa za gigawati 8,356.5 zilizalishwa katika gridi ya taifa, saa za gigawati 80.3 zilizalishwa kwenye vituo nje ya gridi ya taifa na saa za gigawati 144.0 zilinunuliwa kutoka nchi jirani. Kwa upande wa umeme uliozalishwa katika gridi ya taifa, umeme uliozalishwa kwa kutumia mitambo ya nguvu za maji ulikuwa saa za gigawati 3,086.3, gesi saa za gigawati 5,237.2, mafuta mazito na dizeli saa za gigawati 16.2, na tungamotaka saa za gigawati 16.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na umeme wa mitambo ya nguvu za maji saa za gigawati 3,139.2, gesi saa za gigawati 4,509.1, mafuta mazito na dizeli saa za gigawati 10.2 na tungamotaka saa za gigawati 18.8 mwaka 2020. Aidha, umeme uliozalishwa na mitambo inayomilikiwa na TANESCO uliongezeka kwa asilimia 9.3 na kufikia saa za gigawati 6,980.8 ikilinganishwa na saa za gigawati 6,387.1 mwaka 2020. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa umeme kwa kampuni binafsi ulikuwa saa za gigawati 1,456.9 mwaka 2021 ikilinganishwa na saa za gigawati 1,290.2 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 12.9.

419. Mwaka 2021, umeme uliouzwa kwa watumiaji mbalimbali uliongezeka kwa asilimia 9.6 na kufikia saa za gigawati 7,313.2 ikilinganishwa na saa za gigawati 6,674.3 zilizouzwa mwaka 2020. Katika kipindi hicho, umeme uliopotea kutokana na uchakavu wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza ulikuwa saa za gigawati 1,181.7 sawa na asilimia 13.8 ya umeme uliozalishwa ikilinganishwa na saa za gigawati 1,110.0 zilizopotea mwaka 2020. Hadi Desemba 2021, Serikali kupitia utekelezaji wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini ilikuwa imeunganisha umeme katika vijiji 8,587 kati ya vijiji 12,345 vya Tanzania Bara, sawa na asilimia 69.6 ya vijiji vyote.

Kielelezo Na. 17.1: Umeme Uliozalishwa Kutoka Vyanzo Mbalimbali kwa Mwaka 2021



Utafutaji wa Mafuta na Gesi

420. Mwaka 2021 hakuna gesi asilia iliyogunduliwa na hivyo kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa kimeendelea kubaki futi za ujazo trilioni 57.5 kama ilivyokuwa mwaka 2020. Kati ya hizo, futi za ujazo trilioni 10.4 zipo nchi kavu na futi za ujazo trilioni 47.1 ziligunduliwa katika kina kirefu cha maji baharini. Katika kipindi hicho, visima vifupi vitatu vilichimbwa katika maeneo ya Kining'inila - Igunga, Nyalanja - Meatu na Luono - Iramba kwa ajili ya utafiti wa mafuta na gesi asilia. Aidha, gesi iliyozalishwa ilikuwa futi za ujazo milioni 64,924.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na futi za ujazo milioni 57,084.2 zilizozalishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 13.7. Hii ilitokana na mahitaji makubwa ya wateja wanaotumia gesi hususani katika uzalishaji wa nishati ya umeme na viwandani. Mapato yaliyotokana na mauzo ya gesi asilia kutoka vitalu vya Songosongo na Mnazi Bay yaliongezeka kwa asilimia 6.9 na kufikia dola za Marekani milioni 58.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 55.1 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya gesi viwandani pamoja na matumizi ya gesi katika kufua umeme kupitia TANESCO.

Jedwali Na. 17.1: Uzalishaji wa Gesi Asilia, Mwaka 2017 - 2021

Mwaka	Uzalishaji wa gesi (SCF)				Badiliko (Asilimia)
	Songosongo	Mnazi Bay	Kiliwani North	Jumla	
2017	29,496,560,000	17,960,300,000	3,597,578,168	**48,323,024,922**	5.7
2018	28,510,280,000	30,412,535,066	27,784,935	**51,054,438,168**	15.5
2019	37,619,760,000	26,201,516,247	-	**58,950,600,001**	8.3
2020	33,149,940,000	23,934,210,000	-	**57,084,150,000**	-10.6
2021	35,095,180,000	29,828,960,000	-	**64,924,140,000**	13.7

Chanzo: Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

Jedwali Na. 17.2: Mapato yaliyotokana na Mauzo ya Gesi Asilia Mwaka 2017 - 2021 (Dola za Marekani)

Mwaka	Songosongo	Mnazi Bay	Kiliwani North	Jumla	Badiliko (Asilimia)
2017	22,795,142	13,763,426	5,702,695	**42,261,263**	-18.7
2018	22,406,171	40,671,729	11,359	**63,089,259**	49.3
2019	28,097,086	35,952,953	-	**64,050,039**	1.5
2020	20,995,963	34,122,450	-	**55,118,413**	-13.9
2021	16,018,066	42,886,054	-	**58,904,120**	6.9

Chanzo: Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

Uagizaji Mafuta

421. Mwaka 2021, lita za ujazo milioni 3,957.7 za mafuta ziliingizwa nchini kwa matumizi ya ndani ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 3,572.0 zilizoingizwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 10.8. Hii ilitokana na kuanza kuimarika kwa shughuli za kiuchumi hususani usafirishaji na kuanza kurejea kwa huduma za usafiri wa anga zilizokuwa zimesitishwa kufuatia kupungua kwa maambukizi ya UVIKO - 19 pamoja na kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya kiasi cha mafuta kilichoagizwa, mafuta ya dizeli yalikuwa lita za ujazo milioni 2,147.6, petroli lita za ujazo milioni 1,603.6, mafuta ya taa lita za ujazo milioni 20.1, mafuta ya ndege lita za ujazo milioni 162.2 na mafuta mazito lita za ujazo milioni 24.2. Katika kipindi hicho, uagizaji wa mafuta ya taa ulipungua kwa asilimia 42.4 kutokana na Serikali kuendelea kuchukua hatua za kudhibiti uchakachuaji wa mafuta ya petroli na dizeli. Aidha, uagizaji wa mafuta mazito ulipungua kwa asilimia 9.7 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa matumizi ya nishati mbadala maeneo ya vijijini pamoja na viwanda kutumia zaidi gesi asilia.

Jedwali Na. 17.3: Mafuta Yaliyoingizwa Nchini kwa Matumizi ya Ndani Mwaka 2021 (lita za ujazo)

	Dizeli	Petroli	Mafuta ya Taa	Mafuta ya Ndege	Mafuta Mazito	Jumla
Januari	142,205,253	137,576,287			4,670,720	284,452,260
Februari	180,698,555	118,579,698	2,586,773	14,370,352		316,235,378
Machi	158,461,181	145,843,883	1,966,497	27,771,770		334,043,330
Aprili	177,961,566	85,652,746	2,338,870	22,115,984	4,486,294	292,555,459
Mei	199,627,580	101,785,091				301,412,672
Juni	69,753,181	141,369,701	1,971,768	18,392,456		231,487,106
Julai	161,791,382	85,247,757	2,857,875	12,213,137		262,110,151
Agosti	133,786,021	118,632,973	1,671,450	6,545,409	5,066,953	265,702,806
Septemba	191,441,773	145,270,667	253,641	6,627,664		343,593,745
Oktoba	204,553,684	128,785,602	2,964,234	32,903,579		369,207,099
Novemba	150,148,781	120,063,615			9,972,661	280,185,056
Desemba	199,816,526	170,832,521	952,720	18,814,226		390,415,993
Mafuta ya nje yaliyouzwa ndani ya nchi (Localized Transit)	177,368,301	103,983,913	2,521,450	2,418,029	42,520	286,334,213
Jumla Kuu	**2,147,613,784**	**1,603,624,454**	**20,085,278**	**162,172,606**	**24,239,148**	**3,957,735,268**

Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Kwenda Nchi Jirani

422. Mwaka 2021, mafuta yaliyoingizwa nchini kwenda nchi jirani yaliongezeka kwa asilimia 41.2 na kufikia lita za ujazo milioni 3,112.4 ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 2,204.8 mwaka 2020. Hii ilitokana na nchi jirani kufungua shughuli za kiuchumi baada ya kupungua kwa maambukizi ya UVIKO - 19. Kati ya kiasi cha mafuta kilichoagizwa, mafuta ya dizeli yalikuwa lita za ujazo milioni 1,886.8, petroli lita za ujazo milioni 1,078.9, mafuta ya taa na ndege lita za ujazo milioni 131.2 na mafuta mazito lita za ujazo milioni 15.5.

Jedwali Na. 17.4: Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Kwenda Nchi Jirani Mwaka 2021 (Lita za Ujazo)

Mwezi	Dizeli	Petroli	Mafuta ya Taa na Ndege	Mafuta Mazito	Jumla
Januari	103,642,115	107,913,502		4,482,926	216,038,543
Februari	209,914,738	89,035,917	10,545,989		309,496,644
Machi	177,090,101	114,951,926	19,664,658		311,706,686
Aprili	201,172,732	75,301,670	13,500,731		289,975,133
Mei	186,134,825	103,621,095			289,755,920
Juni	78,633,633	100,424,928	11,412,991		190,471,551
Julai	202,697,080	96,281,983	11,490,216	8,343,008	318,812,287
Agosti	152,267,360	84,967,582	10,389,332		247,624,274
Septemba	219,600,717	121,151,401	8,799,214		349,551,333
Oktoba	204,974,216	93,862,464	33,033,586		331,870,265
Novemba	120,503,348	85,159,306		2,712,853	208,375,508
Desemba	207,624,027	110,169,898	17,272,878		335,066,803
Toa- Localization (Ujanibishaji) Jan-Des 2021	177,368,301	103,983,913	4,939,479	42,520	286,334,213
Jumla Kuu	**1,886,886,591**	**1,078,857,759**	**131,170,116**	**15,496,267**	**3,112,410,734**

Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

Mwenendo wa Bei za Mafuta

423. Mwaka 2021, wastani wa bei ya mafuta kwa tani katika soko la dunia ulikuwa dola za Marekani 671 kwa petroli, dizeli dola za Marekani 575 na mafuta ya taa dola za Marekani 580 ikilinganishwa na dola za Marekani 426, dola za Marekani 403 na dola za Marekani 390 mwaka 2020 mtawalia. Bei hizo ziliongezeka kwa asilimia 57.5 kwa mafuta ya petroli, asilimia 42.7 mafuta ya dizeli na asilimia 48.7 mafuta ya taa. Kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia kulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mafuta kufuatia kuanza kuimarika kwa shughuli za kiuchumi baada ya kupungua kwa maambukizi ya UVIKO - 19. Aidha, wastani wa bei ya mafuta kwa lita katika soko la ndani ulikuwa shilingi 2,241 kwa mafuta ya petroli, shilingi 2,096 mafuta ya dizeli na shilingi 2,012 mafuta ya taa mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi 1,928 mafuta ya petroli, shilingi 1,862 mafuta ya dizeli na shilingi 1,768 mafuta ya taa mwaka 2020. Bei ya mafuta ya petroli iliongezeka kwa asilimia 16.2, dizeli asilimia 12.6 na mafuta ya taa asilimia 13.8. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia.

Jedwali Na. 17.5: Wastani wa Bei za Mafuta Katika Soko la Dunia Mwaka 2019 - 2021
(Dola za Marekani kwa Tani)

Aina ya Mafuta	Petroli			Dizeli			Mafuta ya Taa		
Mwezi/Mwaka	**2019**	**2020**	**2021**	**2019**	**2020**	**2021**	**2019**	**2020**	**2021**
Januari	635	592	496	606	552	443	644	574	448
Februari	520	580	562	501	571	504	542	585	504
Machi	496	578	617	516	551	513	543	572	513
Aprili	543	529	618	582	475	506	543	484	512
Mei	610	397	644	600	402	548	605	291	555
Juni	677	214	680	618	249	586	625	291	589
Julai	658	261	720	610	300	595	634	291	600
Agosti	597	389	697	546	367	564	570	291	570
Septemba	639	389	732	576	369	614	601	333	617
Oktoba	576	405	793	552	359	710	584	333	721
Novemba	596	394	775	572	320	679	602	333	690
Desemba	574	386	718	560	321	634	574	301	644
Wastani wa Bei	**593**	**426**	**671**	**570**	**403**	**575**	**589**	**390**	**580**
Badiliko (Asilimia)	**-10.3**	**-28.2**	**57.5**	**-8.4**	**-29.3**	**42.6**	**-8.7**	**-33.8**	**48.7**

Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

Jedwali Na. 17.6: Mwenendo wa Bei za Mafuta Katika Soko la Ndani Mwaka 2021
(Shilingi kwa Lita)

Mwezi	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Januari	1,834	1,695	1,650
Februari	1,887	1,829	1,769
Machi	1,981	1,911	1,863
Aprili	2,123	1,996	1,863
Mei	2,169	2,038	1,957
Juni	2,249	2,073	1,957
Julai	2,405	2,215	2,121
Agosti	2,427	2,251	2,176
Septemba	2,427	2,251	2,176
Oktoba	2,439	2,261	2,188
Novemba	2,439	2,243	2,188
Desemba	2,510	2,392	2,235
Wastani kwa Mwaka 2021	**2,241**	**2,096**	**2,012**
Badiliko (Asilimia)	16.2	12.6	13.8

Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

Nishati Jadidifu

Nishati mbadala ya Gesi inayotokana na Petroli

424. Mwaka 2021, gesi inayotokana na petroli (Liquefied Petroleum Gas - LPG) iliyoagizwa toka nje kwa matumizi mbalimbali iliongezeka kwa asilimia 27.6 na kufikia tani za ujazo 248,216 ikilinganishwa na tani 194,597 mwaka 2020. Hii ilichangiwa na kuhamasika kwa umma kuhusu umuhimu wa kutumia gesi itokanayo na petroli yenye gharama nafuu na rafiki kwa mazingira ikilinganishwa na matumizi ya mkaa na kuni.

UWEZO WA MITAMBO YA KUFUA UMEME NA UMEME ULIOZALISHWA MWAKA 2021

Jedwali Na. 63

Kituo	Uwezo (MW)	Umeme uliozalishwa (Saa za Gigawati)
A: Mitambo Iliyounganishwa Katika Gridi ya Taifa		
Kidatu	204.00	1,195.22
Kihansi	180.00	771.12
Mtera	80.00	638.32
New Pangani Falls	68.00	341.88
Hale	21.00	30.70
Nyumba ya Mungu	8.00	53.76
Uwemba	0.84	2.01
Mwenga	4.00	17.96
Yovi	0.95	6.15
Matembwe	0.59	0.45
Darakuta	0.32	2.11
Luponde	0.90	2.21
Andoya	1.00	1.60
Tulila	5.00	22.83
Jumla Ndogo - Maji	**574.60**	**3,086.32**
Ubungo I	102.00	542.73
Ubungo II	129.00	773.54
Ubungo III	120.00	13.71
Kinyerezi I	150.00	511.01
Kinyerezi II	248.22	1,681.80
Tegeta	45.00	221.52
Mtwara	30.60	99.56
Somanga	7.50	7.38
Songas	189.00	1,385.94
Jumla Ndogo - Gesi	**1,021.32**	**5,237.18**
Nyakato	63.00	6.07
Zuzu	7.40	1.88
Biharamulo	4.14	3.24
Songea	5.77	-
Ludewa	1.27	-
Mbinga	1.00	-
Tunduru	1.72	-
Ngara	2.50	5.06
Madaba	0.48	-
Liwale	0.85	-
Jumla Ndogo - Mafuta	**88.13**	**16.24**
TPC	9.00	13.69
TANWAT	1.50	3.02
Jumla Ndogo - Tungamotaka	**10.50**	**16.71**
Jumla - Gridi ya Taifa	**1,694.55**	**8,356.46**
B: Mitambo iliyoko nje ya Gridi ya Taifa *(Off-Grid)*		
Bukoba	2.56	0.11
Inyonga	0.82	2.27
Kasulu	3.75	12.13
Kibondo	2.50	6.81
Kigoma	13.75	30.05
Loliondo	2.25	1.84
Mafia	3.20	6.24
Mpanda	5.00	19.20
Sumbawanga	5.00	1.63
Nextgen- Solawazi	5.00	-
Jumla – Nje ya Gridi ya Taifa	**38.83**	**80.28**
C: Umeme kutoka Nchi Jirani		
Uganda	-	92.91
Zambia	-	44.11
Kenya	-	-
Jumla- Nje ya Nchi	**-**	**144.02**
Jumla Kuu	**1,733.38**	**8,580.76**

Chanzo: Shirika la Ugamvi wa Umeme Tanzania

MAUZO YA UMEME MWAKA 2017 - 2021 (Saa za gigawati)

Jedwali Na. 64

Mwaka	Tanzania Bara			Wateja Zanizibar	Jumla	Umeme Uliopotea	Umeme Uliozalishwa
	Wateja Wadogo	Wateja wa Kati	Wateja Wakubwa				
2017	301.5	2,371.0	2,893.3	390.4	5,956.2	1,159.1	7,115.3
2018	319.8	2,481.9	3,075.0	414.0	6,290.7	1,064.1	7,354.8
2019	307.2	2,655.7	3,198.0	481.5	6,642.5	1,064.1	7,806.4
2020	325.8	2,668.6	3,205.1	474.9	6,674.3	1,110.0	7,862.9
2021	339.9	2,900.0	3,527.0	546.3	7,313.2	1,181.7	8,580.8

Chanzo: Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania

MAUZO YA UMEME KWA MIKOA MWAKA 2017 - 2021

Jedwali Na. 65

Mikoa	Umeme Uliouzwa (Saa za gigawati)				
	2017	2018	2019	2020	2021
Dar es Salaam	2,412.5	2,481.6	2,596.5	2,534.0	2,652.01
Pwani	302.1	393.1	450.7	517.9	597.87
Dodoma	150.4	161.0	179.7	177.7	228.70
Morogoro	242.8	274.9	268.0	266.8	298.50
Singida	43.8	45.7	49.5	53.1	58.09
Tanga	330.4	353.9	351.3	342.2	375.51
Kilimanjaro	179.4	181.7	185.2	183.9	195.18
Arusha	365.9	383.3	406.3	385.6	395.59
Manyara	31.9	32.4	34.8	35.2	53.51
Mtwara	48.3	52.8	55.9	55.9	58.62
Lindi	22.9	25.8	29.7	30.5	33.82
Ruvuma	35.4	41.9	50.3	53.7	56.89
Mbeya	177.6	186.9	201.6	209.9	226.91
Iringa	98.4	103.7	108.9	109.1	117.25
Rukwa	27.0	25.9	27.3	28.6	31.05
Katavi	10.8	11.2	13.6	16.3	21.81
Njombe	35.6	35.4	39.1	42.0	45.65
Songwe	10.1	29.3	33.2	40.4	50.24
Mwanza	283.2	287.7	295.2	300.9	325.55
Kagera	76.9	90.6	80.3	79.2	96.82
Mara	156.9	165.8	163.9	188.1	195.47
Geita	42.7	49.2	53.0	60.8	77.69
Tabora	55.9	60.7	68.4	69.7	76.38
Shinyanga	371.9	339.5	354.0	352.2	421.74
Kigoma	34.8	40.2	40.3	41.0	47.47
Simiyu	18.2	22.4	24.2	24.8	28.60
Jumla Tanzania Bara	**5,565.8**	**5,876.6**	**6,161.0**	**6,199.4**	**6,766.9**
Zanzibar	390.4	414.0	481.5	474.9	546.29
Jumla	**5,956.2**	**6,290.6**	**6,642.5**	**6,674.3**	**7,313.2**

Chanzo: Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania

SURA YA 18

MAJI

Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

425. Mwaka 2021, kiwango cha rasilimali za maji kilichopo na kinachofaa kwa matumizi ni wastani wa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka kama kilivyokuwa mwaka 2020. Kati ya kiwango hicho, mita za ujazo bilioni 105 zipo juu ya ardhi na mita za ujazo bilioni 21 zipo chini ya ardhi. Aidha, kwa mujibu wa tathmini ya maji iliyofanyika mwaka 2019, wastani wa kiwango cha maji kilichopo ni mita za ujazo 2,250 kwa mtu kwa mwaka. Kiwango hicho ni juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 ambacho ni kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kinachokubalika kimataifa kwa mtu kwa mwaka. Katika kipindi hicho, mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali nchini yalikadiriwa kuwa mita za ujazo bilioni 47 kwa mwaka, ikilinganishwa na mita za ujazo bilioni 60 mwaka 2020 sawa na upungufu wa asilimia 21.7.

426. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kutambua vyanzo vya maji vilivyo katika hatari ya kuharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu ambapo vyanzo 2,059 vilitambuliwa ikilinganishwa na vyanzo 1,213 vilivyotambuliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 69.7. Ongezeko hilo lilitokana na Bodi za Maji za Mabonde kuendelea na utekelezaji wa zoezi mahsusi la utambuzi wa vyanzo vya maji. Kati ya vyanzo hivyo, vyanzo 41 viliwekewa mipaka kwa lengo la kuvihifadhi visiharibiwe kutokana na shughuli za kibinadamu.

427. Mwaka 2021, vituo vipya 14 vya kufuatilia mwenendo wa maji juu na chini ya ardhi vilijengwa na hivyo kuongeza vituo vinavyofanya kazi katika maeneo mbalimbali na kufikia 1,189 kutoka vituo 1,175 mwaka 2020. Vituo hivyo vinajumuisha: vituo 341 vya hali ya hewa; vituo 366 vya kufuatilia maji mtoni, katika maziwa na mabwawa; vituo 95 vya maji chini ya ardhi; vituo 33 vya kufuatilia mchanga kwenye mito; na vituo 354 vya ubora wa maji. Katika kipindi hicho, vituo 141 vya kufuatilia mwenendo wa maji vilikarabatiwa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufuatiliaji wa mwenendo wa maji.

Ubora wa Maji

428. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuhakiki ubora wa maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya usambazaji maji ambapo sampuli 6,988 za maji zilikusanywa na kuhakikiwa ikilinganishwa na sampuli 6,855 zilizohakikiwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 1.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa maabara sita (6) zilizopata ithibati, hivyo kutambulika kitaifa na kimataifa. Kati ya sampuli zilizokusanywa na kuhakikiwa, sampuli 5,953 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, sampuli 446 kwa ajili ya ufuatiliaji wa mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji, sampuli 376 kwa ajili ya matumizi ya viwandani, sampuli 27 kwa ajili ya umwagiliaji, sampuli 40

kwa ajili ya ujenzi, sampuli 62 kwa ajili ya utafiti na sampuli 84 kwa ajili ya kupima uwezo wa utendaji kazi wa maabara.

429. Matokeo ya uhakiki yalionesha kuwa sampuli za maji 4,346 sawa na asilimia 73.0 ya sampuli 5,953 kwa ajili ya matumizi ya nyumbani zilikidhi viwango vya ubora na usalama wa maji vinavyokubalika na sampuli 1,607 hazikukidhi viwango. Kutokukidhi viwango kwa sampuli hizo kulitokana na uwepo wa kiwango kikubwa cha madini ya chumvichumvi, *manganese,* chuma na *sulphate* katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na uwepo wa vimelea vya bakteria katika maeneo yasiyokuwa na miundombinu ya kutibu maji. Aidha, sampuli 589 za maji kwa ajili ya shughuli za viwandani, umwagiliaji, ujenzi, utafiti na upimaji wa uwezo wa utendaji kazi wa maabara zilizofanyiwa uhakiki zilikidhi viwango vya ubora vinavyokubalika. Vilevile, matokeo ya uhakiki wa sampuli 446 yalionesha kuwa vyanzo vya maji ni rafiki kwa mazingira na viumbe hai vilivyomo.

430. Mwaka 2021, sampuli 300 za majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira zilikusanywa na kuhakikiwa ikilinganishwa na sampuli 328 mwaka 2020. Matokeo ya uhakiki yalionesha kuwa sampuli 240 sawa na asilimia 80.0 hazikukidhi viwango vya ubora kutokana na uwepo wa kiwango kikubwa cha vigezo vya *Chemical Oxygen Demand* (COD) pamoja na *Biochemical Oxygen Demand* (BOD) katika sampuli mbalimbali zilizochunguzwa pamoja na majitaka kutoka maeneo ya kilimo cha kumwagilia kinachotumia mbolea na viuwatilifu. Huduma ya Maji Vijijini.

Huduma ya Maji Mijini

431. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuboresha miundombinu ya maji vijijini kwa kukarabati na kupanua miradi ya miundombinu iliyopo na kutekeleza miradi mipya. Katika kipindi hicho, miradi 645 yenye vituo vya kuchotea maji 10,103 vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi 3,585,226 ilikamilika. Hadi Desemba 2021, idadi ya vituo vinavyofanya kazi na kutoa huduma ya maji ilifikia vituo 134,225 ikilinganishwa na vituo 114,354 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 17.4. Aidha, nyumba zilizounganishwa na huduma ya maji zilikuwa 171,674 mwaka 2021 ikilinganishwa na nyumba 75,173 mwaka 2020. Hii ilitokana na jitihada za Serikali kuendelea kusogeza huduma ya maji karibu na wananchi maeneo ya vijijini. Kwa ujumla, wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji vijijini ulikuwa asilimia 72.3 mwaka 2021 kama ilivyokuwa mwaka 2020.

432. Hadi Desemba 2021, wastani wa wateja 1,198,618 waliunganishwa na huduma ya majisafi ikilinganishwa na wastani wa wateja 1,060,700 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 13.0. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea na ukarabati wa miundombinu ya maji na kuunganisha wateja kwenye miradi iliyokamilika katika miji mikuu ya mikoa na wilaya pamoja na utekelezaji wa miradi ya kitaifa. Katika kipindi hicho, mauzo ya majisafi na salama yalikuwa shilingi bilioni 329.1 ikilinganishwa na mauzo ya shilingi bilioni 297.3 mwaka 2020, sawa na ongezeko la

asilimia 10.7. Aidha, Mamlaka za maji zilizoongoza kwa mauzo ya majisafi na salama zilikuwa za Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Moshi na Iringa. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa maji ulikuwa mita za ujazo milioni 312.9 mwaka 2021 ikilinganishwa na mita za ujazo milioni 307.7 mwaka 2020. Hata hivyo, uzalishaji wa maji ulipungua katika Mamlaka za maji za miji ya Mwanza, Mbeya, Tanga, Songea, Bukoba na Sumbawanga kutokana na athari za ukame kwenye maeneo hayo.

Uchimbaji wa Visima

433. Mwaka 2021, Serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi iliendelea na uchimbaji wa visima katika maeneo ya mijini na vijijini ili kuboresha huduma za maji. Katika kipindi hicho, visima 944 vilichimbwa katika maeneo mbalimbali ikilinganishwa na visima 853 vilivyochimbwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 10.7. Kati ya hivyo, visima 198 vilichimbwa na Serikali na visima 746 vilichimbwa na sekta binafsi. Ongezeko la idadi ya visima lilitokana na Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini - RUWASA kuongeza uwekezaji wa uchimbaji wa visima kwenye maeneo mengi ya vijijini. Visima hivyo vilichimbwa katika mabonde mbalimbali ya maji ambapo visima 164 vilichimbwa katika bonde la maji la Ziwa Tanganyika, visima 86 katika bonde la Ziwa Rukwa, visima nane (8) katika bonde la Ziwa Nyasa, visima 216 katika bonde la Mto Pangani, visima 158 katika bonde la kati, visima 11 katika bonde la Mto Rufiji, visima 55 katika bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini, visima 170 katika bonde la Mto Wami/Ruvu na visima 76 katika bonde la Ziwa Victoria.

Uondoaji wa Majitaka

434. Mwaka 2021, mtandao wa majitaka ulikuwa na urefu wa kilomita 981.8 ikilinganishwa na kilomita 898.6 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 9.3. Ongezeko hilo lilitokana na ulazaji wa mabomba ya majitaka katika miji ya Arusha (kilomita 27), Dodoma (kilomita 42), Dar es salaam (kilomita 43), Iringa (kilomita 10) na kilomita saba (7) zililazwa katika miji mingine yenye mtandao wa majitaka. Aidha, wateja walioounganishwa katika mtandao wa majitaka walikuwa 53,008 mwaka 2021 ikilinganishwa na wateja 51,183 mwaka 2020. Kwa upande mwingine, huduma ya usafi wa mazingira katika miji ambayo haina mtandao wa majitaka iliendelea kutolewa kwa mfumo usiounganishwa na mtandao katika uondoaji wa majitaka. Mfumo huo hutumia magari maalumu ya ubebaji wa majitaka na kuyamwaga katika sehemu maalumu zilizojengwa kwa ajili ya kuchakata majitaka. Hadi Desemba 2021, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kumi na mbili (12) za Sumbawanga, Kahama, Bukoba, Musoma, Geita, Nansio, Sengerema, Kigoma, Magu, Misungwi, Lindi na Lamadi zilikuwa zinatumia mfumo huo.

UZALISHAJI WA MAJI NA MAPATO YATOKANAYONA MAJI MIJINI

Jedwali Na. 66

Mamlaka	2020		2021	
	Uzalishaji wa Maji (Mita za Ujazo)	Mapato (Shillings)	Uzalishaji wa Maji (Mita za Ujazo)	Mapato (Shillings)
Arusha	15,823,818	16,863,639,378	18,067,443	17,999,825,878
Babati	2,033,740	2,673,483,543	2,078,483	2,838,939,698
Bariadi	272,262	179,187,841	372,070	215,961,974
Bukoba	2,748,120	2,284,101,436	2,278,141	2,572,519,656
Dodoma	15,493,870	18,093,093,316	15,993,870	19,093,093,316
DAWASA	146,437,533	135,380,043,912	147,335,820	152,645,652,026
Geita	1,748,297	1,842,082,283	1,794,293	1,867,011,719
Iringa	4,668,691	8,532,522,161	5,002,774	9,095,652,850
Kahama	4,337,360	9,049,024,770	4,944,602	8,294,405,263
Kigoma	3,250,796	2,208,707,132	3,540,630	2,887,402,099
Lindi	758,513	843,700,012	849,515	915,573,020
Mpanda	944,570	609,492,500	1,102,750	901,273,111
Mbeya	16,892,670	12,074,273,429	15,717,345	14,050,004,654
Morogoro	12,347,306	10,563,745,566	12,488,485	13,911,098,689
Moshi	11,681,145	10,360,287,936	12,230,221	11,278,193,248
Mtwara	3,447,080	3,360,287,173	4,703,859	4,193,008,301
Musoma	5,806,006	3,055,714,297	5,838,684	3,695,758,088
Mwanza	28,882,933	25,631,493,019	27,480,248	27,899,372,169
Njombe	1,287,543	999,653,342	1,297,543	1,019,653,342
Shinyanga	4,216,608	6,545,726,499	4,450,266	6,234,134,647
Singida	2,705,150	3,148,496,303	3,058,935	3,353,780,031
Songea	2,910,973	3,041,166,043	2,870,953	2,799,047,711
Sumbawanga	2,448,249	1,520,152,181	1,979,688	1,647,677,058
Tabora	4,974,294	4,487,577,632	5,769,925	4,624,787,718
Tanga	10,711,585	13,819,213,628	10,686,428	14,981,200,124
Vwawa-Mlowo	868,142	86,448,413	998,142	106,448,413
Jumla	**307,697,254**	**297,253,313,745**	**312,931,112**	**329,121,474,804**

Chanzo: Wizara ya Maji

MAHITAJI NA KIWANGO CHA UPATIKANAJI WA MAJI KATIKA MIJI MWAKA 2021

Jedwali Na. 67

Mamlaka	Mahitaji ya Maji	Wastani wa Upatikanaji wa Huduma ya Maji (Asilimia)
Arusha	40,036,576	86
Babati	5,008,476	92
Bariadi	2,984,605	59
Bukoba	336,987	87
Dodoma	37,080,000	97
DAWASA	207,970,000	88
Geita	18,885	74
Iringa	5,840,000	98
Kahama	5,527,911	88
Kigoma	8,183,480	95
Lindi	5,000	84
Mpanda	4,004,780	85
Mbeya	31,025,000	92
Morogoro	24,352,218	76
Moshi	51,428	100
Mtwara	8,103,730	92
Musoma	8,760,000	97
Mwanza	47,350,000	95
Njombe	3,316,008	88
Shinyanga	637,980	92
Singida	14,410	92
Songea	17,897	96
Sumbawanga	5,952,000	83
Tabora	10,759,589	94
Tanga	727,193	97
Vwawa-Mlowo	3,593,425	49
Jumla	**461,657,578**	**87.5**

Chanzo: Wizara ya Maji

SURA YA 19

ELIMU MAFUNZO YA UFUNDI NA TEKNOLOJIA

Elimu ya Awali

435. Mwaka 2021, kulikuwa na wanafunzi 1,390,825 walioandikishwa katika elimu ya awali ikilinganishwa na wanafunzi 1,377,409 walioandikishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 1.0. Kati ya hao, wasichana walikuwa 684,430 sawa na asilimia 49.2 na wavulana walikuwa 706,395. Kati ya wanafunzi walioandikishwa, wanafunzi wenye mahitaji maalum walikuwa 5,544 (wasichana 2,407 na wavulana 3,137) mwaka 2021 ikilinganishwa na 4,178 (wasichana 1,786 na wavulana 2,392) mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 32.7. Ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi katika elimu ya awali lilitokana na jitihada za Serikali za kuendelea kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ikiwemo ugharamiaji wa elimumsingi bila ada pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu. Aidha, uandikishaji wa wanafunzi katika shule za Serikali uliongezeka kwa asilimia 1.0 na kufikia 1,291,868 mwaka 2021 ikilinganishwa na wanafunzi 1,278,886 walioandikishwa mwaka 2020. Kati ya wanafunzi hao, wasichana walikuwa 635,837, sawa na asilimia 49.2 na wavulana walikuwa 656,031. Vilevile, wanafunzi walioandikishwa katika shule zisizo za Serikali waliongezeka kwa asilimia 0.4 na kufikia 98,957 mwaka 2021 ikilinganishwa na wanafunzi 98,523 mwaka 2020.

436. Mwaka 2021, idadi ya walimu katika shule za elimu ya awali za Serikali iliongezeka kwa asilimia 10.8 na kufikia 8,369 (wanawake 5,787 na wanaume 2,582) kutoka walimu 7,553 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Serikali katika kuajiri walimu wapya ambapo uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi wa elimu ya awali umeimarika na kufikia 1:154 mwaka 2021 ikilinganishwa na uwiano wa 1:169 mwaka 2020. Uwiano huo ulizidi kiwango halisi cha uwiano wa 1:25 unaokubalika kitaifa, hivyo Serikali iliendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi kwa walimu waliopo kazini na walimu tarajali na kuajiri walimu wapya ili kuendelea kuboresha uwiano huo.

Elimu ya Msingi

437. Mwaka 2021, shule za msingi ziliongezeka kwa asilimia 2.2 na kufikia 18,546 kutoka shule 18,152 mwaka 2020. Kati ya hizo, shule za Serikali zilikuwa 16,656 ikilinganishwa na shule 16,406 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 1.5. Ongezeko la shule za Serikali lilitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa azma ya Serikali ya kuhakikisha uwepo wa shule ya msingi katika kila kijiji. Aidha, shule zisizo za Serikali zilifikia 1,890 mwaka 2021 kutoka shule 1,746 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 8.2. Hii ilitokana na Serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na kutambua mchango wa sekta binafsi katika sekta ya elimu.

438. Mwaka 2021, idadi ya wanafunzi katika shule za elimu ya msingi iliongezeka kwa asilimia 2.5 na kufikia 11,196,788 ikilinganishwa na wanafunzi 10,925,896 mwaka 2020. Kati ya hao, wasichana walikuwa 5,639,081 sawa na asilimia 50.3 na wavulana walikuwa 5,557,707 ikilinganishwa na wasichana 5,481,982 na wavulana 5,443,914 mwaka 2020. Katika kipindi hicho, wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za msingi walikuwa 60,823 (wasichana 26,404 na wavulana 34,419) ikilinganishwa na wanafunzi 55,758 (wasichana 23,762 na wavulana 31,996) mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 9.1. Aidha, idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali ilikuwa 10,687,593 mwaka 2021 ikilinganishwa na wanafunzi 10,460,785 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 2.2. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Serikali katika kuendelea kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ikiwemo ugharamiaji wa elimumsingi bila ada pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu.

439. Mwaka 2021, watahiniwa waliofanya mtihani wa kuhitimu darasa la saba waliongezeka kwa asilimia 8.2 na kufikia 1,107,460 kutoka watahiniwa 1,023,950 mwaka 2020. Kati ya hao, watahiniwa 907,802 (wasichana 467,967 na wavulana 439,835) walifaulu sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 82.0.

440. Mwaka 2021, idadi ya walimu katika shule za elimu za msingi za Serikali iliongezeka kwa asilimia 0.8 na kufikia 171,993 (wanaume 86,083 na wanawake 85,910) kutoka walimu 170,569 (wanaume 84,673 na wanawake 85,896) mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Serikali katika kuajiri walimu wapya. Katika kipindi hicho, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi ulikuwa 1:62 ikilinganishwa na uwiano wa 1:61 mwaka 2020. Uwiano huo ulizidi kiwango halisi cha uwiano wa 1:45 unaokubalika kitaifa, hivyo Serikali inaendelea kufanya jitihada mbalimbali ikiwemo kuajiri walimu wapya ili kupunguza uwiano huo.

Elimu ya Sekondari

441. Mwaka 2021, idadi ya shule za sekondari ilifikia 5,289 kutoka shule 5,143 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 2.8. Kati ya hizo, shule 4,002 zilikuwa za Serikali na shule 1,287 zisizo za Serikali ikilinganishwa shule 3,863 za Serikali na shule 1,280 zisizo za Serikali mwaka 2020. Hii ilitokana na jitihada zilizochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaohitimu darasa la saba na kujiunga na kidato cha kwanza.

442. Mwaka 2021, idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita iliongezeka kwa asilimia 8.0 na kufikia 2,671,927 ikilinganishwa na wanafunzi 2,473,506 mwaka 2020. Kati ya hao, wasichana walikuwa 1,389,613 sawa na asilimia 52.0 na wavulana walikuwa 1,282,314. Aidha, idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari za Serikali iliongezeka kwa asilimia 9.6 na kufikia wanafunzi 2,379,945 mwaka 2021 kutoka wanafunzi 2,172,257 mwaka 2020. Katika kipindi hicho, idadi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne iliongezeka kwa asilimia 8.2 na kufikia

2,511,544 ikilinganishwa na wanafunzi 2,322,259 mwaka 2020. Kati ya hao, wanafunzi katika shule za Serikali walikuwa 2,256,489 ikilinganishwa na wanafunzi 2,062,717 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 9.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi waliohitimu darasa la saba na kujiunga na kidato cha kwanza.

443. Watahiniwa waliofanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne mwaka 2021 waliongezeka kwa asilimia 11.1 na kufikia 483,820 (wasichana 229,445 na wavulana 254,375) ikilinganishwa na watahiniwa 435,654 mwaka 2020. Kati ya hao, watahiniwa 422,388 (wasichana 218,174 na wavulana 204,214) walifaulu sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 87.3 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 85.8 mwaka 2020. Vilevile, watahiniwa waliofanya mtihani wa kuhitimu kidato cha sita waliongezeka kwa asilimia 21.5 na kufikia 89,802 (wasichana 38,018 na wavulana 51,784) mwaka 2021 ikilinganishwa na watahiniwa 73,901 (wasichana 32,357 na wavulana 41,544) mwaka 2020. Kati ya hao, watahiniwa 87,043 (wasichana 37,322 na wavulana 49,721) walifaulu sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 96.9 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 99.5 mwaka 2020.

Elimu katika Vyuo vya Ualimu

444. Mwaka 2020/21, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ualimu ilikuwa 17,260 ikilinganishwa na wanafunzi 19,249 mwaka 2019/20, sawa na upungufu wa asilimia 10.3. Kati ya wanafunzi hao, wanawake walikuwa 7,538 na wanaume walikuwa 9,722 ikilinganishwa na wanawake 6,025 na wanaume 13,224 mwaka 2020. Kupungua kwa idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ualimu kulitokana na wahitimu wengi kutoka ngazi za chini kujiunga na vyuo vya ufundi.

Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu

445. Mwaka 2020/21, Serikali iliendelea kufanya kaguzi katika shule na vyuo vya ualimu ili kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa katika ngazi zote inakuwa na ubora na viwango vinavyostahili. Katika kipindi hicho, taasisi za elimu 8,326 zilikaguliwa ikilinganishwa na taasisi 5,166 zilizokaguliwa mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 61.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vitendea kazi, rasilimali watu na rasilimali fedha kupitia utekelezaji wa Programu ya Kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Aidha, kusitishwa kwa masomo katika shule na vyuo katika robo ya mwisho ya mwaka 2019/20 katika kudhibiti maambukizi ya UVIKO - 19 kulichangia kupungua kwa idadi ya shule na vyuo vilivyokaguliwa.

Jedwali Na. 19.1 Ukaguzi wa Taasisi za Elimu Mwaka 2019/20-2020/21

Taasisi/Shule/ Vituo/Vyuo	Idadi iliyokaguliwa (2019/20)	Idadi iliyokaguliwa (2020/21)	Badiliko (Asilimia)
Shule za Awali na Msingi	4,042	6,547	62.0
Shule za Sekondari	1,098	1,722	56.8
Vyuo vya Ualimu	26	57	119.2
Jumla	**5,166**	**8,326**	**61.2**

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Elimu ya Ufundi na Mafunzo

446. Mwaka 2020/21, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ilikuwa 157,420 ikilinganishwa na wanafunzi 151,379 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 4.0. Kati ya hao, wanawake walikuwa 75,194, sawa na asilimia 47.8 na wanaume walikuwa 82,226. Ongezeko hilo lilitokana na kuboreshwa na kuanzishwa kwa programu zinazoendana na soko la ajira na kukamilika kwa ukarabati na ujenzi wa miundombinu ikiwemo mabweni, hosteli, kumbi za mihadhara na madarasa. Aidha, vyuo vipya vya ufundi 36 vilisajiliwa na hivyo kuongeza idadi ya vyuo na kufikia 429 mwaka 2020/21 kutoka vyuo 393 mwaka 2019/20.

Elimu ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi

447. Idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ufundi stadi ilikuwa 380,748 (wanawake 155,127 na wanaume 225,621) mwaka 2020/21 ikilinganishwa na wanafunzi 320,143 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 18.9. Aidha, wanafunzi 237,180 (wanawake 49,591 na wanaume 187,589) walihitimu mafunzo ya ufundi stadi mwaka 2020/21 ikilinganishwa na wanafunzi 296,113 waliohitimu mwaka 2019/20. Kwa upande mwingine, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya maendeleo ya wananchi iliongezeka kwa asilimia 65.1 na kufikia 15,032 (wanawake 6,028 na wanaume 9,004) mwaka 2020/21 ikilinganishwa na wanafunzi 9,106 mwaka 2019/20. Aidha, wanafunzi 11,198 (wanawake 4,204 na wanaume 6,994) walihitimu mafunzo katika vyuo vya maendeleo ya wananchi mwaka 2020/21 ikilinganishwa na wanafunzi 8,568 waliohitimu mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 30.7. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi kulitokana na ujenzi, upanuzi na ukarabati wa vyuo vya ufundi stadi 43 na vyuo vya maendeleo ya wananchi 54 pamoja na kuwepo kwa programu zinazoendana na soko la ajira.

Teknolojia na Ubunifu

448. Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha ilidahili wanafunzi 539 (wanaume 355 na wanawake 184) mwaka 2021 ikilinganishwa na wanafunzi 722 (wanaume 472 na wanawake 250) waliodahiliwa mwaka 2020. Katika kipindi hicho, wanafunzi 78 (wanaume 43 na wanawake 35) walihitimu ikilinganishwa na wanafunzi 494 (wanaume 347 na wanawake 147) waliohitimu mwaka 2020. Kwa upande mwingine, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kilidahili wanafunzi 6,779

(wanaume 5,275 na wanawake 1,504) mwaka 2021 ikilinganishwa na wanafunzi 6,137 (wanaume 4,764 na wanawake 1,373) waliodahiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 10.5. Aidha, wanafunzi 1,176 (wanaume 904 na wanawake 272) walihitimu ikilinganishwa na wanafunzi 1,203 (wanaume 952 na wanawake 251) waliohitimu mwaka 2020. Vilevile, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilidahili wanafunzi 3,581 (wanaume 2,839 na wanawake 742) mwaka 2021 ikilinganishwa na wanafunzi 2,190 (wanaume 1,537 na wanawake 653) waliodahiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 63.5. Hii ilitokana na upanuzi wa kampasi ya Myunga-Songwe pamoja na kuongezeka kwa kozi mpya ikiwemo shahada ya madini na ngozi. Kadhalika, wanafunzi 1,029 (wanaume 770 na wanawake 259) walihitimu ikilinganishwa na wanafunzi 604 (wanaume 466 na wanawake 138) waliohitimu mwaka 2020.

449. Mwaka 2021, Serikali iliendesha Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) kwa lengo la kuchochea ubunifu na ugunduzi nchini ambapo wabunifu na wagunduzi 714 walitambuliwa ikilinganishwa na wabunifu na wagunduzi 651 waliotambuliwa mwaka 2020. Kati ya hao, wabunifu na wagunduzi 70 waliendelezwa ili kufikia hatua ya ubiasharishaji kama ilivyokuwa mwaka 2020. Kwa upande mwingine, Serikali ilitambua na kuhakiki teknolojia 169 na kufanya jumla ya teknolojia zilizozalishwa na kutambuliwa kufikia 479 mwaka 2021 kutoka teknolojia 310 mwaka 2020. Lengo la utambuzi huo ni kuwa na kanzidata ya kitaifa itakayorahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu kuhusu teknolojia na ubunifu nchini.

Elimu ya Juu

450. Mwaka 2020/21, wanafunzi katika vyuo vikuu nchini walikuwa 206,305 (wanawake 88,667 na wanaume 117,638) ikilinganishwa na wanafunzi 189,291 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 9.0. Hii ilichangiwa na: kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa hosteli za wanafunzi, kumbi za mihadhara na madarasa; ongezeko la programu; na juhudi za Serikali kuongeza mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Aidha, wanafunzi 48,621 (wanaume 26,976 na wanawake 21,645) walihitimu masomo katika vyuo vikuu mwaka 2020/21 ikilinganishwa na wanafunzi 51,228 waliohitimu mwaka 2019/20 sawa na upungufu wa asilimia 5.1. Hii ilitokana na kufungwa kwa baadhi ya programu na vyuo kutokana na kutokukidhi vigezo kufuatia ukaguzi uliofanywa na Tume ya Vyuo Vikuu

451. Mwaka 2020/21, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu iliongeza utoaji wa mikopo kwa asilimia 3.1 na kufikia shilingi bilioni 464.0 ikilinganishwa na shilingi bilioni 450.0 zilizotolewa mwaka 2019/20. Katika kipindi hicho, wanafunzi 149,472 walinufaika na mikopo hiyo ikilinganishwa na wanafunzi 132,392 walionufaika na mkopo mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 12.9. Kati ya hao, wanafunzi 55,337 walikuwa wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 94,135 walikuwa wakiendelea na masomo. Aidha, marejesho ya mikopo kutoka kwa wanufaika

yalipungua kwa asilimia 5.1 hadi shilingi bilioni 181.0 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na shilingi bilioni 190.7 zilizokusanywa mwaka 2019/20. Hii ilitokana na Serikali kuondoa tozo ya asilimia 6 ya kulinda thamani ya fedha na tozo ya adhabu ya asilimia 10 ambazo awali zilikuwa ni sehemu ya marejesho ya mikopo hiyo.

Udhibiti wa Mionzi

452. Mwaka 2021, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ilipokea na kutathmini maombi 575 ya leseni za matumizi na umiliki wa vyanzo vya mionzi ikilinganishwa na maombi ya leseni 457 yaliyopokelewa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 26.0 Kati ya maombi hayo, maombi 537 yalipata leseni baada ya kukidhi vigezo ikilinganishwa na maombi 455 yaliyopata leseni mwaka 2020. Hadi Desemba 2021, kulikuwa na vituo 1,129 vinavyomiliki na kutumia mionzi ikilinganishwa na vituo 981 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, vituo 666 vilikaguliwa mwaka 2021 ikilinganishwa na vituo 608 vilivyokaguliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 10.0. Kaguzi hizo hufanyika kwa lengo la kudhibiti usalama wa wagonjwa, wafanyakazi na umma.

453. Mwaka 2020/21, Tume ilipima viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 1,982 wanaofanya kazi katika vyanzo vya mionzi ikilinganishwa na wafanyakazi 1,982 waliopimwa mwaka 2019/20 ambapo matokeo yalibainisha kuwa viwango vya mionzi vilivyopo vinakubalika kisheria. Kwa upande mwingine, Tume ilipima viwango vya mionzi katika sampuli 31,371 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na sampuli 21,044 zilizopimwa mwaka 2019/20 kwa lengo la kudhibiti na kusimamia matumizi salama ya mionzi. Kati ya hizo, sampuli 9,732 zilikuwa za vyakula kutoka nje, sampuli 17,864 za vyakula vilivyosafirishwa nje ya nchi, sampuli 924 za mbolea na sampuli 2,851 za tumbaku na bidhaa nyingine. Matokeo yalionesha kuwa sampuli zote zilizopimwa hazikuwa na uchafuzi wa viasili vya mionzi.

SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO

Jedwali Na. 68

Mwaka	I	II	III	IV	V	VI	Jumla
2003	52,863	60,643	36,906	35,653	7,780	6,885	200,730
2004	98,738	67,294	46,546	36,385	8,353	7,572	264,888
2005	134,963	109,398	46,188	46,489	9,710	8,444	355,192
2006	196,391	151,448	72,167	42,584	18,211	9,691	490,492
2007	401,011	218,060	105,770	70,796	21,789	11,668	829,094
2008	395,930	332,393	175,353	95,214	25,240	11,743	1,035,873
2009	480,529	308,131	159,789	167,355	31,201	12,695	1,159,700
2010	382,207	398,870	293,519	279,995	26,065	20,674	1,401,330
2011	403,873	396,724	380,528	279,117	30,265	25,164	1,515,671
2012	457,321	386,250	355,740	343,376	31,206	28,859	1,602,752
2013	444,532	506,036	193,901	302,963	30,581	26,698	1,504,711
2014	479,089	506,170	356,787	178,246	33,619	26,899	1,580,810
2015	-	-	-	-	-	-	-
2016	467,982	366,396	263,981	278,690	45,533	47,007	1,469,589
2017	491,535	443,614	296,034	236,775	53,749	43,494	1,565,201
2018	587,186	480,327	358,960	278,239	57,287	52,687	1,814,686
2019	637,335	555,087	388,029	334,284	52,428	56,042	2,023,205
2020	659,661	588,561	454,139	360,356	58,402	51,138	2,172,257
2021	718,592	616,791	498,703	422,403	66,576	56,880	2,379,945
Badiliko (%) 2020 - 2021	8.9	4.8	9.8	17.2	14.0	11.2	9.6

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi naTeknolojia

- Takwimu hazikupatikana

IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA JINSIA

Jedwali Na. 69A

Elimu ya msingi	2020			2021		
	Waume	Wake	Jumla	Waume	Wake	Jumla
Jumla ya wanafunzi wote walioandikishwa Darasa Ia I-VII	5,443,914	5,481,982	10,925,896	5,557,707	5,639,081	11,196,788
Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za Serikali Darasa Ia I-VII	5,211,409	5,249,376	10,460,785	5,303,268	5,384,325	10,687,593
Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za binafsi Darasa Ia I-VII	232,505	232,606	465,111	254,439	254,756	509,195
Jumla ya walimu katika shule za msingi	98,887	95,849	194,736	101,250	96,669	197,919
Jumla ya walimu katika shule za msingi za Serikali	84,673	85,896	170,569	86,083	85,910	171,993
Jumla ya walimu katika shule za msingi za binafsi	14,214	9,953	24,167	15,167	10,759	25,926
Elimu ya Sekondari						
Jumla ya wanafunzi wote Kidato I-VI	1,189,410	1,284,096	2,473,506	1,282,314	1,389,613	2,671,927
Wanafunzi wanaosoma katika shule za Serikali, kidato I-VI	1,045,557	1,126,700	2,172,257	1,143,165	1,236,780	2,379,945
Wanafunzi wanaosoma katika shule za binafsi, kidato I-VI	143,853	157,396	301,249	139,149	152,833	291,982
Idadi ya walimu katika shule za Serikali	54,221	30,393	84,614	56,920	31,072	87,992
Idadi ya walimu katika shule za binafsi	16,758	4,634	21,392	16,589	4,754	21,343
Jumla ya Walimu katika shule za Sekondari	70,979	35,027	106,006	73,509	35,826	109,335

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
- Takwimu Hazikupatikana

IDADI YA TAASISI ZA ELIMU

Jedwali Na. 69B

Aina ya Taasisi	2020			2021		
	Serikali	Binafsi	Jumla	Serikali	Binafsi	Jumla
Shule za Msingi	16,406	1,746	18,152	16,656	1,746	18,152
Shule za Sekondari	3,863	1,280	5,143	5,289	1,280	5,143
Vyuo vya Ualimu (Msingi na Sekondari)	35	36	71	35	36	71
Elimu ya Ufundi na Mafunzo	-	-	-	-	-	-
Jumla	**20,304**	**3,062**	**23,366**	**20,304**	**3,062**	**23,366**

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
- Takwimu hazikupatikana

SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO

Jedwali Na. 70

Mwaka	I	II	III	IV	V	VI	Jumla
2004	48,752	46,167	33,240	24,476	8,847	6,229	167,711
2005	45,276	46,321	32,063	29,248	9,183	7,046	169,137
2006	46,968	48,013	42,878	29,796	9,569	7,956	185,180
2007	47,437	46,927	41,340	35,746	11,299	8,667	191,416
2008	42,971	43,232	43,177	35,980	12,576	8,594	186,530
2009	44,255	36,384	37,064	34,061	11,851	9,096	172,711
2010	56,620	57,876	50,778	46,820	12,269	13,006	237,369
2011	63,282	67,205	65,859	54,521	11,083	11,926	273,876
2012	65,058	69,403	64,453	61,209	9,684	11,713	281,520
2013	70,060	77,407	67,998	65,637	8,592	9,651	299,345
2014	109,784	96,732	76,574	66,898	8,865	7,686	366,539
2015	-	-	-	-	-	-	-
2016	70,844	81,499	72,970	73,231	21,091	17,731	337,366
2017	71,160	79,548	77,168	72,056	24,146	19,578	343,656
2018	64,844	71,685	74,932	74,848	24,030	23,441	333,780
2019	63,629	64,488	68,064	74,121	22,050	22,900	315,252
2020	63,232	64,727	64,328	67,255	20,032	21,675	301,249
2021	61,784	64,901	64,889	63,481	17,917	19,010	291,982
Badiliko (%) 2019 - 2020	-2.3	0.3	0.9	-5.6	-10.6	-12.3	-3.1

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
- Takwimu Hazikupatikana

SURA YA 20

AFYA NA MAENDELEO YA JAMII

AFYA

Vituo vya Kutolea Huduma za Afya

454. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuboresha na kusogeza miundombinu ya huduma za afya karibu na wananchi. Katika kipindi hicho, vituo vya kutolea huduma za afya viliongezeka na kufikia vituo 10,153 ikilinganishwa na vituo 9,813 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 3.5. Kati ya vituo hivyo, Serikali ilikuwa inamiliki vituo 6,377 sawa na asilimia 61.5 ya vituo vyote, mashirika ya dini vituo 923 (asilimia 9) na sekta binafsi vituo 2,853 (asilimia 28). Ongezeko hilo lilichangiwa na Serikali kuendelea kuboresha miundombinu ya huduma za afya pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji wa mashirika ya dini na sekta binafsi katika ujenzi wa hospitali na vituo vya afya. Mchanganuo wa vituo vya kutolea huduma za afya kwa mwaka 2021 ni kama ifuatavyo: hospitali zilikuwa 404 sawa na asilimia 4; vituo vya afya 956 (asilimia 9); zahanati 7,189 (asilimia 69); kliniki pamoja na vituo vya huduma za uzazi (*maternity homes)* 1,604 (asilimia 16).

455. Mwaka 2021, idadi ya wagonjwa waliohudumiwa ilikuwa 43,099,118 ikilinganishwa na wagonjwa 44,349,923 waliohudumiwa mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 2.8. Kati ya hao, wagonjwa wa nje walikuwa 41,448,117 na wagonjwa wa kulazwa walikuwa 1,651,001. Kupungua kwa wagonjwa kwa upande mmoja kulitokana na wananchi kuendelea kuzingatia kanuni za afya na kwa upande mwingine wananchi walikuwa na hofu ya kufuata huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya kutokana na maambukizi ya UVIKO-19 na badala yake kutumia tiba mbadala. Aidha, idadi ya vitanda vya wagonjwa mwaka 2021 ilikuwa 86,131 ikilinganishwa na vitanda 84,162 mwaka 2020.

Huduma za chanjo kwa Watoto Chini ya Mwaka Mmoja

456. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuimarisha huduma za afya kwa watoto chini ya mwaka mmoja. Katika kipindi hicho, watoto 1,913,690 walizaliwa ikilinganishwa na watoto 1,823,380 waliozaliwa mwaka 2020. Kati ya hao, watoto waliopata chanjo ya PENTA-3 walikuwa asilimia 96, Surua rubella 1 (asilimia 92), Surua rubella 2 (asilimia 78), Rota1 (asilimia 99), Rota2 (asilimia 94), OPV 1 (asilimia 87) na OPV 2 (asilimia 79). Chanjo hizi hutolewa kwa lengo la kuzuia magonjwa ya kupooza, kuharisha, pneumonia, homa ya ini, homa ya uti wa mgongo, surua, pepopunda, polio na dondakoo kwa watoto chini ya mwaka mmoja. Utoaji wa huduma za chanjo nchini ulifikia asilimia 95, hivyo kukidhi vigezo vya Shirika la Afya Duniani vinavyoitaka nchi kuhakikisha kuwa zaidi ya asilimia 90 ya watoto chini ya mwaka mmoja wanapata chanjo.

Dawa na Vifaa Tiba

457. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika kipindi hicho, upatikanaji wa dawa muhimu zinazofuatiliwa *(30 tracer medicines)* katika vituo vya kutolea huduma za afya ulikuwa asilimia 90.9 ikilinganishwa na asilimia 86.0 kwa mwaka 2020. Aidha, upatikanaji wa dawa muhimu 290 ulikuwa asilimia 76.1 ikilinganishwa na asilimia 75.6 kwa mwaka 2020.

458. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuboresha huduma za uchunguzi kwa kununua na kufunga vifaa tiba mbalimbali ikiwemo MRI moja (1), CT mbili (2), Digital X-ray 21 na Ultrasound 14. Vifaa hivyo vilifungwa na kuanza kutoa huduma katika hospitali ya Muhimbili, Lugalo, Mt. Meru Arusha, Mawenzi, Temeke, Amana, Songea, Njombe, Iringa, Mbeya RRH, Songwe, Katavi, Singida, Geita, Simiyu, Bombo, Tumbi, Sokoine, Ligula, Dodoma, Bukoba, Musoma, Ocean Road, Mwananyamala, Bugando, KCMC, Morogoro, Sekotoure, Benjamin Mkapa, Muhimbili-Mloganzila na Mtwara.

459. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuimarisha huduma za uchunguzi na tiba ya saratani nchini kwa: kununua dawa za kutibu saratani; kununua mashine mbili (2) za kuchunguza matokeo ya tiba ya saratani kwa njia ya damu (tumor markers); kununua mashine moja (1) ya kuchakata sampuli za patholojia (Automated Tissue Processor).

Afya ya Uzazi na Mtoto

460. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuhamasisha wajawazito kuanza huduma ya afya ya uzazi na mtoto kabla ya majuma 12 ya ujauzito na kuhudhuria kliniki angalau mara nne (4) katika kipindi cha ujauzito. Katika kipindi hicho, wajawazito waliohudhuria kliniki walikuwa 2,390,704 ikilinganishwa na wajawazito 2,394,736 mwaka 2020. Aidha, wajawazito waliofanya hudhurio la kwanza kabla ya majuma 12 walikuwa asilimia 37.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 37.7 mwaka 2020. Wajawazito waliohudhuria kliniki angalau mara nne (4) walikuwa asilimia 99.7 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 90.1 ya wajawazito waliohudhuria kliniki mwaka 2020. Kwa upande mwingine, huduma ya kumkinga mama mjamzito dhidi ya malaria ilitolewa kwa asilimia 88.7 ikilinganishwa na asilimia 79.0 mwaka 2020. Vilevile, wajawazito waliohudhuria kliniki na kupima Virusi Vya Ukimwi (VVU) walikuwa asilimia 98.6 ikilinganishwa na asilimia 98.0 kwa mwaka 2020. Kati ya wajawazito waliopima VVU, asilimia 1.9 waligundulika kuwa na VVU na asilimia 98.3 ya waliogundulika na VVU walianzishiwa matibabu ya ART (*Antiretoviral therapy*).

461. Mwaka 2021, vituo vilivyokarabatiwa kwa ajili ya kutoa huduma ya upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni iliongezeka kwa asilimia 29.2 na kufikia 629 kutoka vituo 487 mwaka 2020. Hii ilichangiwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi kuendelea kuboresha miundombinu ya afya. Aidha, Serikali iliimarisha huduma ya uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi kwa kuongeza vituo vya kutolea huduma ya

saratani na kufikia vituo 810 mwaka 2021 kutoka vituo 746 mwaka 2020. Katika kipindi hicho, wanawake 459,822 walifanyiwa uchunguzi ikilinganishwa na wanawake 533,780 waliofanyiwa uchunguzi mwaka 2020. Kwa upande mwingine, asilimia 78 ya chanjo aina ya HPV 1 na asilimia 61 ya chanjo aina ya HPV 2 zilitolewa kwa wasichana wenye umri kati ya miaka 9 hadi 14 kwa lengo la kuwakinga dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi.

Huduma za Matibabu ya Kibingwa

462. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuboresha upatikanaji na utoaji wa huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi. Katika kipindi hicho, wagonjwa 93 walipandikizwa figo ikilinganishwa na wagonjwa 78 mwaka 2020. Kati ya hao, wagonjwa 68 walipandikizwa figo katika hospitali ya Taifa Muhimbili na wagonjwa 25 katika Hospitali ya Benjamini Mkapa Dodoma. Aidha, idadi ya watoto waliopandikiziwa vifaa vya usikivu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili iliongezeka na kufikia watoto 42 mwaka 2021 kutoka watoto 34 mwaka 2020.

463. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuboresha huduma za matibabu bingwa kwa kuiwezesha Hospitali ya Muhimbili kwa mara ya kwanza kutoa huduma ya upandikizaji wa uroto (Bone marrow transplant) ambapo wagonjwa watano (5) walipata huduma hiyo. Aidha, wagonjwa 1,425 walifanyiwa upasuaji wa moyo kupitia tundu dogo katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete mwaka 2021 ikilinganishwa wagonjwa 1,262 waliofanyiwa upasuaji mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 12.9.

Udhibiti wa Malaria

464. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuhakikisha kuwa vipimo, dawa, vyandarua na bidhaa nyingine za kudhibiti malaria zinapatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuendelea kudhibiti ugonjwa wa malaria. Katika kipindi hicho, vipimo 27,075,200 vya vitendanishi vya malaria; dozi 16,035,570 za dawa ya mseto na vichupa 1,970,710 vya dawa ya malaria ya sindano vilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na vipimo 40,821,350 vya vitendanishi vya malaria, dozi 16,514,790 za dawa ya mseto na vichupa 4,102,658 vya dawa ya malaria ya sindano mwaka 2020. Kupungua kwa ununuzi wa vitendanishi na dawa za malaria kulitokana na kupungua kwa visa vya malaria nchini ambapo wagonjwa wa malaria walipungua hadi milioni 4.4 mwaka 2021 kutoka milioni 5.9 mwaka 2020. Idadi ya visa vipya vya malaria kwa kila watu 1,000 ilipungua hadi visa 76 kwa mwaka 2021 kutoka visa 106 mwaka 2020 na idadi ya vifo vitokanavyo na malaria ilipungua hadi vifo 1,811 mwaka 2021 kutoka vifo 2,460 mwaka 2020. Aidha, vyandarua 7,508,122 vyenye dawa vilinunuliwa ikilinganishwa na vyandarua 7,951,345 vilivyonunuliwa mwaka 2020. Vyandarua hivyo vilisambazwa kwa shule za msingi, wanawake wajawazito na watoto chini ya mwaka mmoja katika vituo vya kutolea huduma za afya nchi nzima pamoja na kaya zote katika mkoa wa Katavi.

465. Mwaka 2021, ufuatiliaji na ukusanyaji wa sampuli za mbu ulifanyika katika vituo 15 vilivyopo katika halmashauri mbalimbali ambapo mbu 7,793 aina ya anofelesi walikusanywa na kupelekwa katika Taasisi ya Magonjwa ya Binadamu (NIMR - Muheza) kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara. Aidha, Serikali iliendelea kutekeleza afua ya ufuatiliaji na matibabu ya wagonjwa wa Malaria hadi ngazi ya kaya katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara ambayo ina kiwango kidogo cha maambukizi ya malaria nchini. Hii ni hatua muhimu kuelekea kutokomeza ugonjwa wa malaria hapa nchini.

Udhibiti wa Kifua Kikuu

466. Mwaka 2021, Serikali iliendelea na mapambano dhidi ya kifua kikuu ambapo wagonjwa 87,132 waligundulika na kuanzishiwa dawa ikilinganishwa na wagonjwa 39,044 waliogundulika na kuanzishiwa dawa mwaka 2020. Katika kipindi hicho, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya afya iliongeza mashine 72 za kisasa za GeneXpert ikilinganishwa na mashine 21 mwaka 2020. Vilevile, Serikali ilinunua mashine 179 za ufuatiliaji wa wagonjwa wa kifua kikuu sugu (ECG) na kuzisambaza katika halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, vituo vya kutolea huduma za uchunguzi na tiba ya kifua kikuu viliongezeka na kufikia 1,749 mwaka 2021 kutoka vituo 1,613 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 8.4. Kwa upande mwingine, Serikali ilinunua magari manne (4) yenye vifaa vya uchunguzi wa kifua kikuu ambayo yalisaidia kufikiwa kwa jamii zilizo mbali na maeneo ya kutolea huduma hasa makundi maalumu ya jamii ikiwemo wavuvi, wachimbaji wadogo wa madini na jamii zisizo na makazi maalumu.

UVIKO - 19

467. Mwaka 2021, Ugonjwa wa Virusi vya Korona 19 (UVIKO - 19) uliendelea kuathiri nchi mbalimbali duniani tangu uliporipotiwa nchini China mwezi Desemba 2019. Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizoathiriwa na UVIKO -19 ambapo hadi Desemba 2021 ilikumbwa na mawimbi matatu ya mlipuko wa ugonjwa huo ambayo ni SARS - CoV-2, Delta na Omicron. Katika kipindi hicho, sampuli 325,728 zilipimwa ambapo sampuli 26,115 zilithibitika kuwa na maambukizi na jumla ya watu 725 walipoteza maisha.

468. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kutekeleza mikakati mbalimbali katika kukabiliana na maambukizi ya UVIKO - 19 ikiwemo kuhamasisha jamii kuchukua hatua madhubuti za kujikinga na ugonjwa huo. Katika kipindi hicho, Serikali iliridhia matumizi ya chanjo za UVIKO - 19 kama moja ya afua ya kinga dhidi ya ugonjwa huo ambapo dozi 6,408,750 za chanjo zilipatikana. Kati ya hizo, chanjo aina ya Janssen zilikuwa dozi 1,343,550, Sinopharm dozi 2,578,200, Pfizer dozi 2,110,680 na Moderna dozi 376,320. Kwa upande mwingine, Serikali ilinunua na kufunga mitambo saba (7) ya hewa tiba ya Oksijeni katika hospitali mbalimbali. Vilevile, maabara za uchunguzi wa UVIKO - 19 ziliongezeka na kufikia maabara 10 mwaka 2021 kutoka maabara tatu (3) mwaka 2020.

Hadi Machi 2022, jumla ya watu milioni 2.8 walipata dozi kamili ya chanjo kati ya watu takribani milioni 30.7 wenye umri wa miaka 18 na kuendelea.

Lishe

469. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe wa mwaka 2016/17 - 2020/21 kwa lengo la kukabiliana na athari za lishe duni na kuimarisha ukuaji mzuri wa mwili na akili kwa mtoto. Katika kipindi hicho, zaidi ya asilimia 97 ya watoto milioni 15.7 walio chini ya umri wa miaka mitano walipatiwa matone ya Vitamini A ikilinganishwa na asilimia 90 mwaka 2020. Aidha, asilimia 90 ya watoto waliozaliwa katika vituo vya kutolea huduma za afya walinyonyeshwa ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa ikilinganishwa na asilimia 91.3 mwaka 2020. Vilevile, watoto waliozaliwa na uzito pungufu walikuwa asilimia 6.3 ikilinganishwa na asilimia 5.6 ya watoto waliozaliwa mwaka 2020. Kwa upande mwingine, asilimia 1.2 ya wajawazito waliopimwa wingi wa damu katika hudhurio la kwanza walikuwa na upungufu mkubwa wa damu ikilinganishwa na asilimia 0.9 ya wajawazito waliopimwa mwaka 2020. Upungufu huo ulisababishwa na mabadiliko ya mwili na lishe duni kabla na wakati wa ujauzito.

Mafunzo katika Kada za Afya

470. Mwaka 2021, wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya afya walikuwa 29,519 ikilinganishwa na wanafunzi 20,698 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 42.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vyuo vipya 10 na kufikia vyuo 192 mwaka wa masomo 2021/22 kutoka vyuo 182 mwaka 2020/21. Kati ya hao, wanafunzi 5,041 walijiunga katika vyuo vya Serikali na wanafunzi 24,478 katika vyuo binafsi na taasisi za dini. Wanafunzi hao walidahiliwa katika programu za utabibu, uuguzi na ukunga, famasia, utaalamu wa maabara ya tiba, sayansi za afya ya mazingira, utunzaji wa kumbukumbu za afya na tiba kwa vitendo. Aidha, wanafunzi 24,254 walihitimu katika vyuo vya afya mwaka 2021 ambapo wanaume walikuwa 11,929 na wanawake 12,325.

MAENDELEO YA JAMII

Ustawi wa Jamii

471. Mwaka 2021, Serikali iliandaa Mwongozo wa Uhamasishaji wa Ujenzi wa Nyumba Bora katika Ngazi ya Jamii na kuusambaza kwa maafisa maendeleo ya jamii katika ngazi ya kata, wilaya na mikoa yote ya Tanzania Bara. Aidha, Serikali kupitia kampeni ya ujenzi wa nyumba bora kwa gharama nafuu zinazotumia teknolojia rahisi iliwawezesha wananchi kujenga nyumba bora 4,008 katika mikoa yote ya Tanzania Bara ikilinganishwa na nyumba 751 zilizojengwa katika mikoa minne (4) mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishaji kuhusu ujenzi wa nyumba bora uliofanyika katika mikoa yote.

Mafunzo ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii

472. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kusimamia utoaji wa mafunzo ya maendeleo na ustawi wa jamii kupitia Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Taasisi ya Ustawi wa Jamii - Kijitonyama na vyuo nane (8) vya maendeleo ya jamii vya Buhare, Mlale, Misungwi, Rungemba, Mabughai, Ruaha, Uyole na Monduli.

473. Mwaka 2021, wanafunzi 5,135 (wanawake 3,023 na wanaume 2,112) walidahiliwa katika vyuo nane (8) vya maendeleo ya jamii ikilinganishwa na wanafunzi 4,853 (wanawake 2,982 na wanaume 1,871) waliodahiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 5.8. Ongezeko hilo lilitokana na uanzishwaji wa vituo vya kidigitali vya ubunifu na maarifa, programu za uanagenzi pamoja na ushirikishwaji wa jamii ambazo hazipo kwenye vyuo vingine na hivyo kuvutia wanafunzi wengi kuomba kujiunga na katika vyuo hivyo. Katika kipindi hicho, wanafunzi 2,759 walihitimu ikilinganishwa na wanafunzi 3,953 mwaka 2020.

474. Mwaka 2021, wanafunzi 2,793 (wanawake 1,855 na wanaume 938) walidahiliwa katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii - Tengeru ikilinganishwa na wanafunzi 2,492 (wanawake 821 na wanaume 1,671) waliodahiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 12.4. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Mwaka 2021, wanafunzi 1,464 (wanaume 458 na wanawake 1,006) walihitimu katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 1,003 (wanaume 262 na wanawake 741) waliohitimu mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 46.0.

475. Mwaka 2021, wanafunzi 3,234 (wanawake 2,104 na wanaume 1,130) walidahiliwa katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii - Kijitonyama ikilinganishwa na wanafunzi 2,187 (wanawake 1,434 na wanaume 753) waliodahiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 47.9. Aidha, wanafunzi 2,493 (wanaume 848 na wanawake 1,645) walihitimu katika fani na ngazi mbalimbali mwaka 2021 ikilinganishwa na wahitimu 1,246 (wanaume 318 na wanawake 928) mwaka 2020.

476. Mwaka 2021**,** Serikali iliendelea kutekeleza Programu ya Uanagenzi kwa kuwaunganisha wanafunzi na wahitimu wa taaluma ya maendeleo ya jamii kwenye mashirika, taasisi, na makampuni ili kupata mafunzo kwa vitendo kwa lengo la kuwapatia ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa unaoendana na soko la ajira. Katika kipindi hicho, wahitimu 289 wa taaluma ya maendeleo ya jamii walipata mafunzo kwa vitendo ikilinganishwa na wahitimu 219 mwaka 2020.

Huduma ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto

477. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuratibu utoaji wa huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5) katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana. Katika kipindi hicho, vituo 303 vya kulelea watoto

wadogo mchana vilisajiliwa ikilinganishwa na vituo 134 vilivyosajiliwa mwaka 2020. Ongezeko la usajili wa vituo ulitokana na kuongezeka kwa uelewa wa wazazi juu ya umuhimu wa vituo hivyo. Aidha, watoto 184,557 (wavulana 92,540 na wasichana 92,017) waliandikishwa mwaka 2021 ikilinganishwa na watoto 163,394 (wavulana 85,175 na wasichana 78,219) walioandikishwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 13.0.

478. Mwaka 2021, idadi ya walezi wa watoto katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana iliongezeka kwa asilimia 12.3 na kufikia walezi 3,233 ikilinganishwa na walezi 2,878 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya vituo vya kulea watoto wadogo mchana. Katika kipindi hicho, Serikali iliendelea kuwajengea uwezo wazazi na walezi wa watoto kupitia maafisa maendeleo ya jamii kwa kuunda vikundi vya malezi chanya. Jumla ya vikundi 1,186 vya malezi chanya kwa watoto viliundwa mwaka 2021 ikilinganishwa na vikundi 2,777 mwaka 2020.

Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Watoto

479. waka 2021, Serikali iliendelea kutekeleza afua mbalimbali zinazotoa fursa kwa watoto walio katika mazingira hatarishi kulelewa katika familia kupitia huduma ya malezi ya kambo na kuasili. Katika kipindi hicho, watoto 58 (wasichana 30 na wavulana 28) walio katika mazingira hatarishi walipata huduma za malezi ya kambo ikilinganishwa na watoto 217 (wasichana 110 na wavulana 107) mwaka 2020. Aidha, watoto walioasiliwa walikuwa 51 (wasichana 30 na wavulana 21) mwaka 2021 ikilinganishwa na watoto 95 (wasichana 51 na wavulana 44) walioasiliwa mwaka 2020.

480. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kutoa huduma za msingi ikiwemo, chakula, mavazi, malazi, elimu na huduma za afya kwa watoto walio katika mazingira hatarishi wanaoishi katika makao ya watoto ya Kurasini, Dar es Salaam na Kikombo, Dodoma. Katika kipindi hicho, watoto 76 (wasichana 31 na wavulana 45) walipatiwa huduma hizo ikilinganishwa na watoto 80 (wasichana 40 na wavulana 40) waliopata huduma hiyo mwaka 2020. Aidha, watoto 24,254 (wasichana 13,331 na wavulana 10,923) walipatiwa huduma za msingi kupitia makao ya watoto ya binafsi mwaka 2021 ikilinganishwa na watoto 15,290 (wasichana 7,053 na wavulana 8,237) waliopatiwa huduma hizo mwaka 2020.

481. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kutoa huduma za msingi pamoja na huduma za msaada wa kisheria kwa watoto walio katika mkinzano na sheria katika mahabusu za watoto za Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam. Katika kipindi hicho, watoto 58 (wasichana 7 na wavulana 51) walio katika mkinzano na sheria waliwezeshwa kupata huduma za chakula, malazi, mavazi, matibabu na elimu ikilinganishwa na watoto 138 (wasichana 18 na wavulana 120) mwaka 2020.

482. Mwaka 2021, watoto 49 (wasichana 7 na wavulana 42) waliokuwa katika mkinzano na sheria walichepushwa kutoka katika mfumo rasmi wa haki jinai kwa kuwarekebisha tabia na kuwaunganisha na familia zao ikilinganishwa na watoto 78 (wasichana 5 na wavulana 73) mwaka 2020. Katika kipindi hicho, watoto 58 (wasichana 7 na wavulana 51) walihukumiwa na kupelekwa katika Shule ya Maadilisho Irambo, Mbeya ikilinganishwa na watoto 31 (msichana mmoja (1) na wavulana 30) waliohukumiwa mwaka 2020. Ongezeko la idadi ya watoto waliopelekwa katika shule ya maadilisho lilitokana na jamii kuwa na mwamko zaidi wa kutoa taarifa za makosa ya jinai katika mamlaka husika ambapo awali makosa mengi yalikuwa yakimalizwa katika ngazi ya jamii.

Maendeleo ya Wanawake na Jinsia

483. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuweka mazingira wezeshi katika kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi. Katika kipindi hicho, Serikali kupitia Dirisha la Wanawake katika Benki ya Biashara Tanzania iliendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wajasiriamali wanawake ambapo shilingi milioni 17,593.2 zilitolewa kwa wanawake 3,393 ikilinganishwa na shilingi milioni 9,994.8 zilizotolewa kwa wanawake 5,234 mwaka 2020. Katika kipindi hicho shilingi milioni 4,770.3 zilirejeshwa sawa na asilimia 94.2 ya lengo la marejesho ya shilingi 5,064.9 katika kipindi husika.

484. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuhamasisha na kuwezesha kuanzishwa na kuimarishwa kwa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto katika ngazi ya Taifa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Juhudi hizo ziliwezesha kuundwa kwa kamati 1,843 (kamati 58 katika ngazi ya halmashauri, 457 ngazi ya kata, 1,217 ngazi ya kijiji na 111 ngazi ya mtaa) ikilinganishwa na kamati 4,823 zilizoundwa mwaka 2020.

485. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kufuatilia na kudhibiti makosa ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia ikiwemo ubakaji, ulawiti, kutupa watoto, wizi wa watoto, ukeketaji na vipigo kupitia kikosi kazi maalumu chini ya Dawati la Jinsia. Katika kipindi hicho, matukio ya ukatili wa kijinsia 17,874 yalitolewa taarifa ikilinganishwa na matukio 26,544 yaliyotolewa taarifa mwaka 2020 sawa na upungufu wa asilimia 32.7. Kati ya hayo, matukio 11,138 sawa na asilimia 62.3 walifanyiwa wanawake na matukio 6,736 walifanyiwa wanaume. Aidha, matukio 11,499 ya ukatili wa kijinsia kwa watoto yalitolewa taarifa ikilinganishwa na matukio 15,870 yaliyotolewa taarifa mwaka 2020 sawa na upungufu wa asilimia 27.5. Makosa ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia yaliyotolewa taarifa yalipungua kutokana na jitihada za Serikali na wadau mbalimbali katika kuimarisha huduma za Madawati ya Jinsia katika vituo vya polisi pamoja na kuongeza uelewa wa jamii kuhusu makosa hayo na kuhamasisha wananchi kutoa taarifa kuhusu vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia.

Huduma za Ustawi kwa Wazee

486. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kutoa huduma za msingi kwa wazee wasiojiweza wanaoishi katika makazi 13 yanayomilikiwa na Serikali. Katika kipindi hicho, wazee 275 (wanawake 111 na wanaume 164) walipatiwa huduma za msingi katika makazi hayo ikilinganishwa na wazee 291 (wanawake 111 na wanaume 180) waliopatiwa huduma mwaka 2020. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya wazee kufariki na wengine kuunganishwa na familia zao.

Mashirika yasiyo ya kiserikali

487. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kusimamia mashirika yasiyo ya kiserikali katika kuchangia kuleta maendeleo ya Taifa. Katika kipindi hicho, Serikali ilisajili mashirika yasiyo ya kiserikali 692 (ngazi ya kimataifa mashirika 28, ngazi ya taifa mashirika 633, ngazi ya mkoa mashirika 14 na ngazi ya wilaya mashirika 17) ikilinganishwa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali 377 yaliyosajiliwa mwaka 2020. Ongezeko la usajili lilitokana na uboreshwaji wa mfumo wa usajili wa mashirika kwa njia ya kielektroniki.

488. Mwaka 2021, utendaji kazi wa mashirika yasiyo ya kiserikali 2,717 ulifuatiliwa ikilinganishwa na mashirika 206 yaliyofuatiliwa mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na ufuatiliaji uliofanyika kupitia Mkutano wa mwaka wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali ambapo taarifa za mashirika hayo zilifanyiwa uchambuzi pamoja na ufuatiliaji wa Mashirika kwa njia ya mtandao (zoom). Aidha, katika mikutano hiyo baina ya wizara na mashirika hayo ufafanuzi kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hutolewa. Kwa upande mwingine, Serikali ilikagua mikataba 804 ya kifedha ya mashirika yasiyo ya kiserikali na kubaini kuwa jumla ya shilingi bilioni 1,423.3 zilipokelewa mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 118.4 zilizopokelewa kupitia mikataba ya kifedha 130 iliyokaguliwa mwaka 2020. Kaguzi hizo hufanyika kwa lengo la kuhakiki utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na mashirika hayo kwa mujibu wa mikataba.

.

IDADI YA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Jedwali Na. 71

Aina ya Vituo	2020				2021			
	Serikali	Dini	Binafsi	Jumla	Serikali	Dini	Binafsi	Jumla
Hospitali	185	117	67	369	207	112	85	404
Vituo vya Afya	645	124	157	926	679	150	127	956
Zahanati	5,395	676	1,092	7163	5491	622	1076	7189
Jumla ndogo	**6,225**	**917**	**1,316**	**8458**	**6,377**	**884**	**1288**	**8549**
Poly clinic					0	22	208	230
*Nyinginezo	1	5	1,270	1,276	0	16	1,282	1,298
Martenity/Nursing homes	0	1	78	79	0	1	75	76
Jumla kuu	**6,226**	**923**	**2,664**	**9,813**	**6,377**	**923**	**2,853**	**10,153**

Chanzo: Wizara ya Afya
* Ni pamoja na kliniki
- Takwimu hazikupatikana

IDADI YA WAGONJWA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Jedwali Na. 72

Mwaka	Wagonjwa wa Nje			Jumla ya Wagonjwa waliolazwa
	Hospitali	Zahanati	Vituo vya Afya	
2004	1,532,028	23,552,460	3,758,027	2,125,388
2005	1,619,700	24,900,276	3,973,085	2,237,146
2006	1,754,925	26,979,136	4,304,787	2,837,252
2007	1,842,671	28,328,093	4,520,026	2,979,115
2008	1,934,805	29,744,498	4,746,027	3,128,071
2009	2,128,286	32,718,948	5,220,630	3,440,870
2010	2,341,114	35,990,843	5,742,693	3,784,957
2011	2,622,048	39,917,117	6,431,816	4,239,152
2012	2,815,529	41,333,522	6,657,817	4,388,108
2013	2,903,275	42,682,479	6,873,056	4,529,971
2014	5,910,725	14,008,692	475,295	1,665,935
2015	4,480,781	25,072,487	6,006,466	1,858,956
2016	4,984,645	20,859,281	6,515,219	1,775,835
2017	5,266,252	21,115,639	7,050,725	1,650,224
2018	4,675,045	27,473,506	8,903,461	1,359,264
2019	9,821,148	26,500,182	10,153,322	1,852,720
2020	10,150,504	22,154,653	9,741,820	1,852,720
2021	11,348,037	19,705,594	9,219,985	1,651,001

Chanzo: Wizara ya Afya

IDADI YA VITANDA KATIKA HOSPITALI ZOTE NCHINI

Jedwali Na. 73

Aina ya Huduma	2020				2021			
	Serikali	Shirika la kujitolea/ Dini	Binafsi	Jumla	Serikali	Shirika la kujitolea/Dini	Binafsi	Jumla
Hospitali ya Taifa	-	-	-	-	1,664	-	-	1,664
Hospitali Maalumu za kibingwa	-	-	-	-	1,532	-	-	1,532
Hospitali za Rufaa za Kanda	-	-	-	-	2,407	-	-	2,407
Hospitali za Mikoa	7,307	898	420	8,625	7,239	898	420	8,557
Hospitali za Wilaya	10,328	7,629	409	18,366	10,636	6,228	409	17,273
Hospitali nyingine	1,820	8,753	1,559	12,132	1,098	10,395	2,915	14,408
Vituo vya Afya	16,211	6,223	2,225	24,659	14,363	4,939	2,105	21,407
Zahanati	13,549	3,712	3,119	20,380	14,462	1,863	2,558	18,883
Jumla	**49,215**	**27,215**	**7,732**	**84,162**	**53,401**	**24,323**	**8,407**	**86,131**

Chanzo: Wizara ya Afya

UDAHILI WA WANAFUNZI KATIKA TAASISI ZA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII

Jedwali. Na. 74

Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru	Ngazi ya Elimu	2020			2021			Badiliko (Asilimia)
		Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	
	Astashahada	870	357	1227	456	942	1398	13.9
	Stashahada	229	83	312	307	683	990	217.3
	Shahada	553	366	919	156	211	367	-60.1
	Stashahada ya Juu ya Maendeleo ya Jamii	19	15	34	19	19	38	11.8
	Jumla Ndogo	**1,671**	**821**	**2,492**	**938**	**1,855**	**2,793**	12.1
Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama	Astashahada	375	545	920	373	506	879	-4.5
	Stashahada	145	402	547	204	470	674	23.2
	Shahada	221	469	690	522	1064	1586	129.9
	Stashahada ya Juu	8	12	20	0	0	0	-100.0
	Shahada ya Uzamili	4	6	10	31	64	95	850.0
	Jumla Ndogo	**753**	**1,434**	**2,187**	**1,130**	**2,104**	3234	47.9
Vyuo vya Maendeleo ya Jamii	Stashahada	357	843	**1,200**	**669**	**811**	**1,480**	23.3
	Astashahada	1514	2,139	**3,653**	**1,443**	**2,212**	**3,655**	0.1
	Jumla Ndogo	**1,871**	2,982	**4,853**	**2,112**	**3,023**	**5,135**	5.8

Chanzo: Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu

MCHANGO WA SEKTA KATIKA PATO LA TAIFA MWAKA 2021



WATALII WALIOTEMBELEA VIVUTIO MBALIMBALI NCHINI